

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 15 Februari, 2011**

*(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. *(The Annual Report and Accounts of TCRA Consumer Consultative Council, TRCA – CCC for the year ended 30th June, 2010).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

**Madai ya Walimu Wastaafu – Singida**

**MHE. MWIGULU LAMECK MCHEMA MADELU (K.n.y. MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO)** aliuliza:-

Walimu wanane (8) wastaafu wa Manispaa ya Singida waliokuwa wameajiriwa kwa mkataba bado hawajalipwa madai ya mishahara ya miezi kumi na sita (16) licha ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kulifuatilia suala hili kwa karibu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna walimu wastaafu nane waodai malimbikizo yao ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, kilichojitokeza hapa ni utaratibu wa mikataba kutoeleweka vizuri. Hivyo wahusika kukosea kosea mikataba na kurudishwa ili kujaza upya na hivyo kuchelewesha zoezi la ulipaji wa mishahara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa sasa mwajiri ambaye ni Halmashauri huomba kibali cha kuajiri walimu wastaafu kwa mkataba toka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Baada ya kibali kutolewa Halmashauri husika huingia Mkataba na walimu watakuwa wameridhika na sifa za uwezo wao wa kufundisha mishahara yao na kufundisha katika shule za msingi na Sekondari. Walimu hawa na mikataba yao watalipwa mishahara yao kwa viwango vyao walivyofikia kabla ya kustaafu kwao katika orodha ya malipo (*payroll* ya Serikali Hazina).

Aidha, malipo ya walimu hawa yameandaliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kinachosubiriwa sasa ni kibali cha Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili walipwe madai yao.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri swali hili nimeshauliza ndani ya Bunge hili mara nne leo ni mara ya tano. Kwa kuwa inasikitisha sana Serikali imekuwa ikinihidi ndani ya Bunge hili kwamba malipo ya walimu hawa ni halali na yanaandaliwa mara zote. Mara ya nne nikajibiwa mwaka jana mwezi wa nne kwamba malipo yao yatalipwa kabla ya Bunge la Bajeti Julai mwaka jana 2010. Leo hii tena naambiwa kibali cha utumishi kinasubiriwa.

**SPIKA:** Jitahidi maswali ya nyongeza yawe mafupi.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii iko chini ya Waziri Mkuu naweza nikapewa kauli ya Serikali kuhusu madai haya kwa kuwa walimu hawa wana hali mbaya sana? (*Makofi*)

Kwa kuwa inaonyesha wazi watendaji, ndani ya Wizara ya Elimu ukiacha TAMISEMI ambayo imegatuliwa sasa hivi wanadharau kauli za Mawaziri wanazotoa hapa Bungeni. Je, inasema nini kuhusu watendaji hawa wanaokwamisha utekelezaji wa Serikali ya CCM na kunifanya mimi mwakilishi wa walimu hawa kuonekana sina maana? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba swali hili limeulizwa hapa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, lakini napenda nimhakikishie kwamba kwa kipindi hiki cha ugatuuji wa madaraka kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo kwenda TAMISEMI tukiwa tunashughulikiwa walimu wa elimu ya msingi na sekondari sasa jambo hili tutalifuatilia na mimi sasa kwa kuwa ndio mhusika na ndio mwenye dhamana ya elimu ya msingi na sekondari ndani ya

TAMISEMI nitahakikisha nafuatilia jambo hili mpaka linapata mafanikio. Sitakubali tena hili lije kuulizwa tena hapa mwezi Aprili . (*Makofi*)

Na. 68

### **Hitaji la Umeme Katika Vijiji vya Jimbo la Mbeya Vijijini**

**MHE. MCH. LUCKSON NDAGA MWANJALE** aliuliza:-

Umeme unapitia katika vijiji vya Haporoto, Idimi Kata ya Ihangu na Kijiji na Lwanjilo, Ifupa kata ya Ilungu, Iyawayata Kata ya Inyala, Songwi Juu Kata ya Ijombe kuelekea Wilaya nyingine lakini hakuna *transfoma* kwenye maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali itafunga *transfoma* katika Kata hizo ili wananchi hao waweze kupata huduma ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ni kati ya vijiji 112 vilivyomo kwenye jimbo la Mbeya Vijijini ambavyo bado havijapata huduma ya umeme japo vinapitiwa na njia za msongo wa kilovolti 33 na 11. Zoezi la kutathimini gharama za ufungaji wa *transfoma* na ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 ili kuvipatia umeme vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge linatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2011 na litakamilika mwezi Machi, 2011. Maombi ya fedha kwa ajili ya mradi huo yanatarajiwa kuwasilishwa kwa wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) punde baada ya tathimini hiyo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, zoezi la kuainisha vijiji vyote nchini vinavyopitiwa na njia za umeme msongo wa kilovoti 33 ama 11 na ambavyo havina umeme vikiwemo vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, limekamilika na kukabidhiwa kwa wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa hatua zaidi.

**MHE. MCH. LUCKSON NDAGA MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi hiyo itakamilika mwezi Machi. Je, Waziri atanihakikishia kwamba gharama hizi zitaingizwa katika Bajeti ya mwaka huu na kwamba mwaka huu umeme uanze kufungwa pale? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa sasa hivi katika hii miradi iliyokuwepo pale kwake ni kutoka Izombwe kwenda Santilia, Santilia kwenda Hongoro ambao ndio mradi ambao uko kwenye utekelezaji sasa hivi. Nilichosema ni kwamba baada ya mradi huu kukamilika ambao umeshafanyiwa tathimini mkandarasi ameshafika, vifaa vingine vinakuja, nguzo zilizokuwepo pale kama miaka minane (8) zimesimama tu zimesharibika. Kwa hiyo, zinakuja nguzo mpya zinaanza

kuwekwa kuanzia mwezi wa nne. Lakini tukimaliza kazi hii ndio tunaanza kusambaza sasa kutokana na mradi huu, ni mradi mkubwa kwenda kwenye vijiji alivyovitaja. Kazi ya kufanya tathimini ya vijijini hivyo ndio tunatarajia iingie ikamilike baina ya mwezi wa pili na wa tatu Machi, 2011 na kwa maana hiyo, tunatarajia tutavitumbukiza katika Bajeti ya Wizara na ya REA ili tuone kama tutapata utekelezaji mwaka ujao.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado tuko kwenye maeneo ya Mbeya ningependa kujua ni limi umeme utapelekwa kwenye Kata za Iziwa, Itagano, Itende, Mwansekwa na Tembela zote za Mbeya Mjini ambalo ni Jiji kwa kuwa baadhi ya Kata kama Isiwa tayari wananchi walishafanya wiring kwenye nyumba zao miaka mingi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea Kata hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbilinyi kwamba Wilaya ya Mbeya Mjini inatarajia kupata mradi wa usambazaji umeme kupitia MCC na ambao wakandarasi wameshafika wameshafanya tathimini. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba maeneo mengi kwa sababu ndio sera ya MCC hayo ambayo yatafikiwa na mradi wa MCC baada ya hapo yale mengine tutafanya sisi wenyewe.

Kwa hiyo, naomba tufanye subira ili tukamilishe mradi huu wa awamu ya MCC ya usambazaji katika maeneo mbalimbali Mkoa wake uko katika Mikoa Sita itakayofikiwa na mradi huo halafu tufanye tathimini ya hayo maeneo mengine ambayo yatakuwa hayajafikiwa na mradi huo.

Na. 69

### **Benki Kutoza Riba Kubwa**

**MHE. ABBAS ZUBERI MTEMVU** aliuliza:-

Benki za *CRDB*, *NMB* na *NBC* zilizoko ndani ya Ofisi za Bunge Dodoma, zimekuwa zikitoa mikopo ya riba ya 15% wakati kuna asilimia moja inakatwa kwa ajili ya bima:-

- (a) Je, ni kwa nini riba hiyo ni kubwa sana na wakati mkopaji ana dhamana ya mshahara wake na pia ana bima ya asilimia moja?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuzungumza na benki hizo ili zishushe riba zake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ruhusa yako, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kufuatia mageuzi ya sekta ya kifedha nchini kuanzia mwaka 1991, Serikali ilisitisha upangaji wa riba zinazotowwa na mabanki na kuruhusu riba hizo kuwekwa kwa nguvu ya soko, mahitaji na ugavi. Lengo la hatua hii likiwa ni kuweka riba zinazoendana na hali halisi ya soko kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine, sifa alizonazo mkopaji. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Abbas Mtemvu kwamba japokuwa dhamana ya mishahara na bima ni vigezo muhimu vinavyotumiwa na mabanki katika kupanga viwango vya riba, hivyo siyo vigezo pekee na havitoshelezi. Kwa mantiki hiyo basi mabanki yamekuwa yakitoa sababu mbalimbali za kutoza riba kubwa kwa baadhi ya wakopaji. Kwa mfano, sababu ya kwanza ni sifa alizonazo mkopaji, urahisi wa upatikanaji wa taarifa juu ya sifa za wakopaji, ikiwa ni pamoja na vyombo vinavyoweza kuhakiki usahihi wa taarifa hizo. Sababu nyingine zinazotolewa na mabanki ni ukosefu wa dhamana zinazokubalika na kuuzika kwa urahisi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za sekta ya kifedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza riba kwa ujumla na sio kwa wafanyakazi pekee, Serikali inatekeleza awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha (*The Second Generation Financial Sector Reforms*). Chini ya mpango huu mikakati mahususi imewekwa ili kukabiliana na matatizo kwenye sekta hiyo likiwemo tatizo la riba za juu za mkopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuweka sera za kibajeti (*Monetary and Fiscal Policies*) ili kupunguza mfumuko wa bei ambao ni mhimili mkubwa wa mfumo wa riba. Baadhi ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na kudhibiti ongezeko la fedha, kuboresha mfumo wa malipo nchini na pia kuyashawishi mabanki kupunguza makali ya riba ya mikopo. Hali kadhalika, Benki Kuu imekuwa ikihamasisha mabanki kuwa na miongozo ambayo itawaelimisha wananchi namna ya kutumia na kulipa mikopo waliyokopa toka mabanki na hivyo kuongeza urejeshaji wa mikopo hiyo. (*Makofi*)

**MHE. ABBAS ZUBERI MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imehamasisha wajasiriamali wengi wafungue vikundi kama VIKOBA na wananchi wengi wamepokea na sasa tuna makampuni mengi binafsi ambayo yanakopesha. Lakini bado riba ziko juu. Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hawa ambao wanakopa kwenye makampuni binafsi kuhakikisha riba inakwenda chini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba mikopo inayotoka hasa kwa sekta isiyo rasmi, ina riba kubwa. Serikali inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba riba hizo zinashuka. Hata hivyo kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi ni kwamba taarifa za mkopaji ni muhimu katika kupanga kiwango cha riba. Katika Mikopo inayotolewa hasa kwa VIKOBA na SACCOS ni kwamba wale *benefisharies* wengi wako kwenye sekta isiyo rasmi na hivyo wana upungufu wa taarifa. Taarifa za wapi wanapatikana pia na suala la dhamana.

Kwa hiyo, mifuko inayotoa mikopo kwa watu hawa inakuwa na tahadhari kubwa kuhakikisha kwamba waweke riba kubwa ili watakaokosekana kulipa waweze kurekebisha tatizo hilo kutokana na kipato cha riba.

Hata hivyo Serikali inachukua hatua za kutosha ikiwemo kujenga mazingira bora ya kuhakikisha kwamba taasisi nyingi zaidi zinajitokeza ili kuongeza ushindani jambo ambalo tuna hakika litashusha viwango vya riba. Lengine ni kama suala la kurasimisha rasilimali hili litasaidia kwa sababu wakopaji kwenye mifuko hii watakuwa na vitu vya kuweka dhamana. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi nilitolea kumbukumbu (*reference*) kuhusiana na mikopo ambayo si Wabunge tu hata wafanyakazi wengine ama wa Serikali, kama walimu na kadhalika, ambao wanachukua mikopo kwenye mablenki ambayo kimsingi ni *riskless* kwa sababu taarifa za wakopaji zipo, fedha wanazipata kama mshahara. Serikali iko tayari kushirikiana na Bunge kukutana na mablenki chini ya uongozi wa Benki Kuu (BOT) ili kujadiliana upya kuhusu riba hizi kwa sababu ni kubwa sana, inakuwa kama tunayalipa tu mablenki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri umelielewa swali. Wakati wananchi wengine wanasema taarifa zao sio makini, lakini kuna watu wanafanya kazi na wapo kabisa ni muajili na benki kuchukua hela tu, risk hapa iko wapi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kwa niba ya Waziri wa Fedha naomba kulijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba Serikali lengo lake, ni kuhakikisha kwamba mwekezaji na wananchi wanapata *resources* kwa ajili ya kufanya biashara hiyo ndiyo amabyo italeti tija kwa Serikali. Kwa hiyo, wazo lolote linalokubalika la kutaka kushusha riba Serikali iko tayari kushirikiana nalo ili tuweze kuhakikisha kwamba uchumi unakuwa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibiashara.

Na. 70

### **Haki za Wazee Kupatiwa Mahitaji ya Lazima**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Ibara ya 11(1) ya Katiba ya Nchi ya mwaka 1977 imeweka haki ya Wazee kupata msaada wa mahitaji ya lazima kama vile chakula, matibabu na kadhalika kutoka kwa jamii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wazee wasiojiweza na wasio na msada toka kwa ndugu zao wapate mahitaji yao ya lazima ya kila siku kama chakula, malazi, matibabu na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanaluanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mipango mingi katika kuwahudumia wazee wasiojiweza na baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

1. Kwa kuzingatia masharti ya sheria ya matunzo ya watu wasiojiweza Na. 3 ya mwaka 1982, Serikali imeweka utaraibu wa kuwatumia wazee wasiojiweza na ambao wamethibitika kuwa hawana ndugu wa kuwatumia katika makazi maalum ya wazee. Yapo makazi 17 ambayo yanaendeshwa moja kwa moja an Serikali na makazi 24 yanayoendeshwa na wakala wa hiyari katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwatumia wazee wasiojiweza.

2. Wizara kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii hutoa misaada kibinaadamu ikiwa ni pamoja na fedha za kujikimu kwa watu wasiojiweza wakiwemo wazee na kuwasaidia kuanzisha miradi midogo midogo ili kuwawezesha kujimudu kimaisha.

3. Serikali kwa kuzingatia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2010 sura ya 8 aya namba 209(a) inakusudia kutunga sheria itakayotawala utoaji wa haki ya matibabu bure kwa wazee wasiojiweza katika vituo vya matibabu huko wanakoishi. Chini ya sheria hiyo, kila mzee atapatiwa kitambulisho ili kuwawezesha kutiwa bila usumbufu wowote.

4. Serikali inafanya maandalizi ya mfumo wa kinga ya jamii, *social protection frame work*. Mfumo ambao utaangalia mahitaji ya msingi ya makundi yanayoishi katika mazingira magumu zaidi wakiwemo wazee wasiojiweza.

5. Wizara inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya wazee yanajumuishwa katika mipango yao ya maendeleo ya Halmashauri hizo.

Hata hivyo, sera ya Taifa ya wazee imesisitiza kuwa ni muhimu wazee kutunzwa katika jamii na familia zao na kuainisha kuwa matunzo katika makazi na taasis ni hatua ya mwisho kabisa baada ya kubainika kuwa mzee hajiwezi kabisa kiafya na havezi kumudu maisha yake mwenyewe na hana mtu wa kumtunza.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwanza linahusiana na ile misaada ya kibinaadamu ambayo inatolewa na Serikali, lakini ambayo haijaenezwa Tanzania nzima. Je, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi na wakati mrefu ili misaada hii ya kibinaadamu iwafikie wazee wote wa Tanzania ambao hawajiwezi?

(ii) Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna mpango wa kinga ya jamii ambao unaandaliwa na Serikali. Je, mpango huu ambao unaitwa mfumo wa kinga ya jamii utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Bukombe, jina lako ni gumu naomba nisilikosee, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza anataka kujua hii misaada ya kibinaadamu. Serikali ina mipango ili misaada hii iweze kuwafikia wazee wote.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ninavyozungumza kuna mchakato wa mpango wa majaribio unaofanywa na shirika la *TASAF* pamoja na *Help Age International*. Mpango huo unafanyika katika Wilaya ya Bahi na Chamwino. Wanaangalia namna ambavyo tutatengeneza mfumo wa kuweza kuwasaidia wazee waweze kujisaidia wenyewe wale ambao wana uwezo na wale ambao hawana uwezo tuangalie namna ambavyo tutawasaidia wale ambao wanawategemea waweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa majaribio bado unaendelea, utakapokamilika nafikiri tutafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba umefanikiwa ama haukufanikiwa. Kama haukufanikiwa tutafanya nini ili tuweze kuona kwamba wazee wote wanafikiwa. Lakini kwa sasa hivi kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya tuna mpango wa kuhakikisha kwamba wanafika mpaka kwenye ngazi ya Kata basi wazee wanasikilizwa na pale ambapo hawana chakula, hawana nyumba wanasaidiwa kupitia Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua huu mpango wa kinga ya jamii utamalizika lini. Huu mpango unatayarishwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Sisi tunaweka *input* ndani yake tu, mimi nina amini kwamba huu mpango utakapokamilika, Waziri mwenye dhamana ya Wizara husika, ataliarifu Bunge lako Tukufu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilitaka kufahamu tu kwa sababu ni haki ya kisera lakini pia ya Kikatiba wazee wetu kutunzwa lakini nizungumzie tu kwenye eneo la afya. Hivi Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka dirisha la kuhudumia wazee ambapo ipo sehemu zingine lakini sehemu zingine haipo katika nchi nzima ili wazee waweze kupata urahisi wa huduma hiyo ya afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza sasa hivi maelekezo na maagizo ni kwamba kila hospitali inatakiwa kuwa na dirisha la wazee. Naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika hospitali yetu ya Mkoa wa Dodoma kwa sasa hivi kuna dirisha maalum. Kuna dakitari maalum ambaye anaambatana na pale ambako wanatoa huduma za *National Health Insurance* kwa ajili ya wazee.

Kuna Afisa Ustawii wa Jamii ambaye anawasikiliza na kuwapa maelekezo wazee. Waheshimiwa Wabunge naomba niwakaribishe mkaone. Nendeni wakati wowote tu wala msitoe taarifa mtakuta huduma hizo zipo na wazee wanazifurahia. (*Makofi*)

Na. 71

### **Kushuka kwa Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika**

**MHE. JOSEPH ROMANI SELASINI** aliuliza:-

Inavyoonekana kiwango cha kujua kusoma na kuandika kimeshuka sana nchini kwa rika zote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kufufua elimu ya watu wazima ili kuiwezesha jamii kujisomea na kuweza kutumia utandawazi ipasavyo, hata kupata habari kupitia vitabu, magazeti na majarida mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Romani Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa kiwango cha kujua kusoma na kuandika nchini kimeshuka kutoka asilimia 89.4 kwa mwaka 1986 hadi kufikia asilimia 69 kwa mwaka 2010 miongoni mwa vijana na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu mbalimbali zinazosababisha kutokujua kusoma na kuandika zikiwemo ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya kuendesha shughuli za elimu ya watu wazima na kukosekana kwa juhudi za pamoja katika kuhimiza na kutekeleza mipango ya elimu ya watu wazima baina ya viongozi wa Serikali, Asasi za Serikali, Vyama vya Siasa, Mashirika ya Dini na Asasi zisizo za Serikali kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, ili kufufua elimu ya watu wazima na kuiwezesha jamii kujisomea na kutumia utandawazi ipasavyo, Serikali ina mipango ifuatavyo:-

Kwanza, imeanzisha tena Idara ya elimu ya watu wazima katika ngazi ya Wizara ili iweze kuratibu kwa ukamilifu utekelezaji wa sera ya elimu ya watu wazima.

Kupitia Idara hii Serikali imeteua Afisa Elimu ya watu wazima katika kila Mkoa ili aweze kushauri uongozi wa Mkoa kuhusu utekelezaji wa mipango ya Elimu ya watu wazima na kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo katika Halmashauri zote za Mkoa wake.

Pili, Serikali kupitia mpango wa elimu ya msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA), itaendelea kutoa elimu ya msingi kwa watoto wenye umri wa kuwa shuleni lakini hawapo shuleni kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa vijana na watu wazima kupitia mpango wa uwiano kati ya elimu ya watu wazima na jamii (MUKEJA) ambapo wananchi watapatiwa elimu ya kusoma na kuandika katika vikundi vyao vya uzalishaji mali.

Tatu, Serikali itaimarisha vituo vya Uchapaji vya Kanda vya Magazeti Vijijini, ili viweze kuanza tena kuchapa magazeti yatakayosomwa na wananchi wa Vijijini.

Nne, Serikali ya Tanzania pia inashirikiana na Serikali ya Cuba kuandaa programu ya kutoa elimu kwa vijana na watu wazima wasiojua kusoma na kuandika. Programu hii inategemea kuanza kutekelezwa mwezi Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, pia juhudi za pamoja zinahitajika ili kuwawezesha vijana na watu wazima kujua kuandika, kusoma na kuhesabu. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH ROMANI SELASINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa tabia ya kujisomea inashuka sana miongoni mwa wananchi na kwa kuwa maktaba za elimu ya watu wazima ambazo zilikuwepo kati ya miaka sabini na themanini na sasa hazipo tena na huenda ndiyo zinazochangia kwa kiasi kikubwa wananchi kusahau kusoma na kuandika. Je, Serikali iko tayari sasa kwa kushirikiana na Halmashauri kurejesha maktaba hizo ili wananchi wapate fursa ya kusoma majarida na vitabu mbalimbali hasa vile ambavyo vinahusu miongozo na sera mbalimbali za Serikali?

(ii) Kwa kuwa ikama ya elimu ya watu wazima ilikuwa ni kuanzia Wizarani mpaka kwenye Kata na kwa kuwa Mratibu wa elimu Kata ndiye hasa alikuwa anajihusisha na uhamasishaji wa elimu ya watu wazima, lakini sasa anahusika tu na kuhamasisha elimu ya msingi. Je, Serikali iko tayari sasa kuwatumia Waratibu wa Elimu Kata kwa ajili ya uhamasishaji ya Elimu ya Watu Wazima kama ilivyokuwa hapo zamani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Joseph Romani Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Maktaba za Kata miaka ya 1970 mpaka 1980 zilikuwepo na kwa sasa tunataka tuboreshe mpango wa elimu ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, nadhani mimi nilichukue kama ni ushauri kwa ajili ya kwenda kuboresha hizo Maktaba za Kata. Nashukuru sana kwa ushauri wako.

Lakini pili, namna ambavyo mratibu Kata wa elimu anavyoweza kutumika katika programu yetu hii ya elimu ya watu wazima. Mheshimiwa Mbunge tunavyosema Mratibu Kata wa Elimu anashughulikia masuala yote ya elimu katika Kata. Kwa hiyo, hata tunapoanzisha au kufufua hii programu ya elimu ya watu wazima, huyu ndiyo *coordinator* Mkuu upande wa Vijiji na hata Kata katika maeneo yake. Kwa hiyo, tutamtumia ipasavyo.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa jitihada za kujisomea za aina hiyo zimekuwa zikiendelea kwa watu wazima wanaofanya mitihani kama *Private Candidates* na wale wanao *re-seat*.

Je, Serikali haiona sasa kuwa ni vyema kuwaunganishia *grade* wale watahiniwa wanapozipata katika miaka tofautitofauti ili wawe na cheti kimoja kinachowaruhusu kuendelea na masomo na kuhamasisha zaidi tabia ya kujisomea?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge nataka tu kusema kwamba masuala ya elimu ni mapana sana na haya yote ambayo angalau yanakuja kama ni ushauri kwa sababu wote tumeshaona kwamba kiwango cha elimu nchini ni kidogo, mimi naomba ili nilichukue kama ushauri tuwasiliane na watu la Baraza la mitihani kwa sababu wao ndiyo wenye dhamana kubwa ya kuanza kuunganisha vyeti. Naomba nilichukue kama ushauri.

Na. 72

**Serikali Kupatia Ufumbuzi Changamoto za  
Wanafunzi wa Vyuo Vikuu.**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Moja ya changamoto kubwa zinazowakabili wanafunzi wa Vyuo Vikuu hapa nchini ni kutopata mikopo yao kwa wakati muafaka licha ya Serikali kujua Vyuo hivyo vinafunguliwa lini na udahili ukoje.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu changamoto za wanafunzi wa Vyuo Vikuu yanapatiwa ufumbuzi mapema ili kuondoa usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ambapo idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo imeongezeka kutoka wanafunzi 42,729 mwaka 2005/2006 hadi wanafunzi 92,542 mwaka 2010/2011 na fedha za ukopeshaji kuongezaka toka Sh. 56.1 bilioni mwaka 2005/2006 hadi Sh. 237.8 bilioni mwaka 2010/2011, bado kuna changamoto nyingi katika utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tume maalum ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, imeteuliwa na imeanza kazi tarehe 14 Februari, 2011 kupitia utendaji wa Bodi ya Mikopo na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua. Aidha, Tume hii inatakiwa iwasilishe mapendekezo na taarifa yake yote kwa ujumla kabla ya tarehe 15 Aprili, 2011.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wanavyuo wamekuwa wakiangaika kufuatilia mikopo mbali na vyuo vyao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Ofisi za Kanda kwa ajili ya mikopo ya wanavyuo kwa Kanda hapa Tanzania?

(b) Kwa kuwa baadhi ya uongozi wa vyuo umeonekana kuwa ni chanzo cha migogoro inayopelekea wanavyuo kugoma. Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha tabia hii ili wanavyuo wasome kwa amani na utulivu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuanzisha Ofisi za Kanda, zitakazokuwa zinashughulikia Bodi ya Mikopo huko Mikoani. Naomba na mimi nilichukue vile vile kama ushauri japo hapa Dodoma tayari tuna Ofisi kwa sababu tuliona Chuo Kikuu cha Dodoma kina wanafunzi wengi sana.

Lakini vile vile Serikali inajipanga katika kuboresha Muungano, tuweze kujenga Ofisi kule Zanzibar.

Swali la pili, kuhusu migogoro ya wanafunzi pamoja na kero zao, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tayari Mheshimiwa Rais ameshaunda Tume na hiyo Tume ndiyo itakayoangalia mambo yote na matatizo jinsi yalivyojitokeza *and then* watatuletea mapendekezo tuweze kuona ni hatua gani za kuchukua.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika angalau kwa kuniona leo. Kwa kuwa Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi na migogoro hii imekuwa ya muda mrefu na kwa vile Rais ameshaunda Tume na

imeanza kazi jana. Je, Serikali iko tayari au Waziri yuko tayari kutusaidia, hii Tume ikaja ikaonana na Wabunge wote kwa kusaidia michango muhimu ambayo ni namna gani ya kutatua matatizo haya yaliyoingia? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, aliyeunda Tume ni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na nadhani hata mapendekezo yote yatakwenda kwake *and then* yatakuja Wizara ya Elimu tutayaangalia na mapendekezo kama kuna haja ya kuleta Bungeni tutaleta na kwa sababu nia ni kujenga ili wanafunzi wetu wasihangaikete tena.

Kwa hiyo, mimi nataka vile vile nilichukue, tunajaribu kuwasiliana na Tume ili tuweze kuona kama kuna mambo mengine ya msingi ambayo ni ya kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wakaweza kutushauri ili tuweze kuendesha elimu yetu vizuri hapa nchini. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, hata Kamati inayohusika inaweza kutafuta habari hizo, siyo lazima wote sisi. Tunaenda Wizara nyingine, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 73

### **Kuimarisha Soko la Mbaazi Ndani na Nje ya Nchi**

**MHE. PAULINA P. GEKUL** aliuliza:-

Mbaazi ni zao la kibiashara kwa wakazi wengi wa Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha soko la Mbaazi ndani na nje ya nchi ili kuwanufaisha kiuchumi wakulima wa zao hilo Mkoani Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paulina Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Babati ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Manyara zinazolima zao la Mbaazi kwa wingi nchini na kulifanya zao hilo kujipatia umaarufu katika soko la nchi za Asia hususan India.

Juhudi zinazofanywa na Serikali kuboresha soko la Mbaazi nchini ni pamoja na kuhamasisha wadau kupitia sera mbalimbali kama vile tamko la Kilimo Kwanza, mkakati wa kukuza mauzo nje ya nchi, kuanzishwa kwa sera ya masoko ya mazao ya kilimo na mkakati wa kutekeleza sera hiyo na uimarishaji wa soko la ndani la mazao ya kulima nchini kwa kuimarisha vikundi vya wakulima, ushirika, umoja wa wakulima na hata mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, kwa Sheria Na.19 ya Mwaka 2009 (*The Cereals and Other Produce Act,2009*). Bodi hii ambayo imezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika jana tarehe 14 Februari, 2011 pamoja na majukumu mengine itafanya biashara ya mazao ndani na nje ya nchi na kuhakikisha kwamba mkulima anapata soko la uhakika na kumwongezea bei.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa taarifa muhimu kwa wadau hususan taarifa ya bei za mazao na mahitaji katika masoko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Juhudi ambazo zitasaidia kupanua wigo wa soko la Mbaazi.

Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wadau juu ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, kuwekesha katika usindikaji wa mazao ya kilimo (*Agro-Processing*) kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao hayo ikiwa ni pamoja na zao la mbaazi.

Mheshimiwa Spika, elimu inaendelea kutolewa kwa wakulima wakiwemo wale wa mbaazi kujiunga katika vikundi au vyama vya ushirika ili kurahisisha upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani utakaosaidia kuongeza ubora na uzalishaji wenye tija hali itakayosaidia kukifanya kilimo cha mbaazi kuwa cha kiushindani zaidi katika soko la ndani na nje ya nchi.

Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kushirikiana na Bodi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala inatarajia kuanzisha mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika Wilaya za Karatu na Babati katika msimu wa mwaka 2011/2012.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Ahsante Mheshimiwa Spika kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa zao la mbaazi limekuwa ni tegemezi kubwa sana au zao linalotegemewa na wakulima wa Babati kama zao la biashara. Je, Serikali ipo tayari kuwapatia wakulima hao mbegu bora ili waweze kuongeza uzalisha wa zao hilo?

(b) Kwa kuwa mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa mipya iliyoanzishwa miaka ya 2000 na mikoa hii haina viwanda bado. Je, Serikali iko tayari kuanzisha kiwanda cha kutengeneza biskuti ili kuweza kutoa soko la ndani na la nje kwa wakulima wa zao hili la mbaazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, jana tulizungumza vizuri na Mheshimiwa Paulina, tulielewana vizuri tu na nilimshauri na naomba kabla sijatoka hapa nimemwandalia kijarida kwa ajili ya zao la mbaazi. Kijarida kitachomwelekeza namna ya kupata mbegu na namna ya kuhudumia zao hili mpaka lipate uthamani unaotakiwa. Naomba tuonane hapa ndani au nitampa mhudumu ampatie.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kiwanda, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, tumeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Bodi hii ni mahususi kwa ajili ya mazao yale ambayo hayana Bodi maalum na mbaazi ni mojawapo na moja ya kazi ya Bodi hii ni kuwashauri wakulima namna ya kupata masoko ndani na nje ya nchi.

Naomba tena nimwelekeze Mheshimiwa Paulina namna ya kuwasiliana na Bodi hii, Wizara ya Viwanda na Biashara na hata kituo chetu cha uwekezaji ili tujue namna ya kuwapata wawekezaji kwa ajili ya kufungua viwanda. Kwa sababu kimsingi Serikali haianzishi viwanda, hii ni kazi ya sekta binafsi.

Naomba Mheshimiwa Paulina tena kwa kuwa swali lake ni zuri sana basi tuonane kusudi nimwelekeze namna ya kuwasiliana na vyombo husika. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo Mheshimiwa Salum Khalfani Barway atauliza swali hili. Waheshimiwa kama mnataka kuuliza swali la nyongeza unasimama tu mara baada ya Waziri kujibu swali la msingi au swali lililotangulia. Mnasimama mimi nitamwita mwenyewe lakini nimeshawaona.

Na. 74

### **Mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

**MHE. SALUM K. BARWAY** aliuliza:-

Zao la korosho ni uti wa mgongo wa uchumi wa wakulima wa Mikoa ya Kusini, Tanga na Pwani lakini kumekuwa malalamiko mengi kuhusiana na utaratibu mzima stakabadhi ghalani kwa sababu hauwatendei haki wakulima, badala yake huenda kinyume na mfumo wa biashara huria:-

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kufanya marekebisho kuhusiana na utaratibu wa stakabadhi ghalani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfani Barway, Mbunge wa LIndi Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Bodi ya Korosho Tanzania, imekuwa ikifuatilia kwa karibu ufanisi wa mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani, ili kuhakikisha kuwa mfumo huo unafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani ya mwaka 2005 (*The Warehouse Receipts Act No. 10 of 2005*) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2006 (*Warehouse Regulations of 2006*).

Aidha, Sheria hiyo na Kanuni zake inasomwa pamoja na Sheria ya Tasnia ya Korosho (*Cashment Industry Act. 2009*), na Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003 (*Co-operative Act. of 2003*).

Kutokana na juhudi hizo mfumo wa Stakabadhi wa mazao ghalani umekuwa na mafanikio kwa wakulima wa korosho. Bei ya zao la korosho kwa wakulima imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 250/= kwa kilo mwaka 2006/2007 hadi shilingi 800/= kwa kilo katika mwaka 2009/2010.

Kutokana na mafanikio hayo, Serikali kwa sasa haina mpango wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutathmini changamoto zinazotokana na matumizi ya mfumo huo kwa lengo la kuendelea kuuboresha baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi wa mazao Ghalani unafuata utaratibu wa soko huria kwani wanunuzi hushindana sokoni kwa mtindo wa mnada. Mnunuzi anayetoa bei kubwa ndiye anayepata korodho na sio vinginevyo.

Kwa kufanya hivyo, tumeweza kwa miaka mitatu mfululizo, mwaka 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 kuhakikisha mkulima anapata bei ya haki kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya zao la korosho hapa nchini Tanzania.

**MHE. SALUM K. BARWAY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa bei ya dira hufanyika mara mbili kwa wakulima wa zao hilo la korosho. Je, si wakati muafaka kwa sasa kwa Serikali kuona kwamba malipo hayo ya awali kwa maana ya malipo ya kwanza na pili yakafanyika mara moja kuwawezesha wakulima wakamudu gharama zao za kilimo mapema wanapoandaa mashamba yao?

Pili, Mheshimiwa Spika, makato ambayo wakulima wanakatwa katika zao hilo ni makubwa na ni mengi wakati huo huo wakulima hao wanalazimika kulipia huduma muhimu za jamii kama elimu, afya na mambo mengine.

Je, Serikali haijaona umuhimu kwa sasa kuangalia upya mapato hayo ili kuwawezesha wakulima kufikia muafaka juu ya zao lao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kweli kama nilivyosema katika jibu la msingi bei dira ambayo tunaitoa ni bei ambayo mkulima anapata ili angalau iweze kumsaidia kukidhi yale mahitaji ya msingi wakati ule ana matarajio ya kupata zile bei zingine zinazoongezeka takriban mbili za ziada. Kwa mfano nimesema zimeongezeka mpaka sh. 800/= kutoka 250 mpaka 800/= kwa hicho siyo kiasi kidogo.

Sasa kinachofanyika ni kwamba ukisema wachukue fedha zote wampe kwa mkupuo itakuwa vigumu kwa sababu wakati huo bado kuna *process* nyingine ya kuuza



mazao hayo mpaka nje. Sasa wakati huo itakuwa ni vigumu kujua bei ni kiasi gani iliyoko katika soko kabla haijauzwa.

Mimi nadhani mfumo huu bado ninaona kwamba ni mzuri lakini nakubaliana naye kwa upande wa makato haya kwamba yako mambo fulani ambayo yamejitokeza kuna haja ya kuangalia kupunguza gharama fulani fulani ambazo zinamletea shida sana mkulima kwa mfano gharama za magunia, gharama za ushuru wa Wilaya, gharama za waendesha maghala yale. Hizi gharama kwa kweli tutakubaliana kwamba lazima tuangalie namna ya kuzipunguza kwa sababu mwisho wa siku inapunguza ile *take home* kwa mkulima.

Lakini kwa vyovyote vile mfumo huu mimi nataka niseme kwamba ni mfumo mzuri, kinachotakiwa ni kuangalia zile kasoro zinazotokana na hawa wanaotaka kuingia, ili mkulima asipate bei nzuri basi tuwadhibiti. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sababu moja inayomwezesha mkulima kupata bei nzuri ni kwa mazao hayo kuweza kuwa *processed* hapa nchini na kwa kuwa ukiangalia pamba ni asilimia 10 tu inakuwa *processed* hapa nchini. Korosho kama asilimia 30, Serikali kwa nini sasa hivi serikali haiweki kipaumbele kuhakikisha kwamba badala ya kusafirisha mali ghafi tukaanza kuzi-*process* katika viwanda vyetu ili wakulima wakapata bei nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali sasa hivi tumeweka mkazo kwa kuweka viwanda ndani ya nchi kwa ajili ya kusindika mazao hayo. Hata ukienda huko Kusini sasa hivi utaona viwanda vimeanza kuwekwa angalau kwa kiwango kidogo, lakini mwelekeo ni huo huo kuweka viwanda kwa ajili ya kusindika mazao yote si korosho tu. Hata mazao mengine.

Na. 75

### **Kusuasua kwa Mradi wa Maji wa World Bank**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Mradi wa maji wa *World Bank* ulioianza kwenye baadhi ya vijiji unasuasua, hasa uchimbaji wa visima virefu na maeneo mengi kuchimbwa bila kupata maji:-

Je, Serikali haioni kwamba, fedha nyingi zinapotea bila mafanikio na wananchi kuendelea kuteseka bila ya kuwa na maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi katika vijiji kumi umeanza. Katika jitihada za kuchimba visima vya maji, jumla ya visima 13 vimechimbwa katika vijiji vya Sinya, Mundarara, Longido, Mairowa, Orgira na Kiseriani. Kati ya hivyo, visima 6 katika vijiji vya Longido (2), Mairowa (1), Sinya (2) na Mundarara (1) vina maji ya kutosha ambapo visima 7 vilivyo katika vijiji vya Longido (2), Mairowa (1), Orgira (2) na Kiserian (1) havina maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika teknolojia ya kuchimba maji chini ya ardhi kwa maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na wilaya ya Longido, uwezekano wa kupata maji unategemea hali ya kijiolojia na kihaidrolojia ya maeneo ambako visima vitachimbwa. Aidha, upimaji wa maeneo ya kuchimba visima huwa hauonyeshi uwingi wa maji yaliyopo katika kisima kinachochimbwa. Upatikanaji wa maji hufahamika tu baada ya uchimbaji kufanyika. Hivyo uwezekano upo kupata maji, kupata maji kidogo au kukosa maji kabisa.

Kutokana na hali hiyo, katika utekelezaji wa programu ya maji katika miradi yenye visima kama vyanzo vya maji, visima vya majaribio vyenye kipenyo kidogo vinachimbwa kwanza na vinapoonekana kuwa vina maji ya kutosha visima husitishwa na haviendelezwi. Hivyo kupunguza gharama za uchimbaji kwa ujumla utaratibu huo ndiyo unatumika katika sehemu mbalimbali duniani.

Mwezi Desemba, 2010 utafiti zaidi ulifanyika katika maeneo mapya ya kuchimba visima kwenye vijiji vilivyokosa maji vya Mairowa, Orgira na Kiseriani. Halmashauri ya Wilaya inawasiliana na mkandarasi ili aende kuchimba visima katika maeneo husika.

Hivyo, uchimbaji wa visima katika baadhi ya vijiji katika wilaya ya Longido hausuisui bali unafanyika kwa makini kwa njia ambayo ina gharama nafuu kwa Serikali na fedha hazipotei bila mafanikio.

Kati ya miezi Julai 2007 na Juni 2009 miradi midogo yenye kuleta matokeo haraka ilijengwa katika vijiji vya Rosirwa, Tingatinga, Kitendeni, Mundarara, Mutale, Otopesi, Lundwa, Ngereyani, Nondoto, Orugira, Tanganye na Sinya na vinafanya kazi. Mradi katika kijiji Kimokua unaendelea kujengwa. Kati ya mwezi Juni, 2007 na Desemba 2010 jumla ya shilingi bilioni moja, tisini na tisa milioni mia mbili hamsini na mbili, mia sita themanini na saba, zimetumwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Aidha, mtaalam Mshauri anayeitwa Huward Humphrey Tanzania akishirikiana na Humphrey Tanzania akishirikiana Humphrey East Africa walijaliwa na walijajiriwa na Halmashauri tarehe 28 mwezi wa tano ili kusaidia Halmashauri kusanifu miradi katika vijiji 10. Vile vile tarehe 15 mwezi wa sita Halmashauri iliajiri Kampuni ya *Hydro Tech Tanzania* kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji mbalimbali nilivyovitaja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kumwuliza kwa kuwa visima vilivyochimbwa ambavyo

viko tayari na vimepatikana maji. Lakini haikuendelezwa je ni lini Serikali itaendeleza visima hivyo ili wananchi walioko katika maeneo haya wapate maji?

Swali la pili, kwa mji wa Longido ni mji ambao unakua kwa kasi sana, na wana tatizo la maji, maji wananunua kwa shilingi elfu moja kwa debe. Kwa hiyo, wananchi wanashindwa hata kujenga. Na kwa kuwa mji ule ulikuwa na mradi wa *Gravity* kutoka mlima Meru, je Serikali hawawezi wakafanya haraka sana hayo maji yakaletwa kutoka Mlima Meru ili wananchi kupata maji ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa jana Waziri wa Maji alitoa kauli hapa Bungeni kuhusu mradi mzima wa kuendeleza maji vijijini na katika visima vile ambavyo tumeweza kupata maji tutaendelea kuvikamilisha ili kusudi maji yaweze kupatikana.

Lakini maeneo mengine tunaendelea kupima vile vijiji kumi (10) vyote ambavyo tumeahidi kwamba vitafanyika ni lazima tupate maji kwa njia zozote zile.

Kuhusu swali la pili la nyongeza; Mji wa Longido, unapata maji kwa njia ya mtiririko. Asilimia 47 ya Wananchi wa pale wanapata maji na tutaendelea kutafuta vyanzo vingine ili tuongeze upatikanaji wa maji ili uweze kufikia mpaka asilimia 80 au asilimia 90 ili Wananchi wote wa Mji wa Longido waweze kupata maji.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi huu wa *World Bank* umesuasua kwa muda mrefu sana kama maelezo ya muuliza swali yanavyoonesha. Je, bado kuna uwezekano wa kufikiwa lengo la kusambaza maji katika vijiji kumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Telele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, inaonekana kama Mradi huu wa Maji wa Vijiji Kumi unachukua muda mrefu. Tukubaliane kwamba, kazi ya kutafiti kuweza kujua ni wapi maji yanapatikana ndiyo inayochukua muda mrefu, lakini tukishajua ni wapi maji yapo tunamaliza. Ndio maana tumesema kwamba, vijiji vingi na ile ripoti ya jana inaonesha hatua kubwa imeshafanyika katika utafiti. Sasa tunaingia awamu ya pili ya utekelezaji. Kwa hiyo, tutafikia lengo.

Na. 76

### **Utaratibu wa Kutega na Kuhifadhi Maji ya Mvua**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Sasa hivi Taifa linakabiliwa na upungufu mkubwa wa mahitaji ya maji kutokana na kuharibiwa kwa vyanzo vya maji kwenye maeneo mengi ya nchi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutengeneza sehemu maalum ya kuhifadhi maji ya mvua yanayoishia baharini, ambayo yangefaa kwa matumizi makubwa kama ya kusaidia nchi na jamii hata kwa upatikanaji wa umeme na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya uvunaji maji ya mvua inahusu kuinga maji yatokanayo na mvua kwa kutumia njia mbalimbali na kuyahifadhi katika miundombinu yake ili yatumike wakati yakihitajika hususan wakati wa kiangazi. Njia zinazotumika katika uvunaji wa maji ya mvua ni kwa kuinga maji ya mapaa ya nyumba na kuhifadhi maji kwenye magari ama makaro, kuchimba malambo, mabwawa madogo na makubwa, kuinga maji kwa kuweka matuta kwenye miteremko na makorongo.

Maji yanayohifadhiwa yanaweza kutumika kukidhi mahitaji mbalimbali ya maji. Mabwawa makubwa yanayokinga maji ya mito hutumika katika uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, katika Sura ya sita vifungu (f) na (g), inaelekeza ujenzi wa malambo na mabwawa nchini pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kwenye majengo ya Taasisi za Serikali na Zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi na Nyumba Binafsi za Kisasa Mijini na Vijijini. Ngazi mbalimbali za Serikali zina jukumu la kuhamasisha na kuratibu uendelezaji wa uvunaji wa maji ya mvua hapa nchini. Jukumu kubwa la uendelezaji lipo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, chini ya Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Maji, uvunaji wa maji ya mvua ni moja ya maeneo yanayoshughulikiwa chini ya Programu Ndogo ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira ili kutoa msukumo wa kuendeleza uvunaji wa maji ya mvua hapa nchini. Mifano ya uvunaji maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba ni Bukombe matanki 32, Kahama matanki 33 na Kishapu matanki 50. Vile vile, katika kila kijiji kwenye vijiji kumi vya Programu, kutajengwa matanki matatu ya mfano, yenye ujazo tofauti. Lengo ni Wananchi kuona na kuiga. Katika maeneo stahiki, mabwawa madogo na ya kati yatajengwa chini ya Programu hii, kutoa huduma ya maji kwa matumizi mbalimbali na hivyo kupunguza kero ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha Wananchi na kuiendeleza njia hii ya uvunaji maji katika maeneo yetu. Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inaendelea kuzishauri Halmashauri zote nchini, kuweka ujenzi wa mabwawa ya maji madogo na ya ukubwa wa

kati katika mipango yao kulingana na vipaumbele vyao. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri wa kitaalam kila unapohitajika.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa nchi yetu kwa sehemu kubwa imezungukwa na bahari; na kwa kuwa bahari katu haiwezi kukauka; na kwa kuwa kuna nchi nyingi tofauti zinatumia teknolojia ya kubadilisha maji ya bahari kuwa maji ya kawaida na kutumika katika matumizi mbalimbali hata ya umeme:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kutumia teknolojia kama hiyo ili kuyabadilisha maji ya bahari ambayo yametuzunguka hapa Tanzania kuwa katika maji ya kawaida na kutumika kwa matumizi ya kawaida na vile vile kutumika katika matumizi ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna nchi zinazotumia maji ya bahari kama sehemu ya rasilimali za maji, lakini teknolojia ile ni aghali sana. Mimi ninawaomba sana ndugu Wananchi mnaoniskiliza pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwanza, tuhifadhi vyanzo vya maji tulivyonavyo ili rasilimali hii iwe endelevu; tukishindwa kufanya hivyo, nchi ikiwa jangwa ndiyo tuanze kuangalia uwezekano wa ku-*desalinate*, maana ile *process* inaitwa *desalination*; yale maji ni ya chumvi na kuyaweka katika hali ambayo yanaweza yakatumika. Kwa hiyo, ninaomba sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Faida Bakar, kwa kuleta wazo hili na kuwa na uchungu wa kuweza kulinda rasilimali za maji. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo vingi vya maji vimekuwa vikiharibiwa kutokana na uharibifu wa mazingira na kusababisha *World Bank* wanaojitolea kusaidea kuchimba visima, kuchimba na kukosa maji kwa sababu ya uharibifu huo; kwa mfano, Kijiji cha Papa wamechimba mara tatu; na wataalamu wale wanapokwenda kukagua hawashirikiani na wenyeji; je, Serikali au Wizara ina mpango gani sasa wa kuielekeza *World Bank* ishirikiane na wenyeji kwa ajili ya kuwaelekeza vyanzo vya maji vilipo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tuna tatizo la kulinda vyanzo vya maji. Suala la kulinda vyanzo vya maji siyo la *World Bank*; ni suala letu sote sisi Wananchi na kila kijiji kimeunda Kamati za Maji na ndiyo kazi zake kubwa kuhakikisha kwamba, vyanzo vya maji vinalindwa, maana hiyo ndiyo itakayokuwa endelevu. *World Bank*

watatusaidia baada ya kuwa na chanzo kuweza kusambaza, kama chanzo cha maji hakuna; utasambaza kutoka wapi? Kwa hiyo, mimi ninadhani tuweke msisitizo katika ulindaji wa vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la maji linawaathiri sana Wanawake wa Tanzania kwa sababu ndiyo wadau hasa na watafutaji wa maji; na kwa kuwa taaluma hii haijafika katika Mkoa wetu wa Iringa; je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha taaluma hii katika Mkoa wetu wa Iringa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabati, anazungumzia kuhusu taaluma ya kuendeleza rasilimali za maji katika Mkoa wa Iringa; tutaendelea kuwaelimisha Wananchi wote namna ya kuhifadhi haya maeneo ambayo tumeshayachagua kwamba ndiyo vyanzo vya maji, kuweza kuvitambua na kuwaelekeza kila mahali Wananchi walipo na namna watakavyotunza. Kwa hiyo, tutaifanya kazi hiyo.

Na. 77

### **Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Urambo, Tabora – Nzega na Tabora - Manyoni**

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

Tatizo la miundombinu Mkoani Tabora linaonekana kuwa gumu sana kupatiwa ufumbuzi tangu tupate Uhuru:-

Je, Wananchi wa Tabora wawe na matumaini gani juu ya utekelezaji wa ahadi za muda mrefu za ujenzi wa Barabara ya Tabora – Urambo, Tabora – Nzega na Tabora – Manyoni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi tayari imesaini mikataba ya jumla ya shilingi bilioni 443.25 na Makandarasi mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa Barabara za Nzega – Tabora, Tabora – Urambo na Tabora – Nyahua kwa kiwango cha lami. Miradi yote inajengwa kwa kutumia fedha za ndani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Nzega – Puge (Km 56.1): Mkandarasi ni Kampuni ya *China Communications Construction Co. Ltd.* Gharama za Mradi ni shilingi bilioni 66.74 na muda wa utekelezaji ni miezi 27.

Mheshimiwa Spika, Puge – Tabora (Km 58.8): Mkandarasi ni Kampuni ya *China Sinohydro Corporation Ltd* ya China. Gharama za Mradi ni shilingi bilioni 62.74 na muda wa utekelezaji ni miezi 26.

Mheshimiwa Spika, Tabora – Ndono (Km 42): Mkandarasi ni Kampuni ya *China Henan International Group Co. Ltd* ya China. Gharama za Mradi ni shilingi bilioni 53.35 na muda wa utekelezaji ni miezi 20.

Mheshimiwa Spika, Ndono – Urambo (Km 51.98) Mkandarasi ni Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation Ltd* ya China. Gharama za Mradi ni shilingi bilioni 59.76 na muda wa utekelezaji ni miezi 24.

Mheshimiwa Spika, Matonyi – Itigi – Chaya (Km 89.4): Mkandarasi ni Kampuni ya *Sinohydro Corporation Ltd* ya China. Gharama za Mradi ni shilingi bilioni 109.64 na muda wa utekelezaji ni miezi 36.

Mheshimiwa Spika, Chaya – Nyahua (Km 90): Usanifu umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, Nyahua – Tabora (Km 85): Mkandarasi ni Kampuni ya *Chongqing Foreign Trade and Economic Cooperation (Group) Co. Ltd* ya China, gharama za Mradi ni shilingi bilioni 93.40 na muda wa utekelezaji ni miezi 36.

Mheshimiwa Spika, bila shaka Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Tabora, watakubaliana na mimi kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, imechukua hatua kubwa katika kukabiliana na changamoto za miundombinu ya barabara Mkoani Tabora.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa gharama zilizotajwa hapa ni kubwa na Mradi huu ni muhimu kwa Wananchi wa Tabora. Je, Serikali inahakikisha kwamba Makandarasi hawa watalipwa kwa wakati unaotakikana ili Miradi hii isikwame tena ikawa ni hasara na usumbufu kwa Wananchi wa Tabora?

(ii) Nataka kujua Miradi hii itanza kutekelezwa lini kwa sababu sasa hivi ni kweli nimewaona wako Tabora lakini hawajaanza kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nimhakikishie kwamba, Makandarasi wote tayari wamekabidhiwa rasmi maeneo yao ya kazi na wako kwenye kipindi cha maandalizi, tunaita *mobilisation*. Pili, Mradi kweli ni mkubwa lakini siyo mkubwa pekee, tunayo Miradi mingi mikubwa ya aina hiyo inayoendelea kila sehemu Tanzania. Nininamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wakandarasi watalipwa na tutaumaliza huu Mradi na ndiyo azma ya Serikali hii ya Awamu ya Nne.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kujua kitu kidogo tu ambacho mwuliza swali la msingi amekiuliza. Tungependa kujua ni lini Miradi hii itaanza maana ametamka tu miezi; *exactly* ni lini inaanza ili tuweze kufuatilia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nimjibu Mheshimiwa Sakaya, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimesema Makandarasi wote tayari wapo kwenye *site*; sasa sijui waanze kwa kitu gani? Tayari wapo kwenye *site* na kazi imeanza. Ninataka niwahakikishie Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, baada ya muda si mrefu tukimaliza hili Bunge, mimi au Mheshimiwa Waziri, tutakuja Tabora kuhakikisha Makandarasi wapo kazini.

Na. 78

### **Athari Zilizotokana na Upanuzi wa Uwanja wa Ndege Bukoba**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Kazi ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege Bukoba imelazimu kuvunja miamba ya mawe kwa kutumia baruti ambayo imesababisha athari na hasara kubwa ya nyufa kubwa kwenye nyumba za watu zilizoko karibu na maeneo ya uwanja huo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya kufanya tathmini ya uharibifu uliotokana na ulipuaji wa miamba kwenye nyumba za wahusika na katika kuwalipa fidia?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzihamisha Shule za Msingi za Tumaini na Zamzama zilizoko pembezoni mwa uwanja huo ambazo zimeathiriwa sana na ulipuaji wa miamba hiyo ambao unaleta hofu kubwa kwa usalama wa watoto na walimu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leos Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ilifanya tathmini kuhusu upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba ikiwa ni pamoja na



kuzitambua athari za upanuzi wa Kiwanja kwa mazingira na kupata kibali cha upanuzi kutoka Baraza la Mazingira la Taifa (*NEMC*). Katika tathmini hiyo, nyumba na mazao yaliyokuwa jirani na kiwanja yalitathminiwa na malipo kufanywa kwa wahusika kulingana na Sheria za Uthamini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha upanuzi wa kiwanja ambao mchakato wake ulihusisha ulipuaji wa miamba, Serikali itafanya tathmini ya uharibifu uliotokea kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika ngazi ya Mkoa na Taifa. Tathmini hiyo itahusisha pia Shule za Msingi za Tumaini na Zamzama, kuona kama zitalazimika kuhamishwa au la; na matokeo ya tathmini hiyo yatafanywa kazi na Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Waziri wa Uchukuzi amekiri kwamba kuna athari ambazo zimejitokeza baada ya ukamilishaji wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege katika Manispaa ya Bukoba. Je, kupitia Bunge hili anawaeleza Wananchi walioathirika hasa wa Kata ya Kashai; zoezi hili litaanza na kukamilika lini?

(ii) Kwa kuwa kumekuwepo na mpango wa kujenga uwanja mkubwa wa ndege katika eneo la Kajunguti, ambalo liko kilometa 30 kutoka Manispaa ya Mji wa Bukoba katika eneo la Wilaya ya Misenyi. Je, baada ya kuupanua Uwanja wa Bukoba Manispaa ambao kimsingi upo katika makazi ya watu; je, mpango huo sasa umefifia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rwamlaza, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi mbali na kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini pia ni Mbunge wa Jimbo hili. Chimbuko la suala hili na ninasikitika kusema kwamba, si uathirikaji wa watu ambao wapo katika eneo, lakini limekuwa ni jambo la kisiasa kwa muda mrefu. Ninadhani si jambo linalopendeza kutoa siasa Jimboni zikaja kuingia katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, hili suala tumelieleza. Ninapenda kujibu kwamba, athari zilizotokea ni za nyumba kubomoka, ambazo ni kupasuka nyufa pamoja na dari na mabati; na hiyo tathmini imefanyika na tuliwahakikishia Wananchi kwamba watalipwa na wengine wameshaanza kulipwa. Utaratibu umekuwepo na unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwanja wa Kajunguti, huu ni mkakati ambao umekuwepo kwa zaidi ya miaka 30. Tulichoamua, tumeona kwamba, bora tuanze na pale ambapo uwanja ulipo na hilo suala la Kajunguti ni la muda mrefu sana. Mimi niseme tu, hili linakuwa ni suala la kisiasa na wala si suala la Wananchi husika, kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo husika. (*Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyetoka kuzungumza hivi sasa ni Mbunge wa Bukoba Mjini na swali limeulizwa na Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) kutoka Bukoba Mjini. Kitendo cha Mbunge wa Bukoba Mjini kumshutumu Mbunge kwa kazi aliyoifanya ambayo kimsingi wanasaidiana kwamba ni kazi ya kisiasa ni kitendo ambacho hakikubaliki. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Mbunge wa Bukoba Mjini, ninamheshimu sana na anajua Balozi kwamba ninamheshimu sana, afute kauli kwamba Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza anahamishia siasa ndani ya Bunge, kwa sababu ni jukumu lao wote kufanya kazi ya kuhakikisha maendeleo ya Watu wa Bukoba na ni lazima washirikiane badala ya kuja kushutumiana ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto yuko sahihi, mimi nilikuwa najua anajibu kama Waziri, hizo habari za Majimbo nilikuwa sijazipata. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sehemu ya swali imejibiwa. Ningekuwa nimejua kama ni suala la huko kwao Bukoba nisingempa nafasi, lakini nadhani majibu ni sahihi. *(Makofi)*

**MHE. BERNARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imesikia kilio cha Wanakagera na Wabunge wengi ambao walikuwa wanalichangia hili suala na ikakubali na kuupanua Uwanja wa Ndege wa Bukoba na kwa hivi sasa ni mkubwa, kiasi ambacho kwa mara ya kwanza Jumamosi iliyopita ndege kubwa imeweza kutua kwenye Uwanja huo. Je, sasa ni lini Serikali itaukamilisha kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bernardetha Mushashu, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kazi ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba inafanywa katika awamu mbili; hii inahusu kupanua kiwanja ili kiweze kuhudumia ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 50, ambapo njia ya kurukia ambayo ni *runway* itaongezwa kwa urefu wa kutoka mita 1,040 hadi mita 1,430 kwa kiwango cha changarawe. Fedha za awamu hii, kiasi shilingi bilioni 4.7 zilitolewa na Serikali na kazi imekamilika, ambapo uzinduzi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ulifanyika tarehe 12 Februari, 2011.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili, hii itahusu kuweka lami kwenye njia ya kurukia na kushukia ndege na kujenga jengo la abiria. Kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Kwa sasa mchakato wa kupata mshauri na mkandarasi inaendelea. Mshauri atapatikana mwezi huu wa Februari 2011 na mkandarasi wa ujenzi anatarajiwa kupatikana mwezi Mei, 2011. Benki itatoa shilingi bilioni kumi kwa kazi hii.

Na. 79

**Udhibiti wa Bidhaa Bandia Nchini**

**MHE. SALIM HEMED HAMIS** aliuliza:-

Tanzania inatajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizokithiri katika uingizaji wa bidhaa bandia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza udhibiti wa uingizaji wa bidhaa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mbunge wa Chambani, naomba kutoa maelezo mafupi ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bidhaa bandia ni bidhaa iliyotengenezwa na inayouzwa kwa kuiga nembo ya bidhaa halisi kwa nia ya kuiuza kama bidhaa halisi. Kwa hiyo, kujishughulisha na bidhaa bandia au bidhaa feki ni vitendo vya udanganyifu, utapeli au upotoshaji wa makusudi kwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo haya, mwenye kumiliki nembo au alama ya bidhaa ndiye mwenye nafasi kubwa ya kutambua udanganyifu uliofanywa au unaofanywa katika bidhaa kuliko mtu mwingine yeyote. Kuna nyakati hata mwenye nembo hupata wakati mgumu kutambua udanganyifu uliotendelea kwenye bidhaa. Hali hiyo, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zinazoathiriwa na uingizaji wa bidhaa bandia kutokana na kwamba, utaalumu unaotumika kumpotosha mlaji juu ya uhalisia wa bidhaa kuwa ni wa hali ya juu hivyo, ni vigumu kubaini mara moja udanganyifu huu. Aidha, ukubwa wa nchi yetu na ukosefu wa uaminifu wa baadhi ya wafanyabiashara wanaotumia njia za panya vinachangia ongezeko la tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na uingizaji wa bidhaa bandia nchini, Wizara kupitia Tume ya Ushindani, inaendelea kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha Idara ya Kupambana na Bidhaa Bandia kwa kuongeza wakaguzi wa bidhaa katika bandari zetu na sehemu zote zinapoingia bidhaa na kutoa elimu kwa waagizaji wa bidhaa na asilimia 86 ya bidhaa zote zinazoingia hapa nchini zinapitia Bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Kushirikiana na wamiliki wa nembo na alama za bidhaa (*Brand Owners*) ili kupata taarifa za uingizaji wa bidhaa kutoka nje;

(iii) Kuimarisha utoaji Elimu kwa Umma juu ya namna ya kutambua bidhaa bandia; na

(iv) Kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kudhibiti uingizaji wa bidhaa bandia.

**MHE. SALIM HEMED HAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Miongoni mwa sababu ambazo zinatajwa kuwa zinaongeza bidhaa bandia nchini ni wafanyabiashara ambao wamejiingiza mno katika biashara hata zile za reja reja; jambo ambalo lingeweza kufanywa na Watanzania wazawa; je, Serikali ina mikakati gani ya kuwadhibiti wafanyakazi wa aina hii?

(ii) Upo ushahidi wa kutosha kuwa nchi nyingi duniani zinazofanya biashara na Wachina kwa mfano bidhaa zao zinakuwa ubora wa hali ya juu kwa sababu wenyewe wamejiwekea vigezo kutokana na viwanda vya ndani. Je, hapa Tanzania tumetumia vigezo gani; yaani bidhaa zetu zinapimwa na nini kwa kuwa hatuna viwanda vikubwa vyenye viwango ambavyo vimewekewa vigezo kwa bidhaa zetu za hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niseme na nirudie nilichokisema; ni kosa kuingiza bidhaa bandia nchini na wafanyabiashara wote ambao watachukua hatua hizo kwa makusudi wakijua au kwa kutokujua, bidhaa hizo zitakamatwa, zitaharibiwa na watachukuliwa hatua za kisheria.

Tume ya Ushindani imeendelea kukagua bidhaa hizi na kama nilivyosema, asilimia 76 ya bidhaa zote zinapita Bandari yetu ya Dar es Salaam na zingine katika bandari zingine na bidhaa hizi hadi kufikia mwaka jana, makontena 101 yalikuwa yamekaguliwa na kukamatwa na kuharibiwa na waliohusika wote walifikishwa katika vyombo vya sheria.

La pili, Serikali ya Tanzania inathamini na inaendelea kuisitiza kwamba, waagizaji wa bidhaa zote zinazotoka nje ya nchi lazima ziwe na ubora na lazima zikidhi viwango ambavyo vinatakiwa. Sasa kuna *TBS* ambayo inaangalia suala zima la ubora na inakagua ubora wa kila bidhaa hata zile ambazo zimezalishwa hapa ndani.

Tume ya Ushindani inaangalia ni jinsi gani mwagizaji wa bidhaa amefuata masharti ya bidhaa ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa bidhaa husika anafuata sheria na taratibu za kimataifa zinazolinda mlaji lakini pia zinazolinda ushindani ndani ya soko na tutaendelea kufanya hivyo na tutaendelea kuhakikisha sheria hii inalindwa.

Na. 80

### **Bei Kubwa ya Sukari - Wilaya ya Kilombero**

**MHE. REGIA ESTELATUS MTEMA** aliuliza:-

Kiwanda cha Kuzalisha Sukari cha Ilovo kiko Wilayani Kilombero; lakini pamoja na kuwepo kwa Kiwanda hicho, bei ya sukari iko juu sana ikilinganishwa na maeneo

mengine ambayo siyo wazalishaji wa sukari; kwa mfano kilo ya sukari Kilombero inauzwa kati ya shilingi 2,000 wakati kilo moja ya sukari kwa Dar es Salaam inauzwa kati ya 1,500 hadi shilingi 1,800:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hii hasa ikizingatiwa kuwa bidhaa nyingine kama chumvi, viberiti, unga (sembe) na kadhalika vina bei inayolingana nchini kote ukiacha gharama za usafirishaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wazalishaji wanapata huduma hiyo kwa gharama nafuu ili kuwapunguzia gharama watumiaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi, suala la bei ya sukari hutawaliwa na nguvu ya soko, ambapo hali ya mahitaji na ugavi ndiyo huamua bei ya bidhaa hiyo. Kiutaratibu, kiwanda huuzwa sukari yake kwa wafanyabiashara wa jumla ambao husambaza sukari hiyo nchi nzima kwa mawakala wake na hatimaye huuzwa kwa rejareja ili kumfikia mlaji wa mwisho. Mtiririko huo unasababisha bei ya sukari kutofautiana kati ya eneo moja na lingine.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa biashara ya sukari pamoja na bidhaa nyingine, hutoa kipaumbele kwa masoko makubwa ambayo ndiyo chanzo cha faida kwa wakulima na wenye viwanda. Hivyo, kiasi kikubwa cha sukari kinachozalishwa husafirishwa kwenda katika masoko makubwa kama Dar es Salaam na miji mingine mikubwa. Gharama za usafirishaji wa bidhaa hupungua kulingana na wingi wa mauzo unaoweza kufanywa katika kipindi kifupi na hivyo ni suala la kawaida kwa wafanyabiashara kupendelea na kutoa motisha ya bei katika masoko ambayo watauzwa kiasi kikubwa kwa muda mfupi. Aidha, napenda na naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge, avihamasishe Vyama vya Ushirika na Wafanyabiashara Wakubwa wa Wilaya ya Kilombero, kununua sukari kwa bei ya jumla kutoka kiwandani. Utaratibu huo utamuwezesha mlaji kufaidika na bei nafuu kama ilivyo katika maeneo mengine.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya utafiti na kujadiliana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na wenye viwanda ili kuweka utaratibu wa kuhakikisha Wananchi wa wilaya zinazozalisha sukari, wanapata sukari kwa bei ya kuridhisha. Aidha, Serikali imekuwa ikifanya juhudi za makusudi, kuendeleza na kukuza Sekta ya Sukari pamoja na Zao la Miwa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuondoa upungufu wa sukari nchini. Juhudi hizo ni kama zifuatazo:-

- (i) Bodi ya Sukari kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Sukari wameanzisha Kamati ya Mbegu Bora za Miwa (*Variety/Planting*)

*Materials Committee*), ambayo ina majukumu ya kusimamia uingizaji wa aina mpya za mbegu bora za miwa hapa nchini. Hii inawezesha makampuni na wakulima wa miwa wakiwemo wadogo, kuboresha uzalishaji.

- (ii) Kuanzisha mashamba ya pamoja (*Block Farming*) hasa katika Bonde la Kilombero ili kuwapunguzia wakulima wadogo gharama za ulimaji na uzalishaji wa miwa. Katika utaratibu huo, mashamba yanayopatikana hulimwa pamoja na kupewa huduma za mbolea na ugani ili kuongeza tija.
- (iii) Bodi ya Sukari kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali hasa Wakulima Wadogo wa Bonde la Kilombero, kuboresha mifumo ya barabara na madaraja ili kurahisisha na kupunguza gharama za usafirishaji wa miwa kwenda kiwandani na hatimaye bei ya sukari kwa ujumla. Jitihada hizo na nyinginezo, zinatarajiwa kupunguza gharama za uzalishaji wa miwa na sukari Tanzania na kupeleka kumpatia unafuu mtumiaji.

**MHE. REGIA ESTELATUS MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Ninakubaliana na majibu ya Naibu Waziri na amekiri wazi kwamba, bei ya sukari inategemeana na nguvu ya soko. Katika hali ya kawaida kabisa, kwa vyovyote vile sehemu kama Majiji kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na kwengineko ndiyo kutakuwa kuna soko kubwa. Hivyo, wale wazalishaji wote wa Kilombero lazima soko lao litakuwa chini. Katika hali ya kawaida kabisa, haingii akilini kwamba, watu ambao wanazalisha sukari, tununue bei ya sukari juu, eti kwa kigezo kwamba bei ya sukari inatokana na ukubwa wa soko.

(i) Je, Serikali haioni sasa iko sababu ya muhimu ya kurekebisha sera hii ili wale watu ambao wanazalisha wanunue kwa bei ya chini halafu hao wengine kulingana na nguvu zao za soko wanunue kwa bei hiyo? (*Makofi*)

(ii) Ningependa kuuliza kwa Mheshimwia Naibu Waziri kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kwa Wafanyakazi hasa wa chini wa Kiwanda hiki cha Kilombero kuhusiana na haki zao za msingi kama Wafanyakazi. Je, Serikali haioni sasa wakati muafaka umefika kuingilia kati ili wafanyakazi hao wa chini wapate haki zao zote kama wafanyakazi kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara yeyote Tanzania ikiwa ni pamoja na Wafanyabiashara wa Kilombero, wanaruhusiwa kwenda kiwandani na kununua sukari

kwa bei ya jumla na kama wakinunua kwa bei ya jumla moja kwa moja inampunguzia sana mlaji na mtumiaji wa pale Kilombero.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, wana duka lao la jumla na bei ya sukari kwa kilo ni shilingi 1,450, ambayo iko chini ya kiwango cha bei ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wafanyakazi katika viwanda vyetu ikiwa ni pamoja na kile cha Kilombero, wana haki ya msingi ya kulindwa, haki ya msingi ya usalama wao wakiwa kazini, haki msingi ya maslahi na mafao ambayo wanastahili kupata kwa mujibu wa sheria. Mimi ninasisitiza kwamba, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba, Sheria za Kazi zinazohusika zinafuatwa wakati wote.

**SPIKA:** Ahsante. Muda wa maswali umekwisha, tumekopa dakika tano lakini zilitumika zile za kuwasilisha Hati, kwa hiyo, zimetumika kujibu swali.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa saba na nusu mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Januari Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na kikao cha dharura cha Kamati kuanzia saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement*, bila shaka ni hapa hapa chini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahamoud Mгимwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 227; hapa tutakuwa na uchaguzi saa 5.00, kwa hiyo haiwezekani; ninawashauri kwamba, mkutane saa saba katika Ukumbi Namba 227 kwa sababu ya uchaguzi hapa; kwa hiyo, mtakutana saa saba.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao leo hii na yeye amesema saa 5.30, mimi nasema hapana ni saa 7.00. Kikao kitafanyika kwenye Ukumbi Namba 219, ghorofa ya pili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Msekwa B.

Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM, Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa CCM kuwa, leo kutakuwa na kikao kuanzia saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa na mwingine alisema pia Ukumbi wa Msekwa.

Kamati ya Mheshimiwa Edward N. Lowassa, labda mkaangalie pale, hii ni Kamati ndogo kuliko wale wengine; mtajuana wenyewe namna ya kuweza kupishana maeneo ya kukutania.

Halafu nina tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Said Nkumba, anaomba niwape taarifa Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, wakutane leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 133, *Wing C*.

Mwisho wa matangazo, Katibu kwa shughuli inayofuata.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Hali ya Umeme Nchini na Utekelezaji wa Miradi Yake**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo yako uliyoyotoa tarehe 11 Februari, 2011 kwa Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa majibu ya maswali ya nyongeza ya Swali Namba 39 na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni Namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Hali ya Umeme Nchini na utekelezaji wa Miradi ya Umeme katika kipindi kifupi na cha kati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwezo halisi wa mitambo yote ya kuzalisha umeme, yaani *Install Capacity* katika Gridi ya Taifa ni *megawatt* 1006. Mitambo ya maji ikiwa na uwezo wa *megawatt* 561 na mitambo ya gesi ya asili na mafuta ikiwa na uwezo wa *megawatt* 445. Kutokana na sababu mbalimbali za kiufundi na umri wa mitambo, uwezo wa kuzalisha umeme hapa nchini katika mfumo wa Gridi ya Taifa bila kuwepo mgawo wa umeme ni *megawatt* 935, ambapo *megawatt* 523 ambayo ni sawa na 56% hutokana na maji, *megawatt* 322 ambayo ni sawasawa na 34.4% hutokana na gesi ya asili na *megawatt* 60 ambayo ni sawa na 9.6% hutokana na mafuta mazito.

Kina cha maji katika Bwawa muhimu la Mtera kufikia tarehe 14 Februari, 2011 kilikuwa kimeshuka hadi kufikia mita 691.31 juu ya usawa wa Bahari na kwa leo kina kimefikia mita 691.30, hii ikiwa ni mita 1.31 hadi juzi tu juu ya kina cha chini kinachoweza kuruhusu uzalishaji wa umeme katika Bwawa hilo ambacho ni mita 690. Kutokana na hali hii ya uhaba wa maji, kwa sasa mitambo ya maji inazalisha wastani wa *megawatt* 180 tu wakati mitambo ya mafuta na gesi ya asili ikizalisha *megawatt* 290. Hii inafanya jumla ya umeme wote unaopatikana kwenye Gridi ya Taifa kuwa wastani wa *megawatt* 470 tu, ambayo ni 67% tu ya mahitaji ya wastani wa umeme au 57% tu ya mahitaji ya juu katika Gridi ya Taifa na kiwango cha juu kabisa cha mahitaji ya umeme ni *megawatt* 533 kwa sasa. Hii inaleta upungufu wa wastani wa *megawatt* 230 kwenye Gridi ya Taifa, upungufu huu ndiyo unaosababisha mgawo wa umeme unaendelea kwa sasa nchini. Serikali imenunua mafuta mazito ya kuendesha mtambo wa IPTL ili kuzalisha *megawatt* 80 kwa siku kutoka *megawatt* 10 kwa siku kama ilivyokuwa awali kabla ya kununua mafuta.



Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme nchini yanaongezeka kwa kasi ya wastani wa kati ya *megawatt* 80 hadi 120 kwa mwaka. Kasi ya uwekezaji katika miradi ya kuzalisha umeme imekuwa haimudu ongezeko hili, kiasi kwamba, mfumo wa uzalishaji umeme unaendeshwa pasipokuwa na umeme wa akiba, yaani *reserve margin*. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mgawo wa umeme wa mara kwa mara hata itokeapo hitilafu kidogo tu kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa. Pamoja na upungufu wa maji katika mabwawa yetu, kutofanyika uwekezaji wa kutosha katika Miradi ya Uzalishaji wa Umeme katika kipindi kirefu hususan kipindi kati ya mwaka 1997 hadi 2005, ambapo Shirika la Umeme TANESCO liliwekwa chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma, yaani *Public Sector Reform Commission* ikisubiri kubinafsishwa ni moja ya sababu zilizosababisha uwezo wa mfumo wa Gridi ya Taifa kuzidiwa na mahitaji ya leo hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, chini ya uendeshaji, yaani *Management Contract* wa *NET Group Solution*, mwaka 2004 hadi 2006 hapakuwa na uwekezaji kwenye miundombinu na hivyo kufanya upatikanaji wa umeme kutokuwa wa kuaminika kutokana na uchakavu wa miundombinu hiyo. Pamoja na kutokuwa na uwekezaji wa kukidhi mahitaji ya sekta, upatikanaji wa Nishati ya Umeme katika mfumo wa Gridi ya Taifa pia umekuwa ukiathiriwa na uhaba wa mvua kwa kipindi kirefu. Kwa mfano, mwaka 2006 uzalishaji wa umeme uliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na uhaba wa mvua katika nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2003 hadi mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, uzalishaji wa umeme katika vituo vinavyotumia nguvu za maji ulishuka kwa zaidi ya 60% baada ya kina cha maji katika Bwawa la Mtera kushuka chini ya kina cha chini cha mita 690 juu ya usawa wa Bahari.

Upungufu mkubwa wa maji kwenye mabwawa ya kuhifadhia maji ya kuzalishia umeme ulilazimisha TANESCO kutoa umeme kwa mgawo katika Mikoa yote iliyounganishwa kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Serikali ilichukua hatua za dharura zifuatazo: Kwanza, kukodisha mitambo yenye uwezo wa kuzalisha *megawatt* 185 kutoka kwa Kampuni za *Richmond* na baadaye *Dowans megawatt* 105, *Arstom Parentos megawatt* 40 na *Aggreko megawatt* 40.

Pili, kununua na kujenga mitambo ya kudumu ya kuzalisha umeme wa *megawatt* 145 ambapo Ubungo ilifungwa mitambo ya *megawatt* 100 na Tegeta *megawatt* 45 yote ikitumia gesi ya asili.

Zaidi ya hapo, Serikali ilichukua tahadhali ya kuzuia mgawo usijirudie tena kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kuhamasisha uzalishaji umeme wa *megawatt* 200 kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira na pili kuhamasisha uzalishaji wa *megawatt* 300 kwa kutumia gesi asilia ya Mnazi Bay Mtwara.

Miradi hii ambayo ilitarajia kuanza uzalishaji kabla ya mwisho wa mwaka 2010, haikutekelezwa kama ilivyopangwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mdororo wa uchumi duniani mwaka 2008 ulioathiri Mradi wa Umeme wa Mtwara ambapo mwekezaji alilazimika kuahirisha uendelezaji wa Mradi huo. Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kiwira ulisitishwa kufuatia dosari zilizojitokeza wakati wa ubinafsishwaji wa mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa umeme huleta hasara kubwa kiuchumi na usumbufu mkubwa kwa jamii, tathmini kuhusu athari za mgawo wa umeme kwa mwaka 2006 ilionesha kwamba, Serikali ilipata hasara ya Dola za Marekani milioni 331,309 kutokana na TANESCO kutokutoa huduma ya umeme ya jumla ya *unit* milioni 287,539,296.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa umeme ulijirudia tena mwaka 2009 katika miezi ya Septemba hadi Novemba ambapo takriban *megawatt* 160 zilikosekana kwenye mfumo wa gridi kutokana na upungufu wa maji katika mabwawa ya kuhifadhia maji ya kuzalishia umeme pamoja na kuharibika kwa mitambo ya TANESCO na SONGAS kwa wakati mmoja.

Katika kipindi cha mwishoni mwa mwezi Desemba, 2010 na Januari mwaka huu wa 2011, upungufu uliongezeka kutoka na matatizo ya kiufundi katika moja ya visima vya gesi huko Songosongo Kisiwani, pamoja na matengenezo ya mitambo ya umeme wa gesi Dar es Salaam. Aidha, kwa sasa matatizo hayo yamepatiwa ufumbuzi na mitambo inafanya kazi vizuri, Serikali ilichukua hatua za haraka kwa kupendekeza mitambo ya IPTL itumike kufua umeme kwa mkataba kwa kipindi cha mpito kwa miezi sita kuanzia mwezi Novemba, 2009 hadi Aprili, 2010.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuendesha mitambo ya IPTL ulifanyika kwa makubaliano ya msingi ya kuiomba Serikali kununua mafuta pamoja na kulipia sehemu ya gharama ya kuendesha mitambo hiyo. Aidha, Serikali ililazimika kutenga kiasi cha shilingi bilioni 46.4 kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa mafuta mazito ya mitambo ya IPTL kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Novemba, 2010 hadi Februari 2011 ili kuimarisha kiwango cha uzalishaji umeme kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Wataalamu wa TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini inaonesha kwamba, patakuwepo na upungufu wa wastani wa *megawatt* 264 katika mwaka wa 2011 kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa ikiwa hali ya ukame itaendelea kuwa kama ilivyo sasa. Aidha, kufuatia taarifa za hivi karibuni za Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, hata mvua zikinyesha kwa wingi, bado nchi yetu itakumbwa na upungufu wa umeme wa wastani wa *megawatt* 67 mwaka 2011 kutokana na sababu zifuatazo:-

Moja, mahitaji ya umeme kuongezeka kwa kasi kuliko uwekezaji katika miradi mipya ya kuzalisha umeme ambapo mwaka 2008 mahitaji ya juu, yaani *pick demand* yalikuwa *megawatt* 729 na mwaka jana 2010 mahitaji ya juu yalifikia *megawatt* 833.

Pili, kupungua kwa maji katika Bwawa la Mtera kulikosababisha uwezo wa kuzalisha umeme kuwa chini ya nusu. Hadi kufukia tarehe 14 Februari, 2011 kina cha maji katika Bwawa la Mtera kama nilivyosema, kilikuwa mita 691.31 juu ya usawa wa Bahari au mita 1.31 tu zilizosalia kwenye Bwawa hilo ili kufukia kina cha chini cha mita 690 na kama nilivyosema leo kina kimefikia 691.30. Bwawa la Mtera lilikuwa limejaa ambalo ni Bwawa mhimili linakuwa na maji ya mita 698.50.

Mheshimiwa Spika, mvua tunazoziongelea ambazo zinawezesha maji kuongezeka katika mabwawa yetu ni mvua zinazohitajika katika Mkoa wa Dodoma, Singida, Iringa na maeneo ya Mkoa wa Mbeya. Kwa sisi tukipata mvua za kutosha katika maeneo hayo, Bwawa letu la Mtera linajaa na kwa sababu ni bwawa mhimili, manufaa yake yataonekana katika kiwango cha uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pengo la *megawatt* 67 linaweza kuzibwa endapo Serikali itaendelea kutoa fedha za kutosha na kwa wakati za kununua mafuta ya kuendesha mitambo ya IPTL kwa uwezo wake wote, yaani *megawatt* 80 na kama mvua za kutosha zitanyesha kujaza mabwawa yetu.

Mheshimiwa Spika, hatua za dharura za kuondokana na mgawo wa umeme nchini: Ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa umeme uliosababisha mgawo wa umeme unaoendelea kwa sasa Serikali kwa kushirikiana na TANESCO imechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kuhakikisha fedha za kununulia mafuta ya kuendesha kituo cha kuzalisha umeme cha IPTL zinaendelea kupatikana kwa wakati ili kituo kiweze kuzalisha katika kiwango chake cha juu cha *megawatt* 80.

Pili, kuhakikisha kwamba miradi ya kudumu ya kuzalisha umeme ya *megawatt* 160, *megawatt* 100 Dar es Salaam na *megawatt* 60 Mwanza inakamilishwa kwa wakati kama ilivyopangwa mwezi Desemba mwaka huu au ikichelewa kidogo mwaka 2011 mwezi wa kwanza.

Tatu, kuharakisha mchakato wa kukodi mitambo ya dharura yenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya *megawatt* 260 endapo mvua za kutosha hazitanyesha kuwezesha ongezeko la umeme utokanao na maji.

Nne, kutekeleza mpango wa kupanua miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi kutoka kwenye visima vya Songosongo hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaarifu Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, sasa hivi EWURA anaendelea na usimamizi wa taftishi au mchakato wa kuwezesha wawekezaji katika upanuzi wa miundombinu ya gesi, lakini pia Wizara kwa

kushirikiana na wawekezaji waliopo, tunafanya kazi kwa muda mfupi kuongeza uwezo wa kuzalisha gesi zaidi kama mitambo mingine ya kutumia gesi itapatikana.

Tano, kuendelea kutekeleza Miradi ya Kupunguza Upotevu wa Umeme kutoka 21% ilivyo sasa hadi 15% kati ya mwaka huu 2011 hadi 2015.

Sita, TANESCO kusimamia mgawo wa umeme kwa umakini zaidi na kuhakikisha kwamba, umeme kwenye shughuli za uzalishaji na sehemu nyingine nyeti za huduma za jamii kama Hospitali, Zahanati, Vituo vya Afya, Ulinzi na Usalama unaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya umeme kwa kipindi cha muda mfupi kati ya mwaka 2011 hadi mwaka 2015 tunapoendelea hadi mwaka 2018, Miradi ya Uzalishaji, yaani *generation*: Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Washirika wa TANESCO, inaendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kuongeza Uwezo wa Kuzalisha Umeme katika kipindi kifupi cha mwaka 2011 hadi mwaka 2015 ili kuepusha tatizo la mgawo wa umeme siku za usoni kama ifuatavyo:-

Moja, ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kama nilivyosema *megawatt* 100 Dar es Salaam na *megawatt* 60 Mwanza, ujenzi wa mitambo ya kutumia gesi asili ya Songo Songo na Mnazibay, miradi ambayo kwa pamoja itatuongezea uwezo wa *megawatt* 870 kwa mpangilio ufuatao:-

Kinyerezi kuna Mradi ambao utazalisha umeme *megawatt* 240 na hapa unatarajiwa kukamilika mwaka 2013 kwa kushirikiana na Kampuni ya *SUMITOMO Cooperation* ya Japan. Mradi huu utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 510 na mchango wa Serikali ni Dola za Marekani milioni 10.

*Mnazibay megawatt* 300, Mradi huu utakamilika mwaka 2013, kampuni moja ya Kichina inayoitwa CMEC, mkataba wa EPC umeshasainiwa tayari. Mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 660 na mchango wa Serikali ni Dola za Marekani milioni 132.

Somangafungu kule Kilwa tunatarajia kuzalisha *megawatt* 230, Mradi huu utakamilika mwaka 2013, Sekta Binafsi kupitia kampuni inayoitwa *Pro-energy Services* inaendelea na maandalizi ya Mradi huu na Mradi huu unatarajiwa kugharimu takriban Dola za Marekani milioni 350.

Makaa ya Mawe ya Kiwira, Mchuchuma na Ngaka, kwa pamoja tunatarajia kuzalisha umeme wa *megawatt* 1200 kwa mpangilio ufuatao:-

Kiwira ni *megawatt* 200 unatarajiwa kukamilika mwaka 2013, awali tulikuwa tunaendelea na mazungumzo na China walishakubali kutufadhili Dola za Kimarekani milioni 400, lakini hivi karibuni pia Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limeonesha dhamira yake na mazungumzo yanaendelea na Serikali; ni Mradi utakaoiva ndani ya miaka miwili.

Mchuchuma *megawatt* 600 unatarajiwa kukamilika mwaka 2015, Mradi utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 1000, sawasawa na bilioni moja Dola za Kimarekani, mchango wa Serikali ni Dola za Marekani milioni 250.

Ngaka Mkoani Ruvuma *megawatt* 400, Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2015, kampuni husika ni *TANCO Energy Limited* na tathmini ya kitaalamu inaendelea. Gharama zinakaribia kufikia Dola za Marekani bilioni moja kupitia kwa mwekezaji.

Miradi ya kuzalisha umeme kwa nguvu ya upepo Mkoani Singida *megawatt* 100, Mradi huu utakamilika mwaka 2012 na kampuni inayoendeleza Mradi huu ni kampuni inayoitwa *Wind East Africa Limited*. Mradi huu unatarajiwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 250 lakini pia kuna kampuni nyingine inayoitwa *Power Pool East Africa Limited*, kwa kuanzia itazalisha *megawatt* 50 ifikapo mwaka 2013 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 123.

Miradi ya kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji (*Hydro*), inayohusisha kuongezeka kwa uwezo wa *megawatt* 600 kupitia Miradi ifuatayo kwa kipindi kati ya mwaka huu na mwaka 2018 na hii ni Miradi ambayo inaweza kutekelezwa katika kipindi cha muda wa kati.

Tuna Rusumo ambayo ni Mradi unaoendelezwa na nchi tatu; Tanzania, Rwanda na Burundi kiasi cha *megawatt* 60, lakini kwa upande wa Tanzania tutapata *megawatt* 20 na Ruhuji *megawatt* 358. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2016 na ule Mradi wa Rusumo unatarajiwa kukamilika mwaka 2015.

Rumakari tunatarajia kuzalisha *megawatt* 222, tumeshasaini makubaliano ya awali na Kampuni ya Kirusi lakini taratibu zote za ukamilishaji wa Mradi zinaendelea na Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingine ni pamoja na Miradi ya Mpanga *megawatt* 144 na *Stiglers' Gorge megawatt* 2100, ambayo Serikali inaendelea kutafuta wafadhili na waendelezaji na sasa hivi tuko katika mazungumzo na wadau mbalimbali na hasa washirika wa maendeleo katika Miradi hii.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Miradi midogo ambayo haizidi *megawatt* 10, tumeanzisha utaratibu maalum unaojulikana kama *Snow Power Purchase Agreement* kupitia Mamlaka ya Udhambi wa Nishati na Maji (*EWURA*), wanaendelea kusimamia utaratibu huo na Miradi mingi imeibuliwa na mingine imeshaanza kuzalisha ikiwemo *TPC* ya Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, pia tuna Miradi ambayo tumepata ufadhili wa Taasisi moja ya Uholanzi inayoitwa *ORIO*. Taasisi hii imetufadhili katika kuendeleza Miradi ifuatayo:-

Miradi katika Miji ya Ngara, Biharamuro na Mpanda ambapo wakati juhudi za Serikali zinaendelea kuiunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa katika Gridi ya Taifa, tumeona Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda, kila mmoja uongezewe uwezo kwa kufunga mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito yenye uwezo wa *megawatt* 2.5 na Miradi hiyo itakamilika mwaka 2013.

Serikali itafunga mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 2.5 katika kila Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda ifikapo mwaka 2013 ili kuimarisha huduma za umeme katika miji hii wakati juhudi za Serikali kuiunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa kwenye Gridi ya Taifa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme: Sambamba na utekelezaji wa Miradi ya Kuzalisha Umeme, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na TANESCO, inaendeleza Miradi ya Kuimarisha na Kupanua Miundombinu ya Kusafirisha Umeme kwa lengo la kufikisha kwa wateja umeme utakaozalishwa chini ya programu niliyoeleza na kuipatia umeme wa Gridi Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa, kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa *Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)* unafadhiliwa na Benki ya Dunia na unahusu Mikoa ya Dar Es Salaam, Arusha na Kilimanjaro, 132kV, (2015, WB (IDA), utekelezaji unaendelea). Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 55 kwa usambazaji wa umeme na Dola milioni 34.252 kwa Miradi ya Usafirishaji Umeme;

(b) Mkataba wa ujenzi wa laini ya Mtwara-Singida DC line 330kV (2013, CEMC, EPC imesainiwa;

(c) Bulyanhulu-Geita 220kV (2014, BADEA/OFID, fedha zimepatikana); Mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 28.8;

(d) Geita–Nyakanazi kV 220 (2014, BADEA/OFID, mazungumzo yanaendelea kuhusu ufadhili); gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 4.5;

(e) Morogoro–Tanga–Moshi –Arusha kv 400 (2015, Exim Bank ya China, MoU imeshasaniwa, *Technical Proposal* zinapitiwa na TANESCO); Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 75;

(f) Singida - Arusha kV 400 (2015, RSMI/GENIVAR, upembuzi yakinifu unaendelea na utakamilika Februari, 2012); gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 190, Serikali itachangia Dola za Marekani milioni 28.5;

(g) *North – West Grid extension* – kuunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa kwenye Gridi ya Taifa kV 220 (2015, Exim Bank ya China, MoU imeshasainiwa, matayarisho ya upembuzi yakinifu yanaendelea); Mradi utagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 226, mchango wa Serikali ni Dola za Marekani milioni 34; na

(h) Serikali za Zambia, Tanzania na Kenya zinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuunganisha miundombinu ya usafirishaji umeme katika nchi hizi (*ZTK - Interconnector Project*).

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Mradi wa *Iringa-Shinyanga Backbone Transmission Investment* ambao mchakato wa ujenzi wake umepangwa kuanza robo ya kwanza ya mwaka 2011, baada ya Serikali kukamilisha zoezi la kupata fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 550 mwezi Desemba, 2010 kwa ajili ya ujenzi wa Mradi. Mradi huu umefadhiliwa kwa pamoja na World Bank (WB), JICA, EIB, AfDB na Korea EDCF.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingine ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme na hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Makambako-Songea: Mradi huu unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 70.4 kutoka Serikali ya Uswidi kupitia Shirika lake la Maendeleo (Sida). *Specific Agreement* na *Credit Agreement* za Mradi zilisainiwa tarehe 16 Desemba, 2008 na tarehe 10 Agosti, 2010 sawia. Kwa sasa taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi huu wa Februari, 2011. Mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Oktoba 2011 na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014 na utahusisha kazi zifuatazo:-

- Ujenzi wa laini ya umeme ya msongo wa kilovolti 132 ya urefu wa kilometa 250 kutoka Makambako hadi Songea; na

- Ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya kV 132/33 katika maeneo ya Madaba na Songea.

(b) Mradi wa *Electricity V*: Huu ni Mradi wa kuboresha na kuendeleza miundombimu ya umeme kwa ajili ya huduma za kiuchumi na kijamii maeneo ya vijijini, makao makuu ya wilaya na pembezoni mwa miji katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Shinyanga na Dar es Salaam. Mradi unakadiriwa kugharimu shilingi za Kitanzania bilioni 60, chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mshauri atapatikana mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2011 ili makabrasha ya zabuni yaandaliwe.

(c) Mradi unaofadhiliwa na *Millenium Challenge Corporation (MCC)*: Mradi huu umegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

- Mradi wa *Zanzibar Interconnector Project*. Katika Mradi huu inajengwa njia mpya ya pili ya kupeleka umeme Zanzibar. Mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 63.125. Kwa sasa Mkandarasi ameshapatikana na anafanya *route survey* ya mwisho na matarajio ni kukamilika kwa ujenzi wa Mradi mwishoni mwa mwaka 2012;

- *Malagarasi Hydropower and Kigoma Distribution Project* – Mradi wa kupata umeme wa MW 8 kutokana na nguvu za maji ya Mto Malagarasi na kujenga miundombinu ya kusambaza umeme Kigoma, Uvinza na Kasulu. Mradi huu unatarajiwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 53.68. Upembuzi yakinifu wa Mradi wa

kuzalisha umeme wa Mto Malagarasi ulikamilishwa mwezi Machi, 2010 na kubainisha kuwepo kwa konokono adimu. Kulingana na taratibu za masuala ya mazingira, utekelezaji wa Mradi ulisimama. Hata hivyo, MCC wamekubali kufadhili upembuzi yakinifu mpya katika eneo lingine kwenye Mto Malagarasi (Igamba III); na

- *Distribution Systems, Rehabilitation and Extension (T&D) Project* - Huu ni Mradi wa Ukarabati na Ujenzi wa Laini za Umeme kwenye mfumo wa usambazaji umeme kwa Mikoa ya Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mwanza na Mbeya. Mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 89.666. Wakandarasi wa Mradi wameshapatikana na wameshaanza kazi ya *mobilization* na matarajio ni Mradi kukamilika mwishoni mwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Mradi chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) katika mikoa 16, unafadhiliwa na Serikali kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini ulio chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga. Mradi huu utagharimu zaidi ya Shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, Mradi utahusisha ujenzi wa njia za umeme msongo wa kilovolti 33 na 11 jumla ya urefu wa kilometa 1600, ufungaji wa transfoma 350 za ukubwa tofauti, ujenzi wa njia za umeme msongo wa kilovolti 0.4 zenye jumla ya kilometa 900 na uunganishaji wa wateja wapya wanaokadiriwa kufikia 20,000. Utekelezaji wa Mradi huu umeshaanza na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2011.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ununuzi wa Jenereta katika Makao Makuu ya Wilaya za Sumbawanga, Kasulu, Kibondo, Nkasi na Namtumbo unajumuisha ununuzi na ufungaji wa jenereta zenye uwezo wa kuzalisha MW 1.25 kila moja kutoka kwa mzabuni ambaye ni Kampuni ya Zwart Techniek ya Uholanzi. Utekelezaji wa Mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Sumbawanga jenereta nne zenye uwezo wa kuzalisha MW 1.25 kila moja zitakamilika kufungwa mwezi Mei, 2011.

(ii) Namanyere (Nkasi): Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi (Namanyere), yanategemewa kupata huduma ya umeme kutoka Mjini Sumbwanga baada ya kukamilika Mradi wa Ufungaji Jenereta Mjini Sumbawanga.

(iii) Loliondo (Ngorongoro): Jenereta nne zenye uwezo wa kuzalisha MW 1.25 kila moja zitakamilika kufungwa mwezi Septemba, 2011.

(iv) Kasulu na Kibondo: Ilipangwa kuwa na jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha MW 2.5 kwa kila wilaya; na kazi ya ujenzi na ufungaji mashine imeshakamilika. Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme (*distribution*) inaendelea kwa sasa na umeme utawashwa kuanzia mwezi Machi, 2011.



(v) Mradi wa Namtumbo: Ufungaji wa jenereta yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1.9 katika Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo utakamilika mwezi Desemba, 2011.

(vi) Somanga Fungu: Kituo hiki kinazalisha umeme utokanao na gesi MW7.5 kwa ajili ya matumizi ya Wilaya za Kilwa na Ikwiriri ambazo zinatimia kiasi ambacho hakizidi MW 2.5.

Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Umeme wa Mwaka 2008 uliofanyiwa durusu mwaka 2009 (*Power System Master Plan - PMSP 2009*), unaonesha kwamba mahitaji ya juu ya umeme ya MW 833 yatakua na kufikia MW 1482 mwaka 2015, MW 2,218 mwaka 2020 na MW 6,091 mwaka 2033. Ili kuhimili ukuaji huo, hatua madhubuti zinaendelea kuchukuliwa ili kuongeza kiwango cha uzalishaji umeme hatua kwa hatua, kwa lengo la kuhakikisha kwamba, Sekta ya Umeme inahimili na kukidhi mahitaji ya umeme katika kipindi kifupi, cha kati hadi kirefu, kama ilivyoelekezwa na Ibara ya 63 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Kuendeleza Sekta ya Umeme: Utekelezaji wa vipaumbele 13 vya Dira ya Maendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo kama ilivyoainishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake wakati akizindua Bunge la Kumi pamoja na makisio ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii wa nchi yetu, utategemea upatikanaji wa nishati ya umeme ulio wa uhakika na unaokidhi mahitaji ya sekta zote za kiuchumi na kijamii. Ufanikishaji wa vipaumbele na utekelezaji wa mikakati ya Serikali ya kushamirisha uchumi na kupunguza umaskini nchini kama vile MKUKUTA II, Kilimo Kwanza na Malengo ya Maendeleo ya Milenia kwa pamoja unategemea uimarishaji wa Sekta ya Umeme kwa kujenga kwa wakati Miradi iliyoainishwa katika Kauli hii.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kipaumbele iko katika makundi mawili, yaani miradi itakayotekelezwa na sekta binafsi bila mchango wa Serikali na miradi itakayohitaji mchango wa Serikali katika hatua za mwanzo kulingana na masharti ya wakopeshaji fedha. Aidha, miradi ambayo inafadhiliwa na Serikali kwa asilimia mia moja inabidi itengewe fedha za kutosha katika Bajeti za Serikali. Mahitaji hayo ni:-

(a) Dola za Marekani takriban milioni 4,721 zinazohitajika kugharamia uwekezaji wa Miradi ya Uzalishaji wa Umeme kwa kipindi cha 2010-2018. Kati ya hizo, Dola za Marekani takriban milioni 725 zitahitajika kutolewa na Serikali kama mchango wake katika kugharamia uwekezaji wa Miradi ya Uzalishaji wa Umeme kwa kipindi cha 2010-2018; na

(b) Dola za Marekani takriban milioni 946 zitahitajika kugharamia uwekezaji katika upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme kwa kipindi cha 2010-2018. Kati ya hizo, Dola za Marekan takriban milioni 142 zitahitajika kutolewa na Serikali kama mchango wake katika kugharamia uwekezaji katika upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme kwa kipindi cha mwaka 2010-2018.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utekelezaji wa miradi ya kipaumbele yataiwezesha nchi:-

- (a) Kupata uwezo wa kuzalisha nishati ya umeme yenye viwango bora inayokidhi mahitaji ya nchi;
- (b) Kuwa na mfumo wa umeme wenye umeme wa akiba (*reserve margin*);
- (c) Kupunguza utegemezi wa uzalishaji wa umeme unaotokana na vyanzo vya nguvu za maji (*optimized hydro-thermal mix*);
- (d) Kuweka mazingira mazuri ya kushiriki kwenye biashara ya umeme katika nchi za jirani na za kanda kupitia Taasisi za *Southern African Power Pool (SAPP)* na *Eastern African Power Pool (EAPP)*;
- (e) Kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii nchini kwa kutekeleza kwa ufanisi mikakati na mipango ya maendeleo ya Serikali; na
- (f) Kuleta utengamavu na imani kwa wawekezaji katika sekta za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu, yanategemea kuwepo kwa huduma ya umeme iliyo bora. Juhudi za makusudi zilizoanza kuchukuliwa toka mwaka 2006 zinalenga:-

- (a) Kuhakikisha kupanuliwa kwa wigo wa vyanzo vya kuzalisha umeme ili kuondoa utegemezi kwenye umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji;
- (b) Kukwepa mgawo wa umeme wa mara kwa mara;
- (c) Kuboresha hali ya kifedha ya TANESCO;
- (d) Utekelezaji wa marekebisho katika Sekta ya Umeme (*Power Sector Reforms*); na
- (e) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Sekta ya Umeme 2009 – 2033.

Mheshimiwa Spika, mipango ya kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme ipo, ila fedha nyingi zinahitajika. Miradi hii inawezeshwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu, sekta binafsi na washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili mipango niliyoifafanua hapo juu itekelezwe kikamilifu na kwa wakati, ni lazima fedha zote zipatikane kwa wakati. Miradi yote mikubwa huchukua muda mrefu kuanzia ununuzi wa vifaa, makandarasi na washauri mbalimbali. Kwa uzoefu tulioupata, inatulazimu tuchukue tahadhari kubwa ili kuepuka matukio kama yaliyotokea kwenye baadhi ya Miradi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

### **HOJA YA DHARURA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Nini? Samahani sikusikia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Hoja ya dharura, kuna nini? Hebu eleza mazingira ya hoja kwanza kabla hatujapoteza muda.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, muda mfupi uliopita, Waziri amemaliza kutoa Kauli ya Serikali kuhusu suala la umeme. Kwa mujibu wa maelezo yake, anayo mapendekezo ya dharura aliyoyazungumza, lakini la ziada tu ni kwamba, maelezo yake yanaashiria hali tete sana katika Taifa kuhusiana na suala zima la umeme. Katika mazingira ya namna hiyo, hili ni jambo la dharura sana, linalohusu siyo uhai wa uchumi wa taifa, bali maisha ya mwananchi mmoja mmoja. Pamoja na hayo, mapendekezo ya Waziri yamezungumza mipango ambayo inahusu mapendekezo ya dharura lakini yanahusu kiwango kikubwa sana cha pesa. Nimepiga mahesabu ya haraka tu kinafikia takriban shilingi bilioni 300. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa jambo la dharura kama hili na kiwango kikubwa cha namna hii cha fedha, nadhani ni vizuri Bunge lako Tukufu sasa likarejea kwenye Kanuni, tukatumia Kanuni ya 55 na ninatoa hoja hii kwa mujibu wa Kanuni ya 55(3)(e) pamoja na Kanuni ya 47(1) ili jambo hili sasa lijadiliwe na Bunge lako Tukufu hivi sasa kama jambo la dharura na shughuli nyingine ziweze kuahirishwa kuweza kuruhusu mjadala kuhusu jambo hili la dharura. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Pamoja na kwamba, hoja imeungwa mkono, kwa mujibu wa Kanuni kama Spika ataona kwamba hoja hiyo haiendi sawasawa na mwenendo wa kuendesha shughuli za Bunge, hataikubali hiyo hoja.

Waheshimiwa Wabunge, tayari nimeunda Kamati ya Nishati na Madini na bahati nzuri mzungumzaji wa sasa hivi ndiye Waziri Kivuli wa Wizara hiyo ya Nishati na Madini. Sasa jambo kubwa kama hili tusijifanye sisi hapa ndiyo ma-*panacea* wa kila kitu. Kamati hiyo nimeipa muda, wiki ijayo tarehe 21 itakwenda Mtera halafu wataendelea kwa karibu siku tano.

Sasa Mimi ningeshauri Waziri Kivuli ashirikiane na ile Kamati ili waweze kuja na kitu ambacho ni cha maana, kwa sababu mimi huyo huyo nilikuwa nimeagiza tupewe taarifa hii. Sasa tukiwa na taarifa juu ya taarifa, hatutakuwa tunakwenda inavyopaswa. Kamati ile inaendelea na Mheshimiwa Waziri Kivuli, naomba ushirikiane nao moja kwa moja kule.

Juzi tulikutana na *Private Sector Foundation*, nao pia nimeagiza Kamati wakutane nao Dar es Salaam kwa sababu nao wana mawazo yao na ninafikiri kwa mtindo huu tutakuwa tunajibu suala la ukweli na siyo suala la kusema tunazuka hapa na dharura. Ninaagiza hivyo, Kamati iendelee na ifanye kazi yake. (*Makofi*)

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2010 (*The Public Procurement Bill, 2010*).

Muswada wa Sheria ya Famasi wa Mwaka 2010 (*The Pharmacy Bill, 2010*).

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*).

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011 (*The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*).

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 93(1) ni kwamba, Miswada inayosomwa mara ya kwanza haitafanyiwa kazi na Bunge kwa hatua zote katika kikao kile ambacho Miswada ile imesomwa kwa mara ya kwanza kama alivyofanya Katibu pale Mezani. Maana yake ni kwamba, Miswada sasa hivi imeshagaiwa, tukishasoma hapa kwa sababu tumeshapewa, Waheshimiwa mnategemewa kwenda kuisoma, mnaweza kushirikisha Wataalam wa aina mbalimbali na mpaka Bunge lijalo kama itakuwa tayari, basi itabidi Kamati inayohusika ikaribishe watu ambao ni wataalam wa maeneo hayo ili waweze kusaidia kujadili kabla hatujaingia katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili. Hii ni fursa ya kuweza kutafuta utaalim unaoweza

kujua na namna yoyote ile. Kwa hiyo, Miswada hii inakuwa sasa wazi kwa watu wote, kila mtu anaweza kuupata na katika *Website* ya Bunge ipo. Kwa hiyo, mtu yeyote ana haki ya kuisoma na kuifanyia utafiti unaostahili Miswada iliyosomwa mara ya kwanza hapa.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, tulisema hii Miswada mingine ilisomwa mara ya kwanza Bunge la Tisa, lakini kwa utaratibu wetu Miswada inayokuwa imesomwa mara ya kwanza kabla ya Bunge kuvunjwa, likija Bunge jipya kama hili, inabidi tuanze upya kwa sababu sisi hatuifahamu na ndiyo utaratibu wetu. Kwa hiyo, Miswada ipo na itawekwa kwenye *pigeon holes* zenu, lakini tulikubaliana pia kwamba kwa sababu tumejifunza hii Miswada Bunge linanunua, siyo kwamba tunapewa nakala za bure, tunanunua; kwa hiyo, *Pigeon holes* zenu tutaweka karatasi inayoeleza Miswada yote hii na inapatikana wapi. Kwa hiyo, wewe unakwenda unachukua kule na utakuwa ume-*register* jina lako kwamba, umechukua Miswada kwa Katibu au *Library*. Kwa hiyo, ukishachukua pale unaweza kufanya kazi yako, huwa tunajikuta kwamba inakuwa ni hasara kwa sababu Miswada inajaa kwenye *pigeon holes* halafu haitumiki inatupwa na hivyo tunasababisha gharama zisizo na sababu.

## **UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE BODI ZA VYUO VIKUU NA TAASISI ZA ELIMU YA JUU**

**SPIKA:** Msimamizi wa uchaguzi.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia siku ya tarehe 9 Februari, 2011 na jana tarehe 14 Februari, 2011, leo Jumanne tarehe 15 Februari, 2011 baada ya Kipindi cha Maswali kama inavyooneshwa kwenye *Order Paper*, kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge watakaowakilisha Bunge kwenye Vyuo Vikuu na Taasisi mbalimbali. Muda wa mwisho wa kurudisha fomu za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumatatu tarehe 14 Februari, 2011 saa 10.00 jioni. Muda huo ulipofika, Wabunge waliokuwa wamejitokeza kuchukua na kurejesha fomu ni kama ifuatavyo na nitawasoma wote kwa pamoja kwa maana ya Vyuo vyote na utaratibu wote nitautoa baadaye:-

Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, kina nafasi mbili; moja ni Mwanamke na nyingine ni Mwanamume. Waliojitokeza na kuchukua fomu na kuzirejesha ni Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza.

Chuo Kikuu cha Dodoma kuna nafasi moja. Waliochukua fomu na kuzirejesha ni Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis na Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe. Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa ameniletea barua leo hii akionesha kujitoka kugombea nafasi hii, kwa hiyo, watabakia wagombea wawili.

Chuo Kikuu cha Mzumbe ziko nafasi mbili; mwanamke mmoja na mwanamume mmoja. Waliojitokeza na kuchukua fomu walikuwa wanne lakini mmoja amejitoka; kwa

hiyo, wanaobaki ni Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa; Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi amejittoa.

Chuo Kikuu cha Sokoine ni nafasi moja. Waliochukua fomu na kuzirudisha walikuwa watatu lakini mmoja amejittoa. Wabunge hao ni Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Sonz; Mheshimiwa Sara Msafiri Ally amejittoa.

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ziko nafasi tatu na hizi zinapatikana kwa kuzingatia jinsia na Muungano. Waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ni Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba na Mheshimiwa Henry Shekifu.

Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, ziko nafasi mbili; nafasi moja kwa ajili ya Mbunge Mwanamke na nafasi moja kwa ajili ya Mbunge mwanamume. Waliojitokeza na kuchukua fomu walikuwa watano, mmoja amejittoa. Waliobaki ni Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile. Mheshimiwa Pindi Hazara Chana amejittoa.

Chuo Kikuu cha Ardhi ni nafasi mbili; moja ya mwanamke na nyingine ni kwa ajili ya Mbunge mwanamume. Waliochukua na kurudisha fomu wako wawili. Kwa nafasi hii, tutaliomba Bunge kutumia *convention* kwa sababu wako wawili na wanatakiwa wawili; yupo Mheshimiwa Gosbert Blandes pamoja na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo.

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuna nafasi moja. Waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha walikuwa watatu, lakini mmoja amejittoa wamebaki wawili; Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile. Mheshimiwa Pindi Hazara Chana amejittoa.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi nafasi moja, amejitokeza mgombea mmoja na kuchukua na tutaomba Bunge litumie *convention*; ni Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa.

Chuo cha Ufundi Arusha nafasi moja. Waliojitokeza wako wagombea watatu; waliorudisha fomu ni Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene.

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, aliyejitokeza ni mmoja na nafasi ni moja, tutaomba Bunge lako litumie *convention*; Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania waliochukua fomu na kuzirejesha wako wawili, nafasi iko moja; ni Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina pamoja na Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani. Uchaguzi huu unaendeshwa kufuatana na masharti ya Kanuni 5(2) na nyongeza ya (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo 2007, ambazo zinafafanua taratibu za

Uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha Bunge katika Vyuu Vikuu. Kwa mujibu wa kifungu cha 8(2)(b) cha nyongeza ya (2) ya Kanuni za Bunge, kila mgombea atatakiwa apite mbele ya Waheshimiwa Wabunge kujieleza kwa dakika zisizozidi tatu na kujibu maswali yao kama yatakuwepo na baada ya kujieleza, karatasi za kupiga kura zitatolewa.

Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Hiyo ndiyo taarifa ya Msimamizi wa Uchaguzi. Tunaendelea, tutawahoji wote au tuhoji chuo kimoja. Fomu ya kupigia kura ikoje; ni moja au kila kundi?

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Fomu za kupiga kura tumezitofautisha baada ya kuona kwamba, jana zilitaka kuleta usumbufu, kwa hiyo, kila chuo kinajitegemea.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunaweza kuwahoji wote halafu tuwapigie kura au kila chuo tupige kura wakati unaPofika. Haya basi wote waliotajwa hapa watoke.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni 68 kifungu cha (7).

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi niliwasilisha barua kwa Katibu wa Bunge na nakala kwako, nikiweka pingamizi juu ya Mgombea wa Uwakilishi wa Wanawake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa ruhusa yako naomba niisome.

**SPIKA:** Mimi sikupata nakala.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Niliwapa hao wahudumu.

**SPIKA:** Mimi sijapata nakala. Katibu alipata barua yako?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Aliipata na amenijibu baadhi ya maswali.

**SPIKA:** Ulisema nini na akakujibu nini?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kwenye barua yangu niliainisha kwamba, nimeweka pingamizi kwa Mgombea wa Uwakilishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nafasi ya wanawake. Nikasema, tafadhali rejea mada hapo juu. Utaratibu ambao uliwekwa katika mchakato mzima wa kupewa ridhaa na Waheshimiwa Wabunge kuwakilisha katika Taasisi mbalimbali, mchakato huo ulianza kwa uchukuaji wa fomu na kurudishwa kwa muda uliowekwa kwa wagombea wote kurudisha fomu, ambao ulikuwa ni tarehe 14 Februari 2011 saa 10.00 jioni. Hili ni suala mojawapo kama sharti muhimu katika mchakato huo.

Pingamizi langu kwa aliyetangazwa kuwa mgombea, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, hakutumiza sharti la kuchukua na kurudisha fomu kwa muda uliopangwa, jambo ambalo lilimfanya kutokuwa mgombea halali.

Mheshimiwa Spika, nimeainisha kigezo hicho cha mgombea tajwa amepoteza sifa ya kupigiwa kura kwa zoezi linalotakiwa kufanyika. Ushahidi wa wazi ni kuwa, hadi jana ambapo ilikuwa tarehe 14 Februari takriban saa 10.18 hakukuwa na mgombea yeyote aliyerudisha fomu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam isipokuwa mimi hata kwa upande wa wanaume.

Kwa kuwa nilitaka kujua ni nani nagombea nae ili niweze kujiimarisha kwenye suala zima la kampeni, niliendelea kufuatilia zaidi katika Ofisi ya Katibu wa Bunge muda mfupi kabla ya kuahirisha Bunge, bado lilikuwa ni jina langu pekee tu kwa aliyerudisha fomu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Cha ajabu leo asubuhi nimeona majina matatu yamebandikwa alikuwepo na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Sasa nikamwandikia barua Katibu wa Bunge akanijibu kwa kifupi sana kwamba, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya alichukua hii fomu tarehe 13 Februari na kuirudisha jana 14 Februari saa 9.30. Cha ajabu kabisa nimerudisha fomu kama dakika 18 kufikia saa 10.00 na nilikuwa ndiyo mgombea pekee *at that time*.

Nikaendelea kumwuliza kwanza inakuwa ni *contradiction* kwa sababu mhudumu mmojawapo katika Ofisi ya Katibu wa Bunge aliniambia Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya dakika kumi kufikia saa 10.00 akajaza fomu na kuirudisha. Kwa hiyo, ningependa ufafanuzi wa *contradiction* hizi na nijue demokrasia ina-*take charge* wapi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nawasilisha.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nimekataa pingamizi lake kwa msingi mmoja; mwenye *authority* za kutoa taarifa ambazo zinahusiana na Ofisi yangu ni Katibu wa Bunge. Hakuna mtu yeyote yule ambaye kama sijampa mamlaka ya kutoa taarifa ya Ofisi anaweza akafanya hivyo. (*Makofi*)

Isitoshe, Mheshimiwa Manyanya amechukua fomu tarehe 13 na amerejesha kwangu jana saa 9.30. Sasa yeye kama amefika saa 10 kasoro dakika 18 na bado akapata taarifa kwamba, hakuna mtu aliyerejesha fomu; ni mambo ya ajabu na mtu aliyetakiwa ampe hizo taarifa ni mimi hakuna mtu mwingine mwenye mamlaka ya kutoa taarifa za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninachojifunza ni kwamba, tutakapokuwa tunapitia Kanuni zetu mbalimbali za kuendesha mambo haya na nyingine hizi, nadhani itabidi tuziangalie upya tena kwa sababu kwa mfano katika hali ya kawaida katika chaguzi zetu kule ikifika saa ile inayohusika, majina yanakuwa nje, kwa hiyo kila mtu anaona yako nje. Sasa kwa utaratibu wetu hapa mpaka unaanza kuuliza; Mheshimiwa Esther ulimwuliza nani akakwambia hakuna majina? Huwezi kuthibitisha.



**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mhudumu.

**SPIKA:** Ndiyo maana unasema, lazima hapa mtabishana mpaka kesho maana mtamwuliza huyu aliyemwambia Esther kwamba yeye yuko peke yake ni nani? Huyo Katibu mwenyewe anasema hakusema, hakukutana naye na wala hakuonana naye. Kwa hiyo, utaratibu mzima wa uchaguzi kuanzia jana nimeona kama una matatizo kidogo kwa sababu zipo kwenye nyongeza za kanuni zetu, nadhani tutatumia muda tuweze kujifunza vizuri zaidi hizi taratibu za uchaguzi. Baada ya kusema hivyo, naomba tuendelee na kazi tuliyonayo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hapana sasa tunaleta ubishi. Nimesema, Kanuni zetu itabidi ziangaliwe. Wote wanaogombea waondoke nje isipokuwa ningomba Waheshimiwa Wabunge tufanye hivi; jana tulikubaliana kwamba, nafasi ambazo zina watu wanaolingana na idadi tunayohitaji tukubali kwamba, wamepita bila ya kupingwa; bado hilo linasimama. Kwa hiyo, tuwakubalie hao ambao nafasi zao hazina mtu zaidi wapite bila ya kupingwa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kuwapitisha Wabunge waliopita bila kupingwa ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Sote tumekubaliana, kwa hiyo basi nafasi gani zinapita bila ya kupingwa?

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Nafasi ambazo hatutapiga kura ni Chuo Kikuu cha Ardhi, ambapo Mheshimiwa Gosbert Blandes pamoja na Mheshimiwa Susan Lyimo wamepita bila ya kupingwa. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa amepita bila ya kupingwa. Pamoja na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge amepita bila ya kupingwa. Wanaohusika wote watoke nje.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, pia nafasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iwe moja ya mwanamume na moja ya mwanamke. Katika wanaume mgombea yuko mmoja pia; je, yeye anapigiwa kura au hapigiwi?

**SPIKA:** Mwanamume anataka raha huyu! *(Kicheko)*

**NDUGU JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna wagombea; mmoja mwanamume kwa misingi hiyo hiyo ni kwamba, kwa

sababu nafasi ziko mbili, moja ya Mbunge mwanamume na nyingine ya Mbunge mwanamke, kwa hiyo, hatutapiga kura.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza amepita bila ya kupingwa. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, pia kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe kuna nafasi mbili; mgombea mmoja mwanamume na mmoja mwanamke na kwa upande wa nafasi ya mwanamke ni mgombea pekee kwa jina langu. Sasa sijui hapa itakuwaje?

**SPIKA:** Ahaa na wewe umepita bila ya kupingwa. (*Makofi*) Na wewe unataka kupita bila ya kupingwa; unaitwa nani?

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Mimi naitwa Abdul Mteketa, Mbunge wa Kilombero. Kuna mgombea wa *Open University* wa Zanzibar naye yuko peke yake nafasi ya wanawake.

**SPIKA:** Hebu sema tena hatujakuelewa; ni chuo gani, Chuo Kikuu Huria cha ...

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Chuo Kikuu cha Zanzibar.

**SPIKA:** Wako watatu ukizingatia jinsia na Muungano.

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Katika jinsia ya wanawake yuko mmoja tu.

**SPIKA:** Mbona tunaona kuna Zainab Rashid Kawawa, Susan Lyimo; wako wawili tu au umeangaliaje? Hii ni nyingine?

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Nasema mwanamume wa *Open University* ya Zanzibar.

**SPIKA:** Nani huyo aliyepita bila ya kupingwa? Nafikiri Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Jimbo la Dole na hii tunasema ni nafasi tatu kwa kuzingatia jinsia na Muungano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sylvester Mabumba amepita bila ya kupingwa. (*Makofi*)

### **T A A R I F A**

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kutoa taarifa kwamba, katika uteuzi wa Chuo Kikuu Huria, nilijitoa. Naomba niseme rasmi kwamba, nimejitoa baada ya kupata Chuo cha Ardhi.

**SPIKA:** Ulitoa jina lako? Hatujaona maandiko hapa.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, aliniambia kwa mdomo jana wakati tunatoka kwamba anataka kujitoa, lakini nikamwambia kwa masharti unawajibika kuandika barua. Nikamshauri kwamba, pengine itakuwa ni busara kama hawezi kuandika barua wakati huo akajitoa hapa hapa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tutakapofika zamu hiyo utajitoa wakati huo.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna jambo ambalo linatokea sasa kwamba, naanza kupokea vi-*memo* vingi tu vya kujitoa. Nilidhani kwamba, badala ya kuisumbua Meza, waitwe halafu watajitoa hapa hapa itakuwa ni vizuri zaidi.

**SPIKA:** Wakifika hapa mtu atajitoa na sisi tutatumia muda vizuri hatutamhoji wala nini. Sasa naomba wale wengine wote waende huko nje tutaita chuo kwa chuo. Haya changamkeni jamani mtoke haraka sana; bado mnaomba kura?

Tunaanza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nafasi mbili; mwanamke mmoja na mwanamume mmoja, wako wanawake wawili.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Tutapiga kura kwa wanawake tu. Namwita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko aingie. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, tunakupa dakika tatu kujieleza halafu utaulizwa maswali yasiyozidi matatu kama yapo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu hii ndiyo nafasi yangu ya kwanza kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu. Vile vile napenda kuwashukuru Wananchi wote wa Tanzania, kwa imani yao kubwa waliyoionesha kwa chama chetu kwa kutupa ushindi mkubwa ambao umenisababisha leo hii niko Bungeni. Salamu zangu za kipekee kwa Wananchi wa Mkoa wa Mara hususan Wananchi wa Tarime.

Natoa pia salamu zangu za kipekee kwa familia yangu hasa kwa mwanangu Nicole, kwa uvumilivu aliounesha kipindi cha kampeni. Nawasalimia pia wafanyakazi wenzangu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, napenda kusimama mbele yenu, kwanza kabisa, kuelezea ni nini kilichonisukuma kugombea hii nafasi ya kuwa Mwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nilijiona nitakuwa ni mwakilishi mzuri kwa kuzingatia kwamba, nimekuwa nafanya kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mhadhiri Msaidizi kwa takriban miaka mitano. Ninajua changamoto, ninajua ni nini Chuo Kikuu kinafanya, ninajua muundo mzima wa Chuo Kikuu; ila kwa kusikitishwa sana, nimeamua kutogombea

nafasi hii ya Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nimegundua demokrasia haitumiki kabisa hata ndani ya Bunge letu Tukufu. Mfanyakazi wa Katibu wa Bunge amejaribu kusema kwamba yeye ndiye anayehusika, lakini mbona nilivyokwenda kuchukua fomu yangu na kurudisha sikumwona nimkabidhi? Kwanini inakuwa *specific* kwa watu wengine? Kwa sababu ukiangalia hata ile *registry* iliyokuwepo hakukuwepo jina la Mheshimiwa Eng. Manyanya. Kulikuwa na jina la Mheshimiwa Mwaiposa na wanaume watano, hadi kufikia hiyo jana. Nimesikitika sana na ukizingatia ndiyo nafasi yangu ya kwanza katika Bunge hili na umri huu nimepata *experience* mbaya ambayo nimeanza nayo na itaendelea kuwepo katika *mind* yangu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa na nia ya kunipa kura, waniwie radhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko nilikupa nafasi pale ukaeleza. Nilikusikiliza vizuri sana na nikasema kwamba inaelekea taratibu zetu hizi inabidi turudie tena kuziangalia. Nimesema hivyo, sasa kama kujieleza unamsema mwenzio mbona haiji! Maana yeye hana hatia. Kwa hiyo, naomba uombe kura au useme kama umejitoa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ilitibi nipate *clarification*. Lakini kwa heshima, naomba nisiombe kura. Nawashukuru sana na waliokuwa wana nia ya kunipigia kura, nawaomba radhi sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize mgombea swali moja, kwamba yeye alikuwa na taarifa toka jana kwamba hakutendewa haki na alikuwa na haki ya kumwona Katibu wa Bunge mapema tu akajua haki yake ilipo, kwanini alisubiri mpaka leo?

**SPIKA:** Ameandika barua na Katibu amemjibu. Sasa nilichosema hapa ni kwamba inaelekea taratibu zetu za uchaguzi humu ndani inabidi tuzirejee kwa sababu toka jana hazikukaa vizuri na leo hazijakaa vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Matiko tumemaliza. Anayefuata ni Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya aingie.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya Esther Matiko kujitua, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya anapata nafasi ya moja kwa moja.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya amepita bila kupingwa. Tunaendelea.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma. Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis aingie na nafasi ni moja. Tunakupa dakika tatu za wewe kujieleza na kama yatakuwepo maswali hayatazidi matatu.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mimi ndiye Sadifa Juma Khamis, ni Mbunge wa Jimbo la Donge Zanzibar, nagombea nafasi ya kuwa Mjumbe wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Nina uzoefu wa kutosha, nina elimu ya kutosha kuwa Mjumbe wa Bodi hiyo. Kwa heshima na taadhima naomba kura zenu za ndiyo, ahsanteni.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa mgombea swali moja lifuatalo:- Yeye anagombea nafasi ya ujumbe wa Bodi ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu na katika taasisi hizo tumekuwa na tatizo moja la *field attachment position* hasa kwa *female students*. Wengi wao wamekuwa hawapati nafasi hizo. Aidha, wakubaliane na Wakuu wa Idara au Vitengo kuwa na uhusiano wa kimapenzi, imetokea *for my experience*. Sasa kama Mjumbe ambaye tutakupa ridhaa ya kwenda kutuwakilisha huko ni ushauri gani atazipatia Bodi hizi kuhakikisha kwamba tatizo hilo linatatuliwa? Ahsante sana.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Sabreena kwa kutumia haki yake ya msingi ya kisheria kifungu namba 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba kila mwananchi ana haki ya kupata na kutoa ushauri au kuuliza swali na kupata taarifa. Hongera sana.

Mimi kwa upande wangu, hili tatizo bado sijakumbana nalo. Lakini kwa kupitia fani yangu ya Sheria, najua hilo ni kosa, kwa hiyo, tutapitia katika pande tofauti. Tutapitia kwa njia ya Mahakama, lakini pia kwa kushauri Taasisi husika kwa kupitia mbinu mbalimbali kuonana na wanafunzi kwa yule ambaye tatizo hilo litakalomkabili kuweza kuachana na suala hilo.

**SPIKA:** Tunaendelea swali la tatu, hakuna. Mheshimiwa Sadifu Juma kachukue nafasi yako.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, narejea tena kwa heshima na taadhima naomba kura zenu za ndiyo.

**SPIKA:** Ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. Tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama yatakuwepo maswali hayatazidi matatu. Karibu.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kujieleza mbele ya Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuomba nafasi ya uwakilishi wa Bunge katika Chuo cha Dodoma, kwa kifupi wanaita *UDOM*. Naitwa Pudenciana Kikwembe - Mbunge Viti Maalum (CCM) kutokea Katavi. Lakini kabla ya hapo, nilikuwa Mhadhiri wa Chuo cha Mipango hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, sioni sababu ya kueleza mengi. Kwa heshima na taadhima, naomba kura zenu.

**SPIKA:** Maswali. Maswali mara ya pili, maswali mara ya tatu. Ahsante sana Mheshimiwa Pudencia Kikwembe.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

**SPIKA:** Tunaendelea na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mzumbe tulipata taarifa ya awali kwamba Mheshimiwa Gosbert Blandes amejitoa. Kwa hiyo, wamebakia wagombea wawili. Nafasi ziko mbili mwanamme na mwanamke. Kwa hiyo, tunaelekea kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine. Salim Hemed Khamis.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim Hemed Khamis aingie. Tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama yatakuwepo maswali, hayatazidi matatu. Karibu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ingawa hayupo, kwa niaba: Kwa heshima na taadhima nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuomba ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge wanichagua katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, nina uzoefu mkubwa katika mambo ya kilimo. Kwanza, nina Shahada ya Pili katika mambo ya Kilimo; pili, nimepata mafunzo mbalimbali katika nchi mbalimbali kwa mfano Uingereza na Swaziland; tatu, nimefanya kazi katika Wizara ya Kilimo na Shirika la Sukari na Manukato Zanzibar; nne, nimekuwa mkulima na hodari na wa kibiashara katika Mkoa wa Morogoro ambako hicho chuo kipo kwa muda wa miaka mitano na mwisho, nimekuwa Waziri Kivuli katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika Bunge lote la Tisa.

Mheshimiwa Spika, kama mtanichagua, nitawawakilisha vizuri katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Sokoine ili kuifanya Sokoine na Bunge letu viwe karibu zaidi.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya kwanza, maswali kwa mara ya pili, maswali kwa mara ya tatu. Hakuna. Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, naomba uchukue nafasi yako.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kura zenu zote ili niwawakilishe vizuri katika Bodi ya Chuo Kikuu Sokoine.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, anayefuata ni Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama yatakuwepo maswali hayatazidi matatu. Karibu.

**MHE. JITU VRAJLAL SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, asalaam aleykum, Bwana Yesu asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo. Mimi niliyesimama mbele yenu naitwa Jitu Vrajlal Soni, natokea Jimbo la Babati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa heshima na taadhima ninawaombeni kura zenu wote ili niwe Mwakilishi wenu katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine. Mimi ni mkulima na nilikuwa Mwakilishi katika Taasisi mbalimbali nikiwakilisha wakulima *Agricultural Council of Tanzania*, nilikuwa mwakilishi wa wakulima katika kikundi kazi cha kilimo Mkoani Manyara, nilikuwa Katibu wa Chama cha Wakulima, Mwenyekiti wa Tume ya Maji - Bonde la Kiru na katika ngazi nyingine kuanzia ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya.

Kwa heshima kubwa, ninaomba kura zenu zote. Nitawawakilisha vizuri na kuhakikisha kuwa tunaendelea kuboresha chuo pekee ambacho kinatoa mafunzo makubwa katika sekta hiyo ya kilimo ambayo inawakilisha asilimia 100 ya Watanzania wote. Asilimia 95 ambayo moja kwa moja ni walengwa wa wakulima, lakini asilimia tano ni wale ambao bado na nyie wote mnawategemea kwa ajili ya chakula na mambo mengine. Ahsante sana. Naomba kura zenu zote. (*Makofi*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza swali mgombea. Mheshimiwa Mgombea tutajie jina la Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine, Morogoro.

**SPIKA:** Hajafika huko, atakwenda kumjua huko huko. Swali la pili, swali la tatu, hakuna. Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni naomba uwende ukachukue nafasi yako.

**MHE. JITU VRAJLAL SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kura zenu zote.

**ND. JOHN JOEL –KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, Wagombea wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**SPIKA:** Hapa tuna nafasi tatu. Mheshimiwa Mabumba kutoka Zanzibar amepita bila kupingwa. Mheshimiwa Gosbert Blandes tunakupa dakika tatu kujieleza na kama yatakuwepo maswali hayatazidi matatu. Karibu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wenzangu: Niliyesimama hapa naitwa Gosbert Begumisa Blandes - Mbunge wa Karagwe. Awali nilikusudia kuomba nafasi hii, lakini kwa kuwa nakusudia kuomba nafasi nyingine ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, ninajitoa katika nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante. Anayefuata.

## TAARIFA

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kama nimemsikia vizuri Katibu Mezani alishasema Mheshimiwa Blandes amejitoea Chuo Kikuu Mzumbe. Sasa hapa Mheshimiwa Blandes anasema anajitoea Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Katibu hebu atupe maelekezo mazuri maana tunaweza kujichanganya wenyewe hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Blandes unajitoea wapi sasa?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ninajitoea katika kugombea Ujumbe wa Bodi Chuo Kikuu Huria, sio Mzumbe.

**SPIKA:** Haya, sawa. Anajitoea Chuo Kikuu Huria. Ajieleze kuhusu?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nadhani hapa ndicho nilichosema kwamba vikaratasi hivi vilikuwa vinatuchanganya kwa sababu aliposimama Mheshimiwa Umbulla kutamka kwamba Mheshimiwa Gosbert Blandes amepita bila kupingwa na anajitoea, kwa hiyo, nafasi zile mbili zinabakia na Wabunge wawili katika Chuo Kikuu cha Mzumbe. Ilikubalika hapa hapa na mimi nikawa nimetoa hapa hapa. Sasa imebadilika ghafla, ndiyo maana nilikataa nikasema kwamba sasa sio busara kuendelea kupokea vikatarasi hivi kuja Mezani.

**MBUNGE FULANI:** Hatujaelewa!

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uchaguzi huu wa Mzumbe utabakia pale pale kwa maana ya wagombea wako watatu, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Umbulla na Mheshimiwa Mnyaa. Kwa sababu wanatakiwa wawili, mmoja mwanamke na mwingine mwanaume, Mheshimiwa Umbulla anapita bila kupingwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gosbert Blandes pamoja na Mheshimiwa Mnyaa watapigiwa kura.

**SPIKA:** Sasa, ngoja tuelewane hapa. Tunavyoona hapa, Chuo Kikuu cha Mzumbe walipita wote wawili bila kupingwa, ambao ni Mheshimiwa Umbulla na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa. Hebu eleza tena upya kwa utaratibu wasikie wote maana peke yangu haitoshi. Sasa, Mheshimiwa Blandes wewe uliomba Chuo Kikuu cha Ardhi, mlikuwa wewe pamoja na Mheshimiwa Susan Lyimo, tukasema amepita bila kupingwa. Kwa hiyo, mnachosema sasa unataka ugombea wapi tena?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba nilitumia haki yangu ya kidemokrasia kwa kujaza Vyuho Vikuu viwili.

**SPIKA:** Vitatu, vitatu!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, vitatu. Cha kwanza nikajaza *Open University* ambayo ndiyo nimesema nimejitoea hapa mbele. Cha pili,



nikajaza Chuo Kikuu cha Ardhi, nafasi zilikuwa mbili, tulipatikana wawili, tukapita bila kupingwa. Cha tatu nikaomba Chuo Kikuu cha Mzumbe ambacho mimi na Mheshimiwa Mnyaa tunakuja hapa kwenye kinyang'anyiro.

**SPIKA:** Aah, basi sawa. Sawa endelea. Kwa hiyo, kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutakuwa na wagombea wawili, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Mnyaa. Sawa basi umemaliza. Hakujieleza katika ile.

**NDG. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, inabidi sasa ajieleze kwa sababu tumepata ufafanuzi hapa Mezani, inabidi ajieleze na Mheshimiwa Mnyaa itabidi aje mbele.

**SPIKA:** Anajieleza chini ya Chuo cha Mzumbe.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge: mimi ni Gosbert Begumisa Blandes - Mbunge wa Karagwe kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nimekuja hapa kuomba ridhaa yenu niwe mwakilishi wa Bodi ya Chuo Kikuu cha Mzumbe. Kusema kweli uwezo wangu ni mkubwa sana wala msije mkaogopa kwamba huyu amepata nafasi mbili hatazimudu. Mimi kwa taaluma ni Mwanasheria, ni Wakili wa Kujitegemea, ninao uwezo wa kufanya kazi zangu kwa haraka sana.

Nimekuwa mtumishi wa Serikali, nimekuwa Mwanasheria wa Serikali kwa muda mrefu, nimekuwa Mwanasheria wa Benki ya *CRDB*, nimekuwa Mwanasheria wa Bodi ya *Architects and Quantity Surveyor*, mimi ni Mkurugenzi wa Bodi ya Mawakili ya *United Law Chambers*.

Waheshimiwa Wabunge, ninakusudia kuingia kule kutumia taaluma yangu ya sheria kwa sababu kama mnavyojua vyuo hivi tumevianzisha kwa sheria ya Bunge na sheria zinabadilika, zinakua. Nina imani kabisa kwamba mchango wangu nikiingia kule nitaweza kuleta mabadiliko ikiwa ni pamoja na kushauri mabadiliko (*amendments*) katika sheria hizi. Lakini, napenda kuwahakikishia, nikiwemo mle kwenye Bodi ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, hata ile migomo mnayoisikia ya wanafunzi, mwarobaini wake uko hapa. Kwa heshima kubwa na taadhima naombeni kura zenu wote. Asanteni sana. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Maswali! Mheshimiwa Khalifa!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kumwuliza mgombea, moja katika jambo tunalolijenga hapa ndani ya Bunge ni umoja na mgawanyo wa madaraka. Kwa kuwa yeye ameshapata nafasi moja ya kuliwakilisha Bunge hili katika chuo, haoni ni busara ya kawaida tu na hapa akamwachia mwenzake ili tukawa na uwakilishi mzuri Bungeni? (*Makofi*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Khalifa kwa swali lake zuri sana. Suala la kugombea siyo suala la kuachiana madaraka tu, unaangalia na uwezo wa nafasi ya mtu anayoigombea.

Mheshimiwa Spika, nafasi hii ninayoigombea kusema kweli ukinilinganisha na Mheshimiwa Mnyaa, uwezo wangu ni mkubwa sana kuliko wa Mheshimiwa Mnyaa.

**SPIKA:** Hapana! Namna hiyo siyo sawa sawa! Hiyo siyo sawa Mheshimiwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Blandes katumia nafasi yake ya Kanuni kuomba nafasi zaidi ya moja. Sasa swali langu ni hili, ikitokea kwa mfano, kuna vikao viwili vinafanyika wakati mmoja, utafanya nini ili kuwakilisha vizuri Bunge letu?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa swali lake zuri. Unapokuwa kwenye vikao, mimi bahati nzuri nimekuwa Sekretari wa Bodi mbalimbali. Kwenye vikao mnakuwa na kalenda, mnakuwa na utaratibu wa vikao vya mwaka. Ninyi wajumbe mnapokuwa mle mnaangalia kwamba ni tarehe zipi ambazo wajumbe mna nafasi. Kwa hiyo, nikiwa kwenye Bodi moja wakati napanga kalenda ya vikao vingine, nitashauri kwamba tarehe hii ibaki wazi kwa ajili ya kikao kingine. Kwa maana hiyo, siyo rahisi vikao vyote vikagongana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mgombea kwa kuwa una majukumu mengi, huoni kwamba utashindwa kutekeleza majukumu yako kwa kazi nyingi zitakazokuzonga? Majukumu mengi uliyonayo ambayo umetueleza na hayo unayoomba yatakuwa ni mengi mno, utashindwa kuyatekeleza. Je, unasemaje juu ya suala hilo?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, wakati ninakusudia kuchukua *form* hii kwanza nilijipima majukumu yangu ni yapi niliyonayo na uwezo wangu nilionao. Jukumu kubwa sana nililionalo mimi ni Mbunge wa Jimbo la Karagwe. Ninayo ratiba yangu ya kufanya shughuli zangu Jimboni. Kwa hiyo, siyo kwamba nina majukumu makubwa sana. Ni jambo la kawaida hata hapa tulipo Waheshimiwa Wabunge, unakuta mwingine ni Waziri, unakuta mwingine ana shughuli kwenye Chama chake, lakini pia mambo yote yanakwenda vizuri sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, muda wangu najua kuu-*manage* vizuri sana kama nilivyokwambia, taaluma yangu mimi ni Mwanasheria, kwa hiyo usiwe na wasiwasi nitakuwakilisha bila wasiwasi wowote.

**SPIKA:** Haya, maswali yamekwisha. Omba kura zako, halafu uende ukachukue nafasi yako.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima kubwa naomba kura zenu nyote, msiwe na wasi wasi, uwakilishi wangu utakuwa mzuri na nyie mtafurahia matunda yangu, mtayaona hapa Bungeni.

**SPIKA:** Asante. Kwa hiyo, tunamwita Mheshimiwa nani sasa?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa chuo hicho hicho tumwite Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa aingie. Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa, tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali, basi hayatazidi matatu. Endelea.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa jina naitwa Mhandisi Mohamed Habib Mnyaa. Nimesimama hapa kwa kugombea nafasi ya uwakilishi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote: nimesimama hapa kuomba kura zenu. Kitaaluma kama mlivyosikia ni Mhandisi, nina Shahada ya Chuo Kikuu (*Engineering*), nina Stashahada ya Udhamili ya Chuo Kikuu cha Norway na Stashahada ya Uongozi, Sweden. Nina uzoefu wa kazi Serikalini miaka 15. Nimeshawahi kuwa *Project Manager* wa Usambazaji Umeme Vijijini Zanzibar, kazi ambayo utumishi wangu uliotukuka unakumbukwa mpaka leo na shughuli nyingi sana.

Sina haja ya kujieleza sana, nina uwezo kamili wa kuliwakilisha Bunge katika Bodi hii ya Chuo Kikuu cha Mzumbe. Kwa kuzingatia umoja wa Kitaifa, inafaa na Bodi za huku uweko uwakilishi kutoka Zanzibar. Nafikiri katika muundo wa sasa hivi kwa kuzingatia ule umoja na ushirikiano ambao tunauhitaji, nadhani na nina hakika Waheshimiwa Wabunge mtanichagua kwa sababu kazi yangu nyote mmeijua.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maswali?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali. Kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la wanafunzi kugoma katika Vyuo Vikuu na wanalazimika kugoma kwa sababu wanadai haki zao: Je, yeye kama mjumbe wa Bodi hiyo atawasaidiaje wanafunzi hao wasifukuzwe na waendeele na masomo pale wanapolazimika kufanya migomo kudai haki zao?

**MHE. MOHAMED H.J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali zuri sana. Swali kama hilo leo asubuhi ndiyo maana nikasimama kwa swali la nyongeza nikaomba hiyo Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais ipate muda ije ionane na Wabunge wote hapa Bungeni kwa sababu sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi na masuala ya wanafunzi yanatugusa sana na tunapata kero hizo nyingi sana, ili tuje tusaidie ushauri kwa hiyo Tume. Kama watafanya hivyo, sawa. Lakini kama hawatafanya hivyo, huko tutakakokwenda, kwa kutumia uzoefu wangu hasa wa miaka ya 1979/1980 wa hali ilivyokuwa na masomo na tofauti iliyopo leo, ndiyo nitatumia uzoefu wangu huo kuishauri hiyo Bodi na wenzangu ili kulifikisha suala kunakohusika.

**SPIKA:** Ahsante. Swali la pili, Mheshimiwa Sungura!

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumwuliza mgombea swali moja lifuatalo:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la wanafunzi wa Kitanzania kulipishwa pesa za kigeni wakiwa katika nchi yao, hasa hasa ada na *fees* nyingine, wamekuwa wakilipishwa *US Dollars*.

**SPIKA:** Samahani, wanafanywaje?

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Wanalipishwa fedha za kigeni na wakati wao ni Watanzania.

**SPIKA:** Wapi huko?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Vyuho Vikuu vya Tanzania. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Zanzibar *University* watu wanalipa *in terms of US Dollars*. Sasa suala hili wanafunzi imekuwa ni kero kubwa kwao kwa sababu ukija katika ku-*convert* ile pesa inakuwa ni pesa nyingi sana. Kama mwakilishi, utatusaidiaje juu ya hilo?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nafasi ninayogombea ni Chuo Kikuu cha Mzumbe na kama liko tatizo hilo, nitajitahidi huko na naamini Chuo Kikuu cha Zanzibar wako wenzangu wanaogombea nafasi hizo na tatizo hilo nao wameshalisikia, tutasaidiana kushauriana kwa kila mtu upande wake kutatua tatizo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho! Hakuna. Mheshimiwa Mnyaa, ahsante, hakuna maswali tena.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mara nyingine tena, kama nilivyosema, naomba kura zenu kupata uwakilishi mzuri wa kimuungano. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea. *Returning Officer!*

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania sasa.

**SPIKA:** Anayepaswa kuingia nani?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Tutamwita Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa kwa sababu Mheshimiwa Blandes amejitoa hapa hapa wakati anajieleza.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa aingie. Tunakupa dakika tatu za kujieleza na iwapo kutakuwa na maswali, hayatazidi matatu. Hebu endelea.

**WABUNGE FULANI:** Simama! (*Kicheko*)

**MHE. ZAINAD R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesimama, ahsanteni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Upinzani, Waheshimiwa sana viongozi wenzangu, Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Asalaam aleikhum. Wazee wangu shikamooni. Niliyesimama hapa ndiye Zainab Rashid Kawawa, ni Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukue nafasi hii kuwashukuru kwa kunikubalia kuomba nafasi ya ujumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria. Nianze kwa unyenyekevu mkubwa sana kwamba ninaomba kura zenu zote za ndiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa uchache tu kwamba Baraza hili la Chuo Kikuu Huria ndicho chombo kikuu kinachoendesha mambo yote ya Chuo Kikuu Huria na lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 Ibara ya 43.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni chombo cha maamuzi, wakati nafanya uamuzi wa kuwania nafasi hii nilizingatia uzoefu wangu wa kushiriki kwenye vyombo vya maamuzi na kutoa michango inayoleta manufaa kwenye vyombo hivi. Kama vipeperushi vyangu vinavyojieleza, mimi ni mzoefu niliyefanya kazi Serikalini kwa takriban miaka zaidi ya saba kwa nyadhifa mbalimbali. Nimekuwa Afisa Utumishi Mwandamizi, nimekuwa Afisa Utumishi, nimekuwa Afisa Pensheni, nimekuwa Mtafiti wa Kisayansi (*Research Scientist*), lakini, vile vile kwa kuheshimu elimu yangu, nimesomea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Masters of Business Administration* na *BA Sociology*. Kwa heshima na taadhima ninaomba kura zenu zote za ndiyo ili niweze kukitumikia chombo hiki muhimu.

**SPIKA:** Ahsante. Maswali! Mheshimiwa Anna Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize mgombea swali moja. Kwa kuwa kumekuwa na maandamano na migomo kutoka Vyuo Vikuu vingi sana, lakini hatujawahi kusikia maandamano wala migomo kutoka Chuo Kikuu Huria: Je, Mheshimiwa Zainab Kawawa, atatuhakikishia kweli kwamba atakwenda kudumisha nidhamu iliyoko kwenye Chuo Kikuu Huria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab, jibu!

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swali zuri. Labda nitoe kwa ufahamu tu tofauti ya Chuo Kikuu Huria na Vyuo Vikuu vingine. Chuo hiki kinafundisha katika mazingira huru zaidi, hasa kina-*base* kwa wale watumishi. Ni vigumu sana kwa watumishi, mtu anayefanya kazi halafu anakwenda darasani eti

kujiunga kwenye migomo, hasa ukizingatia kwamba sababu zenyewe za wanafunzi kugoma wanaigomea labda Serikali haijawapa pesa ya chakula, wanataka iwaongezee.

Lakini ni *rare* sana kwa wanafunzi hawa wa Chuo Kikuu Huria ambao unakuta labda, tunao Wabunge hapa ambao wamekuwa wanasoma kwenye Chuo Kikuu Huria, sidhani kama wao wanakuwa *sponsored* na Serikali, sidhani kwamba wao wanaweza wakajiingiza kwenye migomo. Lakini, niseme tu kwamba endapo nitakuwa mjumbe wa Baraza hilo, nitaendelea kusimamia ustawi wa Chuo hicho, nitaendelea kusimamia nidhamu ya wanafunzi pamoja na *staff* waliopo pale. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la tatu, hakuna. Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa tunashukuru, unaweza ukaenda kuchukua nafasi yako ukakaa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kura zenu zote za ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali, basi hayatazidi matatu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu: Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa kunipitisha bila kupingwa kuwa Mwakilishi wenu wa Chuo Kikuu cha Ardhi. Nafasi hii mlinipa katika kipindi kilichopita na niliwawakilisha vizuri na ninaamini nitaendelea kuwawakilisha vizuri. Ninaomba ushirikiano wenu na ninawashukuru sana, Mungu awabariki. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kusema kwamba nimejitoa katika nafasi ya uwakilishi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa sababu nimeona kuna mwanamke mwenzangu na ninaamini ana uwezo, kwa hiyo, nimeamua kumwachia nafasi hiyo ili mumpatie kura.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumwomba Mheshimiwa Zainab Kawawa kura ili awe mwakilishi wetu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wabunge ndani ya Bunge hili, kwa hiyo, ameanza kuonesha uwajibikaji wake, ahsante sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa amepita. (*Makofi*)

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Suzan kujitoa na Mheshimiwa Gosbert Blandes, wanabakia wagomba watatu kwa nafasi ambazo zinazingatia jinsia na Muungano.

**SPIKA:** Kwa hiyo, hawa wote wamepita.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa Wabunge waliobakia wana sifa kwa mujibu wa matakwa ya Chuo, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa ni Mbunge Mwanamke, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba anatoka Jimbo la Dole, ni upande wa Pili wa Muungano na Mheshimiwa Henry Shekifu anatoka upande mwingine wa Muungano. Kwa hiyo, wana *qualify*.

**SPIKA:** Ahsante. Kwa hiyo, wajumbe wetu hapa ni Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba na Mheshimiwa Henry Shekifu. Tuendelee.

### **CHUO KIKUU CHA SAYANSI ZA AFYA MUHIMBILI**

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika tunaendelea na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya cha Muhimbili. Wagombea wapo wanne, nafasi ziko mbili, moja kwa Mbunge Mwanamke na moja kwa Mbunge Mwanaume. Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasikila aingie. Mheshimiwa Kasikila wewe umepita bila kupingwa kwa sababu upo peke yako. Anayefuata. (*Makofi*)

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa heshima na taadhima, nimesimama mbele yenu nikiomba mnichague niwe mwakilishi kwenye Bodi ya Chuo Kikuu cha Muhimbili.

Jina langu naitwa Dr. Hamis Andrea Kigwangwala, ni Mbunge wa Jimbo la Nzega nimebahatika kuwa na elimu ya *degree* tatu.

*Degree* ya kwanza ni ya udaktari wa tiba za binadamu ambao nilipata kutoka Chuo cha Muhimbili na *degree* yangu ya pili ni ya Afya ya Jamii ambayo nilipata katika Chuo cha Caroliska *Institute* kilichopo nchini Sweden, *degree* yangu ya tatu ni *Masters in Business Administration* ambayo nilipata nchini Sweden kutoka Chuo cha *Black Institute of Technology* na nimebahatika kufanya kazi katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili kama Daktari Mfawidhi lakini pia nimefanya kazi katika mashirika mbalimbali na katika *organisation* mbalimbali kama mshauri wa kitaalamu kuhusiana na mambo ya *Health Systems*, mambo ya *Infectious Diseases* na mambo ya *Health Management*.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka ya Bodi na madaraka iliyonayo, Bodi ya Muhimbili ninajiona nina uwezo na sifa stahiki za kuweza kukabili mikikimikiki ya zama tulizopo ukizingatia mimi nimesoma katika chuo hiki, ninafahamu historia ya Chuo changu lakini zaidi ya yote nilipata fursa ya kuwa Rais wa Serikali ya wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Muhimbili na kwa nafasi yangu kama Rais wa Serikali ya wanafunzi nilipata fursa ya kuteuliwa na Waziri wa Sayansi na Elimu ya Juu, enzi hizo Dr. Pius Mwandu

kuwa Mjumbe wa Bodi ya Utawala wa Chuo cha Muhimbili kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kwa hiyo, majukumu, kazi za Mjumbe wa Bodi ya Muhimbili ninayafahamu kwa sababu nimewahi kufanya kazi ya Mjumbe wa Bodi, lakini sio hivyo tu, pia nimepata fursa ya kuwa Mjumbe katika Bodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ni Mjumbe wa *International Cotton Association* nikiwa nawakilisha Afrika nzima kutokea *private sectors*. Mbali na hivyo, pia ni Mjumbe wa *International Safe Communities Network* ambayo ina Makao Makuu yake Chuo Kikuu cha Caroliska pale *Stockholm*, pia ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya *TCA*.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba nina uwezo na uzoefu wa kutosha wa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Chuo Kikuu cha Muhimbili. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Maswali kwa mara ya kwanza, mara ya pili, na kwa mara ya tatu. Ahsante Dr. Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kura zenu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Kebwe tunakupua dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali, basi hayatazidi matatu. Naomba uendelee.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Wabunge wenzangu: Aliyesimama mbele yenu ndiye Dr. Kebwe Stephen Kebwe, ni Mbunge wa Jimbo la Serengeti.

Mheshimiwa Spika, niwape *profile* yangu kwa kifupi. Mimi ni Daktari wa Binadamu. *Degree* ya kwanza niliisomea Muhimbili, *degree* ya uzamili nisomea *KCMC* lakini pia nimewahi kufanya kazi kama Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bunda miaka 12; nimekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara kwa muda wa miaka miwili na pia nimekuwa Mganga Mkuu wa Kagera kwa muda wa takribani miezi sita. Lakini sio hilo tu, wakati nikiwa Naibu Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Bungando ambayo ni hospitali kubwa ya pili hapa nchini, nimekuwa nafanya kazi ya kufundisha Chuo Kikuu cha Madaktari pale Bugando nikiwa *full time Lecturer*, lakini baada ya kuingia katika masuala mazima ya siasa, mimi bado ni Mhadhiri kwa vipindi, *Visiting Lecturer* wa Chuo Kikuu cha Bugando cha Madaktari.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kikubwa zaidi, mimi nikiwa Chuo Kikuu cha Muhimbili nimekuwa mwakilishi wa wanafunzi, nimekuwa mwakilishi wa Wanafunzi, nimekuwa Waziri wa Elimu ambapo imeniwezesha mimi kuhudhuria vikao mbalimbali vya maamuzi kusaidia uongozi wa Chuo ikiwemo *Faculty Body* na wakati ule *transition*



ya Chuo Kikuu kishiriki cha Muhimbili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nilikuwa ni mwakilishi wa Bodi ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu, nimekuwa Mjumbe wa Bodi ya Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa suala la uzoefu wa masuala haya ya Uongozi, Chuo na Taaluma ni kama unamchukua samaki unamrudisha kwenye maji, hilo mimi sina shaka nalo kwa sababu hata kufanya kazi za kushauri nje ya nchi nimefanya hivyo nikiwa Mganga Mkuu Wilaya ya Bunda, nimefanya kazi na *WHO* nikitumwa na nchi yangu ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya kushauri nchi ambazo ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara juu ya Mfumo wa huduma ya afya hususan ubora katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa suala zima la uzoefu wa shughuli za kushauri na kufanya kazi ndani ya Wizara ya Afya pamoja na Vyuo Vikuu, naomba ndugu zangu nipeni kura samaki arudi kwenye maji. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Swali kwa mara ya kwanza, swali kwa mara ya pili, Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, mgombea moja ya matatizo ambayo tunayo makubwa sana hivi sasa ni migomo inayoendelea karibia vyuo vyote. Kama tutakupua nafasi hii ya kuwa mwakilishi wetu pale utafanya nini au utakwenda na nini cha kusaidia ili kuzuia mambo haya yasitokee?

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru mwuliza swali kwa swali zuri kabisa ambalo ni kweli wote tunafahamu kuna changamoto kubwa na masuala ya migomo ambayo yanaendelea nchini. Lakini kubwa zaidi, ina maana kwamba ukiimarisha mawasiliano mazuri kati ya Uongozi wa Vyuo pamoja na Jumuiya ya Wanafunzi ni sehemu nzuri na ngazi nzuri ya kujikita kwa sababu wakati mwingine *payment* za Vyuo hivi zinaweza kuona kwamba kama uongozi wa wanafunzi ni maadui fulani, wanakata mawasiliano. Kwa hiyo, kubwa zaidi, cha kuanza nacho ni kuimarisha suala la mawasiliano kati ya uongozi wa Vyuo pamoja na Wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika uzoefu wangu, mimi nilishiriki vizuri kwa uzoefu huo kwa kupata *Ad hoc Committee* kuangalia *mass failure* katika Chuo Kikuu cha Muhimbili jambo ambalo lilisaidia kuleta mazingira rafiki ambayo tunaona leo hii ya masomo yanapokuwa yanafundishwa unakuta kuna *weekly test* lakini baada ya hapo tukapata *semesters* ambazo zilianza katika juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kushirikiana na Serikali na wakati ule mnakumbuka ikiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sheria ya kuanzisha Chuo Kikuu alitakiwa kuonana na Rais wa nchi, kwa hiyo, mara kwa mara tumekwenda Ikulu kushauriana juu ya masuala mazima ya mikopo na namna ya kuanzisha malipo katika Vyuo Vikuu hapa nchini.

**SPIKA:** Swali la mwisho. Hakuna. Mheshimiwa Dr. Kebwe chukua nafasi yako.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Ahsante sana. Naomba kura zenu kwa heshima na taadhima.

**SPIKA:** Ahsante. Anayefuata.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, anayefuata ni Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali, basi hayatazidi matatu.

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nilikuwa ni mmoja wa walioomba kugombea nafasi ya uwakilishi wa Bunge katika Chuo cha Afya na Sayansi ya Jamii Muhimbili, lakini ninaomba nijitoe katika nafasi hiyo nikiamini kabisa waliobaki wana uwezo na vigezo vya kuweza kutuwakilisha vyema, ila nitaomba nifikiriwe katika nafasi ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaweza kuendelea. Tumemaliza katika nafasi hii, tunao wagombea Mheshimiwa Dr. Hamis Kigwangalla na Mheshimiwa Dr. Kwebwe Stephen Kebwe. Kwa hiyo, tunao wawili nafasi moja. Tuendeleo kwa nafasi nyingine.

#### **CHUO CHA KUMBUKUMBU CHA MWALIMU NYERERE**

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa tunakwenda Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambapo kuna wagombea wawili na nafasi ni moja. Yupo Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile.

**SPIKA:** Kama nilivyosema, tunakupa dakika tatu za kujieleza. Kama kutakuwa na maswali hayatazidi matatu. Endelea.

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru tena kwa kunipa nafasi hii, Waheshimiwa Wabunge naitwa Dr. Faustine Ndugulile - Mbunge wa kuchaguliwa kwa Chama cha Mapinduzi Jimbo la Kigamboni. Chuo ambacho nakiombea kipo katika Jimbo langu la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, ninaamini nina uwezo na kila sababu ya kuweza kuwa mwakilishi mzuri wa Bunge hili Tukufu katika taasisi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, naomba kura zenu ili niwe mwakilishi katika taasisi hii.

**SPIKA:** Ahsante. Kuna swali? Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:**Mheshimiwa Spika, Mgombea amesema anaweza, lakini kwa dalili zake za kuomba sehemu mbili na ghafla kujitoa atatuthibitishia vipi kuonekana kwamba ni mtu ambaye yuko *focused*?

**SPIKA:** Akijitoea nongwa! Akibakia nongwa. (*Kicheko*)

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE:**Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa swali zuri ambalo ameuliza Mheshimiwa Msigwa. Hii ni katika kupanua demokrasia na katika vyuo vyote viwili nilikuwa na sifa na vigezo vya kuwa mwakilishi mzuri, lakini niliona kwamba sio busara na hekima kuwa nahodhi nafasi mbili zote kwa wakati mmoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:**Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa mgombea anaomba kwenda kuongoza katika Chuo cha Uongozi na kwa kuwa maadili ya Uongozi yanaharibika katika maeneo mengi hata kwetu sisi Wabunge kiasi cha kwenda hata kupekuapekua *documents* katika maeneo: Je, utatusaidia vipi sisi katika Bunge letu na maeneo mengine?

**SPIKA:** Swali hilo silikubali. Swali la tatu, hakuna. Mheshimiwa chukua nafasi yako, tuendeleo na anayefuata.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, anayefuata ni Mheshimiwa Musa Haji Kombo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musa Haji Kombo aingine ndani. Tunakupa dakika tatu za kujieleza, halafu tutakuuliza maswali kama yapo yasiyozidi matatu.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote: Mimi ni Mbunge kutoka Jimbo la Chakechake kwa Chama cha Wananchi (*CUF*). Nimekuwa nikikamata madaraka makubwa sana katika Chama cha CCM wakati kilipokuwa chama kimoja. Nilikuwa ni mwanafunzi wa Chuo hiki ambacho tunapiga kura. Nimetembezwa katika vyuo vingi sana katika nchi za nje wakati kuna *East and West Block*. Nimekuwa Urusi, Bulgaria na nchi nyingine.

Kwa hiyo, heshima ya kutaka kumuezi na kutazama heshima ambayo Mwalimu Nyerere alitufanyia nikaona ni bora niombe nafasi hii niwe mwakilishi wenu katika chuo kile. Bahati mbaya sana Wabunge wengi hawana nafasi ya kuamua wenyewe. Sisi sote ni watumwa wa vyama.

Mimi ni mtumwa wa Chama changu cha *CUF*, wengine watumwa wa Chama cha CCM, wengine CHADEMA, hawa hawana uwezo wa kuamua zaidi ya *three lines*. Sasa mimi nasema, nimekuja kuwakilisha kwamba natoka katika Chama kimoja, mtumwa wake. Sasa wenzangu nawaomba kama hamtakuwa watumwa wa vyama vingine, naomba kura zenu. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya shauri yenu, ninyi watumwa. Je, kuna mtu anataka kuuliza swali? Mara ya kwanza, mara ya pili, mara ya tatu? Mheshimiwa Mussa Haji Kombo ahsante, ukachukue nafasi yako.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Bado naendelea kusema watumwa wenzangu wa vyama, nawaomba kama mtakuwa na uamuzi, nipeni kura zenu.

### **CHUO CHA UFUNDI ARUSHA**

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunakwenda Chuo cha Ufundi Arusha, wagombea wako watatu. Wa kwanza ni Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani.

**SPIKA:** Aje kwanza Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani. Hapa ni nafasi moja tu ndio inayotakiwa.

Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani tunakupua dakika tatu uweze kujieleza na iwapo yatakuwepo maswali, basi hayatazidi matatu. Naomba uendelee.

**MHE. ENG. RAMO MATALA MAKANI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wote: Asalaam aleikum, Bwana Yesu asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo.

Mheshimiwa Spika, jina langu ni Eng. Ramo Makani, nimesimama hapa kwa ajili ya utaratibu wa kujieleza katika kugombea nafasi ya uwakilishi kwenye Chuo cha Ufundi Arusha (*TCA*). Lakini napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge ndani ya jengo hili kwamba licha ya kujaza fomu ya kugombea nafasi hiyo kwa Chuo cha Ufundi Arusha, mimi pia nimejaza fomu kwa ajili ya kugombea nafasi kama hiyo kwenye Tume ya Vyuo Vikuu Nchini (*Tanzania Commission for Universities TCU*).

Sasa baada ya kuangalia vizuri na kwa ukaribu nafasi zote hizo mbili na kuzingatia ufanani wake wa majukumu yake na tofauti zilizomo na kwa kuzingatia kwamba ile ambayo ni ya *TCU* inabeba kwa ndani hii nyingine ya (*ITC*) ya Chuo cha Arusha kwa sababu ile nyingine ni kwa ajili ya vyuo vyote vikuu, naomba kuchukua nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, kwamba naomba wakubali kwamba kura zote zile ambazo ilikuwa wanipigie kwa ajili ya nafasi hii ya Chuo cha Ufundi Arusha, sasa wasizipige kwa ajili ya nafasi hii, bali wazihamishe kura hizo waje wanipigie wakati nitakapokuja kusimama kwa nafasi ya Tume ya Vyuo Vikuu nchini.

**SPIKA:** Kwa maelezo mengine, umejitoe katika Chuo Kikuu cha Ufundi Arusha.

**MHE. ENG. TAMO MATALA MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Aje, mwingine.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ENG. TAMO MATALA MAKANI:** Nafasi hizi zinafuatana, nilitaka kujua kama nitapaswa kutoka nje na kusubiri kuitwa tena kwa ajili ya maelezo kwenye ile nafasi ya mwisho ama naweza kuendelea kukaa humu ndani.

**SPIKA:** Kwa sababu ya kuchanganya watu, tunaomba utoke nje, tutakuita kwa nafasi hiyo. Aje mwingine anayefuatia.

Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, tunakupua dakika tatu za kujieleza, halafu kama kutakuwa na maswali, basi hayatazidi matatu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliyesimama hapa naitwa Rajab Mbarouk Mohamed, nimesimama hapa kuwaomba ridhaa yenu kwa ajili ya kuliwakilisha Bunge letu hili Tukufu ili niweze kuliwakilisha Bunge katika Chuo cha Ufundi cha Arusha. Nina uwezo, niko makini na niko tayari kuwa mwakilishi wenu katika Chuo kile.

Nasema hivyo nikiwa na sababu moja kuu. Mimi ni mmoja kati ya matunda mazuri ambayo yametokana na vyuo kama vile. Yaani nimetokea katika chuo cha Ufundi cha *Karume Technically College* kilichoko Zanzibar ambacho mitaala yake, mafunzo yake na kila kitu chake ni sawa na Chuo hiki ambacho kiko Arusha.

Mbali ya hayo, katika kipindi cha miaka isiyopungua 20 vile vile ni mdau katika sekta nzima ya ufundi ambapo nimeweza kupokea wanafunzi wanaotoka vyuo kama hivi kwa ajili ya kuwapa mafunzo. Kwa hiyo, ninaamini kwamba niko tayari na nina uwezo wa kuweza kuliwakilisha Bunge pale na kushughulikia matatizo ya wanafunzi ambayo yako pale hususan katika kuwajengea uwezo wao, lakini vile vile kuweza kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kura, pale niliomba ridhaa. Waheshimiwa Wabunge akina mama, mna lugha huwa mnasema kwamba mkitaka mnaweza. Sasa mmedhirisha moja la Spika, tunataka leo mlidhirishie tena Bunge hili kwamba mnaweza kwa kunipa zenu zote.

Lakini vile vile kwa kutumia fursa hiyo hiyo ya kwamba mnaweza kila mmoja ageuke amtazame mwanamume amwambie kwamba naomba kura yako umempelekee Mheshimiwa Rajab. Lakini akina baba vile vile Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba na ninyi mna sauti simba ya kuunguruma. Mwanamke kawaida yake anavyosikia sauti kama ile kidogo huwa anarudi katika hali yake ya chini muitumie nafasi hiyo vile vile kuniombea kura kwa Wabunge wenzangu. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Swali kwa mara ya kwanza, mara ya pili, mara ya tatu. Basi kwa mara nyingine Mheshimiwa Rajab Mohamed, ahsante sana. Chukua nafasi yako.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kifungu cha 28 (5) napenda kuongeza muda ili tuweze kupiga kura halafu twende zetu kwa ajili ya kupumzika, kwa sababu tusipofanya hivyo tutachanganya majina. Kwa hiyo, tunaongeza dakika 30.

Mheshimiwa George Boniface Simbachawene tunakupa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuweco na maswali, basi hayatazidi matatu. Naomba uendelee.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza niwashukuru sana kwamba kipindi cha miaka miwili nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha na bahati nzuri historia yangu ni kwamba nilisoma Chuo kile mwaka 1989 hadi 1991. Kwa kuwa kuna mambo ambayo tulikuwa tumeyaanza katika kipindi cha miaka miwili baada ya kukipa kile Chuo *autonomous* nilidhani ni busara wenzangu mkaniamini na kunirejesha tena katika kile Chuo ili tuweze kwenda kuyaendeleza yale tuliyoanza.

Kwa maneno haya na kwa imani mliyonipa kipindi kilichopita na kwa sababu kazi zile ni endelevu, bado nahisi kwamba mchango wangu unahitajika na wenzangu niliokuwano kule, wameendelea kuniomba na ndio sababu jana nikatoa jina langu kwenye Kamishna. Kwa sababu hiyo, naombeni wote kura zenu.

Mheshimiwa Spika, naomba kura yako, Mheshimiwa Waziri naomba kura yako, Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla naombeni kura zenu. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Swali.

**WABUNGE:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Simbachawene, basi chukua nafasi yako.

#### **TUME YA VYUO VIKUU VYA TANZANIA**

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Tunakwenda Tume ya Vyuo Vikuu vya Tanzania, wagombea ni wawili, nafasi ni moja, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, tunakupa dakika tatu za kujieleza. Halafu kama kutakuwa kuna maswali, basi hayatazidi matatu. Naomba uendelee.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa sana Wabunge. Kwa jina mimi naitwa Luhaga J. Mpina. Ukiwa Kisesa wananiita Lechimije Mwanakengela. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niko hapa mbele yenu nagombea nafasi ya Tume ya Vyuho Vikuu (*Tanzania Commission for Universities TCU*) ninayo *Bachelor of Accounting and Finance*, ninayo *Masters of Science in Finance*, kwa hiyo, nina uwezo mkubwa wa kutekeleza hili jukumu langu la uwakilishi wenu katika taasisi muhimu sana ya Vyuho Vikuu (*TCU*). Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima sasa nimesimama hapa leo mbele yenu kuwaombeni mniwahishe kule Chuoni, kule *TCU* najua matatizo yaliyoko katika Vyuho kwa sasa. Nitumeni tena. Mlinipa miezi miwili tu Bunge likavunjwa, sikuwa na nafasi hata ya kufanya uwakilishi wa aina yoyote. Kwa hiyo, leo nimekuja kwa heshima na taadhima kuwaomba sasa mniwahishe. (*Makofi*)

Ukiona jina la Mpina, najua litakuwa namba moja, wameweka namba moja, wasimamizi wanajua kabisa ni namba moja. Kwa hiyo, ukiona pale wewe weka vema kubwa. Niliwaambia kipindi kile wekeeni vema kubwa iliyotiliwa mashaka. Leo pale mbele ya Mpina, weka shwaa! Shwaa! Unamwangalia na jina anavyoiweka ile Shwaa!

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nawaheshimu sana, najua sasa hivi mtachagua wawakilishi wengi wa kwenda kwenye vyuo mbalimbali. Mimi nikiwa kama kiongozi sasa ambao mnanituma kwenda *TCU* nitawatumia sana hawa viongozi ambao leo mtawachagua kwenda kwenye hizo taasisi, waliokwenda Muhimbili na kadhalika. Sasa hawa ndio tutakuwa tunakaa nao kuona namna gani tunaweza kumaliza migogoro iliyoko Vyuho Vikuu sasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa heshima na taadhima naomba kura zote za *TCU* bila mashaka yoyote mpeni Mpina. Ahsante sana.

**SPIKA:** Kuna mwenye swali?

**WABUNGE:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina chukua nafasi yako.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mgombea wa mwisho wa kujieleza atakuwa Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani aingie. Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, tunakupa dakika tatu za kujieleza halafu tutakuuliza maswali yasiyozidi matatu kama yapo.

**MHE. ENG. RAMO MATALA MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote. Nilisimama hapa punde tu, na nadhani bado mnakumbuka kile nilichosema kwamba niliwaomba kura zenu zihamie kwenye nafasi hii ya uwakilishi kwenye Tume ya Vyuho

Vikuu. Naomba awali kabisa nitangulize kuomba kura kwenu halafu baadaye niseme kwa nini nastahili.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuu Vikuu ndiyo chombo mwanvuli au *umbrella organisation* ya Vyuu Vikuu vyote nchini zikiwemo Taasisi za Elimu ya Juu ambavyo sio Vyuu Vikuu. Maana yake ni kwamba ukizungumzia taaluma achilia mbali kote unakotoka kule kwenye msingi na ngazi nyingine, kwenye elimu ya juu, hiki ni chombo muhimu sana. Ndiyo chombo ambacho kinawezesha nchi ikaweza kupata wataalam tena sio wataalamu tu peke yake bali wataalamu walio mahiri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi yetu ni mojawapo kati ya nchi tano zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni mpya tu. Maana yake ni kwamba tumeingia kwenye ushindani pia. Taaluma na utaalamu ni mojawapo ya maeneo ya ushindani. Kwa hiyo, kila mtu anaweza kuona umuhimu wa chombo hiki tunachokizungumzia.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mhandisi kwenye taaluma yangu ya Uhandisi, nimefanya kazi kama Naibu Msajili wa Bodi ya Usajili ya Wahandisi kwa miaka kadhaa, lakini bado pia kupitia chombo cha wataalamu Tanzania, *Tanzania Association Of Professional Organisations* nikiwa kama Katibu Mtendaji, niliweza kufanya kazi za kusimamia taaluma na utaalamu kama ambavyo inaonekana kwenye karatasi yangu ya maelezo. Kuna vipeperushi ambavyo naamini viko katika kila *desk* kule ambako wako Waheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, bila kuwachosha sana, naomba nimalizie kwa kusema nitashirikiana au nitawakilisha Bunge katika kuhakikisha kwamba kwanza jukumu kubwa kabisa la chombo hiki cha kusajili baada ya kukidhi viwango Vyuu mbalimbali nchini, nashiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba jukumu hili linakamilika.

Ninayo taarifa juu ya usajili wa *MIST*, Chuo chetu cha Mbeya kile ambacho Mwalimu Nyerere alikipigia chakuo sana kwamba kifikie wakati kisajiliwe kuwa Chuo Kikuu, lakini pia hata hotuba ya Mheshimiwa Rais ya juzi imesisitiza pia juu ya hilo. Nitasimama kidete katika kuhakikisha kwamba kwenye uwakilishi wangu, hayo yanakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimese juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nimeshiriki kama inavyoonekana kwenye kipeperushi kwenye uandishi wa Itifaki ya soko la pamoja hasa kwenye kipengele cha wataalam na taaluma, nimesema *Protocol* ile ya *mutual recognition of Academic and Professional Qualifications za East Africa*. Kwa hiyo, kwa ujuzi huo na utaalam huo na uzoefu nilioupata katika nyanja mbalimbali, naahidi kwamba mkinipa ridhaa kwa kura zenu nyingi ambazo naziomba kutoka kwenu wote, basi nitaweza kuhakikisha kwamba nawakilisha vizuri Bunge kwenye chombo kilicho muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuishia hapo, naomba kura.



**SPIKA:** Maswali mara ya pili? Maswali mara ya tatu. Waheshimiwa nashukuru, Mheshimiwa Eng. Ramo ahsante sana. Chukua nafasi yako. Waheshimiwa naona tumemaliza kuzungumza na wagombea sasa Vyuho Vikuu utakavyopigia kura kitakuwa Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Ufundi Arusha na mwisho Tume ya Vyuho Vikuu. Kadiri tunavyokwenda nitaeleza ni nafasi zipi za kupigia. Naomba hatua nyingine zifuatwe. Nadhani kwanza ipigwe kengele, halafu idadi ya Wabunge tuambiwe.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ile kauli yako ulitoa nakala chache Wabunge wengi hawajapata, tunaomba mfanye hivyo kipindi cha mchana. Halafu Katibu wa CHADEMA hapa Bungeni - Mheshimiwa Mnyika anawaarifu Wajumbe wa Kamati yake kwamba Kikao kile kilichopangwa kianze saa 7.00 sasa wamehamishia mpaka saa 9.00 kutokana na Kamati mbalimbali kuwa zinakutana. Mheshimiwa Mnyika anatangaza hivyo, tuwakumbushe.

Waheshimiwa Wagombea, mimi sina kura, kwa hiyo, mmeniomba hapa, sina kura. Kwa hiyo, msije mkakosa kura mkasema hata Spika ameninyima. Mimi sina kura. Tunaomba tufanye haraka, muda tuliojipa hautoshi.

Mheshimiwa Godbless Lema aliwasilisha utetezi wake kwa Spika kama ilivyoagizwa kwa maandishi. Kwa taarifa niliyonayo hapa, Wabunge waliopo humu ndani ni 230. Kwa hiyo, karatasi zigawiwe kwa haraka na msimamie kila *segment*.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tutaanza kugawa karatasi za Chuo Kikuu cha Dodoma na kura inayopigwa ni moja tu.

*(Hapa Karatasi za Kura Ziligawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Wale wa Masanduku wasogee.

**MBUNGE FULANI:** Karatasi.

**SPIKA:** Waonyeshe Wabunge kama yako *empty*. Ah! Sikusanyi, nasema waonyeshe kama yako *empty*. Hamjapiga kura? Ebu wasikilizeni huko.

*(Hapa Masanduku ya Kupigia Kura yalionyeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shibuda ungekaa, maana wewe sio *Returning Officer* na Mheshimiwa Serukamba nawe ungekaa. Kwanza Kanuni hairuhusu kuzurura humu ndani, maana mnazurura saa hizi. Hebu mkakae huko! Naomba muwasikilize hao wanaonyoosha mikono. Mgekuwa mnagawana maeneo mgejua namna ya kila mtu kuhudumia. Tayari mmepiga kura? Hamjapiga kura!

**WABUNGE:** Tayari.

**SPIKA:** Haya mkusanye. Kusanyeni kwanza hizo ndiyo muwape nyingine zitachanganyika. Nyeie mnaokusanya muende kwa *speed*, mko wangapi sijui. Makaratasi mengine mwandae sasa. Mnaokusanya hakikisheni mnakwenda haraka.

*(Hapa Karatasi za Kura Zilikusanywa)*

**SPIKA:** Nani bado ana karatasi? Eeh! Naomba mgawe nyingine, mgawe aina nyingine. Nyeie mnaogawa karatasi, sasa mgawe za Mzumbe.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunagawa sasa za Mzumbe na Mzumbe, wagombea ni wanaume tu kwa sababu na kura inapigwa moja, kwa wanaume tu. Kura ni moja kwa wanaume tu, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge Mwanamke amepita bila kupingwa. ni kwa wanaume tu.

*(Hapa Karatasi za Kura ziligawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Gaweni kwanza kusudi watu waweze kuelewa vizuri. Haya mgawe watatuambia. Wanaogawa jamani fanyeni haraka, muda wenu unaKWisha. Mgawane maeneo ya kugawa karatasi za kura. Wanaogawa kura wafanye haraka, naona eneo lile hakuna mtu. *Segment* ile haina mtu, ile ya nne, mkono wa kulia. Kwa hiyo, katika hizo karatasi jina la Umbulla hamlipigii kura. Hebu wewe nenda *segment* ile, nende *segment* ile, wewe nenda kule.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, samahani tumeongezeka wawili.

**SPIKA:** Nyeie mlikuwa watoro, kwa hiyo,... Ahsante. Mchukue nafasi zenu mkae. Mtatupa hesabu nyingine. Nyeie mnaokusanya mgawane sehemu za kukusanyia. Kwani ma-box yako mangapi? Anzeni kukusanya huko walioanza kupata kura.

*(Hapa Karatasi za Kura Zilikusanywa)*

**SPIKA:** Kinafuata Chuo Kikuu gani?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kinafuata Chuo Kikuu cha Sokoine.

**SPIKA:** Muandae kura za Sokoine.

*(Hapa kura zilikusanywa)*

**SPIKA:** Naomba muongeze spidi ya kurudisha kura. Chuo Kikuu cha Sokoine kuna maelezo yoyote ya ziada.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Chuo cha Sokoine inapigwa kura moja tu.

**SPIKA:** Malizeni kurudisha hizo kura za Sokoine, za sayansi ndiyo mnapewa sasa. Mnaogawa karatasi fanyeni haraka bwana. Anzeni kukusanya mnapeana mwingine anakwenda, siyo wote mwende sehemu moja. Abdallah unakwenda kule mbele. Mkizikusanya pamoja nyie wapiga kura nyie zikawekwa pamoja tutachukua muda mfupi zaidi.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, laini hii yote hatujapata hapa karatasi za kura.

**SPIKA:** Wapi? Nyie mnaogawa kura, mmewasikia, wapi hawajapata? Nyosheni mikono. Nyie mliochukua kura za Sokoine gaweni hapo. Naomba tukusanye upesi, maana yake kazi bado ndefu. Chuo gani kinafuata?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu kinachofuata ni Chuo cha Afya Muhimbili.

**SPIKA:** Muandae karatasi hizo na nyinyi mnaokusanya kusanyeni. Nani bado hajarudisha karatasi, mnaogawa mgawe karatasi zingine. Mgawane maeneo haraka kwa sababu muda bado. Naomba mfanye haraka, kila mtu si anagawa eneo lake, mbona naona mnagawa tu. Kukusanya za Sokoine kugawa zinagawiwa za Sayansi.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Naona kama kuna wengine walishajitoa hapa, labda wangetueleza.

**SPIKA:** Katika Sayansi?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwenye Sayansi.

**SPIKA:** Sawasawa tunaomba uwaelekeze watu. Mkigawiwa inakuwa vizuri kuelekeza.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwenye Chuo Kikuu cha Sayansi za Muhimbili wanapigiwa Waheshimiwa Wabunge wawili tu na ni wale kati ya Mheshimiwa Dokta Hamisi Andrew Kigwangala pamoja na Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, inapigwa kura moja tu kati ya hao wawili.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunafuta namba moja, maana yake amepita bila kupingwa. Namba ngapi tunafuta.

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Namba nne.

**SPIKA:** Na namba nne tunafuta?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunafuta namba moja na tunafuta namba nne halafu inapigiwa kura namba mbili na tatu, tunachagua mmoja tu. Tunasema hivi ukipata ile karatasi ya kura ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Sayansi hii ya Afya ya Muhimbili kama unayo, namba moja amepita bila kupingwa, kwa hiyo hatumpigii kura. Namba mbili anapigiwa kura Dokta Hamisi Andrea Kigwangalla anapigiwa kura. Anapigiwa Mheshimiwa Dokta Kebwe Kebwe, Mheshimiwa Dokta Faustine Engelbert Ndugulile, alifuta jina lake. Wanaotakiwa ni wawili, mwanamke na mwanamme lakini mwanamke amepita bila kupingwa, tunampigia mwanamme mmoja kati ya namba mbili na namba tatu. Tuko sawa? Mnaogawa karata changamkeni kidogo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kuna Rais wa Simba alikuwa ana mkutano na waandishi wa habari amerudi Bungeni. Kwa hiyo, tunaomba karatasi moja.

**SPIKA:** Anayeongea yuko wapi? Nyoosha mkono watakuona. Mnaogawa kura gaweni msilete sababishi.

**MBUNGE FULANI:** Huyu hapa amenyoosha mkono.

**SPIKA:** Sawa, Bwana Aden Rage. Nyeie mnaogawa karatasi kule nyuma kuna Bwana Aden Rage. Tukipunguza maneno itakuwa nafuu kidogo. Naomba mzikusanye pamoja. Ingawa nilipoongeza muda nilisema mpaka kazi hii iishe, basi kwa sababu Kanuni inasema dakika 30, basi naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi atoe hoja tuongeze muda mpaka tumalize kazi hii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu uliongeza dakika 30 kwa mujibu wa Kanuni ya 28 na shughuli bado hazijaisha, naomba nitoe hoja kwamba Bunge lako Tkufu likubali kuongeza muda hadi tutakapokamilisha shughuli inayoendelea sasa. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Ilitolewa na Kuamliwa)*

*(Bunge liliafiki utekelezwaji wa hoja iliyotajwa hapo juu)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo tutaendelea mpaka tupige kura, kwa sababu kuhesabu itachukua muda, tutakwenda kupumzika halafu matokeo mchana.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Kinafuta Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

**SPIKA:** Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Nyeie mnayegawa mngejipanga

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, karatasi ya kura moja huku hatujapata.

**SPIKA:** Zile za Sayansi? Kura ya Sayansi pale mmeonyeshwa mkono pale. Kura ya Sayansi kwanza pale. Nyie mnagawa zipi sasa? Mheshimiwa Bwana Warberg kura ya Sayansi iko wapi? Na pale kwa Mheshimiwa Dokta Maua pale. Kura ya Sayansi kwanza mmalize mtachanganya. Warberg kura ya Sayansi pale mstari wa Mheshimiwa Dokta Maua pale hawajapewa.

Kura ya Sayansi hapa hawajapata. Kura ya Sayansi hawajapewa pale, Mheshimiwa Dokta Daftari umepata? Nyie mnayekusanya si mngeenda kuchukua? Nyie *Page Girls* mkachukue kusudi muwape ya Chuo Kikuu cha Sayansi. Chukua kwanza karatasi, unachukua wapi sasa si ukachukue inayopigwa? Hawajapewa karatasi. Nimeshachoka. Nyie mnaogawa karatasi mngekuwa mnagawana maeneo kila mtu anafanya pale pale, mngewawana haya yasingetokea.

*(Hapa Karatasi za kura zilikusanywa)*

**SPIKA:** Mkiweka pamoja hawa watakwenda kwa spidi zaidi. Kwa hiyo Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, mnakusanya sasa. Nani hajapata karatasi? Wakusanyaji changamkeni. Kinafuata Chuo Kikuu gani? Wote tumekusanya? Chuo Kikuu gani kinafuata?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kinafuata Chuo cha Ufundi Arusha ambacho mgombea namba moja amejitoea, kwa hiyo tutapiga kwa kura namba mbili na namba tatu.

**SPIKA:** Naomba mgawe upesi, mkipata karatasi hizo tunapigia namba mbili na tatu. Namba moja alishajitoea. Hiki ni Chuo cha Ufundi Arusha. Tunampiga mmoja tu, majina yako mawili.

*(Karatasi zilianza kukusanywa)*

**SPIKA:** Muanze kukusanya huku, walioanza kupewa karatasi. Wote wamepata karatasi? Naomba mkusanye upande mmoja. Chuo kingine kinachofuata ni nini?

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Chuo cha mwisho ni, *I mean* Taasisi ni Tume ya Vyuo Vikuu.

**SPIKA:** Tume ya Vyuo Vikuu karatasi muandae.

*(Hapa karatasi za kupiga kura ziligawiwa)*

**SPIKA:** Tume ya Vyuo Vikuu majina yako mawili, kwa hiyo rahisi. Tume ya Vyuo Vikuu mmepata makaratasi? Anzeni kukusanya.

*(Hapa kura zilianza kukusanywa)*

**SPIKA:** Kuna mtu ambaye hajakusanya karatasi zake? Ama asiyepata karatasi? Wote mmerudisha na wote mmepata karatasi za kupigia kura? Kuna Bwana Makamba pale anaingia saa hizi. Waheshimiwa Wabunge mimi sijui itakuwaje, Mawakala makundi mbalimbali kama wanataka kwa sababu hizi kura zitahesabiwa wakati sisi tunapumzika. Matokeo tunapokea jioni.

Kwa hiyo, ni muhimu kama mtu anataka kwenda kuwa wakala mwenyewe aende. Kama anamchagua mwenzake ampeleke. Tukianza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunaanza cha Dodoma kwanza, Mheshimiwa Sadifa Juma Hamisi, Wakala wako nani?

**MHE. SADIFA JUMA HAMISI:** Mheshimiwa Sabrina. Anatokea CHADEMA.

**SPIKA:** Anayetajwa tu aende. Mheshimiwa Sabrina. Utakwenda kushiriki kwenye kuhesabu kura. Sogea hapa Mheshimiwa Sabrina Sungura. Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe?

**MHE. PRUDENSIANA KIKWEMBE:** Mheshimiwa Peter Serukamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Peter Serukamba usogee huku, sogea hapa katikati. Tunakuja Chuo Kikuu cha Mzumbe, Mheshimiwa Gosbet Blandes.

**MHE. GOSBET B. BLANDES:** Namwomba Mheshimiwa James Lembeli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lembeli wakala wake. Mheshimiwa Engineer Mohamed Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, naanza kuwafahamu. Chuo Kikuu cha Sokoine. Mheshimiwa Salum Hemed Khamis.

**MHE. SALUM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa, Amina Abdallah Amour.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, mngesogea hapa, tungewaona hapa katikati, halafu tuwaruhusu muende wapi. Sogeeni hapa wote mliotajwa akina Serukamba, akina Lembeli, akina Kuruthum. Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa

**SPIKA:** Nani?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Dr. Mary Mwanjelwa

**SPIKA:** Naomba msogee hapa. Msogee hapa katikati tutawaelekeza wapi pa kwenda. Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili. Mheshimiwa Dokta Hamis Andrea Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**SPIKA:** Nani huyo anaitwa, hebu msogee huku. Mheshimiwa Dr. Kebwe Stephen Kebwe?

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Dokta Ndugulile.

**SPIKA:** Nani?

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Dr. Ndugulile.

**SPIKA:** Na yeye ana mahali anahitaji, mtaje mwingine bwana.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Halafu nafasi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, mimi naamini tu utaratibu utakuwa sahihi, siibiwi.

**SPIKA:** Yaani unaamini tu hawa watu watakaokuwepo hao? Haya Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile?

**MHE. DKT. FAUSTINE NDUGULILE:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**SPIKA:** Nani?

**MHE. DKT. FAUSTINE NDUGULILE:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**SPIKA:** Ahaa huyo jirani yako. Halafu Chuo Kikuu cha Ufundi Arusha. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Haroub Shamis.

**SPIKA:** Haya naye asogee huku. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. Nitawaonyesha kwa kwenda.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naiamini Sekretarieti.

**SPIKA:** Haya na yeye hakuweka mtu. Tume ya Vyuho Vikuu. Mheshimiwa Luhanga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**SPIKA:** Esther?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**SPIKA:** Halafu Mheshimiwa Engineer Ramo Matala Makani.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nitawakilishwa na Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad, haya ninyi wote mnakuwa Mawakala wa wagombea hawa, mwende *Speaker's Lounge* hapo. Mtafanya hapo kazi mkimaliza matangazo tutayafanya mchana. Kwa hiyo, naomba mwelekee huko.

Sasa nina matangazo machache hapa, kwanza nina matangazo kutoka kwa Mheshimiwa Rosemary Kirigini, anaomba Wabunge wote wa kutoka Mkoa wa Mara wakutane saa mbili usiku mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kwenye eneo la Hoteli linaitwa *Munich* mimi sijui iko wapi? Nadhani mtajua wenyewe.

Halafu Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, yeye ameomba niwatangazie vijana wenye umri chini ya miaka 45 wa Chama cha Mapinduzi wakutane kwenye ukumbi wa Pius Msekwa baada ya kuahirisha Bunge jioni leo hii.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine Waheshimiwa Wabunge naahirisha Bunge mpaka saa 1100 jioni.

*(Saa 7.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

### **MATOKEO YA KURA**

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha kuhesabu kura, sasa naomba niyatangaze matokeo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamepiga kura.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, wagombea wake walipita bila kupingwa baada ya mgombea mmoja kujitoa. Wajumbe wale ni Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma, waliopiga kura ni 249, kura mbili zilizharibika. Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, alipata kura 92. Mheshimiwa Pudenciana



Kikwembe, amepata kura 155. aliyechaguliwa kuwakilisha Bunge katika Chuo Kikuu cha Dodoma, ni Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mzumbe. Mgombea mmoja amepita bila kupingwa, ambaye ni Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla. Zilipigwa kura kwa Waheshimiwa Wabunge wawili na kura zilizopigwa zilikuwa ni 254, iliyoharibika ni kura moja. Mheshimiwa Godbless Blandes, amepata kura 114. Mheshimiwa Mhandisi Mohamed Mnyaa, amepata kura 139. kwa hiyo, Mheshimiwa Mhandisi Mohamed Mnyaa, ameungana na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kuwa Wajumbe kwenye Chuo Kikuu cha Mzumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine, kura zilizopigwa ni 251. Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, amepata kura 62. Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, amepata kura 189. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jitu Soni, anakuwa mwakilishi wa Bunge katika Chuo Kikuu Cha Sokoine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Wagombea wote wamepita bila kupingwa na hao ni Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba na Mheshimiwa Henry Shekifu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili. Mgombea mmoja alipita bila kupingwa, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila. Zilipigwa kura 256 kwa ajili ya kumpata Mbunge mwanaume, hakuna kura iliyoharibika. Mheshimiwa Dokta Hamis Andrea Kigwangalla, alipata kura 117. Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, amepata kura 131.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, anaungana na Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, kuliwakilisha Bunge katika Chuo Kikuu cha Sayansi Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Ardhi, walipita bila kupingwa. Hawa ni Mheshimiwa Gosbert Blandes pamoja na Mheshimiwa Susan Lyimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kura zilizopigwa ni 259. Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, amepata kura 54. Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, amepata kura 203. Kwa hiyo Mheshimiwa Faustine Ndugulile, anakuwa mwakilishi wa Bunge katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Arusha. Kura zilizopigwa ni 257, kura tisa zimeharibika. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, amepata kura 55. Mheshimiwa George Simbachawene, amepata kura 193. Kwa hiyo, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, anawakilisha Bunge katika Chuo cha Ufundi, Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu. Kura zilizopigwa ni 261, kura zilizoharibika ni 12. Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, amepata kura 53,

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, amepata kura 195. Kwa hiyo, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, anakuwa Mjumbe katika Tume ya Vyuo Vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi. Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, amepita bila kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, Mbeya. Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge, amepita bila kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hayo ndio matokeo ya upigaji kura wote wa leo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba mchakato ulikuwa mgumu, lakini tunawapongeza hawa walioshinda. Kwa hiyo, Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, ndio watakaotuwakilisha. Anayewakilisha Chuo Kikuu Cha Dodoma ni Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. Chuo Kikuu cha Mzumbe ni Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Mhandisi Mohamed Mnyaa. Chuo Kikuu Cha Sokoine ni Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ni Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa, Mheshimiwa Silvester Massele Mabumba na Mheshimiwa Henry Shekifu. (*Makofi*)

Chuo Kikuu Cha Sayansi za Afya Mhimbili ni Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila na Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe. Chuo Kikuu cha Ardhi, ni Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo. Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ni Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile na Chuo cha Ufundi Arusha, ni Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, ni Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, ni Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa na taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, ni Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge. Kwa hiyo, hawa ndio watakaotuwakilisha katika vyuo hivi vilivyotajwa na kwa hiyo zoezi hili tumelimaliza, Katibu!

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Kujadili Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyokuwa ada, wachangiaji wetu walikuwa wengi na wameachwa karibu wengi sana, mpaka tunamaliza tumewaacha 54. Leo ndio siku ya tano na itakuwa tukichangia bila kupata ufafanuzi wa Serikali katika maeneo mbalimbali, tutakuwa hatujakamilisha ngwe hii. Kwa sababu Mtoa Hoja alikuwa ni Waziri Mkuu na kawaida yake ndio hiyo.

Kwa hiyo, kuna wengine tulifikiri labda tutapata muda wachangie wawili au watatu, lakini inaonekana orodha ya Mawaziri kuchangia imefika Mawaziri 14. Kwa hivyo, inatufikisha kwamba kwa dakika 10 na wao ni saa 1.40, halafu Kiongozi wa Serikali atatumia dakika 45 na tutakuwa tumemaliza hizo dakika na pengine wengine wasifikwiwe.

Kwa hiyo, ninyi wote ambao hamkupata nafasi ya kuchangia mtanisamehe, hatuna namna, kila kitu ni lazima kiwe na mwisho wake. Kwa hiyo, wanaoanza kuchangia hapa, ataanza Waziri wa Mambo ya Ndani, atafuatiwa na Waziri wa Uchukuzi.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. CHISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Hotuba ya Rais katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha Sekondari za Kata, lakini matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka jana (2010), yameonesha sekondari hizo zimeshindwa kufaulisha wanafunzi kwa kiwango kinachotakiwa. Sababu za kufeli ni hizi zifuatazo:-

- (a) Shule nyingi hazina madarasa ya kutosha kuwaweka wanafunzi wote waliofaulu;
- (b) Shule hazina maabara za kufanyia majaribio ya kisayansi;
- (c) Shule hazina maktaba na vitabu vya ziada na kiada;
- (d) Shule hazina mabweni ya kulala watoto wa kike na wa kiume;
- (e) Shule hazina majiko na mabwalo ya kulia chakula;
- (f) Shuel hazina walimu wa kutosha, waliopo ni wale waliopitia *Crash Programme*, hawakusoma kwa muda wa miaka miwili uliowekwa na Wizara ya Elimu;
- (g) Hazikuwa na uzoefu wa ku-*handle* wanafunzi wanaofanya Mtihani wa Taifa; na
- (h) Wanafunzi waliomaliza ni matokeo ya kufutwa kwa mchujo uliokuwa unafanyika wanafunzi wanapokuwa *Form II* 2008.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike:-

- (a) Serikali ijikite zaidi kutika kuimarisha shule hizo kwa kuhakikisha zinarekebisha upungufu wote niliouainishia hapo juu;

(b) Serikali iboreshe mishahara ya walimu na iboreshe mazingira ya kujifunzia ya wanafunzi pamoja na waalimu;

(c) Mtihani wa *Form II* uwe ni wa mchujo, mwanafunzi akishindwa arudie darasa mpaka atakapofaulu; na

(d) Mheshimiwa Spika, Serikali itilie mkazo katika kuchagua wanafunzi wanaokwenda kusomea ualimu; wanafunzi wanaopata *Division I* na II ndiyo wasisitizwe kusomea ualimu ili kuepokana na wanaofeli kuwafundisha wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Juu, Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Ibadilishe mfumo wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu badala ya kutoa mkopo kwa madaraja, itoe mkopo kwa wanafunzi wote waliopata udahili vyuo vikuu vyote vya Binafsi na vya Serikali, tena itoe mkopo kwa 100% kwa sababu utarudishwa;

(b) Mkopo pia utolewe kwa wanafunzi wanaosoma kazi zote kwa sababu hakuna kozi ambayo ni ya maana kuliko nyingine, tunahitaji wataalam wa fani zote;

(c) Serikali iwe makini katika kuanzisha au kuruhusu vyuo vingi kwa wakati mmoja, maana kuna madhara katika kupata rasilimali watu ya kutosha. Uanzishwaji wa vyuo vikuu uende sambamba na uzalishaji wa rasilimali watu kupitia vyuo vikuu vilivyopo. Hili linawezekana kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wa Vyuo Binafsi na vya Serikali ili kupata wataalam wengi, maana wanafunzi wanaosoma vyuo vya binafsi nao ni sehemu ya jamii ya Watanzania na wanawajibika kutoa huduma kwa Taifa lao pindi wanapomaliza masomo yao; na

(d) Serikali iongeze *lecture theatre* ili wanafunzi waliodahiliwa waweze kusoma vizuri. Kuna matatizo makubwa ya upungufu wa vyumba yva kutolea muhadhara ambao unapelekea wanafunzi wengi kukaa nje au kuchungulia madirishani kwa kukosa nafasi ndani.

Mheshimiwa Spika, ili Tanzania iwe lango kuu la biashara yafanyike yafuatayo:-

(a) Urasimu (*bureaucracy*), upunguzwe katika kusafirisha na kupokea mizigo;

(b) Uaminifu wa watumishi wa bandari zetu uimarishwe, hii ni pamoja na kukomesha udokozi wa mizigo; na

(c) Ushuru upunguzwe; kuna wafanyabiashara wa hapa nchini wanaopitisha mizigo yao Mombasa, inapita Uganda - Mtukura na kurudi Tanzania, bado wanakuwa na faida kuliko mizigo hiyo inapoteremshwa katika Bandari ya Dar es Salaam. Mfanyabiashara anayeagiza bidhaa nje kwa *container* la nguo la *Ft 40*, likiteremkia Dar es Salaam ushuru wake ni dola 8000 lakini kwa Uganda ni dola 400.

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara akipitisha *container* Kenya na Uganda kuja Tanzania anaweza akatumia wiki moja wakati Tanzania kwa muda mfupi ni mwezi mmoja, hapo bado rushwa wanayodai watumishi wahusika. Tutawezaje kuifanya Tanzania lango kuu la biashara kwa mtindo huu?

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo katika kipengele cha utawala bora:-

Mheshimiwa Spika, kunapotekea dosari kwa watumishi wa umma na Serikali wakiwemo Mawaziri ni lazima kuwepo kuwajibika ama mtu kujiwajibisha mwenyewe au kuwajibishwa. Linapokosekana hilo, dosari zinajikusanya na kuwa mzigo kwa Wananchi na kuwafanya wauchukie utawala kwa maana ya kutoona ubora wake. Mfano, mabomu ya Mbagala, hakuna aliyewajibika isipokuwa Wananchi ambao kodi zao zimetumika kuwafidia waathirika wa mabomu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaongoza kwa *deposit* ya madini ya Nickel Duniani, lakini madini hayo yananufaisha mataifa ya kigeni. Mfano, eneo la Ntaka, Nachingwea, limefikia kuitwa *Canadian Province* kutokana na Wakanada kuchukua madini hayo kutoka hapo wanavyotaka.

Maeneo mengine yenye *nickel* ni Kabanga - Kagera, Zanzuwi - Shinyanga na Dutwa, ambalo ndilo eneo linaloongoza duniani kwa madini hayo. Liko tatizo katika kulinda rasilimali zetu hasa madini ambayo ni mhimili mkubwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, kuna madini mengine ya Tantalum ambayo yemekuwa yakisombwa kama mchanga kwenda kufanyiwa utafiti nje ya nchi kumbe ni madini. Madini hayo yanapatikana kwa wingi Kondoa ambako uchumi wa Wananchi ni duni sana.

Mheshimiwa Spika, ningepomba Wizara husika ilisimamie na kulifuatilia kwa dhati suala hili kwa mustakabali wa Taifa letu.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kupata fursa ya kuchangia Hotuba hii. Pili, nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Wete, kwa ukarimu wao mkubwa wa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka mitano hii. Aidha, nakupongeza wewe kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu na ninakutakia uongozi bora.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa Hotuba yake nzuri, ambayo tayari ni mpango ambao unahitaji tafsiri ya utekelezaji. Hotuba hii kama Watanzania tutaweza kuitafsiri na kuifanyia kazi, basi baada ya miaka mitano, tunaweza kujitathmini tulipofika kwa mapana kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hii ningelipenda nianzie kwenye Kamati ya Pamoja ya Kutatua Kero za Muungano. Wanaokereketwa na kero hizi ni Watanzania wa pande mbili za Muungano; yaani Tanzania Visiwani na Tanzania Bara. Tatizo linajitokeza kwamba, kinachofanyika hakiko wazi, watu hawaelewi matokeo ya utatuzi wa kero hizo; na hili matokeo yake ni kupelekea unyanyaswaji wa watu zaidi katika sekta za ki-muungano. Hivyo, uwazi ni muhimu sana kwa kila hatua ya utatuzi wa kero hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningelipenda kuchangia ni kuhusu Umoja wa Watanzania na kwanza nimpongeze Rais Kikwete, kwa juhudi zake katika kutafuta suluhisho la migogoro ya Zanzibar. Katika uchaguzi huu Wazanzibari walipiga kura kwa usalama na amani na hakukuwa na bugudha yoyote.

Katika uchaguzi huu na mashirikiano yaliyopo mpaka sasa hivi kwa kweli tumepata sifa nyingi duniani kote. Hivyo, umoja huo si wa kubezwa bali ni wa kutunzwa na kuendelezwa, cheche za siasa mbovu zimeanza kuashiria Tanzania Bara waishauri Serikali, hali hiyo si ya kuidharau kwani watu wameshaanza kupoteza maisha na ikiachiwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kushauri kuwa, Tanzania sasa hivi hali imebadilika; Watanzania wameanza kuelewa demokrasia hivyo wanaunga mkono upande au chama wanachokipenda kwa mategemeo ya kutatuliwa kero zao.

Mheshimiwa Spika, hivyo; ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa, vyama vinashirikishwa katika kila pembe ya uendeshaji wa Serikali ili kujenga imani nzuri ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningelipenda kwa leo nichangie kipengele cha mazingira; suala hili bado ni zito kwa Watanzania wa ngazi zote kutoka Serikalini mpaka Vijijini. Uhifadhi wa mazingira bado unatajwa juu juu tu na kwa sababu hii ndito tukaona kila kitu au jambo tunalolifanya Watanzania linashindikana; kilimo uzalishaji wake ni mbovu/mdogo kwa sababu tunalima lakini kilimo ambacho kinaasi uhifadhi wa mazingira. Matatizo ya umeme ambayo yanatokana na uhaba wa maji katika vianzio vyetu vya maji, yote ni kwa sababu hakuna kipaumbele kilichowekwa cha kuhifadhi mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nashauri tubadilike na Serikali ichukue juhudi za makusudi za kuhifadhi mazingira ya nchi yetu hususan katika maeneo nyeti kama vile vianzio vya maji na maeneo muhimu ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba niliishie hapa na naendelea kushukuru tena kwa kupata fursa hii na naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais, kwa Hotuba nzuri, yenye matumaini kwa Watanzania. Hotuba hii imegusia mambo muhimu hasa katika vipaumbele 13.

Katika mchango wangu nitajikita zaidi katika kipaumbele cha pili, kinachozungumzia habari ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuchukua hatua thabiti katika kuboresha sekta muhimu. Sekta zilizotajwa ni Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Viwanda.

Sote tunatambua kuwa, zaidi ya 80% ya Watanzania, wanategemea kilimo ili kuinua hali zao za kiuchumi. Kilimo kilichopo hakina tija. Ninaomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwawezesha Wananchi wa vijijini kwa kuwapa zana bora za kilimo. Benki ya TIB ambayo inashughulikia uwezeshaji upande wa kilimo, iangalie na iweke utaratibu maalum, namna itakavyowawezesha wakulima wa vijijini. Wananchi wengi wakiwezeshwa, nina imani kubwa kwamba watainua uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya pili muhimu ni ya Uvuvi. Vifaa vya Uvuvi ni ghali sana kiasi kwamba, Wananchi wa hali ya chini wanashindwa kumudu kununua vifaa hivi. Katika Jimbo la Busanda, kuna Wananchi wanaotegemea uvuvi katika kuendesha maisha yao, hasa katika Vijiji vya Bukondo, Kasanghwa na Kageye. Ninaiomba Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwawezesha Wananchi hawa kwa kuwapa zana muhimu za uvuvi. Sambamba na zana hizo, pia wapewe elimu katika uvuvi wa kisasa. Hii itaboresha maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu muhimu ni Mapinduzi ya Viwanda. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo. Hii italeta mabadiliko makubwa sana kwa sababu vijana wote wanaomaliza sekondari wataajiriwa na kujijiri kutokana na kuanzishwa kwa viwanda hivi. Mapinduzi ya viwanda yatapunguza tatizo la kukosa ajira kwa vijana walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuboreshwa kwa sekta hizo muhimu ambazo ni Kilimo, Uvuvi na Viwanda, nina uhakika maisha ya Wananchi hasa walio vijijini yataboreshwa na uchumi wao utakua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mmoja wa wawakilishi wa Wananchi katika Bunge lako Tukufu. Aidha, nakishukuru sana chama changu cha CHADEMA na Wanawake wa Mkoa wa Singida, kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza nitaelekeza katika Sekta ya Elimu ya Juu hapa nchini. Serikali pamoja na kuanzisha vyuo vingi vya Elimu ya Juu, imeshindwa kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Limekuwa ni jambo la kawaida, kuwaona wanavyuo wetu wakiandamana ama kugoma ili

kuikumbusha Serikali wajibu wake wa kuhakikisha mazingira bora ya kujifunzia, ikiwa ni pamoja na Bodi ya Mikopo kutoa mikopo kwa wakati na bila kuwasumbua wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kuwa, kwa muda mrefu sasa Serikali imeshindwa kuondoa kero zinazoikabili Sekta ya Elimu ya Juu na hasa katika Bodi ya Mikopo ambayo imeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuwafanya wanafunzi kutumia muda mwingi kufuatilia malipo yao badala ya kuwa madarasani. Jambo hili ni hatari sana kwani linaathiri maendeleo ya wanafunzi kitaaluma na mwisho ushindani wao katika soko huru la ajira pia utakuwa umeathiriwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, nitaelekeza katika Sekta ya Maji. Miaka hamsini ya Uhuru, maeneo mengi ya nchi yetu hususan ya vijijini, bado yanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la maji katika Wilaya yote ya Singida Vijijini, hususan katika Vijiji vya Kata za Misughaa, Kikio, Mang'onyi na Unyahati. Tunaelewa kuwa kukosa maji safi na salama ni hatari sana kwa afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali katika miradi yake ya kupeleka maji safi vijijini, iwape kipaumbele Wananchi wa Kata za Kikio, Misughaa, Mang'onyi na Unyahati za Wilaya mpya ya Ikungi ili waondokane na kutumia maji ya kwenye madimbwi, ambayo nayo upatikanaji wake ni wa shida hasa nyakati za kiangazi na ni hatari sana kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie juu ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anaposema kwamba, tutaimarisha na kuendeleza Muungano wetu maana yake pia ni kwamba, anakusudia kuyaenzi mawazo na fikra nzuri za Waasisi wa Muungano huu, lakini pia vigezo vya Muungano huu, haikuwa uwiano wa Wananchi wa nchi hizi mbili zilizoungana bali vigezo ilikuwa ni kuunganisha nchi ya Zanzibar na nchi ya Tanzania Bara. Hivi ndivyo vigezo vilivyotumika na si uwiano wa idadi ya Wananchi katika nchi hizo. Ilikuwa inafahamika vizuri kwamba, Zanzibar ilikuwa na watu laki nne na Tanganyika ilikuwa na watu zaidi ya milioni tano, lakini hilo halikuwa tatizo katika kuungana kwetu.

Mheshimiwa Spika, inapotokea Mheshimiwa Mbunge akafananisha Wananchi wa Majimbo 20 ya Zanzibar kwamba ni sawa na Jimbo moja la Tanzania Bara, hii ni dharau; huku ni kukebehiana na hatupo hapa kuoneshana kebehi. Unaposema hivyo pia ni sawa na kusema kwamba, Wabunge 20 wa Zanzibar ni sawa na Mbunge mmoja wa Tanganyika. Hii ni dharau kubwa kwa Zanzibar na hatukuletwa hapa na Wananchi kuja kuoneshana ufundi wa kudharauliana. Hili si jambo zuri hata kidogo.



Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni Utawala Bora, hasa suala la malipo ya pensheni kwa Wazee wetu wastaafu. Wastaafu ni Watanzania ambao wanatumia muda na nguvu zao zote katika maisha yao kwa kulisaidia Taifa hili. Kila mmoja katika Taifa hili leo anajivunia msingi na kazi zilizofanywa na Wazee hao ambao leo ni Wastaafu.

Mheshimiwa Spika, kwa mapenzi yao kwa nchi yao hawakupenda kustaafu, lakini hili la kustaafu ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu, kwani msingi wake ni umri wa kustaafu kwa anayestaafu. Wazee hawa (wastaafu), naomba pensheni zao ziendane na viwango vya mishahara vilivyopo ili nao waweze kujikongoja hasa ukizingatia hali ngumu ya maisha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, naomba pensheni hizo zilipwe kwa kila mwezi badala ya kipindi cha miezi sita kama ilivyo sasa.

**MHE. ANNA JOHN MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mungu, kwa kutupa uhai na kutukutanisha tena katika Bunge hili Tukufu. Nichukue nafasi hii, kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kuteuliwa kwake tena kuwa Waziri MKuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii, kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Umeweka rekodi ya kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge hili na kuonesha kuwa wanawake tunaweza. Tunakuombea kwa Mungu azidi kukupa afya ili uliongoze Bunge hili kwa amani na utulivu bila ubaguzi wowote, ukiamini Wabunge wote humu ni Wawakilishi wa Watanzania na Watanzania wanategemea kuona sisi tunawawakilisha vipi na tunawatetea vipi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa siyo mwingi wa fadhila nisipoweza kuwashukuru Wananchi wa Mpanda, Jimbo la Mpanda Mjini. Nawashukuru sana kwa uamuzi wao wa busara wa kumchagua Mheshimiwa Said Amour Arfi kuwa Mbunge. Ninawaomba wazidi kumwombea ili awatumikie kwa kutatua kero za Wanampanda.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye kuchangia Hotuba ya Rais, lakini hapa nitaongelea vipaumbele 13 alivyovieleza Mheshimiwa Rais. Naomba niongelee kipengele namba tisa, kinachoongelea kuongeza jitihada za kupanua, kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii hususan afya, maji, umeme, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nianze na afya. Jitihada hizi za kupanua na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii, zimeleta mgawanyiko mkubwa baina ya Watanzania wa mjini na vijijini. Watanzania waishio vijijini wanaumia sana na kupoteza maisha kwa kukosa huduma muhimu za kijamii.

Wananchi vijijini wanajitolea sana kuchangia Serikalini lakini hawapewi kipaumbele kwa kufikishiwa huduma muhimu za kijamii. Mfano, Wananchi hao wanajitolea sana katika ujenzi wa zahanati na majengo ya madarasa, lakini unakuta Serikali haiangalii kupeleka wafanyakazi vijijini wala dawa za kutosha. Unakuta zahanati ina muuguzi mmoja; huyo huyo ndiyo mkunga; je, Wananchi hawa wanaishi vipi? Wakati Serikali inategemea kipato kutoka kwa wanakijiji hao hao, ambao ndiyo wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, tukija upande wa barabara; Serikali inaweka kipaumbele mijini na siyo vijijini ambako ndiyo mazao ya chakula na biashara yanatoka. Hali hii haimwendelezi mkulima wa kijijini ambaye anashindwa kutoa mazao na kuyafikisha sokoni kwa sababu ya ubovu wa barabara. Je, hapa kweli tunakuza uchumi wa Mtanzania hasa mkulima wa kijijini ambaye anasomesha watoto wake katika Shule za Kata ambazo hazina walimu wa kutosha, maabara, wala vitabu vya kutosha? Je, kuna haja ya kusema Watanzania wote ni sawa na wanastahili kupata huduma sawa?

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii; Serikali inaandaa Taifa gani la baadaye?

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, Bahari Kuu inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa Uchumi wa Taifa. Samaki wengi sana wanapatikana katika Bahari Kuu. Maelfu kwa maelfu ya tani za samaki wanaporwa na meli za kigeni zinazovua katika eneo hili. Linalohitajika ni Serikali kudhibiti wavuvi haramu katika eneo hili.

Vilevile Serikali ichukue juhudi ya kutafuta wawekezaji watakaokuwa na uwezo wa kuvua katika Bahari Kuu. Ili kufanikisha hili, lazima Serikali itoe *incentives* ambazo zitaweza kuvutia wawekezaji hao.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Rais, kwa Hotuba ambayo inapanua dira yetu ya kuendesha shughuli na mipango ya Kitaifa kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ushauri kama ifuatavyo: Kipaumbele namba mbili na namba tisa; nampongeza sana Rais kwa kubuni mpango mkubwa wa SAGCOT uliozinduliwa huko Davos, Switzerland mwezi Januari 2011. Pamoja na huduma na Miradi ya Kilimo, naona sasa ni muda muafaka wa kutekeleza Mradi wa Umeme wa *Stieglers' Gorge* ili tuweze kuongeza nishati itakayosaidia pamoja na mambo mengine, ukuaji wa viwanda vya kusindika mazao na uzalishaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba, ili tuwasaidie vijana wanaohitimu katika Vyuo Vikuu hususan SUA, tuandae utaratibu wa kuwakopesha mitaji ili watumie elimu yao waliyoipata kwa kuzalisha mazao katika mashamba yao, wapate ardhi, mashamba, mitaji na wajajiri wenyewe. Utaratibu kama huu unatumika katika Nchi ya Misri.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba saba; mipaka yetu mingi bado haina uwezo wa kukusanya mapato ipasavyo, kwa mfano, katika mpaka kati ya Tanzania na Burundi, wakusanyaji wa mapato na wasimamizi hawatoshi. Wizara zinazohusika, kama Kilimo, Chakula na Ushirika, Mifugo na kadhalika, zishirikiane na mamlaka nyingine kudhibiti utoroshaji wa mazao ya kilimo na mifugo unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba nane; ili Kilimo Kwanza ifanikiwe, suala la elimu ni jambo la msingi. Ningependa kushauri mambo mawili kama ifuatavyo: Moja ni suala la maabara; masomo ya sayansi katika shule zetu ni suala la lazima. Kwa kuwa uanzishwaji wa maabara ni ghali, pengine ni vema tuwe na mpango mkakati wa uanzishaji wa maabara na ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Elimu; pamoja na kwamba, Mifuko ya Elimu ilianzishwa katika maeneo/Wilaya kadhaa huko nyuma na mahali pengine uendeshaji wake ukadorora; ni vema tuliangalie upya. Serikali peke yake haitaweza kusomesha watoto wote. Mifano mingine mizuri (*success stories*) za uchangiaji katika elimu iko huku KNCU Moshi na Pamba Mwanza na Shinyanga, tuige walivyofanya, tuendeleze mfumo huo, siyo lazima tuwachangishe wakulima wa mazao kadhaa tu kama kahawa na pamba, lakini tunaweza kuangalia sekta na wadau mbalimbali wakiwemo wafanyakazi na wafanyabiashara kuchangia Mfuko wa Elimu.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za jamii na kiuchumi; bado kuna mambo ambayo yanachangia kushuka kwa elimu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuteuliwa kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la saba huwa na mihula/awamu mbili, husababisha matokeo mabaya katika maendeleo ya wanafunzi, maana wale wa awamu ya pili hupata kero kubwa katika kujifunza kwa vile wao hufikia kunakili kazi za wenzao ambao hawaelewi kwa vile wanajua kunakili tu na muda wa kuyapitia yale haupo bali huambatana na wenzao pale walipopafikia. Kwa hali hii huweza kuwa na matokeo mabaya mbele ya safari; hivyo, Serikali ilianganalie hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuzungumzia juu ya afya; katika hospitali zetu hali ni mbaya kwani ukienda huko baadhi yake uchukue karatasi wewe mwenyewe kwa ajili ya cheti. Huduma ya daktari pale ni kukupa huduma ya kukuhoji juu ya ugonjwa wako na kukuandikia dawa, lakini kuhusu dawa utaambiwa kanunue dukani kwa fulani.

Pia hata kwa akina mama wazazi, hawa sasa hakuna jambo la siri lisilojulikana kwa wanaume au watoto, kwani hutakiwa wachukue vifaa vinavyohitajika toka nyumbani.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kutokana na tatizo la ukosefu wa maji, mzazi hulazimika awe nayo toka nyumbani. Kwa wale walio katika huduma ya Bima ya

Afya, hawa huchaguliwa magonjwa ya kulipiwa na Mfuko wa Bima na mengine wajitegemee kama vile kuwekewa meno ya bandia, miwani na hata vipimo vikubwa pia.

Mheshimiwa Spika, naomba Seriakli iyaone haya kuwa ni ya msingi na kwamba, yanahitaji yatiliwe maanani ili yawe na unafuu kwa Wananchi. Pia kwa upande wa uchumi, kule Kusini wakulima zao lao la biashara ni korosho, ununuzi/uuzaji wa zao hili kwa mkulima ni wa kulalia; mkulima hawi na uhakika wa bei kwani bei ni ya kupangiwa na Bodi ya Korosho bila kushirikishwa mkulima mwenyewe. Hata hiyo bei inayopangwa, mkulima hupewa nusu nusu kwa mpango wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, mpango wa stakabadhi ghalani siyo mbaya ikiwa mkulima atapewa kwanza kile kiasi kinachopangwa, baada ya mauzo ndipo apewe bonasi maana anapopewa nusu nusu inamrudisha nyuma katika maendeleo yake, kwani kile kiasi pungufu apewacho kwanza kama hakikufikia kiasi ya kufanyia kile alichokikusudia ni vigumu kufanikiwa. Pesa hizi hutumika kwa matumizi mengine nje ya makusudio. Zitakapolipwa ile nusu nyingine lengo lingali limepotea; hii inarudisha maendeleo ya mkulima ili aweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika sambamba na hilo, makato huwa ni mengi mno; kati ya makato hayo kwa mkulima ni kero kwake. Vile vile suala la pembejeo, nyingie hutolewa baada ya msimu wa kilimo kupita na bei ni kubwa na pengine huletwa ingali imepitwa na muda au imeharibika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda kuishauri Wizara husika ilione hilo na kutafuta suluhisho kwa kero hizi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Hotuba ya Rais na kuiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 23; suala la kuwawezesha Wananchi kiuchumi ni jambo muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Baraza la Uwezeshaji Wananchi lipatiwe nguvu na uwezo kwa maana ya ujuzi na fedha za kutosha ili wanachi na hususan Watanzania asili, wapewe kipaumbele. Sera ya uwezeshaji ieleweshwe kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, vyombo na taasisi zinazowezesha Wananchi washirikishwe ili kuchangia nguvu na rasilimali zao kwa ujenzi wa uchumi kwa haraka na ufanisi. Taasisi hizo ni *Pride*, *SACCOS*, *VICOBA*, *FINCA* na *NGOs* mbalimbali, *private sector* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazosaidia Wananchi kuwezeshwa zitungwe kama vile Sheria ya *Microfinance Act*, *Black Empowerment Act* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya kufundisha ujasiliamali vianzishwe kama ilivyo *EDEC* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Benki za Watu Maskini na Benki za Jamii zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 18 Novemba 2010, alipozindua Bunge la Kumi. Katika hotuba yake ya uzindizi, Rais amezungumzia mambo ambayo kimsingi yana mwelekeo wa kuliimarisha Taifa letu katika Nyanja zote. Utekelezaji wa Hotuba hii ukifanywa kwa ukamilifu wake, maisha bora kwa kila Mtanzania yanaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii nzuri iliyotolewa na Rais, inatakiwa sisi Wabunge kwa pamoja kuichanganua na hatimaye kuiongozea nyama ili iweze kutekelezwa vizuri na matunda yake yanaweza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia Hotuba hii, ningependa kuanzia eneo la elimu. Hotuba ya Mheshimiwa Rais, imetoa mwelekeo katika kuiboresha elimu tangu ya awali hadi Chuo Kikuu. Maoni yangu ni kuwa; ni vizuri kupitia upya Sera zetu zinazohusu Elimu na kuzifanyia marekebisho pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha elimu yetu, naiomba Serikali iangalie upya uamuzi wake wa kufuta Mitihani ya Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Lengo la kuwepo kwa mitihani hiyo ilikuwa ni kuwapa fursa vijana ambao uwezo wao ni mdogo, waweze kupata nafasi ya kurudia kwa mwaka mmoja ili waweze kujifunza zaidi na hatimaye mwaka unaofuata waweze kujifunza zaidi na hatimaye mwaka unaofuata waweze kuendelea na masomo ya darasa la tano kwa shule ya msingi na kidato cha tatu kwa wale wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, faida ya mitihani hiyo ni nyingi zaidi kuliko hasara. Kwa maana hiyo ni vizuri kwa sasa kuangaliwa upya na hatimaye kurejesha mitihani hiyo kwa lengo la kuwachuja wanafunzi ili kuimarisha elimu kwa watoto wetu. Wataalam wanasema, unaporudia jambo fulani mara kwa mara, inakupa uwezo wa kulielewa jambo hilo na kudumu kwenye ubongo wa mwanadamu kwa muda mrefu.

Aidha, kama hakuna uwezekano wa watoto/wanafunzi hao wasio na uwezo kuhariri madarasa hayo, basi hakuna haja ya kupoteza fedha nyingi kuandaa mitihani hiyo na badala yake fedha hizo zitumike kwa ajili ya kuboresha maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu afya. Tangu awamu ya nne ianze na kwa kupitia ilani zake za uchaguzi, kwa sasa karibu kila kijiji, aidha, kimejenga zahanati yake au kipo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi. Tatizo lililokuwepo ni kuwa pamoja na baadhi ya vijiji kujenga zahanati nyingi kama ilivyo katika Wilaya ya Rufiji ambako

zaidi ya zahanati 16 zimekamilika, lakini hazijafunguliwa hadi sasa kutokana na ukosefu wa wahudumu. Hali hii inawakatisha tamaa sana Wananchi ambao walijenga zahanati hizo kwa malengo ya kuweza kupata matibabu yao kwa karibu.

Naiomba Serikali ione changamoto hii ya wahudumu/wauguzi ili kuunga mkono Wananchi hao. Aidha, ni vizuri kwa Wizara ya Fedha kutoa maelezo ya kina kwa nini wanatoa ahadi kuwa dawa kwa ajili ya zahanati mpya tayari zimetolewa wakati hadi sasa dawa hizo hazijafika kwenye zahanati hizo mpya. Zahanati hizo ni Mkenda, Nyambili, Mtwanya, Mkupuka na Ndundutawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kero kubwa sana ni kilimo. Tunaiomba Serikali itutengenezee Bwawa na Mto Mkomazi ili tuweze kutumia maji yake kwa kilimo na liweze kulisha mikoa mitatu ya Tanga, Pwani na Kilimanjaro. Pia linaweza kulisha Tarafa tatu za Mombo, Bungu na Magoma katika Jimbo langu. Naomba Serikali itenge pesa kwa ajili ya bwawa hili liweze kuwanufaisha Wananchi wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, eneo la Jimbo langu limezungukwa na mashamba ya mkonge ambayo hajaendelezwa. Naomba Serikali ifute hati miliki ya mashamba haya ambayo hayajaendelezwa ili Wananchi wapate mahali pa kulima, ukizingatia Serikali imetoa kipaumbele cha Kilimo Kwanza. Mashamba yenyewe ni yafuatayo: *Magoma Estate, Lwengera Estate, Hale Estate*, Gomba, Mswaha, Toronto, Mkumbara, Kwashemshe na Mazinde. Baadhi ya Mashamba haya yamekuwa msitu, naomba Serikali yale ambayo hayaendelezwi wapewe Wananchi walime.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna sehemu kubwa haina mawasiliano ya simu hadi Makao Makuu ya Tarafa. Kata za Bungu, Kizara Mkalamo na Mpale zote hazina mtandao wa simu, naomba Serikali kupitia Wizara husika, nipate mawasiliano kwenye sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kuhusu maji; katika jimbo langu Wananchi wengi wamepata magonjwa mengi ya maambukizo kufuatia ukosefu wa maji safi. Ninaiomba Serikali vijiji vifuatavyo vipatiwe maji safi; Bungu Kibaoni, Mali, Mpare, Magoma, Kizara, Mombo, Mkalamo, Kerenge na Makumba.

Mheshimiwa Spika, kuna shida ya umeme kwa muda mrefu kwenye Kata zifuatazo: Dindira, Bungu, Vugiri, Kwashemshi, Kizara na Mswaha. Ninaiomba Serikali ivipatie umeme vijini hivi kwani ni kwa muda mrefu sasa havijapata umeme.

Pia napenda kuchangia kuhusu barabara; kufuatia asilimia 97 ya Wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini kuwa ni wakulima, naomba Serikali itengeneze barabara za Jimbo hilo ili zipitike wakati wote ili wakulima waweze kusafirisha mazao wakati wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja.

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge hili Tukufu.

Nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kwela, kwa kuniamini na kunifikisha hapa Bungeni kwa kunipa kura nyingi za kishindo.

Naishukuru sana familia yangu na mke wangu, kwa uvumilivu mkubwa waliokuwa nao na kunipa moyo katika kipindi chote cha kutafuta nafasi hii. Nami nawaahidi Wananchi wote wa Jimbo la Kwela kwamba, nitaifanya kazi hii kwa uadilifu na uwajibikaji wa hali ya juu. Nawaombeni muendeleo kunipa ushirikiano ili kukidhi matarajio ya safari yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kuchangia Hotuba hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala zima la Kilimo Kwanza limejikita katika malengo makuu mawili; kwanza, kuongeza uzalishaji wa mazao na biashara; na pili, kupunguza umaskini.

Katika kipengele cha kwanza, takwimu za uzalishaji zinaonesha mafanikio makubwa kwa uzalishaji wa mazao kuongezeka. Changamoto kubwa ambayo bado haijaonesha mafanikio ni suala zima la kupunguza umaskini. Hii ni kutokana na kundi hili kutotambulika vizuri na Serikali na kufanya watu wenye kipato kutumia nafasi hiyo kujinufaisha. Hivyo, ili Serikali iweze kufika kwenye lengo la kuwainua kundi hili ni muhimu sasa kuwafahamu kwa takwimu na kwa majina yao ili nia ya Serikali ya kuwasaidia iweze kuwafikia kwa usahihi. Kwa kuwa wanaunganika katika vikundi na kuwapatia misaada mbalimbali kama vile ardhi ya kulima na fedha za mtaji wa kulimia na hivyo itakuwa rahisi kwa Serikali kupima malengo yake katika kundi hili kuliko kuwachanganya pamoja na watu walio na uwezo.

Serikali iwahakikishie soko la mazao wanayozalisha na liwe ni soko la faida. Barabara za kwenda kwenye uzalishaji zitengenezwe. Vilevile katika suala la uvuvi, Serikali itoe mikopo kwa wavuvi ili wapatiwe zana za uvuvi kama vile nyavu, injini za boti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu lipo tatizo la barabara nyingi kutopitika hasa wakati wa masika na hatimaye kuwatenga Wananchi kutofikiwa na Viongozi wa Kitaifa. Kutokana na tatizo hilo, namshukuru Rais, wakati wa kampeni aliahidi kushughulikia mambo muhimu yafuatayo ambayo ni kero katika maeneo hayo: Kutengeneza Barabara ya Kalambazite – Ilemba na kuweka lami maeneo ya mlimani; Barabara ya Miangalua – Kilyamatundu; kutatua tatizo la maji katika Mji Mdogo wa

Laela; na kuweka umeme katika Mji Mdogo wa Laela. Tunamshukuru Rais, kama ilivyo kawaida yake, hatuna mashaka na utekelezaji wa ahadi hizo atazitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kwela bado ni kubwa sana na mbaya zaidi limekuwa na maeneo mawili yanayotofautiana kijiografia; hivyo, tunaiomba Serikali iongeze Jimbo lingine au Wilaya ili kusogeza huduma karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD ABUU JUMAA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, napenda nikupongeze sana kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza pia Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuiongoza nchi yetu kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Hii inadhihirisha kazi nzuri aliyoifanya ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya awamu iliyokwisha. Nichukue pia nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, kwa kunichagua kuwawakilisha hapa Bungeni. Shukrani hizi ni pamoja na wale wote walionisaidia kwa namna moja au nyingine. Nawahakikishia kwamba, nitawawakilisha kwa uadilifu mkubwa na sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza kabisa, kwa kumpongeza kwa usajiri, uvumilivu, upeo mkubwa alionao pamoja na mambo mengi ya maendeleo ya Nchi yetu, ambayo ameyaweka bayana kwetu Wananchi. Pamoja na Hotuba yake nzuri sana, aliongelea mambo mengi ya muhimu katika mustakabali wa Taifa letu; Umoja, Amani, Mshikamano na Upendo miongoni mwetu Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Rais aliweka msisitizo katika Kilimo Kwanza ikiwa kilimo ni uti wa uchumi wa Mtanzania. Katika Jimbo langu la Kibaha Vijijini kuna ardhi nzuri sana ambayo ina rutuba ya kutosha kwa kuendeleza Kilimo cha Mahindi, Mpunga na Mbogamboga, kinachokosekana ni mtaji kwa Wananchi kuweza kufanya kilimo cha kutumia matrekta, pembejeo na kadhalika. Pamoja na hayo, wapo wafugaji ambao wana ari kubwa ya kuchangia maendeleo ya nchi hii, lakini kwa upande huu kidogo wamesahaulika katika masuala ya kupatiwa elimu ya ufugaji bora, ardhi ya kulisha mifugo, majosho ya kuoshea mifugo na vituo vya *Veterinary* vya kutibia mifugo na kutoa chanjo.

Mheshimiwa Spika, Mto Ruvu unapita katika Jimbo la Kibaha Vijijini. Utaona kwamba Mto huu maji yake yanatumiwa kusambaza maji Mkoa wa Dar es Salaam wakati Jimbo la Kibaha Vijijini sehemu nyingi hazina maji na Wananchi wanategemea kuchimba maji ya visima vifupi au madimbwi yanayotegemea maji ya mvua. Maji haya hakika si safi wala salama. Nampongeza na kumshukuru Rais, kwa kuona maji ni mhimili mmojawapo wa maisha na kuunda Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nimpongeze pia Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa kufanya ziara katika Jimbo langu, kuangalia vyanzo vya maji ya Mto Ruvu. Natumaini hali halisi aliiona na atafanya jitihada za kuhakikisha kuwa, Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wananufaika pia na maji yake.



Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu Hotuba ya Rais na Maendeleo ya Elimu na Teknolojia. Ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa za kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma na shule nyingi za sekondari kila Kata. Hili ni jambo la ufanisi mkubwa na ameweka historia itakayokumbukwa katika vizazi vijavyo vya Tanzania. Nashauri Elimu inayotolewa iendane na maazimio ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa mfano, tukichukulia Kilimo Kwanza; tumeona bila pembejeo za kisasa, yaani matrekta, mbegu bora, mbolea na umwagiliaji, bado dhana hii itabaki kwenye nadharia.

Mheshimiwa Spika, turudi katika historia, naamini kabisa nchi yetu inao wataalamu wengi katika fani mbalimbali. Taifa likiwawezesha, tunaweza kuwatumia vizuri kutengezeza hata matrekta ambayo tunaagiza nje ya nchi. Miaka ya 1984/85, tulishuhudia Wanajeshi wa JWTZ pale Kibaha Nyumbu, wakitengeneza malori, vifaru na zana nyingine nyingi. Yawezekana lori lile la Nyumbu halikuwa na sura nzuri kama scania, lakini hadi leo tunalionna barabarani. Naamini kwa umaskini wetu pale palikuwa na mafanikio na hatua ya kuanzia. Wataalamu wale wako wapi?

Tulikuwa na *Kilimanjaro Machine Tools*, Kiwanda hiki kilijengwa kutengeneza mashine na vipuri kwa sasa hivi hakisikiki. Naamini Serikali ikiweka nia, tunaweza kuanza kukitumia kutengeneza matrekta, majembe ya kukokota kwa ng'ombe na kadhalika. Pia TAMCO Kibaha, inaweza kutumika kuwa kituo cha *research*, kufanyia utafiti au kujenga uwezo kwa wataalamu wetu. Kumekuwa na dhana ya watoto wetu kuogopa masomo ya hesabu na sayansi; tuangalie chimbuko lake, yawezekana hawajaona faida yoyote au kutambulika kwa fani ya *engineer* kama fani myingine zilivyo na maslahi makubwa na heshima kama wanasheria, madaktari, wanasiasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa, Tanzania tunao uwezo mkubwa wa kuweza kujenga uchumi wetu. Changamoto nyingine ni masoko ya mazao yetu; mkulima anapolima anategemea auze mazao yake, anapokosa soko huvunjika moyo sana kuona mazao yake yakioza na kuharibika. Wizara husika Kilimo, Umwagiliaji, Viwanda, Uchukuzi na Ujenzi, wahakikishe wanashirikiana kuona jinsi watavyojipanga kutatua matatizo ambayo yataweza kuvunja moyo wakulima.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye ukarimu, kwa kuniwezesha mimi pamoja na Wabunge wenzangu wa Bunge lako Tukufu, tukiwa wazima wa afya.

Pili, shukurani zangu za dhati ziwaendee Wananchi, Wanachama na Viongozi wa Chama cha Wananchi (*CUF*) wa Jimbo langu la Kojani, pamoja na usimamizi wa Chama Taifa, leo hii kunisimamisha hapa nikiwa Mbunge ili niweze kuwawakilisha katika maamuzi ya nchi hii. Shukurani zangu pia zikufikie wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge letu hili, kwa kuweza kuchaguliwa miongoni mwetu sisi Wabunge na kuwa Spika wetu. Nasema Mungu akubariki pamoja nasi ili atuongoze vema na akupe afya milele. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa Hotuba yake nzuri, iliyosheheni busara, hekima na maelekezo ambayo ni dira ya kuweza kutuletea maendeleo ya Watanzania katika kipindi cha 2010/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, mimi nataka nichangie Hotuba hii kwa kuangalia vipengele vifuatavyo kutoka vipengele 13 vya Hotuba hii kama ifuatavyo; Suala la amani na utulivu (ukurasa wa kwanza); na kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia (ukurasa wa nane) na Utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nizungumzie suala la amani na utulivu ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu ndiyo dira ya maisha ya mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Hatuwezi kuishi bila amani. Nchi yoyote haiwezi kukalika bila amani na utulivu. Nataka nitoe mfano ndani ya Bunge lako hili tusiende mbali; hapa Tanzania imetuchukua vipindi vitatu vya uchaguzi kuanzia mwaka 1995 – 2005 ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Tumeshuhudia Wazanzibari kukosa raha; watu walikuwa hawaeleweki kabisa kwani shughuli za kiuchumi zilisita na kipindi hiki watu waliuawa, walijeruhiwa na wengine kubaki walemavu hadi leo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kulipa kipaumbele suala zima la amani katika Hotuba yake.

Naomba niishauri Serikali juu ya Umoja wa Kitaifa uliopo Zanzibar uendelee kuheshimika na mpango huu usimamiwe zaidi na vyombo vyetu viwili; Bunge na Baraza la Wawakilishi ili kuupa huu nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleweshe Bunge hili kwamba, kwa uzoefu wangu, tatizo kubwa la uvunjikaji wa amani hapa Tanzania na nchi nyingine duniani, husababishwa na usimamizi mbaya usio wa kutoa haki sawa kwenye taratibu za chaguzi zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru Serikali ya Muungano, taratibu za chaguzi zetu ziangaliwe na kurekebishwa upya.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni kile cha kudumisha Utawala Bora, Demokrasia na Utawala wa Sheria. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kutokana na kipengele hiki kwa sababu nchi yoyote inayotekeleza misingi ya Demokrasia na Utawala wa Sheria, hukomaa kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RICHARD MGANGA NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono Hotuba hii kwa asilimia zote. Vipaumbele vyote 13 ni muhimu sana; namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuviainisha vipaumbele hivyo. Naomba nizungumzie kipaumbele kinachozungumzia kuimarisha Demokrasia na nijikite eneo linalozungumzia vyombo vya

habari. Naomba nivipongeze sana vyombo vya habari vyote kwa kazi nzuri inazofanya kwa kuelimisha na kuhabarisha matukio jinsi yalivyokuwa yanatokea.

Vyombo vya habari ni muhimu sana kuanzia sasa ambapo tupo kwenye mchakato wa kurekebisha au kuandika Katiba Mpya; ninaomba vyombo vya habari viwe mhimili wa nne badala ya mitatu (Serikali, Mahakama na Bunge), kutokana na umuhimu wake katika nchi. Pia ninaomba Serikali ilete Sheria ya Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

**MHE. AMINA NASSORO MAKILLAGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru sana wewe kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa ushauri na maoni yangu kuhusiana na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Ufunguzi wa Bunge Jipya la Kumi, tarehe 18 Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupa fursa sisi kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Nawashukuru Wananchi wa Tanzania kwa kukipigia kura Chama cha Mapinduzi na kupata ushindi wa kishindo kwa nafasi ya Rais, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niungane na Wabunge wenzangu waliochangia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuandaa na kuwasilisha Hotuba iliyotoa vipaumbele 13 katika mwelekeo wa kutekeleza Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningependa sasa nichangie Hotuba ya Rais, ambayo imegusa mambo 13 muhimu sana kwa maendeleo yetu, lakini mimi nimechagua mambo sita hivi ya kuyatilia mkazo.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele namba moja Mheshimiwa Rais alitukumbusha Watanzania kuwa nguvu ya mnyonge na maskini ni umoja na akatumbusha umuhimu wa kudumisha amani ya nchi yetu kwa gharama yoyote ile.

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Watanzania, kuendelea kudumisha na kuimarisha amani na utulivu. Ninaishauri Serikali iendeleo kuwa mamcho zaidi na vitendo vyovyote vinavyoashiria kutaka kufanya jaribio la kuvunja amani ya nchi yetu, kwani pale panapokosekana amani wanaoumia ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Rais ameeleza kwa kina mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Kilimo na Chakula. Alieleza vipengele saba katika jitihada za Serikali za kuhakikisha kilimo kinaendelea kuwa chenye tija pamoja na jitihada hizo.

Ninaomba kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, iweke mkakati mpya utakaowafanya baadhi ya Watanzania wapende kufanya kazi hasa katika kilimo, kwani

baadhi ya watu hawapendi kufanya kazi hasa ya kilimo badala yake wamewaachia wanawake na watoto wao wa kike ndiyo walime chakula cha kutosheleza familia na biashara.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 23 wa Hotuba ya Rais, ameelezea jinsi ambavyo Serikali katika kipindi cha miaka mitano imewawezesha Wananchi kiuchumi kupata fursa mbalimbali kupitia Mifuko mbalimbali. Napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya ya kuhamasisha kuanzisha Mifuko na Taasisi mbalimbali kwa ajili ya kuwawezesha Wananchi kiuchumi.

Napenda kumshukuru Rais na Serikali kwa kutekeleza dhamira yake ya dharti kuanzisha Benki ya Wanawake na kuhakikisha Benki hii inaanza kazi. Naomba kuipongeza Serikali kwa utayari wa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji ili Benki ya Wanawake iwe na uwezo wa kufungua matawi yake mikoani kwa manufaa ya wanawake na Watanzania kwa ujumla.

Katika ukurasa wa 38 wa Kitabu cha Hotuba ya Rais, Rais ametukumbusha ahadi yake alipokuwa akifungua Bunge la Tisa lililopita, alitoa ahadi ya kuchukua hatua za makusudi za kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi. Ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali ya CCM kwa kutekeleza dhamira yake ya kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi likiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba Rais, Serikali, Vyama vya Siasa na Asasi mbalimbali, ziendeele kuongeza nafasi za wanawake katika kila chombo cha maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 kwa 50 kati ya Wanawake na Wanaume kwani Wanawake wana uwezo mkubwa sana sambamba na wanaume.

Kuhusu maji na mazingira; katika ukurasa wa 30 Rais ameeleza kuwa pamoja na juhudi za kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi nchini, bado lipo tatizo la maji hasa vijijini. Napongeza dhamira ya Serikali ya kupongeza fedha za Bajeti ya Serikali kwa ajili ya huduma ya maji. Ninaishauri Serikali isimamie vizuri fedha zote zitakazotengwa na Serikali zitumike kwa ajili ya kusambaza maji kwa Wananchi kupitia vyanzo vya maji vilivyopatikana; mfano, Bwawa la Kidunda, Mto Ruvu, Mipera na Kimbiji na kadhalika katika Jiji la Dar es Salaam, badala ya fedha nyingi kutumika kwa kufanya utafiti wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu nami niseme kwamba, matokeo ya mwaka huu katika shule za sekondari hayajaniridhisha, japo hilo lilikuwa ndiyo tegemeo langu kutokana na huu mpango wa kujenga sekondari nyingi (*Crash Program*), tulioufanya kwa lengo la kulinusuru Taifa, nikielewa kuwa zoezi hili ni endelevu.

Kubwa zaidi nililojifunza na kwa nafasi hii, nimpongeze sana mwanamke mwenzetu, Dkt. Joyce Ndalichako, kwa kudhibiti mitihani, jambo ambalo lilikuwa ni tatizo sugu huko nyuma. Tulikuwa tunashangalia ufaulu, kumbe wanafunzi wamekaririshwa majibu na mara nyingine walimu kudiriki hata kusaidia wanafunzi.

Ninaishauri Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, iboreshe mazingira ya utoaji wa elimu, pamoja na kufanya mikakati ya kuwatumia vijana hao kwa kupewa kipaumbele katika Vyuvo vyetu vya *VETA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Demokrasia, Bunge kama chombo cha kuisimamia na kuishauri Serikali lipewe fedha za kutosha.

Aidha, bajeti ya Bunge iwekwe kwenye kifungu cha matumizi maalum ili kuwe na uhakika wa Bunge kupata fedha za kutosha na wakati, ili Bunge na Kamati zake kukutana kwa muda wa kutosha kukamilisha majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba tuwe na maeneo machache ya vipaumbele kwa mfano, miundombinu ya reli na barabara. Tukamilishe ujenzi wa barabara kuu za kuunganisha Mikoa na nchi jirani ili kukuza biashara na kupata mapato ya Serikali.

Pia, tuongeze ukusanyaji wa mapato kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa kukuza wigo na kodi na kupunguza viwango ili watu wengi walipe; *Tax base* iwe kubwa mfano, *USA* ambapo ni wajibu wa kila mtu kulipa kodi na wanawajibika kwa sababu mzigo ni mwepesi.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya Elimu ya juu. Naomba uwekwe utaratibu wa kuhakikisha kila aliyekopa analipa kwa waajiri, kulazimishwa na Sheria kupeleka taarifa za wahitimu waliowaajiri; kila chuo kinachotoa shahada kiwe kinatoa cheti cha Bodi ya Mikopo kuonyesha kama mhitimu amekopa au hakukopa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ije na mpango wa uhakika wa kuzalisha umeme wa uhakika, mfano, *Stiglers Godge* na kuondokana na mipango ya dharura?

Mheshimiwa Spika, nashauri ufanyike mkakati maalum wa kuhimiza wawekezaji binafsi kuwekeza kwenye mashamba makubwa kwa kuwekewa vivutio. Hii itatoa ajira kwa vijana wengi na itakuza viwanda kwa kutoa malighafi, mfano kilimo cha Alizeti, Mahindi na Mpunga.

Mheshimiwa Spika, mfumo unaopendekezwa wa wanafunzi kusoma hadi kidato cha nne utazidisha kudumaza elimu. Lazima kuwe na madaraja ya kuchuja wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kuzungumzia suala la Muungano wetu. Muungano wetu ni kiungo muhimu sana katika nchi yetu kwa kuwa unaleta umoja na mshikamano na wananchi wake. Wako baadhi ya wananchi ambao hawanautakii mema Muungano wetu kwa maslahi yao. Hilo halikubaliki na nashauri Serikali iwe imara katika kuelimisha zaidi umuhimu wa Muungano wetu. Ingawa zipo changamoto za Muungano, lakini kwa kuwa Serikali inazifanyia kazi kwa kila siku, changamoto hizo zinakaribia kumalizika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu na kwa kina ili kumaliza kero za Muungano ili wapinga Muungano wakose hoja za kusema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulinda na kutetea Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Norway kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa dhati na heshima kukipatia umeme wa uhakika kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yanategemea sana nishati ya umeme katika kuleta maendeleo. Napenda kusema kwamba sasa Pemba inang'ara na wananchi wake wanaendelea na kujifanyia biashara mbalimbali na kazi tofauti kwa kujitea maendeleo yao. Wananchi wa Pemba wamekomboka na sasa Pemba itazidi kuimarika na watalii wanaanza kutembelea kisiwa hiki kwa kuwa kina umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu ni jambo jema sana katika kuiletea nchi maendeleo. Napenda kukishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuelimisha wananchi wa Tanzania juu ya kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, nafurahishwa sana na amani na utulivu uliopo Zanzibar kwa sasa. Napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi kwa kuwa na Serikali ya kitaifa na kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar bila kujali vyama vya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Naomba nigusie suala la uwezeshwaji wananchi kiuchumi. Katika kipindi kilichopita, zipo *SACCOS* nyingi ambazo hazikubahatika kupatiwa mikopo kama iliyokusudiwa. Watendaji waliokuwa wanatoa fursa za wakopeshwaji, baadhi walitumia ubinafsi, urasimu na kadhalika na kusababisha *SACCOS* nyingi kutofaidika na mikopo.

Wapo waliohisikuwa mikopo ya JK ni zawadi, wakawa wanasuasua kurudisha mikopo inavyostahiki, lakini wapo waliokuwa wanaona mikopo ni kukopa na kurudisha kwa wakati uliotakiwa lakini hawakuweza kufaidika na mikopo hiyo. Naiomba Serikali

iendelee kuweka mazingira mazuri ya kupatiwa mikopo kwa wale wasiopata kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia sekta ya elimu, afya na Muungano.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alizungumzia elimu katika kuiboresha na kuipa kipaumbele, ninampongeza. Lakini, mtazamo wangu katika elimu kwa kipindi hiki cha wanafunzi wetu kufeli, kwanza, ninawapa pole wanafunzi wote waliofeli, lakini pia ni mtihani wa Mungu.

Pia ninaipongeza Wizara ya Elimu kwamba safari hii imefanya kazi nzuri ya kudhibiti uchakachaji wa elimu na ndio maana vijana wetu baadhi yao walikuwa wanasubiri kupata mitihani kwa walimu na wazazi na kutojali kuhangaisha akili zao. Huo ulikuwa udhaifu katika jamii na sasa imebakia kunyoosheana vidole. Lakini tukubali kwamba jamii nzima inatakiwa kuangalia tulipojikwaa, siyo tulipoangukia.

Mheshimiwa Spika, sasa tuiombe Serikali kuwasaidia vijana wetu kurudia tena mtihani huo. Pia walimu, wazazi na wanafunzi kwa pamoja ni jukumu letu kuona vijana wetu wanafanikiwa badala ya kuilaumu Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa changamoto kwa kuunda Kamati ya Serikali zetu mbili; SMT/SMZ na kuchagua Kiongozi Mkuu wa nchi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile na kuwataka viongozi wakuu watendaji kutoka SMT/SMZ kushirikiana na Mheshimiwa Makamu wa Rais ili kusimamia kero za Muungano. Kwetu sisi Watanzania ni faraja na baadhi ya kero tayari zimeshakamilika na baadhi zinaendelezwa, zimo katika utekelezaji. Mtazamo wa Watanzania ni kuhubiri amani na utulivu ambao ndio mhimili wa ustaarabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anawapenda Watanzania na anaipenda nchi yake kwa vigezo alivyovitoa na changamoto alizotuarifu Wabunge kwamba mtazamo wake katika afya ni vipengele vinne vifuatavyo:-

- Kusogeza huduma za afya karibu na jamii;
- Kujenga uwezo wa ndani wa matibabu badala ya kutegemea kwenda nje;
- Kujenga uwezo wa kupambana na maradhi yanayoathiri na kuua; na
- Kuongeza ajira za madaktari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ni mtu mwenye busara na ari. Pia jambo analolisema tayari anakua amelifanyia utafiti na linakuwa linaweza kutekelezeka na hilo

ni changamoto kwa Watanzania kwa kuona kwamba Mheshimiwa Rais anawajali raia wake kwa kila nyanja ya maisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Masasi kwa kuniamini kuwa ninatosha kuwa Mbunge wao, hivyo kunichagua kwa kishindo sana. Ninasema asante sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, ametoa vipaumbele 13 ambavyo ndiyo itakuwa dira ya utendaji kazi wetu na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuzungumzia suala la amani katika nchi yetu na kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, tuna haki ya kuwapongeza viongozi wetu wakuu wa pande zote za Muungano kwa maridhiano yaliyotokea ya kuunda Serikali ya umoja wa kitaifa hali ambayo imeleta heshima kubwa kwa Taifa letu na kuleta umoja katika utendaji kazi ili kuleta maendeleo na amani huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kudumisha amani na kuwa na Taifa tulivu, ni lazima majibu ya Tume iliyoundwa ya kuchunguza migomo katika Vyuu Vikuu yatolewe.

Mheshimiwa Spika, binafsi napata utata, wanafunzi wa Vyuu Vikuu wanapodai kupata Sh. 10,000/= kwa siku kwa maana kwamba wapate Sh.300,000/= kwa mwezi wakati mfanyakazi aliyeajiriwa wa kima cha chini hajafikia kupata mshahara wa kiwango hicho. Hivyo, nashauri wanafunzi hawa pamoja na wazazi waelimishwe kutambua wajibu wa kuchangia katika elimu ya juu na Serikali isaidie kwa wale ambao uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni juu ya ukusanyaji mapato ya Serikali za Mitaa. Katika eneo hili la ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri zetu ni tatizo kubwa sana kwani watendaji wetu wamekuwa wabadhirifu wakubwa. Mapato mengi yanakusanywa, lakini hayafiki katika Halmashauri zetu, yanaishia mifukoni mwa watendaji wachache, hivyo kuzorotesha miradi na shughuli nzima za maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Masasi ni Wilaya ambayo hali ya uchumi ni nzuri, lakini fedha inayopangiwa kuendeleza miradi ya maendeleo ni ndogo sana hivyo kusababisha kuwa na miundombinu mibovu. Kwa mfano, upungufu wa madarasa katika



shule za msingi, shule za sekondari, nyumba za watumishi, barabara za Vijijini na Mjini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali pale wanaporipotiwa watendaji wanaohujumu mapato ya Halmashauri wachukuliwe hatua kali ili kukomesha vitendo hivi ambavyo vinachelewesha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuondoa umaskini kwa wananchi wetu, Serikali yetu ilipanga utaratibu wa kutoa fedha mkopo maarufu kama fedha za JK. Lengo hili ni zuri sana, lakini hadi hivi sasa wananchi wetu hawajanufaika sana hasa wananchi wa Vijijini ambao ndio hawa wanaoathirika na umaskini uliokithiri. Lakini wanashindwa kunufaika na fedha hizi kutokana na masharti yaliyopo kukidhi kukopesheka. Ushauri wangu kwa Serikali ni kutafuta njia mbadala ya kuwafikia wananchi Vijijini na kutoa mikopo hii kwani kwa kupitia Benki, wamekuwa wakinufaika wachache wenye uwezo waliopo Mijini tu, wale waliopo vijijini wakiendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba awamu hii tuzingatie hili ili mikopo hii ifike Vijijini kwani maisha ya wananchi wetu yanadidimia siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kulitakia heri Bunge hili liwe la amani. Mwenyezi Mungu atuzidishie busara ili tuweze kusimamia maendeleo ya wananchi wetu na kukidhi matarajio ya wananchi waliotupa dhamana kubwa ya kusimamia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, kila kitu ambacho utakiona katika mazingira yetu, katika nyumba zetu, wanasayansi wana mchango mkubwa mno. Zamani tulizoea kusikia watoto wetu waliofaulu mitihani ya kuanza Kidato cha Kwanza katika sekondari kama vile Ifunda, Mazengo, Mtwara, Moshi na kadhalika. Je, utaratibu huu umekwenda wapi? Watu waliomaliza katika shule hizi walikuwa muhimu sana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba ni wakati muafaka sasa kuruidia mfumo ule mzuri kila Wilaya iwe na shule ya ama ufundi au kilimo.

Mheshimiwa Spika, huduma ya afya kama zilivyo huduma nyingine, inakabiliwa na changamoto kadha wa kadha. Kwa mfano, Wilaya ya Ileje kuna hospitali moja ya Kanisa la Moravian ilianzishwa na Wajerumani ambao kwa sasa hawapo. Kwa ajili ya mazingira magumu na miundombinu duni, hospitali hii haina watumishi wa kutosha. Wengi wakifika kule hutoroka baada ya muda mfupi. Matokeo yake, wapo madaktari wazawa ambao wameamua kusaidia wazazi wao na kuendelea kufanya kazi pale.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba, kwa kuwa hospitali hii ndiyo inayotumiwa kama Hospitali ya Wilaya, naomba Serikali itoe chombo cha usafiri

(gari) kwa ajili ya wagonjwa wa eneo hilo na pia kuleta watumishi ambao watalipwa posho maalum ya kujikimu ya mazingira magumu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alieleza umuhimu wa kumarisha utawala bora, demokrasia na utawala wa sheria, pamoja na mambo mengine kama ya matumizi mabaya ya madaraka. Lakini kuna mambo mengi ambayo sisi kama Serikali tunatakiwa tuwe mfano. Hakuna uwajibikaji. Mfano, ni katika Bunge lenyewe. Wabunge hawatulii kuzingatia hoja, majadiliano na Miswada mbalimbali inayotolewa Bungeni. Kwa kuwa utandawazi unawafanya wananchi waone vitendo vyetu Bungeni, nao huamua kuiga na kutowajibika.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi tulikuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuwapata Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Watu hawa wanasimamia maendeleo ya taifa letu. Mimi nashauri turudi kwenye maadili, tuwajibike, watu wanaopewa madaraka wawajibike ili kutawala na wote tutimize wajibu.

Mheshimiwa Spika, naomba ifanyike tathmini ya kujua tangu Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge la mwaka 2005 na anapotoa hotuba hii ya Bunge la Kumi kwa mara nyingine: Je, hali ya mazingira ya nchi yetu ikoje?

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa ichukue hatua kwa Wakuu wa Wilaya na Mkoa na wote wanaohusika wanaoshindwa kusimamia sheria ya mazingira, watu wasimamie ili wasiwe karibu na vyanzo vya maji ili kuisalimisha nchi yetu.

**MHE. KIUMBWA M. MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kuingia tena Bungeni kwa kipindi kingine. Namwomba aniwezeshe niweze kulitumikia vyema. Nawashukuru wapigakura wangu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hotuba ya Rais, naomba nigusie vipengele viwili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hadi sasa katika sekta hii imekuwa inakua kwa kiwango kikubwa kwa kuweza kujenga shule kila Kata. Pamoja na mambo mengine, tunao upungufu wa maabara ya kutosha, walimu wanaoweza kutosheleza mahitaji kulingana na wanafunzi waliopo shuleni na pia ucheleweshaji wa mishahara ya walimu.

Mheshimiwa Spika, mapungufu hayo ndio yanayosababisha wanafunzi kutosoma kwa upana zaidi. Naomba Serikali ili kuondokana na tatizo la wanafunzi kufeli kwa wingi zaidi, ni vyema kero hizo zikashughulikiwa ipasavyo. Watendaji wa Wizara husika watekeleze majukumu yao waliyopangiwa kwa ufanisi zaidi. Suala la ujenzi wa nyumba za walimu yaangaliwe kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wasiokuwa na ajira na kila siku wanaendelea kuongezeka. Serikali iendeleo kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili vijana walio wengi waweze kupata ajira. Kuwahamasisha vijana kuendelea kujiunga na *SACCOS* ili kujikwamua kimaisha. Serikali ihakikishe kwamba wageni wasiwe na nafasi kubwa katika ajira hizo. Kujenga mazingira ya kuwawezesha vijana kupatiwa mafunzo ya namna mbalimbali ili waweze kumudu kazi watazoajiriwa.

Baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanyika na Serikali katika kupanua fursa za watoto na Vijana wetu wengi sana kupata elimu ya awali, Msingi, Sekondari, Ufundi na Elimu ya juu lakini bado kuna changamoto nyingi ambazo zinakabili Serikali na Jamii au walezi wa Vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yetu kwa kuongeza idadi ya Shule za Sekondari. Kuongezeka kwa Shule za Sekondari kumesaidia sana kwa vijana wetu kupandisha kiwango cha elimu toka vijana kuishia elimu ya msingi mpaka kufikia kiwango cha Kidato cha Nne.

Wasiwasi ambao unanipata kwa wazazi wenzangu ni matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne 2011. Lawama zote zinakwenda kwa Serikali na waalimu na kuwaweka wazazi pembeni.

Mheshimiwa Spika, kufaulu kwa wanafunzi kunategemea mambo makuu yafuatayo:-

- (a) Kuzaliwa;
- (b) Malezi;
- (c) Mazingira; na
- (d) Mwanafunzi Mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwanafunzi hawezi kufanya vizuri kama siku aliyozaliwa alipata matatizo ya kichwa, mfano kuvutwa na *vaccum*, kuchelewa kulia na kunyonyeshwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mtoto kuzaliwa ili afanye vizuri shuleni inategemea malezi ya wazazi au walezi. Kama atakuwa kwa kuelekezwa umuhimu wa elimu na kuhimizwa kujisomea, basi mwanafunzi atapenda shule na atakuwa na uhakika na kile anachokisoma na itakuwa changamoto kwake ya kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele hiki ndio kinakusanya mambo yafuatayo:-

- (i) Madarasa;
- (ii) Walimu;
- (iii) Maabara;
- (iv) Vitabu; na

(v) Vifaa vya michezo na kadhalika.

Serikali yetu inawajibika katika kipengele hiki kwa asilimia 100. Lakini pamoja na matokeo mabaya, bado Serikali yetu inajitahidi sana kupambana na changamoto hizo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, zinapungua kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, pia mwanafunzi mwenyewe aonyeshe kama anapenda shule. Kama hapendi Serikali hata kama ingefanya vitu vyote muhimu, kama mwanafunzi hapendi kusoma, hawezi kufaulu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufafanuzi nilioutoa, inaonekana wazi kuwa kuna umuhimu mkubwa wa wazazi kushirikiana na Serikali, waalimu, walezi wakiwaachia walimu na Serikali, basi uwezo wa kufaulu mwanafunzi ni *Division IV*. Vinginevyo maeneo hayo makuu manne wakishirikiana, hapo kuna uwezekano wa wanafunzi kufaulu kuanzia *Division I* mpaka iii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yetu kwa kupanua elimu ya Sekondari na mafanikio yapo sana, bali tupambane na changamoto zilizopo na hasa kutoa motisha kwa waalimu wote kuanzia Shule za Awali, Msingi Sekondari na Vyuvo kutokana na mazingira ya kazi yao na hasa wingi wa wanafunzi madarasani. Tuwapongeze sana walimu, wanajitahidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais na nampongeza sana kwa juhudi zake.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatuba nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nalipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanya hapa nchini hasa kupamaba na majambazi. Pongezi za kipekee ziwandee maaskari Polisi wa Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na *OCD* Kiruwaga. Kazi waifanyayo ni ngumu sana hasa kwa kuzingatia kuwa Wilaya ya Karagwe na Mkoa wa Kagera na Kigoma iko mpakani mwa nchi za Rwanda, Burundi na Uganda. Mara nyingi majambazi kutoka nchi hizi wamekuwa wakizishambulia sehemu za Karagwe na Mkoa mzima wa Kagera na Kigoma na kwa kuwa jeshi letu la Polisi halina vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari, pikipiki, fedha, mafuta na hata askari wa kutosha.

Ningependa kuiomba iutangaze Mkoa wa Kagera na Kigoma kama Mkoa Maalum wa Kiulinzi kama ilivyo kwa Wilaya ya Tarime, Kinondoni, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo na kilimo, naomba Serikali ianzishe haraka iwezekanavyo utaratibu wa kununua mazao ya nafaka kwa vipimo vya kilogramu na siyo kwa debe, gunia au kwa kukadiria. Sambamba na hilo, nashauri Serikali ilete utaratibu wa kununua mifugo minadani kwa kuwapima kwenye mzani badala ya kumkadiria mnyama. Benki ya Kilimo itakayoanzishwa iwe na matawi yake katika kila Wilaya hapa

nchini ili kuwarahisishia wananchi wa vijijini kupata mikopo hiyo bila kusafiri kwenda Dar es Salaam kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa madawa ya mifugo hasa madawa ya kuua kupe na inzi. Lakini kwa masikitiko makubwa dawa hizi za ruzuku haziwafikii wafugaji wa vijijini ambapo ndio walengwa, badala yake dawa hizi zimeishia mikononi mwa wajanja wachache. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha dawa hizi zinawafikia wafugaji wa vijijini na mijini pia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya maji Wilaya Karagwe, ni tatizo kubwa sana. Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe ikiwemo miji ya Kayanga na Omurushaka haina maji na kama yapo ni kidogo sana labda asilimia thelathini tu. Ni kwanini Serikali haipeleki huduma ya maji kwa wananchi hawa? Serikali imekuwa ikilitangazia Bunge hili kuwa mradi wa maji wa Benki ya Dunia katika vijiji mbalimbali Wilayani Karagwe ungeanza. Hadi sasa huduma hiyo haijaanza na wananchi wamechoka kusubiri. Ni vizuri tujue mradi huu umekwama wapi na je ni juhudi zipi zinafanywa na Serikali kuleta maji katika vijiji hivi? Mkoa wa Kagera unapakana na Ziwa Victoria, pia una mto Kagera na maziwa madogo madogo yakiwemo ya songambebe na kadhalika. Kwa masikitiko makubwa, Wilaya ya Karagwe haina maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya binadamu, pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Wanyamapori ya Kimisi na Burigi imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Kata za Nyakasimbi, Ihembe, Kihanga, Nyakakika, Rugu na Rugera kwa wanyama wakali tembo na simba kushambulia wananchi na mali zao. Idara ya Hifadhi ya Wanyamapori imeshindwa kabisa kuwadhhibiti wanyama hao. Naomba na kushauri Serikali kuwa *National Parks* kwa kuzifanya *National Parks* ulinzi utakuwepo kwa kuwadhhibiti wanyama wakali. Naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono mia kwa mia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani imegusa maeneo yote muhimu nchini. Tatizo langu ni maji, umeme na elimu. Mambo haya matatu ni muhimu sana nchini.

Mheshimiwa Spika, maji limekuwa tatizo kubwa sana nchini ukizingatia kuwa mvua hazikunyeshia. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, tunaweza kusema ni janga kubwa la kitaifa. Ninaiomba Serikali itazame janga hili na iweke mipango ya dharura ili kuwanusuru wananchi juu ya tatizo hili nchini.

Mheshimiwa Spika, umeme umekuwa na matatizo ya umeme katika sehemu nyingi nchini kwa kutegemea umeme upatikanao na maji. Tuache sasa kutegemea umeme wa maji wakati tunayo gesi, makaa ya mawe upepo wa kutosha. Mtwara na Lindi hatujawahi kutumia umeme wa *grid* tangu tupate uhuru kwa kuahidiwa kuwa tutapewa umeme wa SongoSongo Kilwa ambao uligunduliwa mwaka 1977 na umeme wa Mtwara Mnzabai uliogunduliwa mwaka 1982. Lindi uhitaji umeme KW 3000 tu katika Wilaya zake zote Kilwa, Liwale, Nachingwea, Ruangwa na Lindi Mjini na Vijijini. Tunaomba

Serikali utuonee huruma, itusaidie umeme. Sasa Liwale, Ruangwa na Nachingwea hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, elimu ni matatizo Mkoani Lindi tangu enzi za ukoloni hadi sasa. Tunaomba tupatiwe walimu wa shule zetu ziboreshwe, Serikali ituone kwa jicho la huruma. Mpango wa dharura ufanyike kwa ajili ya Lindi tu kuhusu elimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SUBIRA KHAMIS MGALU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa maandishi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na wapigakura ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Kikwete na Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kwenye uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, hivyo kupata ridhaa ya kuendelea kushika dola.

Mheshimiwa Spika, pia nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili la Kumi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza katika kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri aliyoitoa iliyojikita kwenye vipaumbele 13 vilivyotokana na Mkataba wa Chama cha Mapinduzi na wananchi, yaani Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Mchango wangu utajielekeza zaidi kwenye kipaumbele Na. 7 juu ya: “kuboresha zaidi ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa pamoja na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele Na. 7 ni muhimu sana kikatiliwa mkazo. Katika kupitia ukusanyaji mkubwa wa mapato, Serikali itaweza kutekeleza vipaumbele vingine vyote mfano, kupitia mapato, Serikali itatoka huduma bora ya elimu, afya maji na uwezesaji wa wananchi na kadhalika.

Ni kweli ulio wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imeongeza sana jitihada katika kukusanya mapato. Hata hivyo, bado ipo mianya ya uvujaji na ubadhirifu katika mapato yanayokusanywa, vitendo vinavyofanywa na watumishi wasiokuwa waaminifu hasa katika Serikali za Mitaa. Naipongeza sana Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa jitihada zao katika ukusanyaji mapato na kuweza kuvuka lengo kila mara.

Mheshimiwa Spika naiomba Serikali ya Awamu ya Nne kuendelea kudhibiti vitendo vya hujuma dhidi ya mapato yanayokusanywa na Halmashauri zetu. Pamoja na nia nzuri ya uboreshaji na ukusanyaji mapato kupitia mawakala hasa katika adhima ya kupinguza gharama za kukusanya mapato kupitia watendaji, bado utaratibu huu umechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa mapato kutokana na Mawakala kukosa uaminifu. Mikataba ya ukusanyaji mapato humnufaisha zaidi Wakala kuliko Halmashauri

husika kama ilivyojitokeza kwenye mkataba wa ukusanyaji mapato wa kituo kikuu cha mabasi ya kwenda Mikoani, Ubungo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, naiomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuangaliwa upya utaratibu wa ukusanyaji mapato kupitia Mawakala hasa juu ya faida na hasara zake kwa kulinganisha utaratibu wa zamani na ikiwekezakana Serikali izishauri Halmashauri mbalimbali kuacha utaratibu wa kutumia Mawakala katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali za Mitaa ziimarisha vitengo vya mapato kwa kuajiri wataalam waaminifu na kufanya tafiti za vyanzo/uwezo wa Halmashauri husika katika ukusanyaji wa mapato kabla hawajaingia mkataba na wakala na ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, naunga mkono msimamo huu wa Mheshimiwa Rai wetu kwani ni miaka mingi sasa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mapungufu ya nidhamu katika matumizi ya pesa za Serikali hasa katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana hatua ya Serikali kuanzisha Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa ndani ambapo Wakaguzi Wakuu wa hesabu wa Ndani wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa watawajibika kwake moja kwa moja.

Wakaguzi Wakuu wa Hesabu wa Ndani ni wadau muhimu sana katika usimamizi wa matumizi ya pesa za umma hasa katika Serikali za Mitaa. Pia nawashauri Waheshimiwa Madiwani katika eneo la usimamizi wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, nashauri:-

- (i) Serikali iwezeshe zaidi Ofisi mpya ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kwa kupitia rasilimali fedha na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake;
- (ii) Serikali Kuu ihakikishe vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa inaimarishwa kirasilimali fedha na watu ili kitengo cha ukaguzi wa ndani kijitegemee;
- (iii) Serikali iendeleo kuimarisha na kiwezesha Ofisi ya CAG kwa kuipa uwezo wa kuajiri na rasilimali fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kiufanisi ya usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali; na
- (iv) Serikali ichukue hatua madhubuti mara kwa mara katika kutekeleza mapendekezo ya Ripoti ya CAG na za Wakaguzi wa ndani ili kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali na kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa watendaji inapodhibitiwa kuwa kuna ubadhirifu wa pesa za umma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imetuma Msajili wa Hazina kuchukua hatua ya haraka na kukaa na Wajumbe wa Bodi wanaoiwakilisha Serikali kuchukua hatua za haraka kunusuru hali ya mambo. Risala ya wafanyakazi na Hotuba ya Menejimenti nilipeleka nakala zake kwa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Rais amezungumzia ujenzi wa barabara kwa mujibu wa ilani ya CCM. Nimepitia ilani husika ambayo imesema tu kwa ujumla kuwa itatenga fedha za maendeleo ya barabara Dar es Salaam (64(b)).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Dar es Salaam inatoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa na kwa kuwa kuna uwezekano wa kuibuka foleni ya zaidi Dar es Salaam wakati wa ujenzi wa barabara za mradi wa mabasi yaendayo kasi, Serikali ijenge kwa dharura barabara za Mbezi - Goba, Mbezi - Ukonga, Kimara - Tabata, Msewe - Ubungo, Korogwe - *External* ziweze kuchuja magari. Upembuzi yakinifu wa barabara hizi umeshakamilika. Katika kupambana na rushwa kubwa kama moja ya masuala yaliyotajwa na Rais, ni vizuri hotuba ya Rais ambayo toka irudishwe Ikulu haijawahi kurejeshwa tena Bungeni, Serikali itoe tamko kuhusu taarifa zinazoendelea kuandikwa na vyombo vya habari kuhusu Kagoda na Dowans kwa kuwa wakati Serikali inasema wahusika hawajulikani, magazeti yanawataja wahusika kwa majina tena wengine ni Wabunge. Kuhusu michezo na utamaduni, ni vizuri katika kipindi hiki Serikali ikakubaliana na CCM kurejesha viwanja vilivyochukuliwa na CCM nchi ilipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu Muweza wa yote kwa kunijalia kuwepo Bungeni tena baada ya mchakato wote wa Uchaguzi. Pia nawashukuru sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT (M) wa Morogoro na hatimaye Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT(T) kwa kuniamini na kunipa dhamana hii ya uongozi tena. Pongezi kwako Spika, Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kushika dhamana hizo bila kuisahau timu ya Serikali nikianza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Waziri wote.

Baada ya Utangulizi huu, nina machache ya kuchangia. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweka msingi wa vipaumbele vyake kuwa cha kwanza ni umoja, amani, usalama na utulivu nchini. Ni ukweli usiopingika kwamba bila amani hakuna maendeleo yoyote yatakayopatikana. Hivyo, ni wajibu wa Watanzania wote bila kujali itikadi, rangi, dini na kadhalika kudumisha amani, umoja uliopo kwa manufaa yetu sote. Hata hivyo, matukio ya hivi karibuni ya maandamano yasiyo na mpangilio, migomo na kadhalika yanaashiria kuwa kuna baadhi ya Watanzania wamechoshwa na amani iliyopo, hivyo natoa rai kwa Serikali kukomesha vitimbwi hivi haraka ili visiwe ni mazoea hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipaumbele cha tatu kinachozungumzia uwezeshaji wananchi wa makundi yote kiuchumi katika jitihada za kupunguza umaskini. Kwanza,



nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa aliyoyasimamia kwa miaka mitano iliyopita na utawala wake kuhusu kipaumbele hiki. Hata hivyo, kwa upande wa kundi la wananchi wenye ulemavu, nashauri kuwa kwa vile kupata mikopo toka Benki mbalimbali ni vigumu, yafaa fedha za mifuko ya vijana na wanawake kwenye Halmashauri zitengwe angalau asilimia 20 ya fedha hizo kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana wenye ulemavu. Mheshimiwa Spika, bila ku-*streamline* suala hili watu wenye ulemavu wanasahaulika katika Halmashauri zilizo nyingi nchini. Ni wajibu wa Maafisa Ustawi wa Jamii walioko Wilayani kuhamasisha kundi hili la jamii kuunda vikundi vya uzalishaji ili liweze kukidhi vigezo vya kukopesheka toka mifuko hiyo.

Kuhusu kipaumbele cha saba kihusucho ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi, nashauri Serikali Kuu na za Mitaa zibuni aina za kodi ambazo wananchi wengi wanaweza kulipa kidogo (kuongeza uwigo) kidogo bila kuathiri sana vipato vyao kuliko hali ya sasa ya kutegemea vyanzo vichache. Kama kodi ya mapato toka kwa wafanyakazi wa Serikalini, wafanyabiashara wachache na wengine hukwepa wajibu wao na kadhalika.

Kwa upande wa matumizi, nakubaliana na Hotuba hii kwamba lazima pawe na nidhamu ya matumizi kwa manufaa ya Umma, la sivyo inakatisha tamaa hata kwa walipaji kodi wenyewe (wafanyakazi) na kuweza kuwa chanzo kimojawapo cha migogoro kazini.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu aliyeniwezesha kurudi kipindi cha pili humu Bungeni. Pili, nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Morogoro na wale wote walioniwezesha kurudi humu Bungeni, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri kwa uteuzi wao. Mheshimiwa Spika, nawapa pongezi Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa wakati akifungua Rasmi Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma 18 Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, sipashwi kuijadili, kwani ni hotuba nzuri, iliyojaa busara, nzuri sana, inayotuongoza tufanye nini ili kuwaletea Watanzania maendeleo wanayoyataka na kuyatamani.

Mheshimiwa Spika, viongozi wote, watendaji wote, viongozi wa Serikali na vyama, inapaswa waisome na kuelewa hotuba ya Mheshimiwa Rais, hotuba inayotaka kujenga na kuleta maendeleo ya nchi yetu. Kwa hilo tuwe wote pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu chini ya uongozi wa Chama Tawala (CCM), inawapenda na kuwajali wananchi wake. Kwa hiyo, ni vizuri kila mwananchi afanye yale yote mazuri ya kuijenga nchi yetu na yanayopaswa kumkomboa Mtanzania kumtoa katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele 13 alivyovitoa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake nzuri, ni vyema kila mmoja wetu, hasa Waheshimiwa Wabunge, wawakilishi wa wananchi waliowachagua, na kuwawezesha kuja humu Bungeni, waangalie vipaumbele hivyo 13 kwa umakini na kuona jinsi ya kuvitekeleza.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vinaeleweka, viongozi, Waheshimiwa Wabunge, tufungue mada na kutafuta kila njia kuona jinsi ya kutekeleza kimoja baada ya kingine au vingine kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, inawezekana. Tufanye kazi kwa pamoja, tuwashirikishe wananchi, yote yatatendeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Rais wetu Dr. Jakaya Mrisho Kikwete imefanya mengi mazuri.

- Kilimo kwanza, vocha zimetolewa kwa wakulima;
- Shule za Sekondari kila Kata zimejengwa;
- Shule za Msingi zimeongezeka, barabara zimetengenezwa, viwanja vya ndege vinaendelea kukarabatiwa, wanufaika wa maji safi na salama wameongezeka;
- Wanufaika wa nishati na umeme angalau kidogo wameongezeka, afya imeboreshwa kwa wananchi, vifo vya watoto wadogo na akina mama wanaojifungua vimepungua, dawa za UKIMWI na vyandarua (Malaria) vimetolewa, Zahanati, vituo vya afya na hospitali zimejengwa na zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, hongera Serikali yetu chini ya CCM. Kweli Ilani yetu ya Uchaguzi imetekelezwa. Cha msingi tuendeleo kutimiza na kutekeleza yote yaliyoko kwenye hotuba. Kwa moyo wote, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SAID R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza wananchi katika kuitikia wito wa ujenzi wa Sekondari za Kata, pia nichukue fursa hii kuipongeza Serikali katika kuwaunga mkono wananchi katika kutekeleza jukumu hilo. Sambamba na hilo, napenda kutoa maoni yangu katika maeneo

manne yafuatayo: *Mass Failure*, Ujenzi wa Vyuo vya VETA, Kuendeleza Elimu ya Kati na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, *Mass failure* tuliyoipata katika matokeo ya kidato cha IV kwa mwaka jana, 2010 ni matokeo ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Nne mara tu baada ya kuchukua dola hapo 2005. Kwa mwaka 2006 Serikali ilitilia mkazo wa pekee katika kuanzisha Sekondari za Kata na wananchi waliitikia sana wito huo. Hivyo, kwa sababu shule zilijengwa nyingi sana mwaka 2006, ina maana ulipofika mwaka 2007 wanafunzi wengi walijiunga na Sekondari na ndio hao hao ambao wamemaliza Kidato cha IV mwaka jana. Ombi langu ni kwamba Serikali iongeze kasi ya kuandaa Walimu ili iende sambamba na wingi wa wanafunzi ambao sasa utaendelea mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, hii pia iwe sambamba na ujenzi wa miundombinu ya Sekondari kama vile nyumba za Walimu, maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Vyuo vya VETA ni jambo la msingi sana. Kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwamba kila Wilaya kitajengwa Chuo cha namna hiyo. Hili ni jambo la muhimu sana kwani kama nilivyosema hapo juu ni kwamba kuanzia mwaka 2007 wanafunzi wanaojiunga na masomo ya Sekondari wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo ni vizuri Vyuo hivyo vianzishwe haraka ili viweze kuwachukua vijana ambao wanamaliza Kidato cha IV. Ikumbukwe kwamba sio wanafunzi wote wataendelea na masomo ya Kidato cha V.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Uendelezaji wa Vyuo vya Kati, yaani *Tertiary Colleges* kama vile *CBE, IMF* na kadhalika. Vyuo hivi ni muhimu sana ili kuweza kuwaendeleza vijana wanaomaliza Kidato cha IV na VI ili kuwapa uwezo wa kupata elimu itakayowasaidia vijana hao.

Mheshimiwa Spika, Suala la mwisho katika elimu ni juu ya Bodi ya Mikopo. Bodi hii inaonesha ina matatizo makubwa katika uendeshaji wake. Binafsi hainingii akilini kuwa inakuwaje Bodi inakawia kuwapa fedha vijana wanaosoma vyuo vyetu, lakini vijana hao hao wanalipwa fedha hizo mara tu baada ya kugoma, kuna nini? Ni kweli pesa hizo hukwama Hazina hadi pale vijana wanapogoma ndio zitolewe, au fedha hizo ziko Chuoni ila kuna mtu anacheza nazo? Naomba Wizara ichukue juhudi za makusudi katika kukomesha utaratibu huo wa Bodi ya Mikopo, ambao kwa hakika haukitakii heri hiki chama chetu cha CCM.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea machache kwenye elimu, naomba nichukue fursa hii kusema machache juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Wananchi katika Kijiji cha Saadani, kilichomo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani, wananyanyaswa sana na askari wa hifadhi hiyo. Kubwa hapa ni Serikali ione umuhimu wa kuongeza angalau kidogo mipaka ya Kijiji hicho kwani kina eneo dogo sana ukilinganisha na Vijiji vingi vilivyomo jimboni kwangu. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba eneo hilo kabla ya kuwa Hifadhi ya Taifa, wananchi wa eneo hilo walikuwa na mapenzi makubwa na wanyama hao na ndio maana kwa muda huo wote waliwatunza na hatimaye Serikali ikaona yafaa eneo hilo sasa liwe Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya ni Sekta ya muhimu sana ambayo ikiboreshwa itagusa maisha ya Watanzania wengi. Kuna mpango wa (MMAM) Sera ya Afya ya 2007 (Maendeleo ya Afya ya Msingi) Sera hii bado haijafikia malengo yake manne ambayo ilikusudia suala la kuongeza Madaktari na Wauguzi kusogeza huduma za afya wanapoishi watu. Huduma hizi za Zahanati bado hazijawafikia watu wengi na wengi bado wanatembea zaidi ya kilometa tano kupata huduma hizo. Japo sera ya MMAM imefikia nusu ya miaka 10 ya utekelezaji wake, mfano bado hospitali za Wilaya hazina vyumba vya operesheni (*thieter*), vitanda, havitoshi, mashuka hayatoshi kwa wagonjwa wa operesheni.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa nchini limekuwa likizidi kukua zaidi. Mfano, Taasisi ya *FORDIA* chini ya Mkurugenzi wake Buberwa Kaiza, ilieleza jinsi Wilaya mbalimbali zikiongoza kwa rushwa kama vile Babati na nyinginezo. *PCCB* iangalie upya mikakati yake ya kupambana na rushwa badala ya kujenga majengo au ofisi katika Mkoa na Wilaya mbalimbali, wamalize kwanza rushwa ndipo waboreshe ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, *Job Centres* zianzishwe kwa Wilaya mbalimbali ili vijana wapate ajira. *Machinga Complex Centres* zianzishwe kila Mkoa na Wilaya, sio tu Mwanza na Dar-es-Salaam, ili vijana wengi ambao ni machinga wapate maeneo ya kufanya biashara badala ya kufukuzwa ovyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha elimu, shule za Kata zipatiwe madawati yakutosha, vitabu, maabara, badala ya kuchangisha wananchi michango yote. Walimu wapelekwe katika shule hizi, mitihani ya *Form II* irudishwe. Bodi ya mikopo iangaliwe upya ili migomo ya Vyuho Vikuu ipungue, mikopo wapatiwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri kwa Watanzania. Kutokana na vipaumbele alivyovitoa, naomba kuchangia mambo machache kuhusu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni suala la maji. Hapa nchini kumekuwa na kilio kikubwa kutoka kwa wananchi vijijini kuhusu tatizo la maji. Kweli hili ni kero kwa wananchi wengi. Lakini imedhihirika wazi kuwa fedha inayotolewa na Serikali ni kidogo sana kwa Sekta hii muhimu. Nashauri Wizara hii iongezewe fedha ya kutosha katika *budget* ya mwaka 2011. Hata hivyo, nashauri pia Wizara iendelee kuratibu miradi mingine inayotekelezwa na Wahisani mbalimbali katika maeneo tofauti hapa nchini, ili Serikali ifahamu namna tatizo la maji linavyoendelea kupungua au kuhitaji ushauri wa kitaalamu katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu afya. Pamoja na juhudi kubwa ya Serikali kusambaza huduma ya afya katika ngazi zote hadi vijijini, ningependa kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nashauri kwamba *Dispensary* zote ambazo zimejengwa katika vijiji hivi sasa zipelekewe vifaa, watendaji wa kutosha kuhudumia maeneo hayo yote, kwani imejitokeza kuna upungufu mkubwa wa mahitaji hayo hali ambayo inafanya wananchi wakate tamaa.

Pili, kwa kuwa ujenzi wa *dispensary* vijijini ni mradi mkubwa sana, nashauri mipango ya kuwaandaa wataalam na vifaa vya kutosha ianze mapema hivi sasa ili nchi isipate matatizo kama ilivyokuwa katika ujenzi wa Shule za Sekondari zilipojengwa shule nyingi katika Kata, wakati walimu hawajaandaliwa wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu hali ya uharibifu wa mazingira. Hapa nchini tatizo hili ni kubwa sana na ni muhimu sana Serikali ikaandaa mpango kabambe wa kuhakikisha suala la kusimamia hifadhi ya mazingira, linasimamiwa kwa nguvu zetu zote. Hali inayoendelea hivi sasa ya mabadiliko ya hali ya hewa inatisha.

Ukame unaoendelea kujitokeza hivi sasa ni kifo kwa viumbe vyote na kuchangia katika matatizo ya njaa. Nashauri Serikali iandae kongamano kubwa litakalowashirikisha viongozi wa kitaifa, Mkoa hadi Wilaya ili kujadili kwa undani juu ya mipango ya kitaifa ya kunusuru hii hali mbaya ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais kwa kujali na kuona umuhimu wa usafiri wa majina na maeneo ya bandari ambamo meli hizo zinafika na kuondoka. Pamoja na hotuba ya Rais, kutaja bandari zitakazopewa umuhimu wa kuwekewa vifaa katika kipindi hiki, ni muhimu kuuangalia usafiri katika Ziwa Nyasa pamoja na bandari zake, hasa ukarabati na ujenzi wa gati katika bandari mpya ya Kiwira, Itungi *Port*, Makonde, Manda, pamoja na *Mbamba Bay*, ambayo iko katika mpango. Kwa kufanya hivyo, wananchi waishio mwambao mwa ziwa hilo watapata unafuu wa usafiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai na kuweza kuwapa karama wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kunichagua kuwa Mbunge wao. Aidha, napenda kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Nanyumbu kwa ushindi mkubwa walionipa na kwa kukipa ushindi Chama cha Mapinduzi (*CCM*).

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake

nzuri ambayo imeainisha vipaumbele 13, hivyo kuwa dira nzuri kwa mustakabali wa Taifa letu katika miaka mitano ijayo. Katika moja ya vipaumbele ndani ya hotuba ya Rais ni kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Taifa lolote lisilokuwa na uchumi unaokuwa na lisilogubikwa na umasikini linakuwa ni Taifa ambalo haliwezi kuendelea na wananchi wake kukumbwa na umasikini mkubwa. Moja ya maeneo ambayo wananchi wake wengi ni masikini ni Wilaya ya Nanyumbu. Kipato cha wananchi katika Wilaya yangu ya Nanyumbu ni kidogo. Umasikini huu unatokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

- kilimo duni kutokana na zana duni za kilimo, ukosefu wa pembejeo na ukosefu wa elimu ya ugani.
- Bei ndogo za mazao wanazopata wakulima ambazo haziwiani na gharama halisi.
- Ukame ambao umeathiri maeneo mengi Wilayani Nanyumbu na athari za tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo kwa wananchi wengi Wilayani Nanyumbu na kutokana na mapungufu au changamoto hizo hapo juu, zimepelekea wananchi wengi kuwa na kipato duni na hivyo kuwafanya wawe masikini. Ninaomba sana Serikali ya Awamu ya Nne iwakwamue wananchi wa Nanyumbu waondokane na lindi kubwa la umasikini. Jitihada ziongezwe na Serikali yetu ya Awamu ya Nne iwawezesha wananchi wa Nanyumbu kiuchumi ili waweze kushiriki na kunufaika na uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, maliasili ni moja ya vipaumbele vilivyopo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wilayani Nanyumbu, kuna urithi mwingi wa Maliasili lakini urithi huu hauwanufaishi watu wa Nanyumbu. Kuna misitu ya uwindaji ambayo ina wanyama wengi lakini haitunufaishi sisi wana – Nanyumbu. Kuna Mto Ruvuma ambao una samaki wengi, lakini wananchi wamekuwa wakinyanyaswa pale wanapovua samaki katika Mto Ruvuma. Ninaomba Serikali iwaelekeze wahusika wawape fursa wananchi wavue samaki ili waweze kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya elimu, Nanyumbu imepiga hatua ndani ya muda wa miaka michache. Pamoja na mafanikio hayo, kuna tatizo kubwa la miundombinu na vitendea kazi. Kuna tatizo la uhaba wa madarasa, tuna tatizo kubwa la uhaba wa madawati, uhaba wa matundu ya choo, uhaba wa nyumba za walimu, uhaba wa hosteli za wanafunzi, uhaba wa maabara na vitabu. Hivyo, ninaomba Serikali ya Awamu ya Nne itusaidie kupunguza kero hizi ili elimu Wilayani Nanyumbu ipate kukua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za kiuchumi na kijamii, maji ni kero kubwa sana Wilayani Nanyumbu. Ninaomba Serikali itusaidie wananchi wa Nanyumbu kwa kutupatia huduma ya maji.

Ninaomba Serikali yangu Tukufu ione uwezekano wa kutumia maji ya Mto Ruvuma ambayo yanapotea bure kwa kuyasambaza kwa wananchi waweze kupata maji safi na salama. Kwa upande wa afya, naishukuru Serikali kwa kukarabati Kituo cha Afya cha Michiga. Lakini tatizo kubwa ni uhaba wa wahudumu wa afya na dawa katika Zahanati zake. Aidha, tunaomba kupatiwa hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara, napenda kuchukua fursa hii kushukuru kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Masasi hadi Mangaka. Ila ninaomba kuikumbusha Serikali kutimiza ahadi za chama (Ilani) kwa ujenzi wa barabara ya kutoka Mangaka hadi Mtambaswala na ile ya kutoka Nangomba hadi Mtambaswala kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa kwanza mwanamke kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Rais kwa kuchaguliwa kwake na kupeperusha bendera ya CCM vyema. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kalambo na Wilaya mpya ya Kalambo kwa kura zao nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi na mimi binafsi kuniwezesha kuingia Bungeni kuwatumikia, nawaahidi kuwatumikia kwa uwezo wangu wote ili kauli mbiu yetu ya nuru mpya ya Kalambo: “Kwa Pamoja Tunaweza” iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, naomba nichangie hotuba ya Rais. Naomba nijielekeze katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuja na mkakati maalum wa Kilimo Kwanza. Sera hii imekuwa na tija pamoja na kwamba imekuwa na changamoto za hapa na pale, naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya pembejeo zimekuwa kubwa kiasi kwamba imekuwa vigumu sana kwa wananchi wa kipato cha chini kuweza kumudu bei kubwa na bei hizi kubwa zikiwa zimetokana na waagizaji binafsi kupandisha bei kiholela na hasa baada ya Shirika la Serikali kushindwa kuagiza pembejeo baada ya kupata hasara iliyotokana na kushuka na kuanguka kwa bei kutokana na mdororo wa uchumi wa dunia. Nashauri shirika hili lifidiwe mapema ili kusiwe na upandaji bei kiholela.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya uwezekano wa kuwapatia bure pembejeo kwa wananchi wasio na uwezo kabisa kama inavyofanya kwa kila kaya. Pia nashauri vituo vya kununulia mahindi viongezwe na wakala *NFRA* kuliko vichache vilivyopo ambavyo vinakuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Kalambo.

Mheshimiwa Spika kuhusu naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayoifanya ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zinazoendelea Mkoani Rukwa na Katavi, zile za kutoka Sumbawanga - Tunduma, Sumbawanga - Mpanda, Sumbawanga - Kasanga.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifikirie kwa umakini sana ujenzi wa barabara iliyokuwa ikitumika zamani maarufu kama barabara ya Mjerumani itokayo Isanga Tunduma kupitia Ilonge Jimbo la Kalambo kupitia Legezamwendo, Kalepula, Mwimbi, Kamawi, Tatanda, Nondo, Kamkolwa daraja la Kalambo na kuunganisha barabra ya kwenda bandari ya Kasanga.

Mheshimiwa Spika, barabra hii ni muhimu sana kiuchumi lakini pia inapunguza mzunguko kwa zaidi ya kilomita 70 kwa mtu ambaye hana haja ya kwenda mpaka Sumbawanga akiwa na nia ya kwenda bandari ya Kasanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uvuvi, naishukuru na kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwajali sana wananchi wajiongezee kipato. Naomba niikumbushe Serikali kwamba ijielekeze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kalambo waishio mwambao wa ziwa Tanganyika ambao shughuli yao ni uvuvi ambao kwa bahati mbaya wanavua kwa kutumia zana ambazo ni duni sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijielekeze kuwasaidia wananchi ili wawe na uvuvi wenye kuleta tija. Kutokana na zana duni uvuvi, wetu umekuwa wa kuhabahatisha na unafanyika muda wa usiku tu na kipindi cha giza na kuishia kuvua samaki wadogo tu na kushindwa kuvuna samaki kama aina moja ijulikanayo kama *English fish*. Aina hii ya samaki wakubwa na wazuri hatuwezi kuwavua kwa zana zetu duni. Naiomba Serikali ielekeze nguvu kwa kuwakopesha na kuweka ruzuku kwenye zana za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika suala zima la ardhi ambalo Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa nia yake thabiti ya kuhakikisha kwamba ardhi inapimwa na kumilikishwa kwa vijiji kwenye mabengi na vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, ardhi imekuwa na migogoro mingi juu ya umiliki kwa mfano katika Jimbo langu la Kalambo, ardhi walioiachia Serikali yao wakati wa uanzishaji wa ranchi ya Kalambo ya Serikali wamejikuta hawana ardhi ya kilimo baada ya shamba hilo la Kalambo kumilikishwa kwa watu binafsi bila hata kuihusisha Halmashauri na vijiji husika, vijiji vilivyoathirika ni pamoja na vijiji vya Katapulo, Mbuluma, Mao na Mkowa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maliasili na mazingira, ninashauri Serikali iongeze nguvu katika kuvitangaza vivutio vyetu vya maporomoko ya mto Kalambo ili yawe na manufaa kama wenzetu wa upande wa pili wa Zambia wanavyofaidi japo maporomoko yanaonekana vizuri zaidi ukiwa upande wa kwetu.

Mheshimiwa Spika, mazingira yanaharibiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na ukataji miti kwa ajili ya mkaa. Naishauri Serikali ijikite katika utafiti ili wananchi



watumie makaa ya mawe katika shughuli za majumbani kwani wananchi wamekuwa wakilalamikia hewa ya mkaa na kutoboka kwa masufuria.

Naomba utafiti ufanyike ili tuweze kutumia makaa ya mawe yanayopatikana kutoka machimbo ya Namwele na Mpanda.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Rais. Kwanza, nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kutunga sera zinazotekelezeka. Napenda kupongeza maendeleo ya afya ya msingi (MMAM) na ikatekeleza, pia kwa kuweza kuongeza ajira ya Madaktari, Wauguzi na watalaamu ili kuongeza na kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais kwa kuweza kutupa upeo wanawake kutaka tujitokeze kwa wingi kugombea nafasi ili nasi tuwe mbele kwa maendeleo. Nashukuru wanawake tumejitahidi sana kujitokeza japo hatukufikia lengo asilimia. Napenda kuwaomba wanawake wenzangu waliokuwa hawajafanikiwa wasivunjike moyo, waendeleo kuwa na nia hiyo hiyo wasikate tamaa watahinda iko siku.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapa changamoto wale wanaoogopa kujitokeza, wasiogope, tunaahidi tutawasaidia. Namwomba Rais atusaidie ili tuwape mafunzo tuondokane na uwoga tulionao. Tunaamini wanawake tunaweza sababu ni kuwa Spika wa Bunge letu ni Mwanamke ambaye anaweza kutuongoza vizuri bila uwoga, anajiamini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza sana kwa kazi yako nzuri, namwomba Mungu akuwezeshe zaidi ili utuongoze vyema zaidi. Napenda kuvipongeza vipaumbele vyote alivyovitoa Rais. Naomba kutoa ushauri kuhusu kulipia kodi kwa kuwa kodi ni jambo la Muungano, ninashauri kama utalipa kodi Zanzibar mfano gari, basi gari hilo likisisafirishwa toka Zanzibar kwenda Dar lisilipiwe tena badala yake itambulike kuwa imelipiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura za kishindo. Hii ni ushahidi wa kutosha kuwa wanawake tuna uwezo mkubwa.

Vile vile ninampongeza Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitakuwa sina fadhila kama sitawapongeza wanawake wa Mkoa wa Singida kunirudisha tena Bungeni kwa Awamu ya Tatu kwa kura za kishindo ambazo zilinipa nafasi ya kwanza kama ilivyokuwa awamu zote mbili zilizopita. Mungu awabariki sana. Ni matumaini yangu kazi hiyo nzuri ilikuwa ya wana CCM wote wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sina fadhila kama sitawapongeza wanawake wa Mkoa wa Singida kunirudisha tena Bungeni kwa Awamu ya Tatu kwa kura za kishindo ambazo zilinipa nafasi ya kwanza kama ilivyokuwa awamu zote mbili zilizopita Mungu awabariki sana. Ni matumaini yangu kazi hiyo nzuri ilikuwa nzuri ilikuwa ya wana CCM wote wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, nimalizie pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili kuwa Rais wetu kwa kura nyingi. Hii ni dalili ya kutosha kuwa Watanzaia bado wana imani naye kwa vile alisimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite kuchangia hotuba yake ambayo aliitoa alipokuwa anafungua Bunge mwaka 2010 ambayo ameanisha vipaumbele 13 ambavyo vimewafurahisha Watanzajia kutokana na umuhimu wake na wana matumaini makubwa kuwa vitatekelezwa ipasavyo na Mungu amtangulie.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana wanaoanza kazi zilizofanywa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika Awamu ya Nne, miradi mingi imetekelezwa ikiwemo barabara. Jiografia ya nchi yetu imefunguka kwa kiwango cha lami hata barabara za vijijini kwa kiwango cha vumbi, lakini imara, ikiwemo Mkoa wa Singida barabara zake za kwenda kila Mkoa ni lami. Miradi ya maji nayo imetekelezwa kikamilifu, wanawake sasa hivi hawatembezi mwendo mrefu kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu nalo Serikali ilitoa kipaumbele, imejenga shule za Sekondari kila Kata tena Kata nyingine shule mbili, kwa ushirikiano mzuri wa Serikali na wananchi sasa watoto wengi wanapata nafasi ya kujiunga na elimu ya sekondari.

Serikali haikuishia hapo, kwa makusudi ikajenga Chuo Kikuu cha Dodoma kikubwa ambacho kinachukua wanachuo wengi sana na kimetuletea sifa Watanzania ulimwengu mzima, leo wengine wanabeza juhudi hizi ni ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kutoa kilio changu juu ya wanafunzi wa Kidato cha Nne kufeli kwa wingi hivyo. Inaonyesha kufeli kwao sio makosa yao, bali huenda hawajapata elimu kama ilivyotakiwa. Hivyo ninapenda kuiomba Serikali pamoja na makosa mengine ambayo yako wazi, mfano walimu kujihusisha na siasa kwa kudanganya kufanya makusudi kuiangusha Serikali ya CCM, uzembe pamoja na miundombinu mbovu au kukosekana ushauri:-

- (a) Ninaiomba Serikali kufanya hima kusomesha walimu wa kutosha;
- (b) Ninaishauri Serikali kujenga miundombinu muhimu mfano maabara, nyumba za walimu, madawati, umeme, maji na vifaa mbalimbali ikiwemo vitabu vya kufundishia; na

- (c) Ninaishauri Serikali kuwahurumia wanafunzi hawa pamoja na wazazi wao ili warudie mitihani tena bure.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu, ninaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kuwakopesha wanachuo nane ada ili waweze kusoma wote hata wale wenye wazazi wasiokuwa na uwezo. Tatizo ni wale viongozi wachache ambao hawafikishi ada hizo kwa wakati muafaka. Ninapata wasiwasi kuwa inawezekana fedha hizi zinawazalishia kwanza ndipo wanachuo wanapewa wakiwa tayari wamesumbuka sana.

Mheshimiwa Spika, lazima jambo hili lifuatiliwe wakibainika wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria. Ajira kwa vijana, ni ukweli usiojificha kuwa suala kuwapa ajira vijana halijatekelezwa ipasavyo kwani vijana wengi sana wenye degree zao wanahangaika mijini na vijijini, lazima Serikali iweke mikakati kabambe ya kuhakikisha wasomi wote wanapohitimu wanapata ajira ama wanawezeshwa kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa pamoja na ushawishi wanaopewa na baadhi ya wanasisa kuigomea Serikali kila mara nafsi zao zitawasuta. Hii inatokana na kukosa matumaini ya kupata ajira baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba watendaji wasiiumize sana Serikali kwa kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo, mfano, Serikali imejenga Mahakama ya Mwanzo Kata ya Utemini Manispaa ya Singida, sasa ni karibu miaka miwili tangu imekamilika lakini haijaanza kufanya kazi. Sijui tatizo ni nini! Hata Bunge la Tisa niliuliza hapa Bungeni. Ni kweli haya ndiyo mambo yanayoipaka matope Serikali. Ninaishauri Serikali kuwawajibisha watendaji wabovu au wenye makusudi mabaya na Serikali kwenye taasisi au sekta zote.

Mheshimiwa Spika, ni kosa sana bei za bidhaa mfano sukari kupanda kiholela wakati wasimamizi wapo. Kama kuna tatizo linalosababisha mfumko huu, basi wananchi waelezwe kwa njia ya vyombo vya habari mfano TV, Redio na Magazeti ili wasipate dhana potofu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiojificha kuwa janga la njaa lipo maeneo mengi. Ikumbukwe kauli ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwamba hatakufa Mtanzania kwa njaa. Hivyo, ninaishauri Serikali suala la kupata takwimu lisicheleweshwe kwani wananchi wana hali ngumu Iramba Mashariki, Singida Vijijini na Manyoni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumaliza mchango wangu kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyolihutubia Bunge. Pia napenda kukupongeza wewe Spika, kwa nafasi hiyo uliyoipata.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imezingatia vipaumbele vyake alivyoainisha katika hotuba yake. Naomba nami nichukue nafasi hii kuchangia hotuba hiyo na hasa kuhusu kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuhamisha uanzishwaji wa *SACCOS* na *VICOBA*. Kwa kweli *SACCOS* ni mkombozi wa wananchi katika kuondoa umasikini. Ushauri wangu ni kwamba, *SACCOS* hizi ungetafutwa utaratibu wa kuziwezesha ili lengo la kuondoa umasikini kwa wananchi wetu liweze kwenda kwa kasi zaidi.

Vile vile, majengo yanayojengwa kwa ajili ya kuasaidia vijana wetu maarufu kama wamachanga yajengwe katika Mikoa yote kusaidia vijana kutokuwa wazururaji na kujijiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu.

Vile vile namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake nzuri amayo imegusa sehemu zote muhimu sana kwa maeneleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, naomba nichangie sehemu ya uvuvi. Kama uvuvi utasimiamia vizuri sana, uvuvi ni endelevu na uvuvi kisasa unaweza kutoa mchango mkubwa wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunayo bahari, maziwa na mito ambayo ina samaki wengi tu ambao wengine hawavuliwi mpaka wanakufa wenyewe kwa sababu hawafikiwi zile sehemu za makazi yao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba, kwanza wavuvi wapewe elimu ya kazi yao ili wavue kwa ufanisi. Wapatiwe zana za kisasa ambazo zinaendana na wakati tulionao. Naiomba Serikali iwaangalie wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapatia mikopo nafuu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la Muungano wetu wa Tanzania. Muungano wetu ni imara na utaendelea kuwa imara pamoja na kuwepo kasoro ndogo ndogo ambazo tunasema kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ya Muungano kufanya juhudi za makusudi kumaliza hizi kero ili Muungano uwe imara zaidi. Nachukua nafasi hii kumshukuru tena Rais wa Muungano kwa dhamira yake ya dhati kuondoa mpasuko wa kisiasa Zanzibar kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana Zanzibar kwa maelewano ya dhati kati ya

Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Wananchi (CUF). Sasa nchi imetengamaa vizuri, umoja, mshikamano na upendano wa Wazanzibar umeonekana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Umoja wa kitaifa imeondoa chuki, ugomvi, ubaguzi, watu wanafanya kazi pamoja, kama Taifa moja na kuwajibishana. Ushahidi wa hayo, tangu mfumo wa Vyama Vingi, Zanzibar haijawahi kufanya chaguzi yoyote pasiwe na fujo, vurugu haa watu kupigana. Lakini uchaguzi wa mwaka 2010 baada ya maridhiano hakuna mtu hata aliyekunwa chungu.

Mheshimiwa Spika, hii ni amani kubwa Zanzibar, amani kubwa Tanganyika, Amani kubwa Tanzania nzima.

Sasa kama kuna mtu anabeza na kudharau, huyo haitakii mema Zanzibar, pia ni adui wa amani Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Kwanza wa Bunge la Jamhuri ya Muungano mwanamke. Mungu akubariki akupe uwezo mzuri wa kuongoza haki itendeke kama vile unavyopenda itendeke.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uwezo wa kuchangia hoja hii ya kujadili hotuba ya Rais. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata na kukiwezesha Chama chetu cha CCM kushinda na hatimaye kushika dola.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia mjadala huu wa hotuba ya Rais, nami mchango wangu nitajikita moja kwa moja kwenye tatizo la umeme na hasa katika kipindi hiki ambapo wakati wowote kuanzia sasa nchi inaweza ikaingia katika janga kubwa sana la giza endapo mvua haitanyesha na kujaa maji Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu napenda kuishauri Serikali kwamba hivi sasa umefika wakati wa Mheshimiwa Rais kuipa kipaumbele cha kwanza na cha dharura Wizara ya Nishati na Madini kwa kuipatia fedha nyingi katika bajeti ijayo ili kuondoa kabisa tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, kama tujuavyo, maendeleo ya nchi hayawezi kupatikana bila kuwepo kwa miundombinu ya uhakika. Kati ya hiyo, ni pamoja na umeme, kwa mfano bila umeme, viwanda haviwezi kuzalisha, bila umeme utendaji kazi mawizarani unazorota, bila umeme sehemu nyingi za uzalishaji zinazorota na hata mjadala ndani ya Bunge lako hili Tukufu haitawezekana kuendeshwa bila kuwepo umeme humu ndani.

Hivyo basi, namwomba sana Mheshimiwa Rais wetu atoe umuhimu wa kwanza kwa Wizara hii ya Nishati na Madini katika bajeti ijayo kuona kwamba tatizo la ukosefu wa umeme la mara kwa mara linaondoka na hapo ndipo maendeleo yetu kiuchumi yataimarika na kuonekana na wananchi wetu hasa wale walioko vijijini.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, sina budi kukupongeza wewe binafsi kwanza kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wetu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa hotuba yake ambayo imeonesha dira ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutukumbusha sisi Wabunge wajibu wetu na kutuasa juu ya hasira ambazo wananchi wanaweza kuzitumia kama silaha yao pale Mbunge ataposhindwa kuonekana katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru kwa ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais ya kutoa ushirikiano wake na wenzetu wote Serikalini katika kufanikisha majukumu yako wewe Spika na ya Bunge kwa ujumla. Nitakuomba Mheshimiwa Spika uitumie ahadi hii na fursa aliyokupa Mheshimiwa Rais, kuimarisha mhimili huu wa nchi yetu kuwa ndio kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa nchi yetu na kuwa ndio msimamizi mkuu wa utekelezaji wa vipaumbele vyote ambavyo Mheshimiwa Rais amevieleza. Naishauri Serikali na watendaji wake kuwa makini na kauli ambayo mimi naipongeza sana ya Mheshimiwa Rais aliyosema: “Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kutimiza ahadi zetu kwa Watanzania”. Napenda nichangie katika suala zima la afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti kwa Wizara hiyo ila kutokana na Sera ya Afya ambayo ilitungwa mwaka 2003, nina mashaka na utekelezaji wake, hasa katika Mpango Na.3 wa Sera hiyo wa kuongeza uwezo wa kupambana na maradhi hasa yale yanayoathiri na kuuu watu wengi. Naiomba Serikali kuwa na dhamira ya dhati katika hili kwani hivi sasa kwa mfano katika hospitali yetu kuu ya Muhimbili, inapofikia saa 12 jioni unashindwa kukaa katika wodi au eneo la hospitali kutokana na adha kubwa ya wingi wa mbu ambao huwauma na kuwashughulisha sana wagonjwa na wale wote wanaohudumia wagonjwa. Naomba Waziri aje alieleze Bunge lako Tukufu, ni lini adha hii ya mbu katika hospitali yetu ya Muhimbili itaondoka kwani mbu husababisha maradhi ambayo huweza kuondoa maisha ya mtu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kumshukuru Rais kwa hotuba yake nzuri na napenda kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JADDY SIMA JADDY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kimaandishi mchango wangu kuhusiana na kipaumbele namba moja cha hotuba ya Rais. Naiomba Serikali kuongeza spidi ya kujadili na kutatua wa Kero za Muungano pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba sita, naomba Serikali itoe tamko rasmi juu ya nini msimamo wa Serikali katika umiliki wa madini ya “*Uranium*” yaliyovumbuliwa nchini ili kuepuka kuibuka upya kwa mjadala kuhusiana na maliasil hiyo kama ilivyotokea kwa mafuta upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba nane, naomba Serikali iweke utaratibu maalum kwa wanafunzi kutoka Zanzibar utakaowawezesha kufuatilia kwa karibu na kwa

gharama ndogo zaidi nafasi za kimasomo wanazozipata wanapochaguliwa kujiunga na Vyuo vilivyoko Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba tatu, naomba Mheshimiwa Rais aendeleze Mfuko wa Mabilioni ya Kikwete ili uweze kuwanufaisha wananchi wetu kiuchumi na hasa wale wa vijijini kwa kuvipa kipaumbele vikundi mbalimbali vya kiushirika vilivyoanzishwa na wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Rais, naomba kuchangia hotuba hiyo katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, uchumi kuendelea kuwa tegemezi. Uchumi wetu utaendelea kuwa tegemezi kwa muda mrefu kwa vile mipango mingi mizuri inaishia kwenye maandishi badala ya kusimamiwa vizuri ikatekelezwa. Moja ya maeneo yenye udhaifu mkubwa ni Idara ya Kukusanya Kodi (*TRA*). Utendaji wa *TRA* ni mbovu sana na ndiyo maana bado hatuwezi kukusanya kiasi cha kutosheleza matumizi yetu. Bado *TRA* wanatoza ushuru na kodi mbalimbali kwa mtindo ambao hauvutii walipaji kabisa. Walipa kodi wananyanyaswa sana na Maafisa wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya Ofisi za *TRA* hayawavutii walipa kodi na ni ya udhalilishaji sana. Napendekeza watafutiwe maeneo makubwa, zijengwe ofisi nzuri zenye hadhi na walipa kodi wakifika, wapewe heshima na ukarimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Mgano ni Ofisi za *TRA Uganda Revenue Authority*. Mahali ofisi zao zilipo, huwezi ukakosa sehemu ya kugesha gari, matusi wala watu kuswagwa kama vile wahalifu wakati kumbe hawa ni raia wema ambao wanakwenda kulipa kodi wachangie maendeleo ya Taifa lao, hakuna.

Mheshimiwa Spika, vilevile mtindo wa ukadiriaji Ushuru wa Forodha wa sasa uachwe kabisa. Mlipa kodi yapaswa afahamu mapema atalipa kodi kiasi gani kwa bidhaa anayoagiza. Orodha ya bidhaa na Ushuru wa Forodha iwe wazi kwa wananchi, hii itapunguza rushwa iliyokithiri maeneo yote kunakotozwa Ushuru wa Forodha. Orodha iwekwe wazi, wananchi wajue wanapaswa kulipa kiasi gani kwa bidhaa wanazoagiza. Hii itaondoa Umungu Mtu ulipo huko *TRA*, Idara ya Forodha.

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa Forodha utozwe bila ubaguzi. Leo mlipakodi wa Zanzibar analipa kidogo ukilinganisha na yule wa Dar es Salaam. Kuna kitu kinaitwa *reassessment*, hili jambo ni kero kubwa kwa wananchi. Ni *double standard* katika kutoza watu ushuru hata kama yapo maelezo. Mtindo huu ukomeshwe mara moja, vigezo vifanane kwa walipakodi wote wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nishati. Nashauri Serikali iwekeze zaidi katika sekta hii. Tuwe na uzalishaji na usambazaji wa uhakika. Hasara leo tuyoipata kwa mgao huu

Kitaifa, naomba itajwe ili tuweze kwa pamoja kuchagua kati ya hasara hiyo au malumbano yasiyo na tija kwa afya ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ajira. Wananchi wengi wanajiajiri katika shughuli mbalimbali za kilimo. Hivyo ni vema mikakati ya makusudi ichukuliwe ili kuhakikisha kilimo kinastawi. Kilimo chenye tija kinahitaji mtaji kama zilivyo biashara zingine. Benki zitungiwe sheria zinazowalazimisha kukopesha wananchi katika kilimo na Serikali iweke kinga kwa benki dhidi ya wawekezaji katika kilimo watakaokumbwa na majanga.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Buchosa. Kivuko cha MV. Geita kifanyiwe ukarabati wa dharura kama ilivyo ahadi ya Rais Kikwete. Ukiisha mwaka, hiyo siyo dharura tena. Wananchi wanasubiri kwa hamu na Wizara iweke katika bajeti ya mwaka huu fedha kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kpya kwa ajili ya kisiwa cha Maisome.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehemu zake nyingi. Pia napenda kukishukuru Chama changu cha *CUF*, familia yangu na wananchi wote wa Jimbo langu la Chonga. Naahidi kuwatumikia wao na Taifa kwa ujumla na hawatajuta kunichagua.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, kwa kuonesha dhamira ya dhati na kuitekeleza, ya kusaidia kutatua mgogoro wa Zanzibar kwa kushirikiana na Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Aman A. Karume na Katibu Mkuu wa *CUF*, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad ambaye sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU). Pia namshukuru Rais wa sasa wa Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Ali Muhamed Shein na Makamu wa Pili, Mheshimiwa Balozi Seif Idd, kwa uungwana wao. Muungano ni kitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kutowaonea aibu ya kuwafukuza kazi mara moja wafanyakazi wa Idara za Muungano wanaoitia doa Serikali na kuisababishia kuchukiwa na wananchi wake kwa kutotekeleza maamuzi ya Serikali hasa kero za Muungano. *TRA* wamekuwa na jeuri, kiburi na kuwanyanyasa wafanyabiashara wanaoleta bidhaa zao Dar es Salaam kutoka Zanzibar kwa kuwatoza kodi mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limekuwa sugu pamoja na kuwa limeshapatiwa ufumbuzi na Tume inayoshughulikia kero za Muungano iliyokuwa chini ya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar. Tatizo hili ni kero sana na limekuwa ni mnyororo waliofungwa wafanyabiasahra hawa ambao ni wadogo na wa kati, wanabaki kuwa wafanyabiashara wadogo miaka nenda, miaka rudi. Iko wapi hapo nia nzuri ya Rais wetu Dr. Jakaya M. Kikwete ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati?

Mheshimiwa Spika, katika kipengele cha saba (7) cha hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameeleza kuhusu kuboresha zaidi ukusanyaji wa mapato, lakini kwa takwimu



zinavyoonyesha kuna misamaha mingi sana ya kodi. Uzoefu unaonesha wanaosamehewa kodi ni wafanyabiashara wakubwa. Ipo haja sasa ya kuwasaidia kuwakomboa wafanyabiashara hawa wa kati na wadogo kwa kutowalipisha kodi mara mbili na kuelekea kwa wafanyabiashara wakubwa ili walipe kodi kihalali na ukusanyaji wa mapato uboreke.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja sasa kwa Mashirika kama Reli kufanya kazi kwa ufanisi na kuchangia mapato ya Serikali badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kupunguza kuwakamua wafanyabiashara tu, hasa wafanyabiashara wa kati na wadogo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa kulizindua Bunge jipya la Kumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo manne yafuatayo, kilimo, barabara, mawasiliano ya simu za mkononi na suala zima la elimu.

Mheshimiwa Spika, kilimo, ni wazi kilimo ndiyo mwajiri wa Watanzania wengi nchini. Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza tayari imeonesha mafanikio kadhaa na yanaleta matumaini. Pamoja na matumaini hayo, zipo changamoto ambazo endapo hazitashughulikiwa kwa ukamilifu, hakika mchango wa kilimo katika suala zima la kupunguza umaskini wa wananchi na Taifa kwa ujumla wake. Changamoto hizo ni kama hizi zifuatazo:-

Kwanza kabisa, suala la kuongeza ruzuku ya kilimo ili ikiwezekana vocha za pembejeo zinazotolewa zikidhi mahitaji halisi ya wakulima wetu yaani kama kuna mkulima anataka kulima zaidi ya ekari moja apate kulingana na maandalizi aliyonayo ili mradi asimamiwe na Maafisa Ugani ambao ni muhimu pia wawepo kila kijiji.

Pili, Mawakala wetu wasajiliwe na wapewe elimu hasa elimu ya uzalendo, ili mchango wao muhimu ulete tija kwa Taifa na endapo watasajiliwa maana yake wataona kazi yao ni ya kudumu na hawatashiriki katika wizi au vitendo vya kutokuwa waaminifu.

Tatu, uaminifu kwa watumishi wa kilimo, ni muhimu sana kwani watarahisisha huduma hii kufika kwa walengwa na kwa kiasi kilichopangwa. Uaminifu ni muhimu kwa watumishi ili wasishirikiane na Mawakala wasio waaminifu.

Nne, pembejeo kupelekwa kwa wakati, napendekeza mwezi Julai, wakati wa mavuno, huu ni wakati muafaka kwani mkulima anakuwa na mazao ambayo anayategemea sana kununulia pembejeo hizo. Mapinduzi katika kilimo yanatega *mechanisation* yaani matrekta makubwa yapatikane, tena bila urasimu kama ilivyo sasa.

Tano, utaratibu wa soko la mazao ya wakulima, nashauri kipindi Serikali inanunua mazao hasa ya chakula, bei zilingane na za gharama za uzalishaji. Masoko pia yasongezwe karibu na wakulima na vilevile kuongezwe vituo vya kununulia mazao. Kwa mfano, Jimbo la Nkasi Kusini, lina kituo kimoja tu cha kununua mazao, jambo ambalo

huleta usumbufu. Naomba kila Kata ikiwezekana kiwe na kituo cha kununua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kilimo, pia tunao wajibu wa kuendeleza uvuvi. Jimbo la Nkasi Kusini, lina Kata tatu za Kala, Wampembe na Ninde zilizoko katika Mwambao mwa Ziwa Tanganyika na kuwa hawajanufaika na rasilimali hiyo kutokana na vyombo duni na butu vya kutafutia riziki zao kutoka Ziwani. Tuwape msukumo mpya kwa kuwasaidia zana za kuvulia na mitaji zitakazokidhi uvuvi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, barabara. Katika kampeni za uchaguzi wa 2010, Mheshimiwa Rais, Jakaya Kikwete, alitoa ahadi ya kuboresha barabara kuunganisha Kata za Mwambao. Kata hizo ni Kala, Wampembe na Ninde ambazo zimekuwa nyuma na huvamiwa na majambazi kutoka Kongo. Naomba Serikali itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kata za Kala, Wampembe na Ninde, hawajapata mawasiliano ya simu licha ya barabara kuwa hazifai. Naomba Serikali ielekeze macho katika kuhakikisha mawasiliano yanapatikana, hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, elimu. Suala la elimu ni muhimu. Katika Jimbo la Nkasi Kusini, Walimu hawatoshi hasa katika Shule za Sekondari ambazo idadi yake ni kumi ukiachia mbali matatizo ya maabara katika shule zote, nyumba za Walimu, zana za kufundishia na kadhalika. Naomba Serikali inisaidie Walimu katika shule za Jimbo la Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, nakupa pongezi kwa kuteuliwa kuwa Spika mwanamke na wa kwanza hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira kwa Wabunge na wananchi wote ili kuleta ufanisi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishukuru familia yangu, wananchi wa Iramba Mashariki, kwa kunitua kuwa Mbunge na mwakilishi wao. Ninaahidi sitawaangusha na nitawatumikia daima. Nakishukuru pia Chama cha Mapinduzi kwa kunipigania na kuibuka mshindi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Rais ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu elimu. Upungufu wa Walimu unachangiwa na ucheleweshaji wa kupangiwa vituo vya kazi. Wanakaa muda mrefu (Miezi 5-6) na hujikuta wanaanza kutafuta ajira mbadala. Wapangiwe kazi mara moja wamalizapo mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Wilaya mpya. Kuhusu Wilaya mpya zilizoteuliwa na Mheshimiwa Rais ikiwemo na Wilaya yangu ya Mkalama katika Jimbo la Iramba Mashariki. Naishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- (i) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa majengo;
- (ii) Umeme wa kuanzia shughuli zote za Ofisi na ujenzi;
- (iii) Maji ni ya muhimu, Serikali ihakikishe yanapatikana ya kutosha; na
- (iv) Watumishi wa kutosha kukabiliana na changamoto za uanzishaji wa Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuchangia eneo la Umoja wa Kitaifa, rejea ukurasa 12. Kwa mfano alivyosema Mheshimiwa Rais, nguvu ya wanyonge ni umoja. Naomba ikumbukwe kuwa Umoja ni Nguvu na Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano inasema Serikali haina Dini ila watu wake wana Dini. Ipo haja ya Mashirika ya Dini kuelewa kuwa hawapaswi kushughulika na siasa na kuwalazimisha wananchi kufuata Chama fulani kama ilivyokuwa Sumbawanga Mjini, Kanisa la RC, kuwalazimisha waumini wake kuchagua Chama cha CHADEMA na wale ambao hawakufanya hivyo, waliambiwa wamekiuka imani ya Kikristo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusema kuwa, Serikali na Mashirika ya Dini inabidi vishirikiane kuleta Umoja katika nchi na amani kwani Mashirika ya Dini huomba kibali cha kuhubiri, kujenga Makanisa na kuingiza bidhaa bila ya kodi kulipwa. Hatutarajii Mashirika haya kufanya kampeni za kisiasa na jambo hili wapewe maonyo mapema Mashirika ya Dini ili Serikali, Misikiti na Makanisa, wote wawe na Umoja na kukemea maovu.

Mheshimiwa Spika, eneo la madini, rejea ukurasa 21 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, alisema tutaendelea kutatua changamoto ambazo bado hazijapata ufumbuzi, changamoto hizi ni pamoja na Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambao kwa miaka mingi haujaanza kufanya kazi. Naomba maelezo juu ya Mradi wa Madini wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue nafasi hii, kushukuru kuwepo kwa Mkoa Mipya, rejea ukurasa wa 35, utawala bora, ikiwa ni pamoja na Mkoa Mpya wa Njombe. Ombi langu ni miundombinu katika Mkoa huu mpya izingatiwe ikiwa ni pamoja na Mkoa Mpya wa Katavi. Mkoa wa Njombe unahitaji Ofisi, barabara ya lami na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo la elimu, rejea ukurasa wa 27 wa hotuba. Ipo haja ya kuwa na VETA (Vyuo vya Ufundi) kila Wilaya hususan Wilaya ya Ludewa na pia umuhimu wa kuwa na *High School* kila Tarafa yaani *Form IV* na *VI*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia maeneo haya machache, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa hotuba ambayo imetoa dira na matumaini kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais amekuwa ni hodari sana hasa katika kushughulikia kero za wananchi ambazo zilionekana kushindikana. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia katika eneo la maji. Kwanza, naomba fedha zaidi zitengwe kwenye bajeti ijayo katika sekta ya maji. Hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi, si nzuri ila katika Jimbo langu la Lulindi hali ni mbaya sana na kufanya wananchi kuhangaika na kukata tamaa. Ndoo moja ya lita 20 huuzwa kwa shilingi 1,000/= hali inayofanya wananchi wengi kutomudu kupata maji. Naishauri na kuiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kuwanusuru wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, elimu, afya na huduma za jamii. Katika maeneo haya, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuonesha dira. Naishauri Serikali kuimarisha Serikali za Mitaa na kuziondolea vikwazo na kero zinazowakabili. Pia kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani ili wazisimamie Halmashauri zao vyema. Pia Halmashauri kuzijali Ofisi za Serikali za Vijiji na Mitaa. Pia kwa kupeleka fedha kwenye Kata kwa ajili ya kuzihudumia Ofisi hizi na Wenyeviti wake.

Mheshimiwa Spika, pili, naiomba Serikali kuacha kunyofoa shughuli zinazofanywa na Halmashauri na kuzirudisha Serikali Kuu. Kwa mfano:-

(i) Serikali kuamua magari yote yanunuliwe na Wizara ya Miundombinu. Jambo hili limesumbua na kurudisha nyuma juhudi za Halmashauri kujiletea maendeleo yao. Naishukuru Serikali kurekebisha utaratibu huu; na

(ii) Serikali Kuu kuamua ajira zote zifanywe na Wizara inayoshughulikia na Utumishi. Jambo hili litadhoofisha juhudi zilizoainishwa kwenye hotuba yake. Naishauri Serikali kurudisha Mamlaka hayo kwa Halmashauri ili ziendelee kuajiri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kuanzisha mkakati wa Kilimo Kwanza. Naiomba Serikali izingatie kuhakikisha kwamba wakulima wanapatiwa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu. Wataalamu wetu wawe karibu na wakulima na pia Serikali isimamie ipasavyo kuhusu masoko ya mazao kwa kuwasimamia wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutafuta soko la korosho kwa kuanzisha utaratibu wa Stakabadhi Ghalani, umeleta manufaa sana. Ombi la wananchi ni kulipwa fedha yote ya bei inayotangazwa na Serikali na wakulima wasubiri bonasi baada ya mauzo ya korosho. Jambo hili litawasaidia wakulima wadogo ambao huzipata fedha hizi huku wakikabiliwa na mikopo ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa Mbunge ili niwawakilishe wananchi wa Tanzania wa Jimbo la Mtoni, Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. Nawaahidi wananchi wa Jimbo hilo, sitawaendea kinyume katika kufikisha kilio chao na kuzima kiu yao ya kupata maendeleo. Aidha, nitatekeleza ahadi zangu pasipo kuvunja Kiapo cha Utii cha Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani nyingine maalum kwa mke wangu Nachum pamoja na wanangu, ndugu, jamaa na marafiki, pamoja na timu yangu ya Kampeni, kwa jinsi walivyovumilia taabu na shida, dhiki ya maisha na tashtiti za kisiasa hadi ushindi wa Jimbo la Mtoni katika Uchaguzi Mkuu wa Serikali yetu ukaja kwangu mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani nyingine za dhati kwa Chama changu cha *The Civic United Front (CUF)*, Chama cha Wananchi tangu ngazi ya tawi la Kidatu “A”, Jimbo la Mtoni, Wilaya ya Magharibi hadi Baraza Kuu la Taifa, kwa kunipatia kura za maoni za kutosha na hatimaye kuteuliwa kuwa mgombea.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mtoni kwa uamuzi wao thabiti wa kunichagua kwa kura nyingi sana bila ya kujali tofauti zao za kiitikadi na kisiasa. Nawaahidi kuwanoa bega kwa bega ili kuondoa kero zilizopo katika Jimbo hususan maji, huduma ya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mama Anne Makinda, kwa kuruhusu michango ya maandishi kwa wanaokosa nafasi za kuchangia kwa kusema hapa Bungeni. Ninakupongeza sana kwa kuipata bahati ukiwa mwanamke, ya kuliongoza Bunge letu katika nafasi uliyonayo. Ni jambo la historia ya heshima kwa Taifa letu, Mungu akujalie umri mrefu na maisha ya fanaka pamoja na hekima, busara na umakini katika kazi yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na Watanzania kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia namshukuru mno, kwa hotuba yake fupi, yenye hoja za msingi katika kuiendesha nchi yetu kwa ufanisi, maendeleo na utangamano, wakati wa kikao cha Bunge letu, cha tarehe 18 Novemba, 2010 alichokiitisha yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie vipaumbele viwili tu katika hotuba ile. Kipaumbele cha kwanza na cha nane kati ya vipaumbele kumi na tatu alivyovieleza.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba moja, umoja, amani na usalama wa Muungano wetu. Tangu 26/4/1964, tunao Muungano wa Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar unaoitwa Tanzania. Mwalimu Julius K. Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume, wakiwa Wakuu wa Nchi hizo mbili, walikubaliana kuunganisha baadhi ya vipengele vya kuendesha nchi na kutangaza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila ya kujali ukubwa au udogo wa Tanganyika au Zanzibar na bila kupiga kura ya maoni ya

wananchi wa pande hizo mbili. Watanzania tuliwakubali na kuwaunga mkono viongozi wetu wawili hao, kwa nia ya kutaka umoja, amani na usalama wa Muungano kama Taifa moja. Leo kumezuka Wanasiasa na wasemaji wanaobeza Zanzibar na hata kudiriki kusema kuwa Majimbo 23 ya Zanzibar ni sawa na Jimbo moja tu la Tanzania Bara! Huu ni uchochezi na dharau ya hali ya juu inayoashiria ubaguzi, utengano, shari na mparaganyiko wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nilidhani Bungeni tutaheshimu historia ya nchi yetu na kuchangia kuisaidia Serikali namna ya kukabili changamoto zinazokwaza juhudi za Serikali za kuleta maendeleo. Kumbe sivyo! Baadhi yetu tunapitikiwa! Hali ni hivyo kwamba wapo watu bado wanatoa kauli za kukatisha tamaa dhidi ya Maridhiano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Zanzibar hata ndani ya Bunge lako Tukufu.

Kwa taarifa yao, hivi sasa Zanzibar ni tulivu na ina amani ya kutosha na hali hiyo ndio ishara bora kwa umoja, amani, usalama wa Muungano wetu. Naiomba Serikali kupitia Bunge hili, kudhibiti maadili ya Muungano wa Tanzania na kuwadhibiti wale wote wanaotaka kuyamomonyoa kwa nguvu yote ya Kikanuni, Sheria na Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 21-29, Mheshimiwa Rais ametoa ufafanuzi kwa ufupi juu ya azma aliyokuwanayo kuhusu elimu kabla ya kutangaza Baraza la Mawaziri. Kama utekelezaji wa sera zilizopo na maelezo yale vitakwenda sambamba na hali halisi ya utendaji kazi wa watendaji wa Serikali, tutajenga Tanzania mpya mapema sana. Naziunga mkono jitihada za Serikali katika fani ya elimu ila napenda kutoa maoni yangu yafuatayo:-

- (1) Mshahara wa Walimu uendeleo kukua ili watu wapende kuwa Walimu;
- (2) Vifaa vya kufanyia kazi mfano vitabu, vifaa vya maabara na maabara zenyewe ziendelezwe;
- (3) Mitihani ya Kidato cha Pili irejeshwe kama kule Zanzibar; na
- (4) *HESLB* ipate marekebisho yanayostahiki baada ya mapendekezo ya hiyo Tume ya watu 11 bila ya kujali undugu na urafiki.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea *UDOM* na kuona tatizo kubwa sana la ukosefu wa maji. Wanafunzi wanasema maji hupatikana kikawaida siku za ziara za Wakuu wa Nchi au Mawaziri. Aidha, kuna tatizo la makaro na mabomba ya maji machafu. Ni hatari kwa afya ya jamii ya Chuoni *UDOM*. Mzabuni wa chakula hapo chuoni anapika chakula kisichoridhisha. Wanafunzi wanadai, mzabuni wa mwanzo alikuwa akipika vyakula vizuri lakini amekoseshwa nafasi hiyo na kupewa huyo wa sasa. Wanafunzi wanatilia mashaka kama rushwa haikutumika katika kumpata mzabuni wa pili. Juhudi za Serikali zifanyike ili wanafunzi wa Vyuoni waweze kupata mazingira yanayowashawishi kusoma na kujifunza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Serikali, hotuba ya Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoa tarehe 18 Novemba, 2010 alipokuwa anafungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nichangie hoja katika suala la elimu, afya na huduma za jamii. Katika suala la elimu, Serikali na taasisi mbalimbali na wadau wa elimu, waangalie upya namna ya kuwasaidia na kuwawezesha vijana wenye vipaji maalum katika fani ya sayansi na teknolojia. Kwa mfano, kijana wa Sumbawanga aliyetangazwa jana yaani tarehe 13 Februari, 2011 ambaye ameweza kutengeneza trekta kwa kutumia injini ya pikipiki. Hawa ni watu ambao wakiendelezwa, wanaweza kufanya vizuri katika suala zima la kupunguza umaskini na kuleta maendeleo si tu ya familia bali Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika suala la afya, Serikali ingeweza kuangalia upya suala la mfumo mzima wa matibabu kwa wazee na wastaafu, kwani wamekuwa wakipata sana taabu wanapokuwa hospitali. Aidha, nashauri Serikali iwaandalie utaratibu wa matibabu kwa wazee na wastaafu kama utaratibu wa bima ya afya kwa watumishi basi na wao wangeandaliwa utaratibu kama huo, kwa maradhi mengi ya uzeeni ikiwa ni pamoja na magonjwa ya sukari, moyo na mifupa. Magonjwa haya ni ghali kwa matibabu ikizingatiwa kwamba wazee/wastaafu ni vigumu kuyamudu, hivyo basi, naomba Serikali ilianganalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali ianganalie namna ya kuwasaidia walemavu ambao wana ulemavu zaidi ya mmoja. Serikali ianganalie namna ya kuwawezesha ili waweze kujikimu kimaisha kama vile inavyofanya kwa mfano wagonjwa wenye VVU na makundi mengine yanayohitaji mambo yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali ianganalie namna ya kupeleka wahudumu wa afya maeneo ambayo wahudumu hao aidha hawapo kwa sababu mbalimbali mfano kusoma, kuugua na mengineyo. Mfano hospitali ya Mpanda mpaka sasa haina mtaalam wa maabara yaani *X-ray* na *Ultra Sound*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kwa maendeleo ya Taifa.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati analihutubia Bunge jipya.

Kwanza kabisa napenda kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika, wadhifa ambao ni mkubwa sana lakini pia kama mwanamke hongera sana.

Katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais nitazungumzia juu ya vipaumbele vifuatavyo; amani, elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, suala la amani ni pana sana linagusa maeneo mengi. Amani sio kutokuwa na vita tu katika nchi bali ni kipengele kimojawapo. Nchi inapokuwa na njaa raia wake hawawezi kuwa na amani, watu wanaponyimwa au kukosa haki zao za msingi amani haiwezi kuwepo. Kwa hiyo basi, amani umoja na mshikamano ni vitu ambavyo kwa sasa hapa nchini kwa mtazamo wangu viko hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Spika, tumeona maeneo mengi yamekumbwa na uhaba wa chakula, mtu mwenye njaa anaweza kufanya lolote. Je, ni kwa nini Serikali isichukue tahadhari mapema hadi isubiri raia wake wapate tabu? Tumeshuhudia migomo mingi ya wazee wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeshuhudia migomo ya wanafunzi wa vyuo vikuu ikiambatana na kufukuzwa kwa baadhi ya wanafunzi hao, migomo ya wafanyakazi toka sekta mbalimbali. Katika hali hii amani itakuwepo namna gani?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini hadi sasa hivi Serikali haijatafuta ufumbuzi wa kudumu ili kudhibiti migomo hii. Naiomba Serikali iangalie upya Bodi ya Mikopo ili wanafunzi hawa watoto wa maskini waweze kupatiwa haki zao kwani madai yao yana msingi. Pia Serikali iangalie watendaji wake watimize wajibu wao katika sekta mbalimbali ili migomo na maandamano haya ambayo yamekuwa kama kitu cha kawaida sasa vipatiwe ufumbuzi kwani vinaharibu sura na amani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la elimu, matokeo ya Kidato cha Nne yamesikitisha sana Watanzania wote. Naomba tuangalie ni wapi tulipojikwaa. Wanafunzi hawa asilimia kubwa ya siku nzima wako mikononi mwa walimu. Walimu hawa ndiyo wale ambao stahiki zao zina matatizo, huo moyo wa kufanya kazi utatoka wapi? Walimu hawa wanapigwa viboko hadharani, hadhi yao imeshushwa, huo moyo wa kazi utatoka wapi? Walimu hawa hawana nyumba hata ile *teaching allowance* ilishaondolewa wakisema wajiongezee kipato kwa *tuition* wanabanwa. Sasa hawa walimu wataishi vipi? Naiomba Serikali kwa dhati kabisa iwaangalie kwa jicho la pekee na la upendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanafunzi, naomba mtihani wa kidato cha pili urudishwe na katika uchaguzi wa wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza haki itendeke ili wachaguliwe wanafunzi wenye uwezo na sio kujali wingi wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nizungumzie suala la afya hususan mama na mtoto. Suala hili limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu. Pamoja na mambo mengine akinamama wajawazito wameendelea kupata matatizo mbalimbali. Wanawake hawa wanapojifungua wamekuwa baada ya kujifungua wakichangia kitanda kimoja wazazi wawili. Hii ni hatari sana kwani uwezekano wa kuambukizana magonjwa ni mkubwa. Hii imejitokeza katika hospitali ya Temeke pengine ni kwa ajili ya wajawazito wengi wanaopokelewa hapo lakini basi Serikali ifanye mikakati ya haraka ili kuwanusuru wanawake hawa na watoto wao kwani hawa ndio wazazi na walezi wa Taifa lolote yaani mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



**MHE. AL- SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, na pia nawashukuru Watanzania, nawashukuru wanawake na pia nakishukuru Chama cha Mapinduzi.

Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yenye kutia matumaini.

Napenda kuchangia kipaumbele cha tatu. Kuwawezesha kiuchumi wananchi wa makundi yote. Mabenki yawekeze kwa wawekezaji wa ndani ili fedha zibaki nchini badala ya kwenda nje ya nchi, wawekezaji kwenye madini, utalii, kilimo na ajira zitapatikana kupitia wao.

Mheshimiwa Spika, ujasiriamali liwe ni somo kuanzia shule za msingi hadi Chuo Kikuu ili kuwasaidia vijana wetu wakimaliza masomo waweze kujiajiri kwa kupatiwa mikopo kupitia mabenki, kuliko kutegemea kuajiriwa tu. Wajasiriamali tabaka la kati wapatiwe mikopo yenye ulipaji nafuu ili urejeshaji uwe rahisi. Nawaomba *Pride*, *FINCA* watoe mikopo kwa kutoa muda wa kutosha kurejesha kwa wakati. Namalizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mungu akupe hekima zaidi na akuwezeshe kuliendesha Bunge letu. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye kipaumbele namba moja kuhusu Muungano. Mimi nawashangaa wale wote wanaohatarisha Muungano wetu na kuibeza Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Nasema hawathubutu na hawataweza kuturudisha kule tulikotoka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Tanzania kwa jumla tumefanya uchaguzi ambao ulikuwa huru na salama, jambo ambalo kwa kule Zanzibar lilikuwa halipatikani na ndio maana niseme hawatohubutu na hawawezi kuturudisha kule tulikotoka, kwani, adhabu ya kaburi aijuaye ni maiti.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 19. Mheshimiwa Rais, amezungumza kuhusu uvuvi kwamba, tutaendeleza kazi vizuri tuliyoifanya katika maziwa na mito. Kwa hili napenda niishauri Serikali, sio tu tuwaendeleze bali pia wavuvi hao wawezeshwe.

Mheshimiwa Spika, kwa nini niseme hivyo ama nishauri hivyo, nasema hivyo kwa sababu mimi binafsi kazi ya uvuvi nimeshapitia. Wavuvi ni watu maskini sana na ni watu wanyonge sana. Kitendo kinachonisikitisha sana ni pale wavuvi wanaposhikiwa mitego yao na kuchomwa na baadaye wavuvi hao kuachwa hivyo hivyo bila kufikiriwa.

Mheshimiwa Spika, sio kwamba hawa wavuvi wanafanya kazi ya uvuvi kwa sababu wanaipenda sana, siyo hivyo, wavuvi wanafanya kazi ya uvuvi kwa sababu hawana kazi nyingine. Naona si uamuzi wa busara wavuvi kushikiwa mitego yao na

kuchomwa moto ila Serikali ionyeshe mapenzi kwa wavuvi hawa angalau kwa kuwawezesha kwa njia ya mikopo ili waweze kununua mitego inayoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, naona kuchomewa mitego yao wavuvi hawa ni kuwarudisha nyuma na kuwafanya wasijue la kufanya, ama Serikali baada ya kuwachomea mitego wavuvi hawa Serikali inawaelekeza nini ama wafanye kazi gani ili waweze kujitafutia riziki, wizi ama uhalifu?

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Bunge hili la kumi bila kusahau wanawake wa (UWT) Mkoa na Taifa pia chama changu cha CCM.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri na kukupongeza pia wewe Spika kwa kupata nafasi hii. Nitumie nafasi hii kulaani kitendo cha Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Demokrasia (CHADEMA) kwa kitendo cha kuonyesha kitendo cha dharau kwa Mheshimiwa Rais siku alipohutubia Bunge.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imegusa karibu kila eneo muhimu katika vipaumbele kumi na tatu alivyovitoa katika hotuba yake. Naomba niongelee zaidi kipaumbele cha nane, kuendeleza juhudi za kupanua fursa za elimu kwa vijana wetu tangu elimu ya awali, msingi, sekondari, ufundi na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi zangu za dhali kwa juhudi kubwa iliyofanyika na Serikali kwa wakati huo wa kutimiza Ilani ya CCM kujenga shule kila Kata, shule hizo japokuwa kwa sasa linaonekana hazisaidii kwa kujitokeza kwa mapungufu mengi sana, naomba nikiri kuwa mwanzo ni mgumu, naiomba Serikali hasa Wizara husika ijitahidi kuweka juhudi katika kuhakikisha mapungufu hayo yanafanyiwa kazi zaidi. Kama maabara na vifaa vyake, shule kupatiwa waalimu wa kutosha na kuboresha mishahara ya Walimu yaani maslahi yao kwa ujumla ili kuwapa motisha kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kabla ya ujenzi wa shule hizi, wimbi la watoto kubaki mitaani lilikuwa kubwa sana hata kupelekea vijana wengi kujiingiza katika biashara ya matumizi ya madawa ya kulevya. Tatizo ambalo limeweza kuharibu nguvu kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili liliweza pia kuleta athari kubwa sana na hasa katika Mkoa wa Iringa, vijana waliokosa uwezo wa kuendelea na elimu ya sekondari mpaka kupelekea vijana kutafuta ajira katika miji mikubwa. Hasa mabinti zetu walikwenda katika kutafuta ajira isiyo rasmi ya kufanyishwa kazi za ndani kwa ujira mdogo, vijana kukimbilia mijini wakifikiria labda kwenda huko ni utatuzi wa maisha yao kumbe ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itupie macho ajira hii kwa sababu imesababisha kujitokeza madalali kuwachukua na kwenda kuwapeleka katika miji mikubwa kwa ahadi za kusomeshwa wakati si za kweli, ni uwongo mtupu.

Pia ajira hii mpaka sasa kila mwajiri anajipangia mshahara wake mwenyewe. Kwa sababu Serikali yetu sera yake ni maisha bora kwa kila Mtanzania basi na waangalie sekta hii isiyo rasmi inaangamiza vijana wetu maana madalali hao sasa wanathubutu hata kuwaondoa watoto waliofaulu na kuwatorosha mijini.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupandisha elimu ya kuishia darasa la saba na iwe mtoto akianza darasa la kwanza basi aishie darasa la kumi na mbili. Nina imani, itasaidia hata watoto wengi waishi kwenye wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuwa ombaomba mitaani tatizo ambalo limesababisha vijana hao kuichukua Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie na ufeli wa mitihani uliojitokeza kwa mwaka huu, pamoja na upungufu wa Walimu na mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika shule zetu za Kata, pia kuna tatizo ambalo sina uhakika kama linajulikana na hasa katika Halmashauri ya Iringa Mjini.

Kutokana na tatizo kubwa tulilonalo la Ugonjwa (*HIV*), Walimu wengi sana katika Mkoa wetu wamepata tatizo hilo ambalo imepelekea Walimu wengi kutokuwa na uwezo wa kufundisha yaani katika daftari kunaonekana shule ina Walimu wengi kumbe zaidi ya nusu wanapokea mishahara na kuongeza idadi bila kufundisha kutokana na hali mbaya walizonazo.

Mheshimiwa Spika, hapa ingetafutwa njia nzuri ya kutatua hili tatizo la Walimu wasio na uwezo wa kufundisha kwa sababu kuathirika na magonjwa vile vile uchaguzi uliweza kusababisha sana Walimu watendaji wetu kujiingiza katika ushabiki wa kisisasa na kusahau kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais na watendaji kazi wake kwa hotuba nzuri inayokidhi mahitaji yetu ya Taifa. Naomba katika mchango wangu nijikite kwenye suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lengo letu pia ni kuwawezesha wafanyabiashara wa kati ili washiriki katika uwekezaji mkubwa. Kwa sasa juhudi kubwa imeelekezwa kwenye wafanyabiashara wadogo wadogo. Maoni yangu ni kwamba:-

Kwanza, juhudi sasa ielekezwe pia kwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa. Wapewe mikopo mikubwa ili wafanye biashara kubwa, waweze kuajiri watu wengi zaidi. Kwa mikopo mikubwa tunaweza kuanzisha viwanda vinavyomilikiwa na wazawa; na

Pili, wazawa wenye uwezo wapewe dhamana *Government Guarantees* ili wakopeshwe na Taasisi za Fedha za nje mikopo mikubwa ili waanzishe viwanda au

biashara kubwa kubwa. Wazawa hawa wataweza kuwaajiri watu wengi zaidi kwa hiyo Taifa letu litaheshimiwa. Kwa sababu tunagemea kuinuka tu kwa njia ya wawekezaji wa nje ambao wengi wao wanayo malengo tofauti na yetu kama akina *RITES*.

**MHE BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais wetu kwa hotuba hii nzuri lakini pia kwa kazi kubwa anazozifanya ili kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii nzuri nisingependa kuichangia ila kuna suala la maji na viwanda ambalo nitachangia kidogo kwa msisitizo. Nianze na maji, maji ni uhai, maji ni maisha ya kila siku, maji ni kati ya masuala yanayopewa kipaumbele na Serikali yetu na kutafutiwa wafadhili mbalimbali wa kutusaidia shughuli hii lakini bado maji ni tatizo.

Naiomba Serikali ifuatilie zile Mamlaka za Maji ambazo huacha maboma yakachakaa sana na maji mengi kupotea bila ya sababu kwani ukiangalia wananchi wanalipia maji.

Jambo hili haliwezi kutupeleka mbele kwani maji mengi hupotea na huwa hayafiki kwa walengwa na hupelekea wananchi hasa wanawake kupunguza shughuli za uzalishaji mali na kusababisha kuongezeka kwa umaskini kwani muda ule wa uzalishaji mali yeye yuko kwenye foleni za maji. Hili ni tatizo kwa wananchi wa kipato cha chini, naomba sana Serikali ilianganalie kwa makini sana suala hili na iwachukulie hatua wale wote wanaoidhohofisha sekta hii ya maji ambayo ni muhimu kwa maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu viwanda. Wawekezaji wanahitajika sana hata wa viwanda vidogo vidogo kwani nchi hii Mwenyezi Mungu kaipa baraka kubwa sana, kuna matunda mengi na huwa hatuna uwezo wa kuyala na kuyamaliza na huwa yanaoza hivi hivi kwani hatuna viwanda vya kutosha vya kutengeneza juisi matunda haya yanayooza kwetu ni changamoto ya kutafuta wawekezaji wa viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza juisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii adimu ili nami nichangie, nitaanza kwa kuwashukuru wananchi wa Bukombe kwa kunichagua kwa kishindo. Ninachowaahidi ni kwamba nitawatumikia kwa uaminifu na unyenyekevu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke. Nimpongeze pia Naibu Spika, Wabunge wote, Mawaziri na Manaibu wao na Waziri Mkuu, nawatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, naona sisi Wabunge tuelekeze umakini wetu katika kupanga mipango iliyo na mwelekeo wa

kutenda haki kwa matabaka au makundi au hata maeneo ambayo hivi sasa yanakabiliwa na kero au matatizo au dhiki za msingi. Nitaelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuna tabaka la wasionacho au mafukara ambalo limeongelewa na baadhi ya wachangiaji. Nimefurahishwa na uchambuzi yakinifu alioutoa Mheshimiwa Zitto Kabwe, n imevutiwa na msisitizo aliouweka Mheshimiwa wa Mwibara na mifano waliyotoa Wabunge wengine, lililo wazi ni kwamba pengo baina ya walionacho na wasionacho linazidi kuongezeka licha ya kwamba takwimu za pato halisi la Taifa zinazoakisi ukuaji wa uchumi zinaonesha kuwa uchumi umekua. Ni dhahiri kwamba ukuaji huu wa uchumi umelinufaisha tabaka la watu wachache wanaomiliki uchumi wetu, kwamwe haujawanufaisha watu wa chini. Napenda kusisitiza kuwa watu wakiwa katika lindi la umaskini ambamo Watanzania wengi wamo kwa hakika hawana amani wala utulivu. Katika hali hii, sisi Wabunge tumsaidieje Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tunaweza kumsaidia Rais iwapo tutajiuliza, kwa kila mradi au mpango, je, mradi au mpango huu utasaidiaje kupunguza pengo lililopo baina ya walionacho na wasioancho? Mimi binafsi naamini kwamba iwapo tutafaulu kupitisha mipango inayowasaidia walionacho tutakuwa tumesaidia kuleta nafuu kwa tabaka hilo na kusaidia kudumisha amani na utulivu kwani kuvurugika kokote kwa mambo hayo hutokana na watu kuchoka na shida.

Mheshimiwa Spika, tofauti nyingine ambayo inabidi iwe dira katika mipango yetu ni ile ya kijinsia. Hapa kwa kila mradi au mpango lazima tujiulize; je, mradi au mpango utawanufaishaje wanawake? Ipo miradi ambayo ina manufaa kwa wote kama zahanati, shule, barabara na kadhalika. Lakini tukitaka kujenga hosteli au mabweni katika shule zetu za Kata, tuwafikirie wasichana kwanza. Au tunapopanga miradi vijijini au mijini, tuhakikishe miradi ya maji inapewa kipaumbele kwa sababu aghalabu ni akinamama wanaohangaika kwenda kutafuta maji. Kitaalam, mkabala huu huitwa kupanga bajeti kwa misingi ya kijinsia, (*gender budgeting*).

Mheshimiwa Spika, upo msingi mwingine muhimu ambao napenda kuupendekeza ili ufikiriwe na Bunge lako Tukufu, ili utumike katika kupanga mipango. Huu ni ule unaozingatia tofauti za kimaendeleo baina ya eneo moja na lingine. Hivi leo hapa Tanzania kuna Mikoa au Wilaya ambazo zimeendelea sana na zile zenye maendeleo duni. Viashiria vya tofauti hizi viko katika, sekta zote; elimu, afya, miundombinu, michezo na kadhalika. Mathalani, Mkoa wa Shinyanga kama ulivyo sasa una maendeleo duni katika maeneo mengi elimu, afya, miundombinu hasa vijijini lakini pia barabara za kuunganisha Wilaya na Wilaya, wakati Mkoa wa Kilimanjaro umeendelea sana katika sekta nyingi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara ametoa mfano wa Jimbo lake kuwa ni maskini sana tofauti na Majimbo mengine. Napendekeza Wilaya au Mikoa iliyo nyuma sana kimaendeleo ipewe upendeleo maalum katika mipango yetu ili iweze kukwamliwa kutoka kwenye tabu za ufukara, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo niliyoyataja yanahitaji mtazamo tofauti unaozingatia mambo yafuatayo:-

- Tuepuke misimamo mgando katika kutafakari nini cha kufanya katika kukabiliana na changamoto zetu.
- Tuepuke njia zilizoshindwa za kufanya mambo.

Mwisho, natoa wito kwa Wabunge vijana wasiogope kuvyaza mawazo mapya, vijana fanyeni utafiti wa kina bila ajizi na mtoe mapendekezo yenu bila woga.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Rais wetu kwa Hotuba nzuri yenye maelezo ya kina kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu. Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Serikali yetu inayoongozwa na CCM kwa kutekeleza Ilani kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba kuchangia kipengele cha kuendeleza sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda na madini. Mafanikio makubwa yamepatikana hasa katika kilimo kwanza lakini kuna changamoto nyingi zinazotakiwa kufanyiwa kazi wa mfano:-

Tayari Tanzania tuna vyuo vingi na wataalam wengi sana katika sekta ya kilimo na mifugo. Tatizo lililokuwepo hao wataalam wengi hawatumiki kwa mujibu wa taaluma zao na pia hawana vitendea kazi vinavyolingana na wakati tulio nao. Pia nafikiri wananchi kwa ujumla wao tayari wengi wameshaeleza jinsi gani ya kulima na kuongeza mazao kwa kutumia virutubisho (mbolea). Tatizo kubwa ni upatikanaji wa mbolea kwa wakati ili waweze kulima na kupata mazao yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna tatizo la msingi zaidi ambalo ni *post harvest* kwani mazao mengi yamepotea mashambani na maghalani hii ni kutokana na elimu ndogo ya kuhifadhi mazao na matumizi ya *end product* na kusababisha mazao mengi yanaoza na kupotea kwa wingi kama matunda na nafaka za punje kama mahindi na mpunga. Pia kukosekana na viwanda vya kusindika mazao Vijijini au Wilaya husika, hivyo Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niunge mkono hoja ya kuwawezesha wananchi kiuchumi inayosema hatutafanikiwa bila ya kuwawezesha wananchi na sekta binafsi ya ndani kushiriki na kunufaika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Serikali kwa kuwepo Taasisi mbalimbali na programu za kuboresha zikiwemo za *TASAF* na *MKURABITA*. Kwa kweli programu hizi ni nzuri na zimesaidia sana kuwaendeleza wananchi hasa wa vijijini. Changamoto zinazotukabili hasa katika sehemu ya kuendeleza wananchi ni kujipanga pamoja kwa wananchi wetu kwa njia za kujiunga pamoja katika vikundi na kuwawezesha kwa kuwapa mikopo midogo midogo (*SACCOS* na *VICOBA*)

hasa wananchi wengi wa vijijini walikata tama kwa kufikiwa maendeleo. Hii kwa kuhakikisha watendaji wetu wanarudisha utaratibu wa kusaidia wananchi Wilayani na Vijijini kwa kuweka huduma za Mabenki au ukopeshaji na nyinginezo.

Naomba tuongeze *speed* ya kuleta maendeleo kwa kudhibiti mapato ya Serikali na matumizi ya fedha za Serikali kwa watendaji wadogo na wa kati na kati, hawa ndio watendaji wetu. Lakini tuwe na umakini nao kwani ndiyo wanaoendesha au kushauri vibaya viongozi wetu, hivyo taratibu za kisheria na taratibu za kazi zifanyike ili kuondoa au kupunguza urasimu unaofanywa na watendaji hao ili wananchi waendeleo kuamini na kuipenda Serikali yao na kutekeleza dhamira ya Serikali zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Awali ya yote napenda kukupongeza wewe binafasi na Wabunge wote kwa kuchaguliwa tena Ubunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele kumi na tatu, nizungumzie kipaumbele namba nane cha kupanua fursa ya elimu. Ni ukweli usiopingika kuwa elimu ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Katika vitabu vitakatifu vinasisitiza kuhusu elimu. Kitabu cha Mithali 4:1-13 kinaeleza umuhimu wa elimu. Kwa nia nzuri sana shule za Kata zimeanzishwa lakini haukufanyika au hatukuwa na maandalizi ya kutosha ambayo yanapelekea wanafunzi wengi sana wafeli katika matokeo ya kidato cha nne. Kati ya sababu nasema shule hizi zilifunguliwa kisiasa zaidi ni kama ifuatavyo:-

Moja shule hizo hazijakamilisha vigezo:-

- (a) Nyingine hazina matundu ya choo ya kutosha;
- (b) Hakuna maji;
- (c) Hakuna maabara;
- (d) Hakuna Walimu wa kutosha; na
- (e) Watoto hawapati chakula cha mchana.

Hii ni tofauti na shule za watu binafsi. Kama shule hizo hazijatimiza vigezo hazipewi vibali vya kufungua shule. Swali, ni kwa nini shule za Kata zinaruhusiwa kufungulia pamoja ma mapungufu yote haya? Je, Serikali inajiandaa kuwasaidia wanafunzi wote wanaofeli ambao hawawezi kuendelea na masomo pia kupata ajira itakuwa ngumu kwao? Watakwenda wapi? Tusipoangalia watoto hawa watakosa cha kufanya na kuanza kufanya vitendo viovu kama ujambazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba tisa, kuboresha afya, maji, umeme, barabara, reli, bandari na anga. Kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani hivi ni vitu muhimu sana. Katika sekta ya afya bado zahanati zetu hazina vifaa vya kutosha hata hospitali za Wilaya unakuta akinamama inabidi waende na vifaa vya kujifungulia kama pamba na kadhalika. Pia hakuna Wauguzi na Madaktari wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Madaktari Bingwa, Manesi na Wauguzi wote walipwe mishahara mizuri ili wasikimbilie nje ya nchi kwa ajili ya kupata cha juu ili wabaki hapa hapa na uhaba utapungua kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, maji yanakuwa ni tatizo kubwa *especially* Jiji letu la Dar es Salaam ambako ndio kituo cha Taifa letu. Mpaka sasa hivi Jiji letu hakuna maji safi na salama. Mabomba mengine yanachanganyika na maji taka. Hii inapelekea magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu ambayo hayatakaa yatoweke katika Mji wetu bila Serikali kuhakikisha yanapatikana maji safi na salama. Kama tujuavyo umeme ni kero na ghali hata mkaa ni ghali, watu wengine hawawezi kumudu bei hizi ili wachemshe maji. Hivyo Serikali ifanye jitihada za makusudi kuondoa kero hii nchi nzima wakianzia na Jiji letu la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu anga, ili kuweza kupata faida katika hili ni vizuri kama nchi tuwe na Shirika letu la Ndege. Je, Serikali ina mikakati gani ya kufufua Shirika la ndege la ATCL? Bila Shirika letu kufufuliwa watalii wengi wanaotembelea vivutio vyetu bado wataona ni *expensive* sana kuja Tanzania kuliko Kenya. Wenzetu wa Kenya huwa wanakuwa na *special price* kwa watalii wanaotembelea nchi yao kwenye tiketi za ndege na hii inawezekana kwao ni kwa sababu tu wana Shirika lao la ndege ambalo linakwenda sehemu nyingi duniani. Hivyo, watalii huona Kenya kuna unafuu kuliko kuja Tanzania. Hata hivyo, watalii bado wanakuja kwetu lakini wangeweza kuwa zaidi kama tukiwa na Shirika letu ambalo linaweza ku-*fly International flights to* nchi za Ulaya na Marekani.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba hii. Pili, nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa kunichagua kwa ridhaa yao na kwa kura nyingi. Pia naishukuru familia yangu kwa ushirikiano ilionipa wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la afya, ni kweli hakuna Taifa linaloweza kuwa na maendeleo safi bila kuwa na wananchi wenye afya bora. Katika Jimbo langu kuna gari moja tu la huduma ya wagonjwa na linakaa kituo kimoja tu cha Afya. Kulingana na jiografia ya Mkoa wa Kagera kuna milima na mabonde mengi tena makali. Leo hii hata usafiri wa pikipiki hauwezekani, gari hili moja halikidhi mahitaji ya Wilaya nzima kwani gari lililopo hospitali ya Wilaya limechoka mno. Niombe Wizara ifanye tathmini upya na Biharamulo tupewe magari watatu ya huduma ya wagonjwa ili kupunguza idadi ya vifo vya akinamama na watoto na hata vifo vinginevyo katika jamii yetu, wote hususan akina mama wanafahamu jinsi uchungu unavyouma, pia mama mwenye uchungu atapanda pikipiki kweli?



Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watumishi, naiomba Wizara ifanye mpango wa kutoa motisha kwa wale wanaofanya kazi maeneo ya vijijini na hususan pembezoni kwani maslahi ni sawa na wale wanaofanya kazi mijini, hivyo hawa wapewe posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu (*Hardship allowance*). Pia wapunguziwe kodi katika mishahara yao (*income tax*), pia wapewe nyumba ili kuepusha suala la kupanga mitaani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wafugaji, sekta hii imeachwa hewani tu. Sekta hii inao uwezo mkubwa wa kukuza uchumi kwa kupata mazao bora yaani nyama safi, ngozi na maziwa bora. Katika Jimbo langu wafugaji hawajatengewa eneo la kufugia ukizingatia tumezungukwa na eneo la hifadhi. Kila siku ni wafugaji kukamatwa na kutozwa faini ambayo muda mwingine huishia mifukoni mwa watu wachache. Naiomba Serikali hususan Waziri mwenye dhamana kutembelea Jimbo langu ili kujionea hali halisi na pia kuhakikisha wafugaji hawa wanatengewa maeneo yao ya kufugia haraka. Pia huduma ya Maafisa Ugani iongezewe nguvu na wafugaji wafaidi huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira kwa vijana, naomba Serikali kuliangalia suala hili kwa ukaribu sana. Leo hii kuna vijana wengi ambao wanaamua kujiajiri kwa shughuli ya uendeshaji pikipiki. Naomba Serikali iwapunguzie gharama ya kupata leseni hizo na zipatikane bila ya mizengwe yoyote. Pia Jeshi la Polisi hususan kitengo cha Usalama Barabarani kuendesha mafunzo ya mara kwa mara ili kuwalinda abiria na vyombo wanavyoendesha wawapo barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi na usalama. Nalishukuru Jeshi letu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Lakini pamoja na hayo Serikali imewasahau maaskari wetu hususan kimaslahi na makazi yao kwa ujumla. Kuna Askari wengi wa JWTZ wanadai fedha zao za uhamisho na mafao ya wastaafu. Naomba Serikali waangalie maslahi yao na madai yao ili wafanye kazi yao kwa moyo mkunjufu. Pia wastaafu walipwe fedha yao katika vipindi vinavyokubalika na sio kucheleweshewa pia viendane na hali ya sasa ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la chakula, ni kweli hali ya chakula si shwari. Tathmini iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 7 Februari, 2011 haikuwa sahihi kulingana na maeneo tunayotoka. Ukizingatia Kata ya Kalenga hali ni mbaya. Kata ya Nyakahura hali si nzuri ukizingatia na tembo wamechangia kuharibu mashamba ya wananchi na wananchi hawa hawajawahi kulipwa fidia, kifuta jasho wala hata kifuta machozi kwa wale ambao wameathirika kutokana na hawa wanyamapori hususan tembo. Niiombe Serikali kufanya tathmini upya na kuwapelekea wananchi hawa chakula na pia mbegu zinazostahimili ukame.

Mheshimiwa Spika, pia Waziri wa Maliasili na Utalii atembelee maeneo haya na kujionea mwenyewe mazingira ya wananchi hawa ambao ni sehemu ya Watanzania wanaopaswa kunufaika na rasilimali za nchi yao, hususan huduma zinazotolewa kwa wananchi wanaozungukwa na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, sina budi kukupongeza wewe binafsi kwanza kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wetu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa hotuba yake ambayo imeonesha dira ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutukumbusha sisi Wabunge wajibu wetu na kutuasa juu ya hasira ambazo wananchi wanaweza kuzitumia kama silaha yao pale Mbunge ataposhindwa kuonekana katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru kwa ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais ya kutoa ushirikiano wake na wenzetu wote Serikalini katika kufanikisha majukumu yako wewe Spika na ya Bunge kwa ujumla. Nitakuomba Mheshimiwa Spika uitumie ahadi hii na fursa aliyokupa Mheshimiwa Rais, kuimarisha mhimili huu wa nchi yetu kuwa ndio kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa nchi yetu na kuwa ndio msimamizi mkuu wa utekelezaji wa vipaumbele vyote ambavyo Mheshimiwa Rais amevieleza.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na watendaji wake kuwa makini na kauli ambayo mimi naipongeza sana ya Mheshimiwa Rais aliyosema: “Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kutimiza ahadi zetu kwa Watanzania”. Napenda nichangie katika suala zima la afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti kwa Wizara hiyo ila kutokana na Sera ya Afya ambayo ilitungwa mwaka 2003, nina mashaka na utekelezaji wake, hasa katika Mpango Na.3 wa Sera hiyo wa kuongeza uwezo wa kupambana na maradhi hasa yale yanayoathiri na kuua watu wengi. Naiomba Serikali kuwa na dhamira ya dhati katika hili kwani hivi sasa kwa mfano katika hospitali yetu kuu ya Muhimbili, inapofikia saa 12 jioni unashindwa kukaa katika wodi au eneo la hospitali kutokana na adha kubwa ya wingi wa mbu ambao huwauma na kuwashughulisha sana wagonjwa na wale wote wanaohudumia wagonjwa. Naomba Waziri aje alieleze Bunge lako Tukufu, ni lini adha hii ya mbu katika hospitali yetu ya Muhimbili itaondoka kwani mbu husababisha maradhi ambayo huweza kuondoa maisha ya mtu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kumshukuru Rais kwa hotuba yake nzuri na napenda kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JADDY SIMA JADDY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kimaandishi mchango wangu kuhusiana na kipaumbele namba moja cha hotuba ya Rais. Naiomba Serikali kuongeza spidi ya kujadili na kutatua wa Kero za Muungano pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba sita, naomba Serikali itoe tamko rasmi juu ya nini msimamo wa Serikali katika umiliki wa madini ya “*Uranium*” yaliyovumbuliwa

nchini ili kuepuka kuibuka upya kwa mjadala kuhusiana na maliasil hiyo kama ilivyotokea kwa mafuta upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba nane, naomba Serikali iweke utaratibu maalum kwa wanafunzi kutoka Zanzibar utakaowawezesha kufuatilia kwa karibu na kwa gharama ndogo zaidi nafasi za kimasomo wanazozipata wanapochaguliwa kujiunga na Vyuo vilivyoko Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba tatu, naomba Mheshimiwa Rais aendelee Mfuko wa Mabilioni ya Kikwete ili uweze kuwanufaisha wananchi wetu kiuchumi na hasa wale wa vijijini kwa kuvipa kipaumbele vikundi mbalimbali vya kiushirika vilivyoanzishwa na wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Rais, naomba kuchangia hotuba hiyo katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, uchumi kuendelea kuwa tegemezi. Uchumi wetu utaendelea kuwa tegemezi kwa muda mrefu kwa vile mipango mingi mizuri inaishia kwenye maandishi badala ya kusimamiwa vizuri ikatekelezwa. Moja ya maeneo yenye udhaifu mkubwa ni Idara ya Kukusanya Kodi (*TRA*). Utendaji wa *TRA* ni mbovu sana na ndiyo maana bado hatuwezi kukusanya kiasi cha kutosheleza matumizi yetu. Bado *TRA* wanatoza ushuru na kodi mbalimbali kwa mtindo ambao hauvutii walipaji kabisa. Walipa kodi wananyanyaswa sana na Maafisa wa *TRA*. Mazingira ya Ofisi za *TRA* hayawavutii walipa kodi na ni ya udhalilishaji sana. Napendekeza watafutwe maeneo makubwa, zijengwe ofisi nzuri zenye hadhi na walipa kodi wakifika, wapewe heshima na ukarimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Mgano ni Ofisi za *TRA Uganda Revenue Authority*. Mahali ofisi zao zilipo, huwezi ukakosa sehemu ya kuegesha gari, matusi wala watu kuswagwa kama vile wahalifu wakati kumbe hawa ni raia wema ambao wanakwenda kulipa kodi wachangie maendeleo ya Taifa lao, hakuna.

Mheshimiwa Spika, vilevile mtindo wa ukadiriaji Ushuru wa Forodha wa sasa uachwe kabisa. Mlipa kodi yapaswa afahamu mapema atalipa kodi kiasi gani kwa bidhaa anayoagiza. Orodha ya bidhaa na Ushuru wa Forodha iwe wazi kwa wananchi, hii itapunguza rushwa iliyokithiri maeneo yote kunakotozwa Ushuru wa Forodha. Orodha iwekwe wazi, wananchi wajue wanapaswa kulipa kiasi gani kwa bidhaa wanazoagiza. Hii itaondoa Umungu Mtu ulipo huko *TRA*, Idara ya Forodha.

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa Forodha utozwe bila ubaguzi. Leo mlipakodi wa Zanzibar analipa kidogo ukilinganisha na yule wa Dar es Salaam. Kuna kitu kinaitwa *reassessment*, hili jambo ni kero kubwa kwa wananchi. Ni *double standard* katika kutoza watu ushuru hata kama yapo maelezo. Mtindo huu ukomeshwe mara moja, vigezo vifanane kwa walipakodi wote wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nishati. Nashauri Serikali iwekeze zaidi katika sekta hii. Tuwe na uzalishaji na usambazaji wa uhakika. Hasara leo tuyoipata kwa mgao huu Kitaifa, naomba itajwe ili tuweze kwa pamoja kuchagua kati ya hasara hiyo au malumbano yasiyo na tija kwa afya ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ajira. Wananchi wengi wanajiajiri katika shughuli mbalimbali za kilimo. Hivyo ni vema mikakati ya makusudi ichukuliwe ili kuhakikisha kilimo kinastawi. Kilimo chenye tija kinahitaji mtaji kama zilivyo biashara zingine. Benki zitungiwe sheria zinazowalazimisha kukopesha wananchi katika kilimo na Serikali iweke kinga kwa benki dhidi ya wawekezaji katika kilimo watakaokumbwa na majanga.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Buchosa. Kivuko cha MV. Geita kifanyiwe ukarabati wa dharura kama ilivyo ahadi ya Rais Kikwete. Ukiisha mwaka, hiyo siyo dharura tena. Wananchi wanasubiri kwa hamu na Wizara iweke katika bajeti ya mwaka huu fedha kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kpya kwa ajili ya kisiwa cha Maisome.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehemu zake nyingi. Pia napenda kukishukuru Chama changu cha *CUF*, familia yangu na wananchi wote wa Jimbo langu la Chonga. Naahidi kuwatumikia wao na Taifa kwa ujumla na hawatajuta kunichagua.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, kwa kuonesha dhamira ya dhati na kuitekeleza, ya kusaidia kutatua mgogoro wa Zanzibar kwa kushirikiana na Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Aman A. Karume na Katibu Mkuu wa *CUF*, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad ambaye sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU). Pia namshukuru Rais wa sasa wa Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Ali Muhamed Shein na Makamu wa Pili, Mheshimiwa Balozi Seif Idd, kwa uungwana wao. Muungano ni kitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kutowaonea aibu ya kuwafukuza kazi mara moja wafanyakazi wa Idara za Muungano wanaoitia doa Serikali na kuisababishia kuchukiwa na wananchi wake kwa kutotekeleza maamuzi ya Serikali hasa kero za Muungano. *TRA* wamekuwa na jeuri, kiburi na kuwanyanyasa wafanyabiashara wanaoleta bidhaa zao Dar es Salaam kutoka Zanzibar kwa kuwatoza kodi mara ya pili.

Tatizo hili limekuwa sugu pamoja na kuwa limeshapatiwa ufumbuzi na Tume inayoshughulikia kero za Muungano iliyokuwa chini ya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar. Tatizo hili ni kero sana na limekuwa ni mnyororo waliofungwa wafanyabiasahra hawa ambao ni wadogo na wa kati, wanabaki kuwa wafanyabiashara wadogo miaka nenda, miaka rudi. Iko wapi hapo nia nzuri ya Rais wetu Dr. Jakaya M. Kikwete ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati?

Mheshimiwa Spika, katika kipengele cha saba (7) cha hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameeleza kuhusu kuboresha zaidi ukusanyaji wa mapato, lakini kwa takwimu zinavyoonyesha kuna misamaha mingi sana ya kodi. Uzoefu unaonesha wanaosamehewa kodi ni wafanyabiashara wakubwa. Ipo haja sasa ya kuwasaidia kuwakomboa wafanyabiashara hawa wa kati na wadogo kwa kutowalipisha kodi mara mbili na kuelekea kwa wafanyabiashara wakubwa ili walipe kodi kihalali na ukusanyaji wa mapato uboreke.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja sasa kwa Mashirika kama Reli kufanya kazi kwa ufanisi na kuchangia mapato ya Serikali badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kupunguza kuwakamua wafanyabiashara tu, hasa wafanyabiashara wa kati na wadogo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa kulizindua Bunge jipya la Kumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo manne yafuatayo, kilimo, barabara, mawasiliano ya simu za mkononi na suala zima la elimu.

Mheshimiwa Spika, kilimo, ni wazi kilimo ndiyo mwajiri wa Watanzania wengi nchini. Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza tayari imeonesha mafanikio kadhaa na yanaleta matumaini.

Pamoja na matumaini hayo, zipo changamoto ambazo endapo hazitashughulikiwa kwa ukamilifu, hakika mchango wa kilimo katika suala zima la kupunguza umaskini wa wananchi na Taifa kwa ujumla wake. Changamoto hizo ni kama hizi zifuatazo:-

Kwanza kabisa, suala la kuongeza ruzuku ya kilimo ili ikiwezekana vocha za pembejeo zinazotolewa zikidhi mahitaji halisi ya wakulima wetu yaani kama kuna mkulima anataka kulima zaidi ya ekari moja apate kulingana na maandalizi aliyonayo ili mradi asimamiwe na Maafisa Ugani ambao ni muhimu pia wawepo kila kijiji.

Pili, Mawakala wetu wasajiliwe na wapewe elimu hasa elimu ya uzalendo, ili mchango wao muhimu ulete tija kwa Taifa na endapo watasajiliwa maana yake wataona kazi yao ni ya kudumu na hawatashiriki katika wizi au vitendo vya kutokuwa waaminifu.

Tatu, uaminifu kwa watumishi wa kilimo, ni muhimu sana kwani watarahisisha huduma hii kufika kwa walengwa na kwa kiasi kilichopangwa. Uaminifu ni muhimu kwa watumishi ili wasishirikiane na Mawakala wasio waaminifu.

Nne, pembejeo kupelekwa kwa wakati, napendekeza mwezi Julai, wakati wa mavuno, huu ni wakati muafaka kwani mkulima anakuwa na mazao ambayo anayategemea sana kununulia pembejeo hizo. Mapinduzi katika kilimo yanatega *mechanisation* yaani matrekta makubwa yapatikane, tena bila urasimu kama ilivyo sasa.

Tano, utaratibu wa soko la mazao ya wakulima, nashauri kipindi Serikali inanunua mazao hasa ya chakula, bei zilingane na za gharama za uzalishaji. Masoko pia yasongezwe karibu na wakulima na vilevile kuongezwe vituo vya kununulia mazao.

Kwa mfano, Jimbo la Nkasi Kusini, lina kituo kimoja tu cha kununua mazao, jambo ambalo huleta usumbufu. Naomba kila Kata ikiwezekana kiwe na kituo cha kununua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kilimo, pia tunao wajibu wa kuendeleza uvuvi. Jimbo la Nkasi Kusini, lina Kata tatu za Kala, Wampembe na Ninde zilizoko katika Mwambao mwa Ziwa Tanganyika na kuwa hawajanufaika na rasilimali hiyo kutokana na vyombo duni na butu vya kutafutia riziki zao kutoka Ziwani. Tuwape msukumo mpya kwa kuwasaidia zana za kuvulia na mitaji zitakazokidhi uvuvi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, barabara. Katika kampeni za uchaguzi wa 2010, Mheshimiwa Rais, Jakaya Kikwete, alitoa ahadi ya kuboresha barabara kuunganisha Kata za Mwambao. Kata hizo ni Kala, Wampembe na Ninde ambazo zimekuwa nyuma na huvamiwa na majambazi kutoka Kongo. Naomba Serikali itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kata za Kala, Wampembe na Ninde, hawajapata mawasiliano ya simu licha ya barabara kuwa hazifai. Naomba Serikali ielekeze macho katika kuhakikisha mawasiliano yanapatikana, hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, elimu. Suala la elimu ni muhimu. Katika Jimbo la Nkasi Kusini, Walimu hawatoshi hasa katika Shule za Sekondari ambazo idadi yake ni kumi ukiachia mbali matatizo ya maabara katika shule zote, nyumba za Walimu, zana za kufundishia na kadhalika. Naomba Serikali inisaidie Walimu katika shule za Jimbo la Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, nakupa pongezi kwa kuteuliwa kuwa Spika mwanamke na wa kwanza hapa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira kwa Wabunge na wananchi wote ili kuleta ufanisi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishukuru familia yangu, wananchi wa Iramba Mashariki, kwa kunitua kuwa Mbunge na mwakilishi wao. Ninaahidi sitawaangusha na nitawatumikia daima. Nakishukuru pia Chama cha Mapinduzi kwa kunipigania na kuibuka mshindi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Rais ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu elimu. Upungufu wa Walimu unachangiwa na ucheleweshaji wa kupangiwa vituo vya kazi. Wanakaa muda mrefu (Miezi 5-6) na hujikuta wanaanza kutafuta ajira mbadala. Wapangiwe kazi mara moja wamalizapo mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Wilaya mpya. Kuhusu Wilaya mpya zilizoteuliwa na Mheshimiwa Rais ikiwemo na Wilaya yangu ya Mkalama katika Jimbo la Iramba Mashariki. Naishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- (1) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa majengo;
- (2) Umeme wa kuanzia shughuli zote za Ofisi na ujenzi;
- (3) Maji ni ya muhimu, Serikali ihakikishe yanapatikana ya kutosha; na
- (4) Watumishi wa kutosha kukabiliana na changamoto za uanzishaji wa Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuchangia eneo la Umoja wa Kitaifa, rejea ukurasa 12. Kwa mfano alivyosema Mheshimiwa Rais, nguvu ya wanyonge ni umoja. Naomba ikumbukwe kuwa Umoja ni Nguvu na Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano inasema Serikali haina Dini ila watu wake wana Dini.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Mashirika ya Dini kuelewa kuwa hawapaswi kushughulika na siasa na kuwalazimisha wananchi kufuata Chama fulani kama ilivyokuwa Sumbawanga Mjini, Kanisa la RC, kuwalazimisha waumini wake kuchagua Chama cha CHADEMA na wale ambao hawakufanya hivyo, waliambiwa wamekiuka imani ya Kikristo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusema kuwa, Serikali na Mashirika ya Dini inabidi vishirikiane kuleta Umoja katika nchi na amani kwani Mashirika ya Dini huomba kibali cha kuhubiri, kujenga Makanisa na kuingiza bidhaa bila ya kodi kulipwa. Hatutarajii Mashirika haya kufanya kampeni za kisiasa na jambo hili wapewe maonyo mapema Mashirika ya Dini ili Serikali, Misikiti na Makanisa, wote wawe na Umoja na kukemea maovu.

Mheshimiwa Spika, eneo la madini, rejea ukurasa 21 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, alisema tutaendelea kutatua changamoto ambazo bado hazijapata ufumbuzi, changamoto hizi ni pamoja na Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambao kwa miaka

mingi haujaanza kufanya kazi. Naomba maelezo juu ya Mradi wa Madini wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue nafasi hii, kushukuru kuwepo kwa Mikoa Mipya, rejea ukurasa wa 35, utawala bora, ikiwa ni pamoja na Mkoa Mpya wa Njombe. Ombi langu ni miundombinu katika Mkoa huu mpya izingatiwe ikiwa ni pamoja na Mkoa Mpya wa Katavi. Mkoa wa Njombe unahitaji Ofisi, barabara ya lami na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo la elimu, rejea ukurasa wa 27 wa hotuba. Ipo haja ya kuwa na *VETA* (Vyuho vya Ufundi) kila Wilaya hususan Wilaya ya Ludewa na pia umuhimu wa kuwa na *High School* kila Tarafa yaani *Form IV* na *VI*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia maeneo haya machache, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa hotuba ambayo imetoa dira na matumaini kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais amekuwa ni hodari sana hasa katika kushughulikia kero za wananchi ambazo zilionekana kushindikana. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia katika eneo la maji. Kwanza, naomba fedha zaidi zitengwe kwenye bajeti ijayo katika sekta ya maji. Hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi, si nzuri ila katika Jimbo langu la Lulindi hali ni mbaya sana na kufanya wananchi kuhangaika na kukata tamaa. Ndoo moja ya lita 20 huuzwa kwa shilingi 1,000/= hali inayofanya wananchi wengi kutomudu kupata maji. Naishauri na kuiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kuwanusuru wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, elimu, afya na huduma za jamii. Katika maeneo haya, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuonesha dira. Naishauri Serikali kuimarisha Serikali za Mitaa na kuziondolea vikwazo na kero zinazowakabili. Pia kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani ili wazisimamie Halmashauri zao vyema. Pia Halmashauri kuzijali Ofisi za Serikali za Vijiji na Mitaa. Pia kwa kupeleka fedha kwenye Kata kwa ajili ya kuzihudumia Ofisi hizi na Wenyeviti wake.

Mheshimiwa Spika, pili, naiomba Serikali kuacha kunyofoa shughuli zinazofanywa na Halmashauri na kuzirudisha Serikali Kuu. Kwa mfano:-

(i) Serikali kuamua magari yote yanunuliwe na Wizara ya Miundombinu. Jambo hili limesumbua na kurudisha nyuma juhudi za Halmashauri kujiletea maendeleo yao. Naishukuru Serikali kurekebisha utaratibu huu; na

(ii) Serikali Kuu kuamua ajira zote zifanywe na Wizara inayoshughulikia na Utumishi. Jambo hili litadhoofisha juhudi zilizoainishwa kwenye hotuba yake. Naishauri Serikali kurudisha Mamlaka hayo kwa Halmashauri ili ziendelee kuajiri.



Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kuanzisha mkakati wa Kilimo Kwanza. Naiomba Serikali izingatie kuhakikisha kwamba wakulima wanapatiwa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu. Wataalamu wetu wawe karibu na wakulima na pia Serikali isimamie ipasavyo kuhusu masoko ya mazao kwa kuwasimamia wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutafuta soko la korosho kwa kuanzisha utaratibu wa Stakabadhi Ghalani, umeleta manufaa sana. Ombi la wananchi ni kulipwa fedha yote ya bei inayotangazwa na Serikali na wakulima wasubiri bonasi baada ya mauzo ya korosho. Jambo hili litawasaidia wakulima wadogo ambao huzipata fedha hizi huku wakikabiliwa na mikopo ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa Mbunge ili niwawakilishe wananchi wa Tanzania wa Jimbo la Mtoni, Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. Nawaahidi wananchi wa Jimbo hilo, sitawaendea kinyume katika kufikisha kilio chao na kuzima kiu yao ya kupata maendeleo. Aidha, nitatekeleza ahadi zangu pasipo kuvunja Kiapo cha Utii cha Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani nyingine maalum kwa mke wangu Nachum pamoja na wanangu, ndugu, jamaa na marafiki, pamoja na timu yangu ya Kampeni, kwa jinsi walivyovumilia taabu na shida, dhiki ya maisha na tashtiti za kisiasa hadi ushindi wa Jimbo la Mtoni katika Uchaguzi Mkuu wa Serikali yetu ukaja kwangu mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani nyingine za dhati kwa Chama changu cha *The Civic United Front (CUF)*, Chama cha Wananchi tangu ngazi ya tawi la Kidatu “A”, Jimbo la Mtoni, Wilaya ya Magharibi hadi Baraza Kuu la Taifa, kwa kunipatia kura za maoni za kutosha na hatimaye kuteuliwa kuwa mgombea. Kwa namna ya pekee, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mtoni kwa uamuzi wao thabiti wa kunichagua kwa kura nyingi sana bila ya kujali tofauti zao za kiitikadi na kisiasa. Nawaahidi kuwanoa bega kwa bega ili kuondoa kero zilizopo katika Jimbo hususan maji, huduma ya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mama Anne Makinda, kwa kuruhusu michango ya maandishi kwa wanaokosa nafasi za kuchangia kwa kusema hapa Bungeni. Ninakupongeza sana kwa kuipata bahati ukiwa mwanamke, ya kuliongoza Bunge letu katika nafasi uliyonayo. Ni jambo la historia ya heshima kwa Taifa letu, Mungu akujalie umri mrefu na maisha ya fanaka pamoja na hekima, busara na umakini katika kazi yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na Watanzania kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia namshukuru mno, kwa hotuba yake fupi, yenye hoja za msingi katika kuiendesha nchi

yetu kwa ufanisi, maendeleo na utangamano, wakati wa kikao cha Bunge letu, cha tarehe 18 Novemba, 2010 alichokiitisha yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie vipaumbele viwili tu katika hotuba ile. Kipaumbele cha kwanza na cha nane kati ya vipaumbele kumi na tatu alivyovieleza.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele namba moja, umoja, amani na usalama wa Muungano wetu. Tangu 26/4/1964, tunao Muungano wa Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar unaoitwa Tanzania. Mwalimu Julius K. Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume, wakiwa Wakuu wa Nchi hizo mbili, walikubaliana kuunganisha baadhi ya vipengele vya kuendesha nchi na kutangaza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Bila ya kujali ukubwa au udogo wa Tanganyika au Zanzibar na bila kupiga kura ya maoni ya wananchi wa pande hizo mbili. Watanzania tuliwakubali na kuwaunga mkono viongozi wetu wawili hao, kwa nia ya kutaka umoja, amani na usalama wa Muungano kama Taifa moja. Leo kumezuka Wanasiasa na wasemaji wanaobeza Zanzibar na hata kudiriki kusema kuwa Majimbo 23 ya Zanzibar ni sawa na Jimbo moja tu la Tanzania Bara! Huu ni uchochezi na dharau ya hali ya juu inayoashiria ubaguzi, utengano, shari na mparaganyiko wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nilidhani Bungeni tutaheshimu historia ya nchi yetu na kuchangia kuisaidia Serikali namna ya kukabili changamoto zinazokwaza juhudi za Serikali za kuleta maendeleo. Kumbe sivyo! Baadhi yetu tunapitikiwa!

Hali ni hivyo kwamba wapo watu bado wanatoa kauli za kukatisha tamaa dhidi ya Maridhiano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Zanzibar hata ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa taarifa yao, hivi sasa Zanzibar ni tulivu na ina amani ya kutosha na hali hiyo ndio ishara bora kwa umoja, amani, usalama wa Muungano wetu. Naiomba Serikali kupitia Bunge hili, kudhibiti maadili ya Muungano wa Tanzania na kuwadhibiti wale wote wanaotaka kuyamomonyoa kwa nguvu yote ya Kikanuni, Sheria na Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 21-29, Mheshimiwa Rais ametoa ufafanuzi kwa ufupi juu ya azma aliyokuwanayo kuhusu elimu kabla ya kutangaza Baraza la Mawaziri. Kama utekelezaji wa sera zilizopo na maelezo yale vitakwenda sambamba na hali halisi ya utendaji kazi wa watendaji wa Serikali, tutajenga Tanzania mpya mapema sana. Naziunga mkono jitihada za Serikali katika fani ya elimu ila napenda kutoa maoni yangu yafuatayo:-

- (1) Mshahara wa Walimu uendeleo kukua ili watu wapende kuwa Walimu;
- (2) Vifaa vya kufanyia kazi mfano vitabu, vifaa vya maabara na maabara zenyewe ziendelezwe;
- (3) Mitihani ya Kidato cha Pili irejeshwe kama kule Zanzibar; na

- (4) *HESLB* ipate marekebisho yanayostahiki baada ya mapendekezo ya hiyo Tume ya watu 11 bila ya kujali undugu na urafiki.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea *UDOM* na kuona tatizo kubwa sana la ukosefu wa maji. Wanafunzi wanasema maji hupatikana kikawaida siku za ziara za Wakuu wa Nchi au Mawaziri. Aidha, kuna tatizo la makaro na mabomba ya maji machafu. Ni hatari kwa afya ya jamii ya Chuoni *UDOM*. Mzabuni wa chakula hapo chuoni anapika chakula kisichoridhisha. Wanafunzi wanadai, mzabuni wa mwanzo alikuwa akipika vyakula vizuri lakini amekoseshwa nafasi hiyo na kupewa huyo wa sasa. Wanafunzi wanatilia mashaka kama rushwa haikutumika katika kumpata mzabuni wa pili. Juhudi za Serikali zifanyike ili wanafunzi wa Vyuoni waweze kupata mazingira yanayowashawishi kusoma na kujifunza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Serikali, hotuba ya Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoe tarehe 18 Novemba, 2010 alipokuwa anafungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nichangie hoja katika suala la elimu, afya na huduma za jamii. Katika suala la elimu, Serikali na taasisi mbalimbali na wadau wa elimu, waangalie upya namna ya kuwasaidia na kuwawezesha vijana wenye vipaji maalum katika fani ya sayansi na teknolojia.

Kwa mfano, kijana wa Sumbawanga aliyetangazwa jana yaani tarehe 13 Februari, 2011 ambaye ameweza kutengeneza treka kwa kutumia injini ya pikipiki. Hawa ni watu ambao wakiendelezwa, wanaweza kufanya vizuri katika suala zima la kupunguza umaskini na kuleta maendeleo si tu ya familia bali Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika suala la afya, Serikali ingeweza kuangalia upya suala la mfumo mzima wa matibabu kwa wazee na wastaafu, kwani wamekuwa wakipata sana taabu wanapokuwa hospitali. Aidha, nashauri Serikali iwaandalie utaratibu wa matibabu kwa wazee na wastaafu kama utaratibu wa bima ya afya kwa watumishi basi na wao wangeandaliwa utaratibu kama huo, kwa maradhi mengi ya uzeeni ikiwa ni pamoja na magonjwa ya sukari, moyo na mifupa. Magonjwa haya ni ghali kwa matibabu ikizingatiwa kwamba wazee/wastaafu ni vigumu kuyamudu, hivyo basi, naomba Serikali iliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali iangalie namna ya kuwasaidia walemavu ambao wana ulemavu zaidi ya mmoja. Serikali iangalie namna ya kuwawezesha ili waweze kujikimu kimaisha kama vile inavyofanya kwa mfano wagonjwa wenye VVU na makundi mengine yanayohitaji mambo yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali iangalie namna ya kupeleka wahudumu wa afya maeneo ambayo wahudumu hao aidha hawapo kwa sababu mbalimbali mfano

kusoma, kuugua na mengineyo. Mfano hospitali ya Mpanda mpaka sasa haina mtaalam wa maabara yaani *X-ray* na *Ultra Sound*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kwa maendeleo ya Taifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunitiua kuwa Mbunge na hatimaye kunitiua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili niweze kukidhi matarajio ya Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu takriban wazungumzaji walionitangulia wanakiri kama ninavyokiri kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa na amani, utulivu na usalama. Hata hivyo, baadhi ya wakati kuna vitendo na matukio ya uhalifu ambayo kwa namna moja au nyingine yanaweza kuhatarisha amani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, upo uhusiano mkubwa kati ya amani, haki na maendeleo. Hii haina maana kwamba sisi kama Taifa, tunapona vitendo au matukio yanayohatarisha amani, tufunge mikono, tusichukue hatua za kudhibiti mambo hayo. Sisi Serikalini kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, tutafanya kila linalowezekana kwa kushirikiana na Watanzania na kila anayeitakia mema nchi yetu, kuzungumzia umuhimu wa kudumisha amani lakini na kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha amani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, wanadhani Mataifa matajiri na yenye neema kuliko sisi hayana changamoto za usalama na amani kwa ujumla. Nitawapa mfano, mwezi uliopita pale Marekani, nchi ambayo ina ustawi mkubwa sana na maendeleo ya kupigia mfano, yupo mtu mmoja alichukua silaha akampiga risasi Mbunge wa *Congress*, kwa bahati nzuri hakupoteza maisha, lakini watu wengine watatu walipoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, kuna nchi moja iliyostawi sana kimaendeleo Kaskazini mwa Bara la Ulaya, ilimpoteza Waziri. Hali hii inathibitisha kwamba sisi Mataifa maskini na tajiri, sote tunakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoweza kuhatarisha amani na usalama wa nchi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa amani na usalama, Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kupitia Jeshi la Polisi, inachukua hatua mbalimbali ili kuimarisha amani na usalama wa nchi yetu. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunaandaa programu ya kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi. Madhumuni makubwa ya program hii ni kuwapatia Askari na Maafisa wa Jeshi la Polisi vifaa vya kisasa, maslahi yaliyo bora na makazi ili kukuza ari na motisha katika utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunalolifanya ni kuwapatia Askari na Maafisa wa Jeshi la Polisi mafunzo, hasa katika masuala ya upelelezi ili kuzisaidia Mahakama mbalimbali kuendesha kesi kwa haraka zaidi. Hivi karibuni nilipata nafasi ya kutembelea Magereza yaliyoko katika Mkoa wa Dar-es-Salaam na kuwaomba Viongozi wa Jeshi la Magereza wanipatie tathmini ya hali ya Magereza kwa ujumla. Katika tathmini hiyo imeripotiwa kwamba Tanzania nzima tunao wafungwa na mahabusu wapatao 38,000 hivi na kati ya hao 50% ni mahabusu.

Hii inadhihirisha wazi kwamba tunayo kazi kubwa katika kusimamia masuala ya upelelezi ili kuharakisha kesi. Ndio maana tunasema sisi katika Wizara ya Mambo ya Ndani tutajitahidi sana kutafuta nafasi ndani na nje ya nchi ili vijana wetu wa Jeshi la Polisi, waweze kufanya kazi ya upelelezi kwa ufundi, utaaalam na weledi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni kuwashirikisha wananchi katika ulinzi na kutoa taarifa za uhalifu mapema iwezekanavyo ili tuweze kudhibiti na kupambana na makosa hayo. Jambo la nne, tunayo dhamira na mipango ya kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshiriki katika vikao mbalimbali vya kero za muungano na katika mikutano hiyo tulijadili mambo yafuatayo na mengi ya hayo yameshapatiwa ufumbuzi. La kwanza, ni Zanzibar, inapatiwa 4.5% ya misaada ya kibajeti, hivi sasa Zanzibar inao uwezo wa kukopa ndani na nje ya nchi bila matatizo. Jambo la tatu, ni maandalizi ya ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, yameshaanza.

Mheshimiwa Spika, nne ni tayari umeshawekwa utaratibu wa kugawana mapato ya uvuvi wa bahari kuu na katika mgawanyo huo, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, inapata 50% ya mapato, Serikali ya Muungano inapata 30% na Zanzibar inapata 20%. Jambo la tano, ni Wizara ya Fedha ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi, zinaagizwa ziangalie nyaraka za uanzishwaji wa Benki kuu ya Tanzania, ili kujua hisa za Zanzibar zilizoko katika Benki hiyo. Jambo la mwisho kubwa ni suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta bado linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kulizungumza ni katika mjadala huu unaoendelea katika Bunge, zimejitokeza hisia za kudharau Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika Majimbo yenye uwakilishi mdogo. Jambo hili halileti umoja na mshikamano miongoni mwetu, kama hadhi utukufu na enzi ya Mbunge inapimwa kwa uwakilishi wa wananchi walioko kwenye jimbo lake basi leo Mheshimiwa Mnyika anayeongoza Jimbo lenye watu zaidi ya 450,000 angekuwa Mwenyekiti wa Chama chake na Mkuu wa Shughuli za Upinzani katika Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani tumekuja katika Bunge hili kujadili hoja, nakuomba unistahimili, naomba dakika moja tu, *Martin Luther King* aliwahi kusema maneno yafuatayo na naomba kuyanukuu, ninayo ndoto kwamba siku moja watoto wangu wanne wataishi katika Taifa ambalo watu hawataangaliwa kwa ajili ya rangi ya ngozi yao bali wataangaliwa kwa hulka na matendo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi Shamsi Nahodha nina ndoto kwamba siku moja Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watawaangalia wajumbe wenzao au Wabunge wenzao si kwa udogo wa Majimbo wanayotoka bali watawaangalia wenzao kutokana na hoja zao kutokana na matendo yao na kutokana na michango yao katika kujadili masuala mazito yanayotukabili sisi kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa kwa watakaofuata naomba muache habari ya kumshukuru Rais kama hamkumwandikia barua basi na mwache habari ya kuwapongeza wengine basi kwa sababu mambo ya kujibu hapa ni mengi dakika kumi ni kidogo kabisa na habari ya kuwapongeza akinamama na watoto wenu nayo mwache.

Unajua kuna mwananchi mmoja ameniandikia anasema Mheshimiwa Spika wanatukera kweli, wanawapongeza wake zao na watoto wao wanadhani wao ndiyo waliowapigia kura. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Mawaziri *I am serious* kweli kwa sababu dakika hizi ni chache, mkipongeza tu *five minutes then other five* hamwezi kujibu kitu anzeni moja kwa moja kujibu. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi atafuatiwa na Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika mjadala unaoendelea. Pamoja na yote namshukuru Mwenyezi Mungu kuzaliwa Mtanzania, kwenye nchi ambayo asili yake ni amani, utulivu na upendo nchi ambayo ina kila rasilimali ambazo mtu ungefikiria nchi yako iwe nazo. Ina bahari, milima, mabonde na ardhi nzuri, nchi ambayo kama ilivyo ina kila ambacho inastahili isonge mbele kimaendeleo. Katika nchi hii ni wazi uchukuzi unakuwa ni kitengo cha muhimu sana ili nchi isonge mbele, uchukuzi kwa ufanisi wake uwe wenyewe lakini pia kwa kufanikisha vitengo vingine vyote vya uchumi tangu kilimo, usafiri wa kilimo, watalii, madini na vingi vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuongea wamejadili mambo mengi na mengi yamegusia uchukuzi, wameonyesha kero zao, wameonyesha wasiwasi wao kuwa uchukuzi wetu utaimarika vipi ili tuweze kwenda mbele. Mimi nitajikita kwenye hilo, nitajikita kueleza kwa uchukuzi Serikali imejipangaje ili nchi yetu ifaidike kwa kitengo hiki na iweze kupiga hatua kwa kasi ile ambayo tunategemea na tunataka ipige.

Mheshimiwa Spika, kwenye reli na bandari, hivi naviweka pamoja kwa sababu mfumo wa reli na bandari huwezi kuugawa hasa ukiangalia kuwa sisi tuna jukumu kubwa la kuifanya nchi yetu iwe lango la biashara na uchukuzi sio kwetu sisi tu peke yetu bali pia kwa nchi ambazo zimetuzunguka na ambazo hazikupata neema ile tuliyopata sisi. Sasa neema hii tuliyonayo ni lazima tuitumie kusaidia wenzetu, unapoangalia bandari na reli kuna suala la kuboresha bandari zetu, tuna bandari ya Dar es Salaam ikiboreshwa sio tu itakuza uchumi wetu sisi lakini pia itasaidia kukuza uchumi wa wengine.

Kwa sasa bandari tunaiendeleza kwa kuongeza gati, kuna gati namba 13 na 14, hiyo itachangia ipanuke bandari yetu na kutoa huduma zinazofaa. Zaidi ya hivyo pamoja na kuwa kuna sehemu ambazo tunaweza kuzitumia kuhakikisha kuwa bandari hiyo inakuwa kubwa ya kuweza kuchukua majukumu yale ambayo imewekewa hapo baadaye, tunafikiria kuiongeza bandari ichukue sehemu ya Vijibweni na Kurasini na kufungua Kituo cha Makontena kule Kisarawe. Ufanisi wa bandari unakwenda sambamba na jinsi unavyofanya kazi ndani ya bandari, sasa hivi nyakati nyingine kuna msongamano, tunaweka mikakati ya kulikabili hili. Tuna mfumo ambao unatumika ambao *Reserved Berthing Window*.

Mfumo huu tutautumia kuwezesha meli kubwa ambazo zinaweza kuja kwa muda ambao unatakiwa, ziweze kupakua upesi na ziondoke ili makontena na vifaa vingine ambavyo vinaletwa kwa Tanzania na kwa nchi zilizozunguka za Burundi, Rwanda, Kongo na pia nchi ya Zambia na Malawi vinafika huko kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, si Bandari ya Dar es Salaam peke yake, tunazo bandari nyingine, tuna bandari ya Tanga ambayo sasa hivi haifanyi kazi vizuri na tuko katika mkakati wa kuirudisha bandari ile ifanye kazi inayostahili. Kwa miezi mitatu ijayo tunawezeza pale takriban shilingi bilioni 10 ambazo zitaifanya bandari ile ichanganye kama ambavyo inastahili ili ihudumie sehemu ya Kaskazini ya Tanzania. Pia tuna mpango wa muda mrefu wa kujenga bandari nyingine pembezoni mwa bandari ya Tanga, bandari ya Mwambani, sio tu ituhudumie sisi lakini pia ihudumie wenzetu wa Uganda, wanaisubiri hiyo. Tukifanya hivyo, miaka mitano ijayo tuboreshe tujenge reli ya kutoka Tanga mpaka Moshi, Arusha na tujenge mpya mpaka Musoma pamoja na kujenga bandari ya Musoma, ili mtiririko wa bidhaa zinazoingia na zinazotoka nchini kwetu na Uganda ziwe zinafaidika kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nirudi tena kwenye reli ya kati. Reli ya kati tunataka kuipanua iingie katika *standard gauge* meta 1.435 ili iweze kuchukua mabehewa mengi kwa uzito ambao utakuwa umeimarika, iweze kukubalika pia kupata treni ambazo zinakwenda kasi katika reli hiyo. Reli hiyo sasa hivi imeshafanyiwa *feasibility study* mpaka sehemu ya Isaka, kutoka hapo tunajiunganisha na wenzetu wa Rwanda na Burundi, kule Kigali na Musongati ili watu wa Rwanda na Burundi wafaidike.

Mheshimiwa Spika, pia katika sehemu ambazo ziko katikati ya Tabora mpaka Kigoma, Isaka-Mwanza, Kaliua-Mpanda, Ruvu-Mruazi, Kilosa-Kidatu, Manyoni-Singida pia kwa miaka mitano tunataka tuweke *standard gauge* huko. Kwa sasa, kazi kubwa tuliyonayo ni kuboresha reli hii ili usafiri wa abiria sambamba na usafiri wa mizigo uongezeke. Hapa tulipo tuna mikakati ya mwaka mmoja ya kulifanya hilo litimie halafu tunakwenda mbele kwa mikakati ya miaka miwili ili ikifika miaka miwili tuwe na angalau treni moja inayokwenda kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na Dar es Salaam mpaka Mwanza kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ni usafiri wa reli na bandari na tumejipanga sawa sawa kuhakikisha usafiri huu unafanya kazi. Tutatumia rasilimali zetu, tutawavutia wenzetu wawekeze ili hilo lifanikiwe na Bunge lako hili lina kazi kubwa sana ya kuunga mkono mikakati hii ifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, kwenye uchukuzi hatuishii hapo, kuna uchukuzi/usafiri wa anga wa abiria pamoja na mizigo Tanzania, usafiri huo haujachanganya. Sasa hivi tunajipanga kuweka mikakati ya kuhakikisha usafiri huo unachanganya. Tunafanya hayo sambasamba na kufanya kila linalowezekana tulifufue Shirika letu la Ndege.

Shirika la Ndege (*ATCL*) ndiyo litakuwa ni kitu cha muhimu cha kwanza katika kufanya usafiri Shirika la Ndege uchanganye. Pia katika mikakati yetu mbinu nyingine ni kuvutia wawekezaji wa mashirika ya ndege hasa katika mfumo ambao unaokubalika kidunia kwa wawekezaji kuweza kuitumia Tanzania kama *their principal place of business* waje waanzishe hapa *Low Cost Carriers* ili nauli zipungue ili watu wengi waweze kuutumia usafiri wa anga, usafiri wa anga uchanganye, ukue, viwanja vyetu vikue, usafiri wenyewe ufikie wakati kuwe na safari nyingi za ndege ndani na nje ya nchi.

Kwa hiyo, tunaweza kutoka Tanzania kwenda nje ya Tanzania, tukitumia ndege zetu za hapa nchini. Ili usafiri huo uchanganye hivyo kuna wajibu wa kuboresha viwanja vyetu vya ndege. Pale Dar es Salaam tumeshatenga sehemu ya kuweka *terminal three* ya kiwanja cha Mwalimu Julius Nyerere *International Airport, Terminal Three* ile imeshafanyiwa *feasibility study* na sasa hivi tuko katika hatua ya kutafuta jinsi gani *terminal* ile itaanza kujengwa. Katika mikakati yetu tumeweka mwaka 2011/2012, kazi hiyo ianze.

Mheshimiwa Spika, viwanja vingine ni vilivyosambaa katika nchi yetu, kuna Kiwanja cha Bukoba. Juzi tu hapa nilikwenda kukizindua baada ya hatua ya kwanza kukarabati ili kiweze kuchukua ndege kubwa. Hivi leo ninavyoongea kimetoka katika ndege ambayo inachukua *passenger 18* na sasa hivi tayari kinahudumia ndege ya ATR 42 inayobeba abiria 50.

Sio hicho tu, kuna viwanja vingine; cha Tabora, Kigoma, Shinyanga na hapa Msalato ambapo tunataka kujenga Kiwanja cha Kimataifa, tunataka pia na tumeanza na tunamaliza ikifika Agosti hiki Kiwanja cha Songwe kilichopo Mkoa wa Mbeya kitakuwa kimekamilika, kile ni Kiwanja cha Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchukuzi ni kitengo muhimu na sisi kwenye Serikali tumejipanga, tunakwenda kwa mikakati imara, tunakwenda hatua kwa hatua mpaka tuhakikishe nchi yetu hii kweli inakuwa ni lango la biashara, ni lango la uchukuzi kwa nchi yetu na kwa nchi za Afrika Mashariki na ya Kati. Haya yanaweza kufanikiwa, narudia tena ile asili ya amani ya nchi yetu ikiendelezwa; amani isipokuwepo nchini kwetu hatuwezi kupiga hatua hizo ambazo tunataka kuzipiga. Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alitabiri akasema kuwa yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyainisha katika hotuba yake yakifanywa yote haya basi tutakuwa sisi tunaingia kwenye nchi



zilizoendelea duniani na hilo ndiyo lengo la chama chenu, ndiyo lengo la Serikali yetu kuingiza nchi hii katika orodha ya nchi zilizoendelea duniani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):**  
Mheshimiwa Spika, dakika moja.

**SPIKA:** Ndiyo imekwisha hivyo, mkifanya hivyo wenzenu hawatafikiwa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):**  
Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa namwita Waziri wa Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba nichangie hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge waliziwasilisha wakati wanachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango kabambe, kwanza wa kufufua viwanda vile ambavyo vilikuwa vinafanya kazi vikabinafsishwa na kwa sababu moja au nyingine wale ambao walikabidhiwa waliahidi kwamba Kiwanda hiki cha Korosho sisi tutakiendeleza na kukiboresha, tutakiongezea mtaji na tutakiongezea teknolojia, hawakufanya hivyo. Wizara yetu imeanza mchakato wa kuviangalia viwanda vyote na wale ambao hawatakuwa wamefanya kazi ambazo tulikubaliana kimkataba, viwanda hivi vitarudi tena Serikalini na kuanza mchakato mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba mfanyabiashara yeyote na kuanzia sasa hivi tunapokwenda mbele anapodhani anaweza akaingia mkataba na Serikali, akaidanganya akijua kwamba atakapochukua kiwanda hiki atakigeuza kuwa godauni ili bidhaa zetu kwa mfano korosho ziendeleo kupelekwa India, ziendeleo kupatia ajira watu wa kigeni, hilo halitavumiliwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vipya ni sera ya Serikali ya Awamu ya Nne, pamoja na kuendelea kuangalia tutafanya nini juu ya viwanda ambavyo vilichukuliwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na idara zingine za Serikali tuna mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba tunaanzisha viwanda vipya, viwanda vipya vidogo vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa. Hivi karibuni nilitembelea *SIDO* Mwanza na nikamtembelea mjasiriamali mmoja ambaye alikuwa kwenye *compound* ya *SIDO* na yeye alianzisha biashara ndogo ya kuweza kusindika kahawa na asilimia 90 ya kahawa yake anauza katika Mji wa Mwanza na kipato chake kwa mwezi kilikuwa kimefika milioni 40 na alikuwa ameajiri watu saba, stahili hii ndiyo ambayo itaweza kutukomboa Watanzania, watu waanze kuwa wajasiriamali, watu waanze kufikiria kupata faida, kufikiria kuleta ajira kwa Watanzania wenzao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha tangu mwaka 2003, Sera ya Viwanda Vidogo na Sera ya Biashara Ndogo ndogo, na tayari mapitio ya Sheria ya *SIDO* yameshakwishaanza, wadau wameshirikishwa na tunatarajia muda sio mrefu tutaiboresha Sheria ya *SIDO* ili waweze kushirikiana kwa karibu na vijana wetu wanaomaliza VETA. Kuwe na *linkage* kati ya vijana wanaosoma na wanaotafuta ajira na kile ambacho tunaweza tukakifanya kwa kushirikiana na wenzetu wa VETA, na wenzetu wa *SIDO*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunategemea na tunatarajia kila Mtanzania achange katika pato la Taifa, kila Mtanzania katika shughuli anayojishughulisha awe sehemu ya kutatua tatizo ambalo tunasema nchi yetu iko chini. Napenda kutumia lugha ya kwamba, tungependa kuona Watanzania wanajishughulisha na shughuli za kuleta faida katika maisha na kuongeza pato la Taifa.

Katika nchi hii asilimia 80 ya Watanzania wote kwa ujumla wanaishi vijijini wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kilimo na takriban asilimia 20 ya Watanzania wengine wanajishughulisha na kazi ambazo tunaziita *informal enterprises*, shughuli mbalimbali wengine wameajiriwa rasmi, wengine wanajishughulisha na kazi zao wenyewe na hoja ya kwetu ni kwamba lazima tuwatambua hawa watu, lazima tukutambue biashara unayofanya na unafanyia wapi? (Makofi)

Ni lazima tutambue Kiwanda unachotengenezea *furniture*, unatengenezea chini ya uvungu, ukauza bila kulipa kodi ya Serikali au tukikufahamu tutakusaidia, tutakupa ujuzi, mtaji, ikiwezekana lakini na wewe uchange katika pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwa takwimu zilizopo Watanzania milioni 20 walikuwa wamejiunga, tunaita *telephone subscribers* walikuwa na simu za mkononi. Watanzania kati ya milioni 45, milioni 20 wana simu za mkononi na kufikia mwaka jana na haya ni mambo ya biashara, kufikia mwaka jana Watanzania hao milioni 20 walitumia bilioni za Kimarekani mbili, *two billions USD* katika kupiga simu ambazo zimekwenda kwa makampuni mbalimbali ya simu. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba tunao watu wengi ambao hawajahusishwa moja kwa moja katika utaratibu wa kuilipa Serikali mapato yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi ya Ujerumani mwaka jana katika bajeti *support* iliisaidia Tanzania *Euro* bilioni 10 na watakaa watakwambia leta hiki na hiki tunaendelea kushirikiana na wadau hawa. Lakini kwa hakika uchumi huu utajengwa kama alivyosema Mwalimu Nyerere na wananchi wenyewe. Uwezo tulio nao wa ndani ni mkubwa kuliko tunavyofahamu na ni azma ya Serikali kuhakikisha tunafahamu. (Makofi)

Katika Wizara yetu tumeanzisha mpango tukishirikiana na Benki ya Dunia na kufikia mwisho wa mwezi huu tutatoa taarifa inayoonesha *Non formal enterprises*, ni shughuli zote za kibiashara ambazo siyo za kilimo, ambazo zinaitwa siyo rasmi ni ngapi na wako wapi, tunapowatambua watu wote wanaojishughulisha na biashara jambo la kwanza tunaweza tukawasaidia. Jambo la pili ni kwamba, Serikali itapata mapato yake

katika kila anachojishughulisha nacho Mtanzania na hili ni jambo jema na zuri ambalo sisi wote tungenda tuliunge mkono.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulitaja aliliuliza mmoja kati ya Wabunge, akasema katika miaka 10 au 20 iliyopita wamesikia habari ya Makaa ya Mawe, anauliza Makaa ya Mawe yako wapi na yanatakiwa yatusaidie nini?

Mheshimiwa Spika, chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) limekasimiwa Mamlaka ya kuendelea kuingiza ubia na watu mbalimbali yaani wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kufufua na kuendeleza mradi wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme duniani ni 50% ya mahitaji yote ya nishati ya umeme inatokana na Makaa ya Mawe. Hapa Tanzania Makaa ya Mawe hadi sasa hivi yanachangia 0%. Mchuchuma peke yake tuna *reserve* ya Makaa ya Mawe inayokadiriwa kuwa milioni 440 *metric tones*, yaani tani zile ambazo ziko chini na katika mradi ambao Serikali imeuibua chini ya *NDC* na mbia ambaye amepatikana tutaanza kuunganisha na kufua chuma cha Liganga ambacho ni zaidi ya bilioni moja *reserve* ya chuma na kuweza kufua umeme wa *megawatt 600*. *Megawatt 600* ni umeme mwingi sana na hili jambo limeanza, mbia amepatikana na Serikali itakapomaliza na tunategemea kwenye mwezi Aprili tutamaliza hili jambo ili kazi hii iweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mbinga nilitembelea pale Ngaka, *NDC* na Shirika lingine la Australia wameanza mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa *megawatt 400* ambao utakuwa chini ya *NDC*. Tunaposema *NDC* ni makusudi kwa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata hisa ambazo zitashikiliwa na Serikali kwa ajili ya vizazi vijavyo na vizazi vitakavyofuata ili mali hii inapotoka ardhini tuhakikishe kwamba Watanzania wana sehemu ya kuishi.

Lakini niseme kwamba tuna Makaa ya Mawe zaidi ya *metric tones* milioni 400 na ule mradi ambao umeanza ni wa kutumia *metric tones* mbili tu kwa mwaka. Unaweza ukatumia miaka 100 ukiwa bado unaendelea kuchimba makaa haya ya mawe.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba nchi hii imebarikiwa na ina baraka nyingi. Serikali hii itakuwa makini kwa kuunganisha Wizara zote zinazohusika. Tutahakikisha tuko makini katika ku-*negotiate* yaani katika kupatana na wawekezaji wapya wanaokuja hapa nchini ili tuhakikishe kwamba mali iliyolala chini ni kama ule mziki unaosema: “Embedodo limelala mchangani”. Mali iliyolala chini tuweze kuifukua ifaidishe kizazi hiki, wanafunzi wote wa vyuo vikuu, wanafunzi wote wanaosoma waweze kupata nafasi ya ajira ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunatamani mwendelee lakini haiwezekani. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):**

Mheshimiwa Spika, na mimi naunga mkono hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Rais. Katika hotuba yake amezungumzia masuala mengi sana yanayohusu barabara na hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa katika kuhakikisha *network* ya barabara zetu imekamilika na zinatengenezwa kwa kiwango kinachowezekana ikiwa ni pamoja na lami. Ukiachia mbali na fedha zinazotokana na *Road Funds* ambazo zinagawanywa kwenye barabara za Halmashauri pamoja na barabara kuu na barabara za Mkoa ambazo ni zaidi ya bilioni 284 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu. Serikali pia imejipanga vizuri katika kuhakikisha barabara nyingi *especially trunk roads* zinajengwa kwa kiwango cha lami.

Ukianzia kwa mfano, kutoka Mtwara upitie Dar es Salaam, uende Mwanza hadi Kagera sehemu iliyobaki kutengenezwa kwa kiwango cha lami ni kilomita 60 ambazo ni kutoka Ndundu hadi Somanga. Pia katika kipindi cha miezi sita tumeshatoa *instruction* kwa Mkandarasi anayefanya kazi pale ahakikishe amemaliza, kwa maana nyingine mtu atatoka Mtwara atakuja Dar es Salaam kwa kupitia Lindi, atapita kwenye Daraja la Mkapa aje Dar es Salaam, apite Morogoro aende Dodoma, Manyoni, Shinyanga na aende Mwanza akazungukie apite Geita, Sengerema, Kyamyorwa, apite Bukoba hadi Mtukura si kwa *taxi* tena bali atapita hata kwa Bajaji. (Kicheko/ *Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukichukua barabara ya Tunduma kwenda hadi Mbamba Bay zile kilomita 230 za kutoka Tunduma hadi Sumbawanga kuna Wakandarasi ambao wanafanya kazi pale kupitia mradi wa *MCC* na kuna jumla ya bilioni 288 zinatumiwa pale. Lakini kutoka Sumbawanga hadi Kibaoni ambapo kuna jumla ya kilomita 150 pia kuna Wakandarasi ambao wanafanya kazi pale kwa kutumia fedha za Serikali karibu bilioni 150. Sasa kutoka Kibaoni-Mpanda-Kigoma hadi Nyakanazi hiyo sehemu ndiyo haina Mkandarasi na tumepanga katika bajeti ya mwaka kesho ikiwezekana tutumie fedha zetu kwa kutumia *design and construct* ili hilo eneo nalo liweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kutoka Nyakanazi kwenda Biharamulo mpaka Kagoma ambapo kuna jumla ya kilomita 154 pale kuna Mkandarasi anaitwa Chiko anayefanya kazi kwa bilioni 191. Kwa hiyo, unaweza ukaona hiyo *corridor* itakuwa imekamilika kwa kutengenezwa katika kiwango kizuri.

Mheshimiwa Spika, ukianzia Dodoma kwenda mpaka Kigoma kwa *section* nyingine, leo katika jibu la asubuhi kuna Wakandarasi ambao wanagharimu zaidi ya shilingi bilioni 422 katika sehemu ya Nzega hadi Tabora na kutoka Manyoni-Itigi kuelekea Tabora hadi Urambo. Kutoka Urambo kupitia Kaliua mpaka kwenye daraja la Malagarasi *design* zimekwishamalizika. Lakini kwenye daraja la Malagarasi kwa sasa hivi kuna Mkandarasi wa kutengeneza sehemu hiyo ambaye ni kampuni ya kutoka *South Korea* kwa zaidi ya shilingi bilioni 75.

Mheshimiwa Spika, ukishatoka pale kwenda Kidawe-Uvinza hadi Kigoma, kutoka Kigoma hadi Kigawe ambapo kuna kilomita 36 eneo hili limeshamalizika kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Limebaki kutoka Kidawe hadi Uvinza ambapo

nako kuna Mkandarasi ambaye ameshapewa kazi kwa gharama ya shilingi bilioni 76. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiingia kwenye *section* nyingine ambayo inajulikana kama *The Great Northern Road* kutoka Arusha, Babati, Dodoma hadi Iringa kwa sababu tunazungumzia juu ya barabara ya *The Great Northern Road* kutoka Cape Town hadi Johannesburg kwamba inatakiwa iwe ya lami, sehemu iliyokuwa imebaki kutokuwa na lami ni Tanzania tu. Kwa bahati nzuri tumesaini Mkataba na Wakandarasi watatu kutoka Dodoma hadi Iringa na wataanza kazi wakati wowote kwa bilioni 221.2 kwa ufadhili wa *African Development Bank*. Lakini pia tumeshasaini Mkataba na Mkandarasi ambaye yuko kwenye *Site, Syno Hydro* kwa kilomita 43 kutoka Dodoma kwenda Mayamaya. Kwa hiyo, sehemu inayobaki ni kutoka Mayamaya hadi eneo la Babati ambapo kuna jumla ya kilomita 160 ambapo tumepanga katika bajeti inayokuja *design and construction* ili tuweze kumaliza hilo eneo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukitoka Babati kwenda mpaka Singida kuna Wakandarasi wanafanya kazi na eneo hilo limeshakamilika kwa kiwango cha lami. Ukichukua eneo lingine la barabara ya kwenda Mbamba Bay ukianzia Mingoyo ukapita Masasi lile eneo lote ni lami pamoja na kilomita nyingine karibu 54. Lakini kwa mwaka huu kwenye wiki kama mbili hivi zilizopita tumesaini Mkataba na Wakandarasi wataanza ujenzi kutoka Tunduru hadi Namtumbo kilomita 197 ambapo kuna bilioni 180 zitatumika pale. Lakini pia kuna Mkandarasi kutoka Songea kwenda Mbinga karibu kilomita 76 hivi, napo kuna Mkandarasi anafanya kazi. Kwa hiyo, sehemu itakayokuwa imebaki ni kutoka Mbinga kwenda Mbamba Bay karibu kilomita 65 nazo tumepanga katika kipindi cha bajeti inayokuja tuziweke ili zianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utaona katika *network* ya barabara zote ikiwepo na ile barabara ya kutoka Mto wa Mbu kwenda Serengeti ambapo kwa bahati nzuri kupitia Ngorongoro nayo iko kwenye mpango ili kuweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Itapita kwenye eneo la mbuga karibu kilomita 53 tu lakini eneo lingine lote linapita ambako si kwenye mbuga na sisi tumeamua ile barabara nayo iwe ni muhimu kwa kufungua maeneo ya Kaskazini mwa Tanzania ili wananchi waweze kupita kwa kiwango cha lami na watu wasafiri kikamilifu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiacha *section* hiyo, kuna eneo lingine ambalo limebaki ambalo ni barabara ya *Trunk Roads* kutoka Biharamuro kwenda Buziku, Bwanga kupitia Lunzewa ambapo kuna jumla ya kilomita 112 na bahati nzuri mmefafanuliwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi. Ile nayo tutaiweka kwenye mpango unaokuja pamoja na daraja ambalo linavusha Kilombero na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete imefanya makubwa sana katika miradi ya barabara. Barabara zinatengenezwa na nataka kuwathibitishia kwamba katika miaka minne ijayo Tanzania hapatakuwa na barabara ya Changarawe inayohusiana na barabara ya *Trunk Roads* ambazo ni jumla ya kilomita 10,000. Kulingana na mipango mizuri iliyopo ukilinganisha na mipango mingine pia inayokuja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika barabara za Dar es Salaam ambazo nazo kuna miradi mingi tu ambayo inafadhiliwa na *World Bank* tutaanza na ujenzi wa barabara ya kutoka Kimara hadi Mtoni pale Kivukoni ambapo kuna jumla ya kilomita 20.9, katika kupunguza msongamano na kuna zaidi ya bilioni 129 zimetolewa na *World Bank*. Labda wiki moja inayokuja tutasaini *contract* na Wakandarasi pamoja na vituo vingine saba. Ninachotaka kusisitiza hapa kwa sababu muda wangu umekwisha ni kwamba wananchi wote na bahati nzuri katika kipengele cha 10 cha hotuba ya Mheshimiwa Rais kimezungumzia juu ya kuheshimu Sheria, nawaomba Watanzania tuheshimu Sheria ikiwa ni pamoja na Sheria namba 13 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria ya mwaka 1967 ambayo ni *Cap 167* inayozungumzia hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, nataka kuthibitisha na kusisitiza hapa kwamba wale wote watakaokuwa wanaguswa ambao wako ndani ya hifadhi ya barabara hakuna atakayelipwa fidia na kwenye barabara hakuna Siasa, CCM, CHADEMA, CUF, UDP wala hakuna mtu ambaye hana chama. Ni lazima tuzingatie Sheria zetu ambazo tumezipitisha sisi Waheshimiwa Wabunge hapa, zikafanye kazi ili barabara zetu ziweze kupitika. Wale ambao wataguswa wako nje ya *Road Reserve*, wale ni lazima walipwe kwa mujibu wa Sheria namba 13 ya mwaka 2007 lakini pia ni lazima walipwe kwa mujibu wa Sheria namba 4 na 5 ya ardhi pamoja na Sheria namba 7 na 8 ya Matumizi Bora ya Ardhi na Maendeleo ya ..... (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niliweke hili wazi ili ujenzi wa barabara usije ukakwamishwa kwa nia nzuri ya Serikali na ya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na mitandao mizuri katika barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuthibitisha kwamba hatatakiwa mtu yeyote kuvamia *Road Reserve* hata kama ni kwa kuweka mabango, kwa mfano huwezi kujenga nyumba yako halafu mpangaji aende akapatane na mtu mwingine kuja kupanga kwenye nyumba yako. Barabara za Dar es Salaam zimejengwa na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, aaaaah! Naunga mkono hoja na Mungu ibariki Tanzania. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa masikitiko sana inabidi nikunyang'anye wakati, sasa nitafanyaje! Mheshimiwa Waziri wa Afya na Waziri wa Elimu ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuomba radhi na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kudra zote alizoniwezesha hadi leo niko kwenye Mjengo huu. Vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu.....

**SPIKA:** Muda haukuruhusu Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nimejipanga nitamaliza tena kabla ya kupigiwa kengele.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hotuba ya Mheshimiwa Rais hasa waliogusia masuala yanayohusiana na Afya na Ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kuchangia kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo alidhamiria wazi kuongeza huduma za afya kuelekeza hasa kwa wananchi wanaoishi vijijini ambao takwimu zote zinatonyesha wananchi wengi wa Tanzania 80% wanaishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, huduma hizo zimeelezwa kupitia mpango wa MMAM ambao ni Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, imeelekeza zaidi huduma hizo zinakwenda vijijini kwa kuanza na Zahanati, Vituo vya Afya, kuelekea Hospitali za Wilaya. Ndani ya mpango huu umesitizwa tena kwamba tutakuwa na Vituo vya Afya ambavyo vitawezesha kutoa huduma zinazohusiana na *operation* ndogo ndogo hasa kwa kuwasaidia akinamama wajawazito pale wanaposhindwa kujifungua kwa njia ya kawaida basi wapate *operation* hizo kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejitayarisha barabara kukabiliana na changamoto na hapa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walizozionyesha na nawaahidi sitawaangusha, nitazifanyia kazi na nyingine nitaziweka katika bajeti ambayo sasa hivi iko kwenye matayarisho, nitazileta kwenu kwa ajili ya kupitisha.

Mheshimiwa Spika, wao wamekuwa na wasiwasi kwamba *are we so ambitious* tutaweza kujenga Zahanati? Ndiyo! Kwa kushirikiana na wananchi kuwahamasisha lakini je, hizo Zahanati zitakuwa na watumishi wa kutosha kuweza kuwahudumia?

Mheshimiwa Spika, la pili, je katika hizo Zahanati dawa zitapatikana kwa uhakika pamoja na vifaa? maana zisiendeleo tu kupigwa bao pale kwenye Zahanati au kwenye Kituo cha Afya, vitumike vifaa vya kusema huyu Bwana au Bibi anaumwa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, naomba nitoe ufafanuzi zaidi hasa nitaanza kwa upande wa upatikanaji wa watumishi wa afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi na taaluma nyingine wanaotoa huduma za afya upande wa Maabara na kwingineko.

Tumejitayarisha kwa vipengele vine. Cha kwanza, ni kuongeza udahili wa watumishi hawa. Tayari mwaka 2010 tumeshaanza udahili wa Madaktari mpaka 2010 katika vyuo vitano, vyuo vikuu vinavyotoa mafunzo ya Shahada katika taaluma ya Udaktari wamefikia 800 kutoka 400 huko siku za nyuma. Vyuo hivi ni Muhimbili, Kairuki, Bugando, *IMTU* na Dodoma na bado tuna mpango wa kuongeza vyuo vingine na kuongeza udahili zaidi ili itakapofika kati ya miaka 10 wakati tumejipanga tuwe na Madaktari wa kutosha na ikiwezekana wengine tuwa-*export*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwamba baada ya kuwatengeneza Madaktari wa kutosha kinachofuata ni kitu gani, je, tuna uwezo wa kuwa-*sustain* kwenye vituo ambavyo tutawapanga na watumishi wengine? Tumewekeza na tumejitayarisha kuweka mipango kwamba, kwanza wakishamaliza kuhitimu tunahakikisha tunawapangia moja kwa moja wataaluma wote upande wa afya kwenye vituo vinavyohusika. Kwenye vituo vile kwa kushirikiana na wenzangu wa TAMISEMI tutaweka vivutio maalum, kimojawapo kikiwa ni nyumba, mafao na kadhalika. Hapa katikati tumesimamisha zile posho ambazo zilikuwa zinatolewa kama Daktari au *Nurse* anavyoitwa kwenye *call*, sasa hivi hizi tutazirudisha angalau zitoe vivutio kwa hawa watumishi wanapofanya kazi zao katika mazingira ambayo ni magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nje ya hayo kuongeza na kuajiri moja kwa moja na kutoa vivutio ikiwa ni pamoja na nyumba na maslahi mengine. Vile vile Wizara yangu naomba niseme kwamba, tulikuwa tumechoka na malalamishi ambayo yanatoka mara kwa mara, wakati mwingine Watumishi hawa, aidha, kwa makusudi wanafanya kutokuwajibika au katika mazingira mengine ya rushwa. Kwa hiyo, nawahakikishia Wabunge wenzangu na wananchi kwamba utawala wa sasa hivi utakuwa ni wa vitendo, tutaiga ule utawala ambao Wajerumani wanasema *Carrot and stick*. Tayari hawa tumekwishawapa karoti, ndiyo hivyo kuna nyumba watapatiwa, watawezesha lakini pale watakapokosa aidha kwa makusudi au kwa uzembe basi watachukuliwa hatua za kinidhamu mara moja. Ndiyo hiyo *system* ya *carrot and stick* ambaye wenzetu Wajerumani wamefanikiwa katika utawala.

Mheshimiwa Spika, imejitokeza changamoto ya upatikanaji wa vifaa na dawa katika Zahanati zetu na Vituo vya Afya. Wizara yangu imejitayarisha kwamba, mfumo ambao ulikuwa unatumika kwa kupitia Wakala wetu wa kusambaza vifaa na dawa (*MSD*), yeye alikuwa anapeleka dawa mpaka Wilayani. Sasa hivi tutauboresha mfumo huu badala ya *MSD* kuishia Wilayani, atakwenda mpaka kituo husika, kama ni Zahanati au Kituo cha Afya au Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hii siyo tunajaribu au kutaka kubahatisha, hapana. Tumekwishaanza hiyo kwa kufanya utafiti. Tumefanya majaribio Mkoa wa Tanga, umeonesha mfumo huo unafanya vizuri sana.

Kwa hiyo, katika bajeti ijayo tutakachofanya ni kuongeza zaidi huduma hizo. Tunaanza na Mkoa minane, baadaye tutakuwa tunatanua zaidi. Ombi langu sasa kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wengine katika Halmashauri, ni kwamba mzifufue au mziwezeshe Bodi za Hospitali, Bodi za Vituo vya Afya, Bodi za Zahanati ziwe na uwezo wa kutekeleza, kusimamia na kudhibiti upatikanaji wa dawa pamoja na vifaa ambavyo vimeelekezwa kule kwenye Zahanati zao au kituo husika.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge vile vile wameonesha wasiwasi wao kuhusu masuala yanayohusiana na rufaa na mawasiliano. Wizara yangu imejitayarisha kuwekeza haya upande wa *Radio Calls* na Simu za Mkononi ambavyo ni miongoni mwa vitu vinavyoweza kuboresha suala la mawasiliano.



Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la rufaa kutoka kwenye Zahanati kwenda kwenye Kituo cha Afya. Kama mtakumbuka mojawapo ya masuala yaliyojitokeza tulizungumza kwamba tutawezesha kuongeza ufanisi kwenye hiyo kwa sababu kikwazo kilichokuwa kinajitokeza ni suala la usafiri. Tutatumia usafiri wa pikipiki ambazo zinakokota *Ambulance*.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya nimeigiza Wizara yangu waniletee sampuli na tayari zimefika pikipiki 20 kwenye Bandari ya Dar es Salaam na nina hakika huenda kabla hatujaahirisha Bunge lako hapo hizo sampuli za pikipiki zitakuja mzione. Kama tulivyosema awali pikipiki hizi zinaongeza ufanisi zaidi katika kubana matumizi kwa sababu zinatumia mafuta kidogo na hata bei ya kununulia iko chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu utaratibu wa rufaa. Hospitali za Mkoa tunaziwezesha nazo pamoja na ku-act kama Hospitali za Mkoa sasa hivi zitakuwa Hospitali za Rufaa na tutaziwezesha kupata Watalaam, *specialists* ili kupunguza mzigo kwenye hospitali kubwa kama Muhimbili, Bugando na *KCMC*.

Mheshimiwa Spika, nilisema nitaongea kwa kifupi sana, kwa hiyo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii angalau niweze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza wakati wa kuchangia Hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninafurahi kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia sana hotuba ya Rais kupitia Wizara ya Elimu, wametoa *challenges* nyingi sana ambazo ni changamoto na sisi kama Wizara tunakubali ushauri wao. Naomba kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya vitu vichache ambavyo angalau Waheshimiwa Wabunge wangependa kuvifahamu.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, tunakubali kabisa kwamba kiwango cha elimu hasa ukizingatia matokeo ya Kidato cha Nne kwa kweli kimeshuka. Matokeo ya Kidato cha Nne kwa mwaka 2010 ambayo yametangazwa mwezi Januari 2011 yanadhihirisha kabisa kwamba kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kimeshuka kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kuanzia mwaka 2006-2010 ilikuwa imejikita katika kupanua Elimu hii ya Sekondari na hasa kikitambua kwamba, hapo mara ya kwanza kulikuwa na Mpango wa Elimu uliokuwa unaitwa MEM.

Baada ya MEM kulikuwa na mrundikano mkubwa sana wa Vijana wanaohitaji kuingia Sekondari, kwa hiyo, Serikali ilichofanya ni kuanza sasa kujenga Shule za Sekondari ngazi ya Kata ambazo tulianza kujenga kwa awamu kwa kupitia Mpango wa MMES I.

Kila Kata sasa ina Shule za Sekondari japo baadhi ya Kata bado Mpango huo hawajakamilisha, lakini nadhani huwa tunafuata vigezo kwamba angalau shule za Msingi zikiwa zaidi ya Nne basi Kata inaweza ikapata Sekondari. Kuna baadhi ya Kata unakuta kuna shule ya Msingi moja kwa kweli inakua ni ngumu sana kuweza kujenga shule ya Sekondari. Kwa hiyo, awamu hiyo ilikuwa ni ya kupanua Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia wananchi wa Tanzania wawe na matumaini makubwa sana na Serikali yao hii ya CCM, kwa sababu tumejipanga sasa. Ilikuwa ni kupanua, sasa hivi itakuwa ni kuboresha kwani tumekwishajenga shule, madawati yapo na wananchi wanatusaidia.

Mheshimiwa Spika, labda kwa *introduction* niseme kwamba tunao ufadhili wa Wamarekani kupitia Chuo cha *South Carolina* ambao wametupatia vitabu milioni tatu (3,000,000) na tayari vitabu mia nane (800) vimekwishafika pale Wizarani na tunaomba Waheshimiwa Wabunge msisitize kwenye Wilaya zenu na Mikoa waje kuchukua vile vitabu hasa Mikoa kama Saba ambayo bado haijachukua. Mkoa wa Lindi, Mtwara, Tanga, Dodoma na Singida. Hawa hawajafika kuchukua vile vitabu na bado viko pale stoo Wizarani. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa mikoa hiyo wawasisitize Maafisa Elimu waje wachukue vitabu. Mikoa mingine angalau vitabu vimekwishaanza kusambaa.

Mheshimiwa Spika, bado kuna vitabu milioni 2.2 nadhani mpaka ifikapo mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumekwishapata vitabu na hivyo tutasambaza mashuleni. Tuna uhakika kabisa kwamba nia yetu ni angalau katika Mpango huu wa MMES II tupate kila *ratio* ya kila mwanafunzi mmoja kitabu kimoja. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba sasa hivi lengo kubwa hata katika bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo mtakayoiona mwezi wa Sita nia ni kuboresha.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunajenga, sasa ni kuboresha na hata msishangae matokeo haya yaliyotoka ni mabaya, ni kweli kwa sababu tusingeweza kufanya mambo yote kwa wakati mmoja. Hata unapojenga nyumba huwezi kuanza kujenga msingi, tofali, sementi hapo hapo, bati, ukanunua vitanda, magodoro, kila kitu ukafanya kwa wakati mmoja. Unakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa hii miaka mitano ya kwanza ya Awamu ya Kwanza ya MMES tulikuwa tunapanua. Naomba Watanzania wote wajue kwamba Awamu ya Pili ya MMES, sasa ni kuboresha, tunaboresha kwa namna gani? Nimekwishasema tayari Mkakati wa Vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije katika mkakati wa Maabara. Vile vile tumepata ufadhili, tutapata Maabara kwa kila shule, tutajengewa maabara kwa ufadhili ambao tumekwishaandika maandiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wakichangia sana hapa kuhusu upungufu wa Walimu. Nataka kuwahakikishia wenzangu

kwamba Serikali ya Awamu hii ya Nne imejipanga kweli kweli kukabiliana na uhaba wa walimu. Tayari tumepandisha hadhi Chuo cha Mkwawa kimekuwa Chuo Kikuu kwa ajili ya kutoa *Faculty of Education*, tayari Chuo cha Chang'ombe - *DUCE* kinatoa programu ya *education* na hapa vijana wetu wa *UDOM* nao tayari tumeweka *College of Education*. Kwa hiyo, tuna uhakika baada ya miaka miwili au mitatu, tatizo la Walimu litakwisha kabisa hapa Tanzania. Tuna uhakika watoto watapata Walimu, watapata vitabu ambavyo tayari nimesema na Maabara zitajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na changamoto nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge walizielezea. Niseme nimezichukua kama ushauri kwa sababu elimu ni pana sana. Unaposema Wizara ya Elimu unagusa hadi Vijijini, ni Wizara pana sana lakini kuna changamoto nyingi hasa, kwa mfano, Watoto wa Vyuo Vikuu nadhani miezi miwili au mitatu mmeona ninyi wenyewe matatizo ya migomo. Wanadai maslahi, wanasema maslahi ni kidogo lakini nadhani kama tulivyosema kwamba, tayari Mheshimiwa Rais amekwishaunda Tume inakwenda kuchunguza matatizo ya Bodi ya Mikopo, tufanye nini angalau tuweze kuboresha zile *procedures* ili watoto waweze kupatiwa fedha zao kwa wakati na fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea suala la michango mashuleni. Suala hili napenda kulitolea ufafanuzi kama ifuatavyo;-

Nadhani ilikuwa ni jana wakati najibu swali la nyongeza lakini hapa nataka tu kusisitiza kwamba, michango mashuleni wenzetu kule TAMISEMI tunashirikiana nao vizuri sana kuhakikisha suala hili tunaliweka sawa.

Mheshimiwa Spika, upo Waraka kutoka kwa Kamishna wetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, unaoelekeza kabisa kwamba Kamati za Shule ndizo zenye mamlaka ya kukaa, wanawakilisha Wazazi, wanapanga mipango yao kama sijui ni kulipa mlinzi au kujenga uzio basi wakae wapange. Lakini, vile vile natoa mwito kwamba ni vizuri wakashirikiana na wazazi kwa kuwapa taarifa, wazazi wapate taarifa kuhusu ile michango ambayo imechangwa na Akaunti Rasmi ifunguliwe ili kuwa na ukaguzi maalum. Nataka kusema kwamba mimi bado ni kijana nitatembea Tanzania nzima katika kila Wilaya kuhakikisha kwamba, haya yanafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakapokuwa napita huko Wilayani kuangalia masuala ya elimu, nitaangalia vilevile hata huu Mpango wa MMES II, kama kweli fedha zinatumiwa vizuri kwa sababu wapo Watendaji wetu wengine kwenye Wizara ya TAMISEMI au Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, hizi fedha sijui nitumie jina gani, kuchakachua au vipi, ni vizuri nitoe wito mmoja kwamba kama tutapita huko tukaona, unakuta unatembelea shule unashika tofali kwa kidole, unakuta linapukutika, hii si haki kabisa, tunapata msaada, tutumie vizuri. Hebu kila mtu aangalie kwamba anatembea na Mungu anamwona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwatangazie ma-*DEO*, hata Wakurugenzi huko Wilayani kwamba, nitapita kuhakikisha kuwa, fedha hizi tulizopata kama msaada

zinatumika vizuri ili tuweze kupata tija na Watanzania waweze kutuelewa, maana yake misaada tunapata lakini namna inavyotumika kidogo inakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa kwamba, hata Wazazi zile Kamati za Shule tutapita kuzikagua. Watu wafungue Akaunti, Wazazi waambiwe angalau kwa mwezi mara moja kuwe na ripoti inayosema kwamba, tulichangisha watoto kadhaa, shilingi kadhaa tukaweka benki na matumizi ni haya. Wazazi wakiishaona hiyo hawana tatizo juu ya kuchangia elimu. Nina hakika Wazazi wa Tanzania wanataka wachangie elimu lakini pale wanapoona matumizi ya michango yao hayaeleweki inakuwa ni ngumu sana. Hilo pia ni hata katika Bodi za Shule kwenye michango ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, vile vile Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusu biashara mashuleni. Hii vile vile nataka niseme kwamba kuna Mwongozo kabisa kwamba biashara mashuleni hazitakiwi. Tunaomba Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na hata Bodi za Shule, na hata nyie Waheshimiwa Wabunge, mnapopita katazeni biashara kwenye shule za Msingi na Sekondari. Naomba Mheshimiwa Mbunge yeyote atakayeona kuna tatizo hilo, anipigie hata mimi simu ili tuweze kuwawajibisha wale ambao sisi tunayaongea haya lakini mambo hayawezi kutekelezeka huko Wilayani au Mikoani.

Mheshimiwa Spika, labda nirudie kwa kusema kwamba suala la Bodi ya Mikopo, ni kubwa na ni suala nyeti ambalo sasa linafika mahali wanafunzi kama mlivyoona miezi miwili, mitatu wanagoma. Nataka niwatangazie wanafunzi kwamba kwa kipindi hiki cha miezi miwili ambayo Rais amekwishaunda Tume na imeanza kufanyakazi jana tarehe 14 Februari, 2011, Watulie miezi hii miwili wavumulie ili Tume ile iweze kuangalia ni wapi pana tatizo, kama ni upande wa *Tanzania Commission of Universities (TCU)* ambayo nayo imeanza kazi mwaka jana ina-*experience* ya mwaka mmoja na kwa hiyo ni lazima haya mengine yangeweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wanafunzi watulie, miezi hii miwili Tume hii itafanya kazi na italeta majibu, kwa sababu ndani ya Bunge kuna Kamati ya Huduma za Jamii.

Namshukuru sana Mwenyekiti wangu ni Mama Margareth Sitta, alishawahi kuwa Waziri wa Elimu, ni mzoefu na haya tutashirikiana vizuri sana kuleta ripoti humu, tuje tuone mapendekezo ya Tume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuungana na wenzangu waliotangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutuvusha wote tukaingia katika Bunge lako hili Tukufu.

Pili, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kabisa kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini walioweza kwa umoja wao kunipa nafasi hii nikaweza kuwa Mbunge bila kupingwa. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, sina budi pia kukishukuru kwa dhati Chama cha CCM na Mwenyekiti wetu, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliyenipa nafasi baada ya kutoka Umoja wa Mataifa nikajikuta kwamba nimetoka *UN-Habitat* sasa niko *Tan-Habitat*, hilo nalo nashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongeze kwa kukupongeza na nina salamu zako rasmi kutoka kwa wasichana wote waliosoma *Marian College (Kilakara Secondary School)* wameniagiza hili nilitamke Bungeni kwamba, wanakupongeza sana kwa kutengeneza historia kwa kuibuka kuwa Mwanamke wa kwanza kuwa Spika, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa katika kujadili Hotuba ya Rais, hoja hii naomba niseme kwamba inaonesha kuna mambo mengi ambayo Serikali ya CCM imeyafanikisha, lakini hapo hapo kwamba kuna changamoto ambazo inabidi tuzikabili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu naomba kwa ridhaa yako nijikite zaidi katika changamoto za sekta yangu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika Ilani ya CCM ukiangalia *paragraph* ya 50 na kuendelea unaona kwamba, hii ni sekta mtambuka (*cross-cutting sector*). Inawezesha sekta nyingine kufanya kazi zake, kwa hiyo, inafafanuliwa kama Sekta ya Uchumi na Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitufundisha kwamba, ili nchi iendeleo kuna vitu vinne hapo vya msingi. Alizungumzia Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi bora. Angalia sasa umuhimu wa ardhi, tusipoweza kuiendeleza ardhi yetu, kuitunza, hatuwezi kwenda mbali.

Lakini naona kazi yangu na kazi yetu imeanza vizuri na nataka niwapongeze kabisa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa sababu Sekta hizi kwa kweli zimeshikamana na zimefungamana.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni zipi na tumejiandaa vipi kuzikabili? Kitu cha kwanza nimesikiliza kwa makini hotuba na mawazo na maoni ambayo ninyi Waheshimiwa Wabunge mmeongezea katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kero ziko nyingi na nitakuwa sio mkweli nikisema kwamba kero hazipo, ila *the good news is* tunazifanyia kazi na msiwe na wasiwasi. Wizara yangu imekwishajipanga kwa umakini kabisa kuhakikisha kwamba, kero hizi zinaondolewa, lakini ili tufanikishe nitaomba na nyie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla mtusaidie katika hili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ardhi ni sekta ambayo haiendeshwi kwa sera tu, inaendeshwa pia kwa Sheria. Naweza kusema kwamba, kama vile ambavyo Bunge lako linakwenda kwa Kanuni na Sekta ya Ardhi inakwenda kwa Sheria.

Kwa mfano, tuna Sheria ya Upangaji Miji, huwezi kupanga miji bila kuangalia Sheria hii. Hii ni Sheria Na. 8 ya mwaka 2007. Tuna Sheria ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Tuna Sheria Na. 4 ambayo ni Ardhi iliyobaki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kusudi tuondokane na migogoro hii, inabidi wote kwa umoja wetu bila kujali itikadi, tuwe tunazielewa Sheria hizi. Nimekuja kuona kwamba matatizo mengi yanatokana na ukiukwaji wa Sheria wakati mwingine na watendaji lakini wakati mwingine na viongozi na wakati mwingine na wananchi kwa sababu sheria hizi bado hazijafahamika vizuri. Sasa Wizara yangu imejipanga, katika Bunge linalokuja kila mmoja wenu atapatata *complete set* ya Sheria zote hizi kusudi mtusaidie na ninyi kuwaelimisha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima niseme kwamba kwa mujibu wa Sera ya *Decentralisation* tunafanya kazi kwa ukaribu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Watendaji wetu wa Ardhi wanafanya kazi chini ya TAMISEMI. Ni kweli kwamba kwa sababu ya *nature* ya sekta hii na kwa sababu inaendeshwa kwa Sheria, wengi wao labda kwa sababu wanakuwa mbali na Wizara Mama, hawakuweza kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Nataka kuwahakikishieni kwamba hilo tumeshalitambua na kwa kufanya kazi na TAMISEMI na Utumishi, natoa ilani kwa Watendaji wetu wa Ardhi kwamba sasa kama mlikuwa kwenye *holiday*, imekwisha. Karibu tutawafikieni bora, kufuata Sheria na maadili ya fani ya upimaji na upangaji miji.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka kabisa ngoja pia niwaeleze wananchi kupanga miji maana yake nini? Kupanga miji ni kitu kigumu sana, kinahitaji nidhamu, mtazamo chanya na kinahitaji kubadilisha utamaduni wetu kwa sababu unapopanga mji unapanga kwa vizazi vijavyo. Unapangua vilivyopo kwa maslahi na mustakabali wa vizazi vijavyo. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kinataka kujitua, kinataka nidhamu na kinataka kuangalia Sheria. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wanaofuatilia mjadala huu napenda kusema kwamba suala hili litahitaji tubadilishe mawazo/mtizamo.

Mheshimiwa Spika, migogoro ambayo tunayo, nataka tu kutoa habari njema kwamba nimeweka kipaumbele katika kuboresha Mabaraza ya Ardhi popote pale yalipo. Hivi sasa Mabaraza ya Ardhi tunayo 39 bado hayajaenea katika Wilaya zetu zote. Natambua kabisa kwamba kukosekana kwa Mabaraza haya imekuwa ni usumbufu kwa wananchi. Kwa hiyo, Serikali iko katika mbio za kujaribu kurekebisha suala hili ili bila ya kuchelewa sana tuweze kuanzisha Mabaraza ya Ardhi au tutaweka namna wananchi wanavyoweza kusikilizwa shida zao katika Wilaya zao wenyewe bila kulazimika kwenda kwenye Mikoa ambapo sasa hivi Mabaraza yapo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nyeti ambalo ningependa niligusie kidogo, Wizara yangu iko mbioni kujadiliana na Serikali kuangalia namna ya kuhakikisha wawekezaji hasa wageni ambao wanakuja kwa manufaa ya kwao yatunufaishe na sisi wenyewe wananchi, nataka kuwaondoeni wasiwasi kwamba Serikali ya CCM, Wizara

yangu kwa makusudi kabisa inaweka sera na taratibu ambazo zitahakikisha kwamba haki za wananchi katika suala la ardhi zinalindwa.

Mheshimiwa Spika, sina budi mimi mwenyewe kama mwanamama hapa kusema kwamba kwa kweli haki za ardhi za akinamama na za vijana bado kuna upungufu. Wizara yangu inatambua hili na iko mbioni kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa inapokuja kwenye ardhi ya Tanzania, tuna takribani kama hekta 94,000,000. Kati yake hekta 88,000,000 ni nchi kavu, nyingine ni maji. Tunatambua kabisa matatizo ya wakazi wa Visiwa hususan vya Lake Victoria. Nataka niungane na Wabunge wenzangu waliozungumza katika Bunge hili Tukufu kwamba kuna haja sasa hivi ya kuboresha usalama katika Ziwa Victoria na ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia huwa inashughulika na tunasimamia pia mipaka. Tumepata matatizo wakati mwingine migogoro inazuka kati ya Wilaya moja na nyingine, kijiji kimoja na kingine. Matatizo kati ya wafugaji na wakulima mnafahamu kwamba kwa kweli yako katika sehemu mbalimbali. Tume ya Migogoro ya Ardhi ambayo iko chini ya Wizara yangu, sasa hivi iko tayari kuwasaidieni kwa sababu tumefanikiwa kukamilisha upimaji wa vijiji vyote Tanzania. Tanzania ina vijiji 12,000 na kati ya hivyo vijiji 11,000 vimeshapimwa, tutakapokutana katika Bunge linalokuja, walio wengi watakuwa wameshapata hati zao. Nataka nitoe Ilani kwa Wenyeviti wa Vijiji kwa sababu Wenyeviti wa Vijiji ndio *custodians* yaani ndio wamekabidhiwa jukumu la kulinda ardhi za kijiji.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kulinda haki za wananchi, katika suala hili, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani popote pale mlipo kwamba na ninyi mshiriki katika vikao husika hasa vinavyogawa ardhi kwa wawekezaji. Nadhani haina tija yoyote kwa Diwani au Mbunge kutokuwa kwenye vikao vinavyogawa ardhi na kuja kuibuka baadaye wakati mgogoro umeshazuka. Kwa hiyo, taratibu hizi zitarekebishwa na tunaamini kabisa Wabunge na Madiwani mtatusaidia katika hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nataka pia nijikite sasa katika ujenzi holela na ukuaji holela wa miji yetu, hili ni tatizo kubwa sana. Tanzania ina takriban wananchi 40,000,000 wengine wanasema 45,000,000. Kwa takwimu za Umoja wa Mataifa, Shirika la Makazi nililokuwa naliongoza, linahesabu kwamba asilimia 37 ya Watanzania tayari wameshaingia mijini kwa sababu tunahesabu miji sio tu Dar es Salaam na Mwanza lakini hata miji midogo inahesabiwa kama *urban areas*. Katika hali hiyo, asilimia 70 ya wakazi wa mijini katika nchi hii wanaishi katika vitongoji ambavyo havijapimwa. Ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, Wizara yangu imeweka mkakati wa upimaji miji kwa namna ya *master plans* kusudi tuweze kupima viwanja na kuwa na *Strategic City Plans* ambazo zinaangalia mkakati wa miaka mingi. Kama nilivyosema hapo awali, unapopanga mji hupangi kwa kesho au kesho kutwa, unapanga kwa miaka 25 au 50 ijayo.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi holela mijini pia linahitaji nidhamu kwa upande wa wananchi ambao wanajikuta katika vitongoji ambavyo vimeota vyenye, tunasema itabidi watuunge mkono tunaporekebisha. Lakini hapo hapo lazima nikemee

kwa mara nyingine tena ndani ya Bunge lako Tukufu wale ambao wanatumia aidha uwezo wao au nyadhifa zao kutwaa maeneo ambayo yametengwa kwa matumizi ya umma. Nawatahadharisheni, tujirudi kwa sababu haina tija yoyote. Hakuna eneo la wazi, wanasema maeneo ya wazi kimsingi ni maeneo ambayo yametengwa kwa matumizi ya umma. Hili likieleweka, ukajua kwamba unapojenga wewe nyumba yako binafsi unaunyima umma mzima wa Tanzania haki ya kutumia sehemu hiyo. Kusema kweli mtaniwia radhi lakini sitawavumilia, itabidi Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kuepokana na kupoteza fedha zenu, watu wanawekeza tena wakati mwingine kwa gharama kubwa sana katika eneo ambalo wanajua hatimaye Sheria hizi ambazo nimewaonyesheni zitakapoanza kufanya kazi basi itabidi aidha watu wabomolewe au itabidi watu wapoteze nyumba ambazo wamejenga mahali ambapo hapastahili. Nadhani tungeshirikiana kuepokana na tatizo hili. Cha kufanya kwa sasa hivi ni Watanzania wote kwa ujumla kupata elimu ya msingi. Kama mtu anataka kukumegea kiwanja, kuwa na wasiwasi naye, hata kama ni Afisa Ardhi, usimsikilize, kusema ukweli anaweza kuwa tu anakulaghai kwa sababu anajua anakupa kiwanja ambacho hatimaye utaingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hiyo ndiyo Ilani yangu, nasisitiza kwamba sekta ya ardhi ni sekta mtambuka, ni sekta ambayo inataka nidhamu na kubadilisha utamaduni na maono yetu kusudi tuwe na miji endelevu. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu, napenda kwa heshima na taadhima, niwashukuru sana wananchi wa Mwanga kwa kunipa ridhaa yao na kunichagua kwa kura nyingi kabisa, zaidi ya asilimia 80 kuwakilisha katika Bunge lako Tukufu. Napenda pia niwashukuru wananchi wa Mwanga kwa kuichagua CCM kwa kiwango kikubwa sana, kwa kumchagua na kumpitisha mgombea wa CCM kwa ngazi ya Urais kwa zaidi ya kura asilimia 80 na kuchagua Madiwani wote 27 kutoka Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia katika Wizara ya Kilimo na wameeleza changamoto mbalimbali ambazo zinatusibu katika kilimo chetu na mimi nitajaribu kwa muda huu niliopewa, kuelezea mipango yetu ambayo tumeipanga kuichukua katika kipindi hiki cha miaka mitano inayokuja na wale ambao hatutaweza kuwajibu kwa sababu muda wenyewe ni mfupi, tutawaletea majibu ya hoja zao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wote wakitoka kwenda kufanya kazi wanakwenda kwenye kilimo. Kwa hiyo, kilimo ndio kila kitu kwa Mtanzania. Napenda nielezee maeneo machache, moja ya hayo, ni changamoto za kuwa na mbegu bora. Kilimo kinategemea mbegu bora na kama Taifa mahitaji yetu ya mbegu



bora ni zaidi ya tani 120,000 lakini mbegu ambazo zinaingia kwenye soko hivi sasa sio zaidi ya tani 30,000. Katika hizo tani 30,000 ni tani chini ya 10,000 ndio zinazalishwa hapa nchini zilizobaki zote zinaletwa kutoka nje ya nchi. Kama mnavyojua mbegu bora ni lazima izalishwe katika *Agro-ecological zone* ambapo itakuzwa ili kuwa zao bora. Lengo letu ni kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kufikia zaidi ya tani 60,000 katika kipindi cha miaka mitatu na baadaye katika kipindi cha miaka mitano tuweze kukaribia kujitosheleza kwa mbegu.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza iliyochukuliwa ni kuunda Wakala wa Mbegu wa Tanzania na kwa sababu Wakala huyu bado ni mchanga sana, tumedhamiria kutumia Makampuni ya Kitanzania na tumeshaandikisha Makampuni ya Kitanzania zaidi ya 46 na tumewakaribisha katika Mkutano ili tukae nao, tupange tunaendaje katika azma yetu ya kuzalisha zaidi ya nusu ya mbegu ambazo tunahitaji kuzizalisha sisi wenyewe hapa nchini katika vituo vyetu vya utafiti ambavyo vimetawanywa katika Kanda zetu za kilimo. Wanasayansi wetu, *Plant Breeders*, wamezalisha mbegu bora nyingi sana. Katika mwaka huu, tumedhamiria kuwatunuku Wanasayansi wote ambao wamezalisha mbegu mpya kwa kuwapa zawadi ya kutambua mchango wao katika maendeleo ya kilimo. Huyu Wakala wa Kilimo tumekubaliana kwamba ashirikiane na Makampuni ya Kitanzania ili kuzalisha mbegu mama na mbegu hizi sasa Wakala wa Mbegu wa Taifa azigawanye kwa wazalisha mbegu ili tuweze kuzalisha mbegu za kutosha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeongelewa kwa undani sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni kuongeza zana bora za kilimo katika kilimo chetu. Ili kuongeza maeneo tunayoyalima, kutengeneza mashamba vizuri na kuweka mazingira mazuri ya kukuza mimea, ni muhimu sana kuongeza na kutumia zana bora za kilimo. Hivi sasa tunayo matrekta makubwa zaidi ya 8,500 ambayo yanafanya kazi na matrekta madogo yapo karibu 3,000. Lakini tunazo zana za wanyamakazi zaidi ya 585,000 na maksai zaidi ya 1,300,000. Mkakati wetu ni kuongeza wingi katika kila *category* ya zana bora.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba chini ya mkopo nafuu wa dola za Kimarekani 40,000,000/=, Serikali inaagiza matrekta mapya makubwa 1,860 ambayo yataingia nchini, kati ya hayo, matrekta 600 yataingia yakiwa yameshaunganishwa kwa maana ni matrekta kamili na matrekta 1,260 yataunganishwa hapa nchini na Shirika letu la Nyumbu pale Kibaha. Aidha, ninayo furaha kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba katika ushirikiano huu, Serikali ya India imeiongezea Tanzania shilingi 92,000,000/= ili kuongeza wingi wa matrekta ambayo yataunganishwa au kwa maana ya kutengenezwa hapa nchini. Matrekta haya yatakuwa ya bei nafuu na kwa hiyo nawahimiza Waheshimiwa Wabunge waone umuhimu wa kuyanunua na kushiriki katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa kwa undani sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni eneo la umwagiliaji. Nchi yetu inayo uwezo wa kuweka zaidi ya hekta 29.4 milioni chini ya umwagiliaji. Aidha, hivi sasa ni hekta 331,490 peke yake ndiyo zipo chini ya umwagiliaji. Lengo la Serikali ni kufikia hekta 1,000,000 katika miaka mitano inayokuja. Kwa sababu hiyo na chini ya *District*

*Irrigation Development Programme (DADP's)* na katika Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji, kila mwaka Serikali imedhamiria kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji ili kuweka hekta 30,000 chini ya umwagiliaji. Aidha, katika mazungumzo yetu na washirika wetu wa maendeleo, nikiwataja Korea, Japan, Marekani na Benki ya Dunia, wote wamekubali kushiriki katika mipango yetu ya kupanua maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na hasa kwa uzalishaji wa mpunga. Michango hii pamoja na kuwahamasisha wakulima binafsi au sekta binafsi kushiriki katika kilimo, tunatarajia kwamba katika miaka mitano, tutaweza kufikia kiwango tulicholenga cha hekta 100,000,000 katika kipindi hiki cha miaka mitano iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia juu ya changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mbolea na pembejeo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ulishukuru watu wa Mwanga na nani, ndiyo muda uliishia hapo.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, ni dakika kumi tu. Kwa hiyo, salamu na nini, muda hautatosha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa lakini sio rushwa. Pili, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kutoka Vyama vyote kwa kuchaguliwa na tatu niwashukuru sana wananchi wa Bunda kwa kunichagua.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo nataka kutilia mkazo ambayo yameandikwa katika Hotuba ya Rais ni yanayohusiana na suala la Umoja wa Taifa letu. Nchi zote duniani zikiwemo hata zile nchi kubwa sana kama Marekani, zina mambo ambayo hayana Vyama. Zina misingi ambayo imewekwa na Waasisi na haitakiwi kuvunjwa na mtu yeyote na wala haitakiwi kuingiliwa na Chama chochote kwa maana ya kuivunja. Ndiyo maana nchi kubwa kama Marekani inapotokea kuna mgogoro baina ya Marekani na nchi za nje, Wamarekani wote wanaungana dhidi ya nchi hiyo inayotaka kudhuru au kuhatarisha maisha ya Marekani. Kwa hiyo na sisi hapa Tanzania, yapo mambo ambayo tumeyarithi kutoka kwa Waasisi wetu. Tunayo habari ya umoja, tuna suala la uhuru, hakuna Chama wala mtu ambaye ana haki ya kuuza uhuru wetu, kwa gharama yoyote, tutazuia asiuze hata kama angelipata soko la namna gani.

Mheshimiwa Spika, suala la umoja wetu ndiyo suala la msingi ambalo limetufanya sisi tuwe tulivyo kwa muda wa miaka 50. Tumeishi kwa pamoja kwa sababu tulikataa ukabila, tulikataa udini na Chama cha *TANU* na *Afro-Shirazi* kilichoasisi Taifa letu, walituoonesha njia. Mwalimu Julius Nyerere, akiwa Mkristo, aliungana na Karume

akiwa Mwislamu kuunda Taifa moja. Hayo ni mambo ya msingi. Sisi ambao tupo katika Bunge hili, mbele yetu kuna Nembo ya Taifa imeandikwa Uhuru na Umoja. Ni misingi ambayo haiwezi kuchezewa na lazima tukatae. Wako watu wanazungumzia sana Katiba Mpya, nadhani ni vizuri siku moja katika Katiba tuseme Umoja, Uhuru na Amani, ni misingi ambayo itaingia kwenye Katiba na haiwezi kuchezewa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu tumeona mambo ya kuvunjavunja umoja kidogo. Labda kabla sijaendelea niseme, kwa sababu ya msingi wa miaka 50 ya Uhuru, Watanzania ni watu ambao wamezoea umoja na hata katika Uchaguzi Mkuu uliopita, wale waliojaribu kuvunja umoja, walipata matatizo sana. Wananchi wamepiga kura bila kuvunja umoja wao. Katika muda wa miezi miwili, mitatu ambayo nimefanya kazi katika Ofisi ya Rais, tumefanya utafiti. Katika kitabu hiki, Rais kuna mahali amesema kwamba nyufa zimeanza kuonekana hapa nchini lakini nyufa hizi hazikuwa rasmi kwamba kuna madhehebu au dhehebu rasmi ambalo linasema tunataka kuchagua mtu kwa sababu ya udini. Halikuwepo dhehebu la namna hilo lakini madhehebu haya yamesambaa nchi nzima. Kwa hiyo, kiongozi wetu mmoja wa kidini mahali fulani aliweza kufanya hivyo, wapo ambao wamefanya. Nataka niwaambie hata wale ambao walijaribu, walishindwa na waliposhindwa wamelionea sana jambo hili. Wako baadhi ya watu ambao nimezungumza nao na wao wanalionea haya.

Mheshimiwa Spika, juzi Jumapili nilikuwa na Viongozi wa Kidini kama sabini wa hapa Dodoma, nimezungumza nao juu ya jambo hili. Wote wanakiri kwamba wakijiweka katika tatizo hili, watakurugua amani ya Taifa letu na hii iko wazi. Msikiti unaendeshwa na Imam na Kanisa linaendeshwa na Mchungaji lakini wafuasi wa Imam ni wafuasi wa Vyama Vingi na wafuasi wa Kanisa wana Vyama vyao. Sasa ukimwambia twendeni tukampigie kura mtu wa dini yetu, watakuuliza, Baba Askofu au Imam mbona huyu unayemsema si wa Chama chetu. Umekwishazua mgogoro, unaanzia Kanisani/Msikitini unaenda mtaani maana wafuasi wa dini yako hiyo wataanza kugombana kwa sababu wanatofautiana itikadi zao za Vyama na utakuwa umesaidia kuvunja amani. Tumezungumza na Viongozi wetu wa Dini, wanaelewa sana jambo hili. Wametuahidi watashirikiana katika kuhakikisha uhuru na umoja unaimarika nchini. Ombi langu kwa viongozi wote na Bunge lako Tukufu, ni kwamba tuongoze katika kuhakikisha nchi yetu inakuwa moja na watu wetu wanakuwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Kidini wameniambia, ni ninyi wanasiasa ndiyo mnatufuatafuata mnapokuwa hamuwezi kuchaguliwa bila sisi. Wameniambia waziwazi, wamesema wanasiasa acheni kutufuatafuata, sisi tutawaombea mkishinda lakini hatuwezi kuwaombea mgombane wala hatuwezi kushirikisha dini katika masuala yanayohusu ugomvi wenu wa kutafuta madaraka kwa sababu mwisho wa yote ukiyapata madaraka utawaongoza watu wote, ukiwabagua, utawaongoza wapi? Hili ni jambo kubwa, jambo la Umoja wa Taifa letu, tusikubali hata kidogo mtu yeyote akachezee umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, tumesikia maneno na kauli, nadhani zilikuwa zinatoka kwa bahati mbaya maana ulimi nao hauna mfupa. Mtu anasema nchi hii haiwezi kutawalika, sasa tunasema isitawalike tena? Isitawalike ifanyeje sasa? Maana tunaulizana sisi wote, Watanzania hii ni nchi yetu wote, unakwenda, unachaguliwa, unashinda au huchaguliwi,

unarudi nyumbani, unapoa. Nimewaomba Viongozi wa Dini kwamba wakiona mtu amechachamaa sana kwa sababu hajazoea kushindwa, wamwite Kanisani au Msikitini wamwombee atulie. Maana sisi wote tutakufa lakini Tanzania haitakufa. Tanzania itaendelea kuwepo kwa sababu Tanzania si mali ya kizazi hiki peke yake. Ni mali ya vizazi vingi vinavyokuja. Juzi huko Serengeti wamegundua nyayo za miaka mamilioni iliyopita, za watu walioishi hapo. Wale wangechoma Tanzania tusingekuwepo sisi na sisi tutaweka Tanzania yenye amani, yenye umoja ambayo itarithiwa na vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tujiepushe kabisa na masuala yoyote ambayo yanawafanya wananchi waweze kugawanyika, waweze kugombana na kuvunja amani.

Mheshimiwa Spika, wako rafiki zangu wamezungumza, wanasema hapa hakuna amani kuna utulivu peke yake. Nasema potelea mbali kama amani haipo lakini utulivu upo si basi. Wacha tutulie basi. Sasa kwa nini tena unataka kuchukua hatua za kuvuruga hata huo utulivu mdogo uliopo badala ya kuchukua hatua za kuleta amani katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, wako waliosema, haiwezekani kuwepo na utulivu kama kuna njaa na mimi nakubali. Wenye njaa hawatulii lakini kazi yetu ni kuweka mipango itakayosaidia kuondoa njaa na kupunguza umaskini katika nchi yetu kwa sababu tukifanya hivyo ninahakika nchi yetu itaendelea kuwa moja kwa sababu sisi ni nchi ya mfano katika Afrika. Hivi nani asiyejua Afrika, wala huna haja ya kwenda Somalia, chukua nchi tunazopakana, zipo tisa ambayo imetulia na ambayo haijapata kuwa na migogoro mikubwa kama Tanzania nipe moja. Kwa nini tumetulia? Sisi si binadamu tofauti, ni Waafrika kabisa kama Wakenya, kama Waganda na ni Waafrika kama Waburundi tena tunapakana. Mimi natoka Mara, upande wa pili kuna Wakurya wa Kenya, upande wa huku kuna Wakurya ndiyo hawa akina *Attorney General*. Wakurya hawa ni walewale, Wamakonde ni walewale mpaka Baba wa Taifa siku moja alituuliza, “hivi ninyi mnasema Wazanzibar si wenzenu ninyi Wakurya na Wamakonde, mlionana wapi”? Ni walewale lakini tunaishi pamoja kwa sababu tumeweka misingi, tumekataa ukabila katika nchi yetu na kwa kweli tumeshinda na Mwasisi wa Taifa letu aliwahi kutuambia, tumeshinda ukabali lakini tuangalie sana juu ya udini huenda ukatusumbua siku zinazokuja na watu wanaouchochea ni watu wanaotafuta madaraka kwa sababu hakuna Sheikh hakuna Askofu anayetaka vita. Wote wanahubiri amani na mimi nimewaomba wafanye kazi yao hiyo ya kuhubiri amani na wakiona mtu anataka kuvunja amani, wamwombee ili atulie.

**MBUNGE FULANI:** Ashindwe kwa Jina la Yesu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**  
Sijasema, hayo umesema wewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa dhati kabisa kwa sababu tunaanza kuona dalili ambazo si nzuri sana. Leo watu wanasema nchi haitawaliki lakini haitawaliki halafu

wewe utajitawala namna gani? Maana isipotawalika na wewe unayetaka isitawalike una matatizo maana amani ikivurugika na wewe utakimbia na wewe utashughulikiwa kwa sababu isipotawalika maana yake kila mmoja anamwinda mwingine.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukubali kuendeleza misingi tuliyoachiwa na Waasisi wa nchi yetu. Wako kaburini, Mungu amewaweka kule lakini shughuli waliyofanya duniani, haitasahauliwa daima. Wangukuwa wachoyo wa fadhila, wangukuwa wadini, tusingefika hapa.

Mheshimiwa Spika, namkumbuka Mwalimu alipochukua nchi kwa sababu kulikuwa na tofauti sana za elimu, yeye alikuwa Mkristo, Mkatoliki na alichukuwa shule za Wakristo ili ziwaseshe watu wote, hakusema hizi za dini yetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kisa kilichotokea Magomeni wakati Mheshimiwa Mwinyi akiwa Rais, watu wanagombana pale kwa sababu ya bucha za nguruwe. Rais akawaambia Katiba yetu inasema nchi hii haina dini, mwenye kula nguruwe na ale anayeikwepa apite mbali. Viongozi wetu wamefuata mfano huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema na narudia, lazima nchi yetu itawalike lakini penye matatizo tukae chini tuongee, tumalize matatizo kwa njia ya amani, si maandamo ya asubuhi.

Mheshimiwa Spika, rafiki zangu na watani zangu, mimi nataka niwaambie la mwisho tu maana Upinzani sio ninyi mmeanza, hata mimi niliwahi kupinga. Sio vibaya kuwashauri, yule Selasini anajua tulikuwa wote na kaka yake lakini sifa ya Upinzani ni hoja na hii ya mkitaka kuamua mnatoka, wananchi watawazoea tena watakuja kushangaa mbona tena hawatoki maana wanadhani shughuli yenu ninyi ni kutoka tu na wale wanaowasikitikia nao wanapata matatizo bure maana wananchi wanasema hawajatoka tena? Watazoea halafu wataona kumbe ninyi hamna kazi ni kutoka tu lakini kama ni kutoka hata mimi baada ya hapa nitatoka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wanasema uzee dawa. Sasa nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye ahitamishe hoja hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niungane tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba nzuri sana aliyoitoa wakati akizindua Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Novemba 2010. Sina shaka kuwa majadiliano ya hotuba hiyo hapa Bungeni yamedhihirisha umakini uliotumika katika utayarishaji na uwasilishwaji wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa namna ambavyo mmesimamia kwa makini mjadala wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia, kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala wa hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais, kwa michango yao mizuri na ambayo imeisaidia Serikali kupima hatua ilizofikia katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 - 2010 na mikakati mingine yote ya kuiletea nchi yetu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 176 wakiwemo Mawaziri wangu wachache wamechangia mjadala huu. Kati ya hao, 116 wamechangia kwa mazungumzo na 60 kwa maandishi. Mjadala huu umetusaidia kwa kiasi kikubwa kujua maeneo tuliyofanya vizuri na yale ambayo hatukufanya vizuri. Ukweli ni kwamba, mjadala umeisaidia na kuirahisishia Serikali kazi yake ya kutekeleza Ilani hiyo ya mwaka 2005 – 2010, 2010 – 2015. Kwenu ninyi wote nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha hoja hii, si nia yangu hata kidogo kujaribu kujadili hoja au kujibu hoja moja moja, sitafanya hivyo. Badala yake nataka tu nijaribu kuchangia katika maeneo machache kwa ujumla kwa lengo la kuonyesha tu kwamba yako maeneo ambayo kama viongozi ni vema tukayatambua na kuyawekea uzito mzito.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, mwaka 2010, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ilifanyiwa Marekebisho ya Kumi, kwa lengo la kutekeleza Azimio la Baraza la Wawakilishi lililotolewa mwezi Januari mwaka 2010 kuhusiana na Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Aidha, chini ya Marekebisho hayo ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, yapo marekebisho mengine ambayo yalipendekezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yaliyolenga kukidhi hali halisi ya mabadiliko yaliyotokea Zanzibar tangu kupitishwa kwa Marekebisho ya Tisa ya Katiba ya Zanzibar, mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, wapo baadhi ya Wabunge ambao walichangia hoja hii. Tunaweza tukasema Wabunge hao wamegawanyika katika makundi makubwa mawili. Wapo Wabunge ambao hawaoni tatizo la kufanyika Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kwa kuona kuwa Marekebisho hayo yanakidhi mustakabali wa Zanzibar, hasa marekebisho yaliyounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kundi hili kimsingi pia hawaoni tishio la Muungano na wanaunga mkono Muungano uendelee kwa manufaa ya watu wote. *(Makofi)*

Aidha, wapo Wabunge wanaoona kuwa, Marekebisho haya ya Katiba ya Zanzibar yaliyofanywa katika mazingira haya, yamekwenda mbali na hivyo kutoa picha kwamba Muungano sasa unatetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasikiliza wote, naungana na wale wanaosema kuwa Muungano huu upo pamoja na Marekebisho ya Katiba kwa mustakabali wa Nchi ya Zanzibar na Watu wake. Bado Muungano wetu ni imara na utaendelea kuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuingia kwa undani sana katika kutazama Marekebisho haya, Ibara moja baada ya nyingine, inatosha tu kusema kuwa, Marekebisho hayo ni mazuri na yameboresha sana Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Vilevile mabadiliko hayo yameleta matumaini mapya kwa wananchi wa Zanzibar, jambo ambalo ni la msingi sana katika maendeleo ya nchi yoyote. Marekebisho hayo ya Katiba pia yamesaidia kuamsha hisia sahihi kabisa za umoja, mshikamano, upendo, kuvumiliana na katika kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, tunaweza kuyaweka katika makundi manne yafuatayo:-

Kundi la kwanza, ni masahihisho madogo madogo ya maneno na nafasi za madaraka ili kuendana na mfumo mpya wa sasa wa uongozi unaotokana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Chini ya kundi hili, mpangilio mzima wa madaraka ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa umewekwa. Vilevile, kumekuwepo na marekebisho ya kuondoa baadhi ya nyadhifa za awali, kama vile, Wadhifa wa Waziri Kiongozi na kuwekwa Wadhifa mpya wa Makamu wa Pili wa Rais ambaye kimsingi kwa kiasi kikubwa ndiye aliyechukua majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, katika Kundi la pili, Katiba imeweka Ibara mpya ambazo zinatambua uanzishwaji wa mifumo mipya ambayo kabla ya Marekebisho hayo ya Katiba hazikuwepo. Kwa mfano, baada ya Marekebisho hayo, Katiba ya Zanzibar inatambua kuwepo kwa Tume ya Pamoja ya Fedha kama moja ya Chombo cha Muungano kama ilivyotambuliwa chini ya Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine muhimu zilizotambuliwa chini ya Marekebisho hayo, ni Tume ya Utumishi wa Mahakama na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Kwa mujibu wa Marekebisho hayo, Kamisheni ya Utumishi wa Umma, itakuwa ndicho Chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi chenye Mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar. Vilevile, marekebisho haya yameanzisha Tume ya Utumishi Serikalini. Maeneo yote haya, hayana sura yoyote inayoonesha kwamba inapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni Katiba kufanyiwa mabadiliko kwa kuwekewa Ibara ambazo baadhi ya Wabunge wamesema kuwa haziwiani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo haya ni pamoja na haya yafuatayo:-

1. Kueleza kuwa Zanzibar ni Nchi;
2. Kuwekwa kwa Mamlaka ya Rais wa Zanzibar kugawa maeneo ya Kiutawala (Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo) badala ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyokuwa awali walivyokuwa wakishauriana;

3. Suala la ukomo wa Mamlaka ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika kusikiliza baadhi ya Mashauri Tanzania Visiwani; na

4. Rais wa Zanzibar kutambulika kuwa ndiye Mkuu wa Nchi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kundi la nne, ni Katiba hii kuwa na vipengele vinavyoendelea kuiweka Zanzibar kuwa Sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo haya ni pamoja na Ibara ya 2, inayoelekeza kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuwa, pamoja na Marekebisho yaliyofanywa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Marekebisho yote yaliyofanywa, kwa maoni yangu, yana utashi wa kuimarisha Muungano wetu. Hili linadhihirishwa na Ibara ya 2 ya Katiba hiyo kama nilivyoitaja hapo juu ambapo Zanzibar inajitambulisha kuwa iko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, endapo kuna sehemu yoyote chini ya Katiba hii, inayoonekana kuwa na mgongano na masharti yaliyopo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuwa, wakati utakapowadia wa kupitia Katiba yetu kwa lengo la kuwa na Katiba Mpya kama Serikali ilivyoelekeza, migongano yoyote inayojitokeza, itaangaliwa wakati huo kwa lengo la kuwianisha Katiba zetu hizi mbili ili kuendelea kudumisha, kuimarisha na kukuza Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba na kuwasihi Watanzania wote kuwa, tunapofanya majadiliano ya Marekebisho ya Kumi yaliyofanywa kwenye Katiba ya Zanzibar, majadiliano hayo yajikite kwenye kuimarisha, kukuza na kuendeleza Muungano. Vivyo hivyo wakati wa majadala wa kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dhamira yetu iwe ni hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba, Muungano wetu umeijengea nchi yetu sifa kubwa, ni Muungano wa mfano, wa aina yake na wa kuigwa katika Bara la Afrika na dunia kwa ujumla. Ni Muungano wa aina yake unaozingatia mazingira halisi ya eneo letu la Tanzania, kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Si kwamba hakuna matatizo katika kukuza Muungano, lakini ni lazima kuendeleza dhamira ya kweli katika kuimarisha Muungano wetu wa Nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati wa uhai wake na katika kipindi ambapo Muungano unazaliwa, aliwaasa Watanzania mambo mengi kuhusu Muungano huu. Mwalimu aliwaeleza Watanzania kuhusu Muungano uliokuwa unapendekezwa kuanzishwa, kuwa ni Muungano ambao hauna budi kuzingatia hali halisi ya nchi zinazoungana. Mwalimu kupitia Hotuba yake ya tarehe 25 Aprili 1964, alisema maneno ambayo kwa maoni yangu, bado yana umuhimu mkubwa sana kwenye kuuendeleza na kuukua Muungano wetu. Maneno hayo aliyasema kwa Kiingereza, lakini mimi naomba nitoe tafsiri isiyokuwa rasmi ili Watanzania wengi



zaidi waweze kujua Mwalimu alisema nini. Mwalimu kwa kifupi, alisema kwa tafsiri isiyo rasmi kama ifuatavyo:-

*“Tanganyika na Zanzibar ni majirani kwa kila hali. Kila mmoja wenu anajua ni kwa kiasi gani tuko karibu kijiografia. Naamini kwamba umbali kati ya Kisiwa cha Unguja na Kisiwa cha Pemba ni mrefu zaidi kuliko umbali kati ya Visiwa hivi na upande wa Bara wa Nchi za Afrika Mashariki. Vilevile Historia inatukumbusha kuwa wakati fulani eneo lote la Zanzibar na sehemu kubwa ya Tanganyika Bara lilikuwa likitawaliwa na Serikali moja, ambayo ni Serikali ya Sultan wa Zanzibar. Ilikuwa ni ajali ya kihistoria tu kwamba hatukuendelea kuwa nchi moja. Wakati Wakoloni walipozitwaa Nchi za Afrika Mashariki, walikubaliana kuwa eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba na ukanda wa Pwani wa Kenya liwe chini ya Himaya ya Uingereza na eneo la ukanda wa Pwani na sehemu ya eneo la Bara ya Tanganyika itawaliwe na Ujerumani. Hivi ndivyo Tanganyika na Zanzibar zilivyotenganishwa. Wakati Nchi zote za Afrika Mashariki zilipotwaliwa na Uingereza, baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, utengano huo uliendelea kuwepo. Uhuru umetupa nafasi ya kurekebisha kasoro hiyo.”*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo hiyo, Mwalimu aliendelea kuisisitiza kwa maneno yafuatayo:-

*“Tanganyika na Zanzibar ni nchi jirani kijiografia, kihistoria na hata kwa lugha; ni jirani kwa desturi, utamaduni na siasa. Urafiki baina ya Chama cha Afro-Shirazi na TANU unafahamika vizuri kwenu nyote. Urafiki baina ya viongozi wa Vyama hivi viwili haukuanza jana. Tuna kila sababu ya kuungana na zaidi ya yote tunazingatia shauku kubwa ya Waafrika kuungana na nia tunayo pia. Mimi kwa niaba yenu na Rais Karume, kwa niaba ya ndugu zetu wa Unguja na Pemba, tulikutana Zanzibar tarehe 22 Aprili na kutia saini Mkataba wa kuunganisha Nchi zetu mbili.”*

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, hali hiyo kwa Watanzania haina budi kuendelea kutambuliwa na kuimarishwa kwani hadi sasa hakuna kikubwa kilichobadilika.

Aidha, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere katika kitabu chake kiitwacho “Uongozi Wetu na Hatma ya Tanzania” alichokitunga katika miaka ya 1990, takriban miaka 26 tangu Muungano uanzishwe, aliendelea kuzidi kuwakumbusha Watanzania juu ya Muungano wetu ambao unazingatia mazingira halisi ya nchi zetu mbili na hapa naomba kunukuu:-

*“Nchi mbili zinapoungana na kuwa nchi moja, mifumo ya kawaida ya miundo ya Katiba ni miwili: Muungano wa Serikali moja au Shirikisho la Serikali Tatu. Kwa Mfumo wa Kwanza, kila nchi inafuta Serikali yake na nchi mpya inayozaliwa itakuwa ni nchi moja yenye Serikali moja. Katika Mfumo wa pili, kila nchi itajivua madaraka fulani ambayo yatashikwa na Serikali ya Shirikisho na itakuwa ni Serikali ambayo itakuwa na mamlaka ya juu ya mambo yaliyobaki. Mambo yatakayoshikwa na Serikali ya Shirikisho ni yale ambayo yakibaki katika mamlaka ya nchi zilizoungana, basi kwa kweli nchi hizo*

*zitakuwa hazikuungana kuwa nchi moja, bali zitaendelea kuwa nchi mbili zenye ushirikiano mkubwa katika mambo fulani fulani.*

*Nchi za Afrika Mashariki zilikuwa katika hali kama hiyo kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zilikuwa nchi tatu zenye ushirikiano mkubwa, lakini hazikuwa nchi tatu zilizoungana kuwa nchi moja yenye muundo wa Shirikisho. Shirikisho halisi la nchi mbili litakuwa ni nchi moja yenye Serikali tatu, Serikali ya Shirikisho na Serikali mbili za awali zilizoungana kuzaa nchi mpya moja.*

*Tanganyika na Zanzibar zilipoungana na kuwa nchi moja, tungeweza kufuata mojawapo ya mifumo hiyo ya kawaida lakini tulishindwa kufanya hivyo kwa sababu ya udogo wa Zanzibar na ukubwa wa Tanganyika. Zanzibar ilikuwa na watu laki tatu (300,000) na Tanganyika watu milioni kumi na mbili (12,000,000). Muungano wa Serikali moja ungefanya ionekane kama Tanganyika imeimeza Zanzibar. Tulikuwa tunapigania Uhuru na Umoja wa Afrika; hatukutaka tudhaniwe, hata kwa makosa, kwamba tunaanzisha ubeberu mpya. Kwa hiyo, mimi nilipinga mfumo wa Serikali moja.*

*Shirikisho la Serikali Tatu lingekuwa ni gharama kubwa mno kwa Tanganyika. Zanzibar ingeendesha Serikali yake na kuchangia gharama za kuendesha Serikali ya Shirikisho na Tanganyika ingefanya vivyo hivyo. Lakini ni dhahiri kwamba mchango wa Tanganyika ndio hasa ungeendesha Serikali ya Shirikisho. Kwa hiyo, Tanganyika ingeendesha Serikali yake ya watu 12,000,000 na pia ndiyo ingetoa sehemu kubwa ya kuendesha Serikali ya Shirikisho la watu 12,300,000. Ni watu wanaofikiri kwa ndimi zao, wanaodhani kuwa gharama ya Serikali yoyote kati ya hizo ingekuwa ndogo, (waulizeni Wazanzibari) na wala gharama ya Serikali ya Shirikisho isingekuwa ndogo hata bila gharama za mambo yasiyo ya Shirikisho na gharama zote hizo kwa kweli zingebewa na Tanganyika.*

*Kwa hiyo, ilipaswa tujiulize kwa nini tunataka kuibebesha Tanganyika gharama zote hizo na hasa kwa nini tunataka Serikali ya Tanganyika? Hivi tuna hofu ya kwamba Tanganyika bila ya kuwa na Serikali yake, itaonekana kuwa imemezwa na Zanzibar? Hofu yetu ni kwamba tukiwa na Serikali moja, Tanganyika itaonekana kuwa imeimeza Zanzibar basi na tutafute Muundo ambao utaiondolea Zanzibar hofu hii ya kumezwa, bila ya kuibebesha Tanganyika mzigo wa kuendesha Serikali mbili zenye uzito unaolingana.*

*Hivyo ndivyo tulivyofanya na hiyo ndiyo asili ya Muundo wa Serikali mbili. Badala ya kutungua mfumo uliopo kama wapumbavu, tulitazama hali halisi yetu ilivyokuwa na tukabuni Mfumo utakaotufaa zaidi". Mwisho wa kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo hiyo Mwalimu aliwatahadharisha Watanzania kwa kusema yafuatayo:-

*“Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Muungano ambao naupendekeza katika Bunge hili, ni suala la muhimu sana linalohitaji umakini wenu zaidi. Ni dhahiri*

*kwamba Muungano huu utakabiliwa na changamoto mbalimbali. Wako watu wengi watakaona kuwa kuendelea kwa Muungano huu ni hatua ya kuwaunganisha Waafrika wote na hivyo watafanya kila njia kuuyumbisha Muungano wetu, watapanda mbegu za hofu na kusababisha chuki za kisiasa. Inabidi tujihadhari na watu wa aina hii kwani mara tu baada ya kuanzishwa kwa Muungano huu, sote tutakuwa na jukumu la kuulinda na kuuendeleza. Tumwombe Mungu atusaidie sisi na ndugu zetu wa Unguja na Pemba katika kutimiza wajibu wetu.” Mwisho wa Kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia haya yote, ninayo imani kubwa kabisa kwamba, Marekebisho haya ya Katiba ya Zanzibar, kamwe hayana nia ya kuua Muungano wetu na ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alieleza kwamba, hata kama jambo hili la Katiba Mpya lisingejitokeza kwa namna lilivyojitokeza, bado Serikali ilikuwa na wajibu mkubwa wa kuchukua mabadiliko haya ya Katiba ya Zanzibar na kufanya marekebisho stahiki katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 yatakayoweza kukidhi matakwa ya Zanzibar bila ya kuathiri Muungano wetu. Kwa kuwa sasa tumeanza mchakato wa kuitazama upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninayo imani kubwa kabisa kwamba kazi hii itafanyika kwa dhamira njema na kwa kuzingatia uhalisia wa Muungano wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la amani na utulivu nchini kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi kuwa amani na utulivu nchini vimeanza kutetereka kutokana na matukio mbalimbali yaliyojitokeza katika kipindi cha miaka kadhaa. Kuna baadhi ya Wabunge waliosisitiza kuwa, kwa hali ilivyo, Watanzania wote kwa ujumla wetu huku tukiweka itikadi zetu za Kisiasa pembeni, hatuna budi kushikamana zaidi ili kudumisha amani na utulivu, upendo na mshikamano tuliokuwa nao siku zote. Vyovyote vile itakavyokuwa, Watanzania wote kwa pamoja hatuna budi kuendelea kulinda na kuimarisha amani, mshikamano na utulivu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanya hivyo kwa kipindi chote cha takriban miaka 50 ya uhuru tukiongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika na Katiba ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na baadaye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Tumeweza kufika hapa tukiishi kwa amani, kwa maelewano na hivyo kuifanya nchi yetu hii kuwa ni kimbilio la majirani zetu ambao wamekuwa wakipata misukosuko mbalimbali. Nchi yetu imekuwa kimbilio la Wakimbizi kutoka sehemu mbalimbali. Hakuna watu wanaokimbilia nchi zenye misukosuko, wanakimbilia nchi zenye amani na utulivu kama Tanzania. Sote tutambue hili, tulikubali na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Tumekuwa nchi ya mfano, ni vizuri tukaendelea kuwa ni nchi ya mfano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanya hivyo kwa sababu wananchi chini ya Uongozi wa Vyama vyao vya Siasa vya TANU na Afro-Shiraz, waliweza kila ilipobidi kufanya mabadiliko katika Katiba kwa lengo la kwenda na wakati katika maeneo muhimu waliyoyaona kwa wakati huo kwamba yaingizwe katika Katiba na Sheria za Nchi katika kuwaongoza Watanzania. Hata baada ya Vyama hivi viwili kuungana mwaka

1977, Muungano uliotokana na ridhaa ya Vyama hivyo na wananchi wakati huo, Tanzania imeendelea kuwa nchi ya amani na utulivu chini ya Chama cha Mapinduzi mpaka mwaka 1992, tulipoona kwamba ni wakati muafaka kwa Taifa letu kuwa na Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa ili kuruhusu demokrasia zaidi, kupanua uhuru wa watu na uhuru wa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa kama ilivyokuwa wakati wa Mfumo wa Chama Kimoja, vinao wajibu mkubwa wa kuhakikisha vinaendeleza Amani, Utulivu, Mshikamano na Upendo miongoni mwa Wananchi wake na visiwe Vyama vya Siasa vya kuleta mifarakano miongoni mwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni takriban miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa hapa nchini. Kipindi hiki ni kipindi kifupi sana na ni kipindi ambapo Dunia inakabiliwa na misukosuko mingi ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa. Tusipokuwa imara, tusiposhikamana, nchi inaweza kuyumba na ikatetereka. Kwa hiyo, pamoja na tofauti zetu za itikadi za Kisiasa, za Dini, za Rangi na Jinsia, ni lazima tusimame kidete wote kwa pamoja kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inasifika ulimwenguni kote kwa kuendeleza amani, mshikamano na utulivu miongoni mwa Wananchi wake. Aidha, tumeishi bila ya kunyanyasana kutokana na imani zetu za Kisiasa, Dini na Kabila. Tumeishi tukiwa na itikadi tofauti za Vyama vya Siasa tangu mwaka 1992, tumeishi tukiwa na imani tofauti za Dini na Makabila tofauti zaidi ya 120 kabla na baada ya Uhuru mwaka 1961 hadi leo; lakini pamoja na tofauti hizo, wote tumeishi kwa uhuru, haki na usawa tukiheshimiana katika uhuru wa mawazo na imani. Aidha, nchi yetu haina Kabila, bali Wananchi wake wana Makabila yenye mila na desturi tofauti. Nchi yetu haina Dini, bali Wananchi wake wana Dini na imani tofauti; na kila mmoja anaheshimu Dini na imani ya mwenzake. Madhehebu ya Dini yana nafasi kubwa kupitia nyumba za ibada katika kuhamasisha amani na utulivu. Hivyo, nawaomba Viongozi wa Madhehebu yote ya Dini kuunganisha nguvu zenu katika kutetea, kuhifadhi na kulinda amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uko ukweli nchi nyingi Duniani zenye mafanikio ya uchumi imara ni matokeo ya juhudi za Wananchi kuwekeza katika Misingi bora ya amani na utulivu. Kwa maana hiyo, kama tunataka kujenga Uchumi imara ni lazima tulinde Nchi yetu idumu katika hali ya amani na utulivu.

Kwa maoni yangu, Bunge na Wabunge wake, linapaswa kuonesha kwa vitendo, dhamira yetu ya kujenga Taifa lenye amani na utulivu. Sisi kama Wabunge wa Bunge letu Tukufu sasa tuonesha mfano kwanza.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kwamba katika miaka 50 ya uhuru hakuna maendeleo yoyote yaliyofanyika; katika kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaoona kwamba Taifa hili halijapata maendeleo yoyote katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru na kutupa lawama kwa Viongozi na Serikali zake. Lakini wapo pia wanaoona ukweli kwamba Wananchi wa Taifa hili wamepiga hatua kubwa katika kujitelea maendeleo. Naelewa wale wanaosema hakuna

kilichofanyika, wanaweza kuwa wanasema hivyo wakidhani huko ndiyo kutekeleza dhana ya Vyama vya Upinzani au uwepo wa Mfumo wa Vyama vya Upinzani. Mimi siamini hivyo na ninaamini kuwa wengi wenu mtaniunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala hili niliwahi kulitolea maelezo nilipokuwa nahitimisha majadiliano ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tarehe 18 Juni 2010, naomba mnivumilie kidogo niseme nilichosema, nilisema; ninanukuu:-

*“Mheshimiwa Spika, naomba pia uniruhusu nitoe angalau dukuduku langu moja kwa Watanzania wenzangu. Wako baadhi yao na wengine wamo humu Bungeni ambao wamekuwa kwa muda mrefu hivi wanadiriki kubeza baadhi ya juhudi ambazo Serikali imefanya hadi hivi sasa na kuonyesha kana kwamba hapa tulipo, ni pabaya zaidi, duni zaidi, ni mahali panapotisha zaidi na panakatisha tamaa zaidi kuliko hata huko tulikotoka. Mimi binafsi siamini kuwa kauli hizi ni za dhati.*

*Naelewa kuwa, wapo Watanzania waliozaliwa kabla ya Uhuru, wako wa kipindi kati ya Uhuru na Muungano, wako pia waliozaliwa kati ya Muungano na miaka ya sabini, wako pia wa kizazi kipya. Inawezekana kabisa kwa wale wote ambao hawakuzaliwa katika vipindi vya nyuma, isiwe rahisi sana kuona tumetoka wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi; na kwa bahati mbaya baadhi ya kauli hizi zinatoka hapa Bungeni, kwa hiyo, ndio kusema wako katika makundi haya. Kwa wale waliozaliwa baadaye, ni dhahiri hawawezi kujua yaliyowasibu wa enzi hizo isipokuwa kwa kuelezwa au kusoma historia. Hali kadhalika, kwa waliozaliwa nyakati nyingine zilizofuata itakuwa hivyo hivyo. Ni dhahiri kuwa, kauli za namna hii kwa muono wangu, wakati mwingine zinavunja moyo, zinakatisha watu tamaa na zinafanya ionekane kana kwamba hakuna matumaini ya kwenda mbele. Lakini ukweli uliopo ni kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa ya maendeleo na ninalisema hili kwa sababu hata wadau wetu wa maendeleo wanakubali kwamba Tanzania imefanya juhudi kubwa katika kuwasaidia wananchi kujiletea maendeleo. (Makofi)*

*Serikali chini ya Chama cha Mapinduzi, imeweza kuiongoza nchi hii kwa kipindi chote hiki katika hali ya amani na utulivu mkubwa kabisa wa kisiasa. Leo tupo hapa tunajivuna kwa kuwa na demokrasia iliyoapanuka, Mfumo wa Vyama Vingi, uhuru mkubwa sana wa watu kwenda wanakotaka na kusema wanalotaka. Umepanua sana wigo wa Vyombo vya Habari na wakati mwingine watu wanafikiri kwamba pengine tumetoa uhuru kupita kiasi.” Mwisho wa kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimerejea kuyasema hayo kwa kuwa hata sasa katika mjadala huu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais bado kuna watu wenye mawazo ya kwamba katika muda wa miaka 50 ya uhuru, Serikali haijafanya kitu chochote katika kuwaletea wananchi wake maendeleo. Napenda tena kuwakumbusha kuwa, kuna mengi yaliyofanywa na Serikali chini ya TANU na ASP na hadi sasa chini ya Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kulieleza Bunge hili kuonyesha Mkoloni alipoondoka katika nchi zetu, wananchi aliwaachia maendeleo ya namna gani katika masuala ya uzalishaji mali kama vile Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na kadhalika. Sina haja ya

kuwaeleza hali ya elimu tuliyoachiwa ilikuwa ya aina gani kwa mfano, Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu vilivyokuwepo wakati huo. Lakini pia hata kama ningefanya hivyo, kwenye Sekta ya Afya tungeulizana walituachia Zahanati ngapi? Vituo vya Afya vingapi? Hospitali za Wilaya ngapi? Hospitali za Mikoa na Hospitali za Rufaa ngapi? Hata Madaktari waliokuwepo wakati huo kwa kulinganisha na idadi ya wakazi waliokuwepo walikuwa Wangapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba leo tunalaumiwa kwa kutokusaidia kukuza Sekta ya Maji. Lakini yafaa tuulizane, Mkoloni wakati anaondoka aliiacha sekta ya maji katika hali gani? Tuulizane! Tulirithi Visima vingapi vya Maji, tulirithi miradi mingapi ya kupeleka maji katika Miji yetu? Tuulizane yote haya ili tuweze kujilinganisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu leo lina watu takriban milioni 42 kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar milioni 1.3. Mwaka 1964 wakati tunapata Muungano wa nchi hizi mbili Tanganyika ilikuwa na watu milioni 12 na Zanzibar watu laki tatu (300,000). Ni dhahiri kuwa tumeongezeka na hivyo matumizi yetu nayo yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko kubwa kiasi hicho, Serikali haijapuza hata kidogo wajibu wake wa kuwapatia wananchi maji safi na salama. Vijiji vingi sasa vinapata huduma hiyo kupitia visima vilivyochimbwa na kuwekewa pampu au njia nyingine kutoka kwenye vyanzo vilivyo karibu. Tunaambiwa kwamba hali ya upatikanaji maji hivi sasa Mijini ni asilimia 80.3 na Vijijini ni asilimia 58.3. Juhudi za Serikali kuhusu sekta ya maji zinaonekana sehemu mbalimbali ikiwemo kukamilisha Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Viktoria kwenda Shinyanga uliogharamiwa kwa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 260. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kauli iliyotolewa na Waziri wa Maji hapa Bungeni imeonesha mikakati mingi mbalimbali inayochukuliwa na Serikali katika kuboresha sekta ya maji nchini. Hivyo, Serikali imedhamiria kwa dhati kutekeleza ahadi zake kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Elimu, hivi wanafunzi waliokuwa wanakwenda Shule walikuwa wangapi wakati Mkoloni anaondoka? Je, kulikuwa na Sekondari ngapi na Vyuo Vikuu vingapi? Leo tuna Shule za Msingi 15,816 hapa Nchini. Vijiji karibu vyote vipatavyo 11,812 vina Shule za Msingi. Wakati wa Uhuru kulikuwa na Wanafunzi 486,470 wa Shule za Msingi na kufikia mwaka 2010 kulikuwa na jumla ya Wanafunzi 8,419,305, sawa na ongezeko la asilimia 1,700.

Mheshimiwa Spika, aidha, kila mtoto mwenye umri wa kwenda Shule, leo anakwenda Shule. Umoja wa Mataifa umeona na kuridhika kabisa na jitihada za Serikali za kuandikisha watoto waliofikisha umri wa kwenda Shule ya Msingi. Hali hii ilifanya mwaka jana Tanzania kupewa Tuzo kwa jitihada za kutekeleza Lengo la Pili la Malengo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa ya kujivunia.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunazo Shule za Sekondari 4,237 katika Kata 3,338 hapa nchini. Wakati wa Uhuru kulikuwa na Wanafunzi 11,832 wa Sekondari na hadi

kufikia mwaka 2010 kulikuwa na Wanafunzi 1,638,699, sawa na ongezeko la asilimia 13,850. Wakati wa Uhuru kilikuwepo na Chuo Kikuu Kimoja. Leo tunajivuna, tunavyo Vyuu Vikuu pamoja na Vyuu Vikuu Vishiriki 32. Hivi kweli hakuna kilichofanyiak kwa kipindi hicho cha miaka 50?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, lengo ni kuwa na Zahanati moja kila Kijiji na Zahanati zilizopo hivi sasa ni 4,717 nchi nzima. Tunayo dhamira ya kweli ya kujenga Vituo vya Afya katika kila Kata. Hadi sasa tunavyo Vituo vya Afya 534. Aidha, kati ya Wilaya 114 zilizopo kwa sasa, tunazo hospitali za Wilaya 57. Kwa Wilaya ambazo hazina hospitali za Wilaya, Serikali imeweka utaratibu wa kuwa na Hospitali Teule ambazo hadi sasa zipo 18. Mikoa karibu yote ina Hospitali za Mikoa isipokuwa katika Mikoa mipya. Sasa tunazo Hospitali za Rufaa Kanda ya Kaskazini, *KCMC*, Kanda ya Ziwa, Bugando na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Bado Kanda ya Kusini na Kanda ya Kati ambapo juhudi za kujenga zinaendelea. Vilevile, tunayo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambayo ina Vitengo mbalimbali muhimu vinavyotoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sijui Mkoloni alipoondoka hali ya umeme nchini ilikuwa je? Wale wenye umri mkubwa waliokuwepo wakati huo, wanaweza kujibu swali hili vizuri. Kuhusu hali ya umeme pamoja na matatizo yake yote, Serikali imefanya jitihada kubwa za kuwezesha upatikanaji wa umeme angalau kwa kiwango tunachopata leo. Juhudi za kuongeza kasi ya upatikanaji wa umeme zipo na zimeelezwa vizuri na Waziri anayehusika. Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu ili kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kupeleka na kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya na Vijiji mbalimbali. Baadhi ya miradi inayoendelea kutekelezwa hivi sasa ni ile inayogharimiwa na Mfuko wa Changamoto za Milenia (*Millenium Challenge Account*), *JICA*, *Tanzania Energy Development and Expansion Project*, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia bajeti ya mwaka 2010/2011, Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), unaendelea kutekeleza Miradi ya Kupeleka Umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Ngorongoro, Kibondo na Kasulu na maeneo mengine ya Vijiji katika Wilaya mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali kupitia Wakala huo, inatayarisha Mkakati Kabambe wa Kupeleka umeme Vijijini na kuimarisha Mfuko wa Nishati Vijijini. Lengo ni kukamilisha upelekaji wa umeme kwenye Mikoa na Wilaya ambako Gridi ya Taifa haijafika na kujipanga vizuri katika kuongeza kasi ya kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na kuondoa umaskini, hasa katika maeneo ya Vijijini kwa kuwapelekea umeme hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961, mimi nilikuwa na miaka 13. Waliokuwa na umri mkubwa kuliko mimi, wanaweza kueleza vizuri zaidi. Kwa wakati huo nakumbuka, njia ya usafiri iliyokuwa na uhakika katika nchi yetu ni watu kutembea kwa miguu, tena kwa kupita katika barabara zisizo za uhakika. Hakukuwepo na barabara za lami, changarawe na hata za udongo tu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, tumepiga hatua kubwa ndugu zangu katika ujenzi wa barabara. Karibu Mikoa yote sasa imeshaunganishwa na barabara za lami isipokuwa Mikoa minne ambayo ni Rukwa, Kigoma, Tabora na Manyara. Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara za kuunganisha Mikoa hiyo ipo katika hatua mbalimbali za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina ama ujenzi kwa kiwango cha lami. Hivi sasa, barabara zenye urefu wa kilomita zipatazo 5,626 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami, kati ya barabara zenye urefu wa Kilometa 12,809 za Barabara Kuu nchini.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Wabunge katika kuimarisha uono wao kuwa hakuna kilichofanyika hasa na Serikali ya Awamu ya Nne, wamethubutu kusema kuwa Awamu hii haina mradi wowote wa kujivunia hata kama ni wa barabara. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa katika Ilani za Uchaguzi za CCM zilizotangulia pamoja na ile ya 2005 - 2010 na hii ya mwaka 2010 - 2015, zimetilia mkazo kwa Serikali kuendelea kuweka kipaumbele cha juu cha uwekezaji katika miundombinu, hasa ya barabara. Serikali za Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne zimeendelea kutambua umuhimu wa barabara nzuri kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2000, kati ya Barabara Kuu zenye urefu wa jumla ya kilometa 12,809, kulikuwa na kilometa 3,904 tu za lami. Kutokana na jitihada za Serikali katika Awamu ya Tatu na Nne, jumla ya kilomita 1,722 za barabara mpya za lami (*upgrading from gravel to bituminous roads*) zimejengwa kati ya mwaka 2000 na mwezi Desemba 2010 na kufanya Barabara Kuu ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami kufikia jumla ya Kilometa 5,626.

Mheshimiwa Spika, katika Serikali ya Awamu ya Tatu, miradi 14 yenye jumla ya Kilometa 1,226 ilianzishwa. Kati ya miradi hiyo, iliyokamilika katika kipindi hicho ni saba (7) yenye jumla ya urefu wa Kilomita 403. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani ilirithi miradi saba (7) yenye urefu wa jumla ya Kilometa 823 ambayo hivi sasa yote imekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika Serikali ya Awamu ya Nne, miradi mipya 27 ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 1,745 ilianzishwa. Kati ya miradi hiyo, jumla ya kilometa 392 zimekamilika kwa kiwango cha lami hadi kufikia mwezi Desemba 2010 na jumla ya Kilometa 1,353 zilizobaki zinaendelea kutekelezwa katika hatua mbalimbali. Aidha, sambamba na miradi hiyo, Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa barabara za lami zenye jumla ya kilometa 592 kati ya mwaka 2005 na mwaka 2010. Ni ukweli uliowazi kwamba maendeleo ya ujenzi wa barabara yamepunguza kwa kiasi kikubwa kero iliyokuwepo ya usafiri wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo za ujenzi wa barabara mpya kwa kiwango cha lami, Serikali ya Awamu ya Nne imeendelea kuzingatia umuhimu wa kuimarisha mtandao wa barabara zote nchini kwa kufanya matengenezo kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuongeza Bajeti ya Matengenezo ya Barabara kupitia Mfuko wa Barabara. Lengo la Serikali ni kuunganisha Miji Mikuu ya Mikoa kwa barabara za lami na Makao Makuu ya Wilaya zote nchini kwa barabara za changarawe ifikapo mwaka



2018, kulingana na Mpango Kabambe wa Uwekezaji katika Sekta ya Usafiri na Usafirishaji wa Mwaka 2007. Hatua hizo, zitachochea sana uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ni hatua moja kwenda nyingine. Sina haja ya kuendelea kutoa mlolongo wa mambo ambayo ninaweza kuyatolea ulinganisho lakini inatosha kusema Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Watanzania, Taifa hili limejitahidi na ndiyo maana leo tupo hapa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nifanye kitu kimoja kidogo. Kwa kuwa tuna wasiwasi kwamba unaweza usimalize kabla ya muda wetu, kwa kutumia Kanuni ya 28(5) kwamba zikibakia dakika kumi, Spika kama bado kuna shughuli inaendelea anaweza kuongeza dakika thelathini hadi shughuli hiyo iweze kumalizika, kwa hiyo, naomba mkubali kwamba tuongeze dakika thelathini, Mheshimiwa Waziri Mkuu endelea.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nitajitahidi. Tumepita katika hatua nyingi mbalimbali na ndefu. Niwakumbushe tu kwamba miaka ya 1980 ilikuwa ni jambo la kawaida kwa Watanzania na hasa wa Mijini kupata bidhaa zao kwa mgao. Watu tulilazimika kupanga foleni kwa ajili ya kupata robo kilo ya sukari, kipande au mche wa sabuni na mara nyingi Wananchi walipaswa kuwa na daftari la kutunza kumbukumbu za mgao anaopata. Mtu ilikuwa ukienda nje ukirudi ukimletea *Colget*, umemsaidia kweli kweli. Ilifika mahali hata kupata Soda au Bia mpaka upate kibali maalumu. Leo hapa yote yamesahaulika na tunaona kama vile hatukufanya kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanya haya kama nilivyotangulia kusema kwa kuwa kipindi chote tumekuwa ni wamoja. Ndiyo maana Mataifa Rafiki nao wameendelea kuunga mkono juhudi zetu. Kama Taifa, tumejitahidi sana kujenga uchumi imara, licha ya mitikisiko mbalimbali ya uchumi tuliyoipitia. Kuimarika kwa uchumi kumetuwezesha vilevile, kupata mapato ya kutosha. Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa wakati anachukua madaraka mwaka 1995, uwezo wa Serikali wa kukusanya mapato yake ulikuwa hauzidi Shilingi Bilioni 25 kwa wastani kwa kila mwezi. Wakati Rais wa Awamu ya Tatu anakabidhi madaraka kwa Rais wa Awamu ya Nne mwaka 2005, makusanyo yetu ya mapato ya ndani kwa mwezi yalifikia wastani wa Shilingi Bilioni 150. Hii ni sawa na ongezeko la Shilingi Bilioni 125 kwa kipindi cha miaka 10. Leo Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne, amewezesha Taifa hili kupata mapato ya ndani ya wastani wa Shilingi Bilioni 400 kila mwezi. Hii ni sawa na ongezeko la Shilingi Bilioni 275 katika kipindi cha miaka mitano. Mwezi Desemba 2010, mapato yalifikia Shilingi Bilioni 587. Hiki ni kielelezo kingine kizuri kuonesha kwamba Watanzania tuna kila sababu ya kujivuna kwamba juhudi ambazo pamoja tumezifanya, zimetuletea matunda haya.

Mheshimiwa Spika, kama alivyokwisha kusema Waziri wa Fedha, tumepata mafanikio mengi katika kutekeleza Sera za Uchumi Jumla. Mafanikio hayo, ni pamoja na, uchumi wa Nchi yetu unaendelea kuimarika siku hadi siku licha ya athari za

msukosuko wa uchumi duniani, kupanda kwa bei ya mafuata katika soko la dunia na uhaba wa mvua katika baadhi ya maeneo nchini. Katika Kipindi cha mwaka 2005 - 2010, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo ukuwaji ulikuwa chini ya asilimia tano. Matarajio katika mwaka 2010 ni kwamba kiwango cha ukuaji wa Pato halisi la Taifa kitafikia asilimia saba (7). Changamoto kubwa tuliyonayo, ni kuhakikisha kuwa ukuaji huo wa uchumi unaboresha hali ya maisha ya Watanzania wengi pamoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini kwa Wananchi wetu ambao wengi huishi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni imeimarika sana. Hadi Desemba 2010, nchi yetu ilikuwa na akiba ya Dola za Marekani milioni 3,980 ambazo ni sawa na miezi 6.5 ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na miezi 4.8 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Wadau wetu wa Maendeleo, wanaendelea kutuunga mkono katika kuongeza na kutimiza ahadi zao za Misaada na Mikopo kwa Tanzania. Jumla ya Misaada na Mikopo ya Kibajeti (*General Budget Support-GBS*), Mifuko ya Kisekta (*Sector Baskets*) na Miradi ya Maendeleo ilifikia Shilingi Trilioni 2.4 mwaka 2009/2010 kutoka Shilingi Trilioni 1.37 mwaka 2005/2006; sawa na ongezeko la asilimia 57. Hii ni kielelezo kwamba hata wahisani bado wanatuamini na hii inatokana na usimamizi imara na utawala bora unaosimamiwa na Serikali ya CCM na viashiria hivi vinaonesha kuwa Watanzania kupitia Vyama vyao, Viongozi wake na Serikali yao, wamekuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha uchumi na kutekeleza sera zinazochochea kuondoa umaskini na kukua kwa uchumi. Serikali inatambua kuwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijijini wakitegemea Kilimo. Kwa kuwa kasi ya ukuaji wa kilimo imekuwa ndogo ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu, Serikali ya Awamu ya Nne imeweka mkazo kupitia Azma ya KILIMO KWANZA ili kuboresha sekta ya kilimo. Serikali imejipanga kuleta mabadiliko katika kilimo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji na kuanzisha Kongano (*Clusters*) zenye lengo la kuleta msukumo wa ukuaji katika sekta ya kilimo (*Kilimo Kwanza Growth Corridors*).

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, napenda kueleza kuwa Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati akizindua Bunge hili la Kumi, imezingatia na inaendana na ahadi za Serikali ya Awamu ya Nne ambazo zipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. MKUKUTA II, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Milenia na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya hadi mwaka 2025. Kwa mantiki hiyo, ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa utasaidia sana Serikali katika kutekeleza na kufikia malengo ya mipango hiyo.

Aidha, michango hii ya Wabunge itatusaidia sana katika kupanga vizuri vipaumbele vya Bajeti ya Serikali ya mwaka ujao ili vitoe ufumbuzi wa changamoto zinazokabili Taifa kwa sasa na pia kutatua kero mbalimbali za wananchi. Kwa hiyo,

tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika kuleta maendeleo kwa Watanzania wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, naomba nizungumzie kidogo juu ya migomo Vyuoni na maandamano. Migomo hii ambayo imehusisha wanafunzi katika baadhi ya vyuo pamoja na Wahadhiri imetokea kwa zaidi ya Vyuo 17 vya elimu ya juu hapa nchini. Sababu za migomo hii ni nyingi lakini zimeelezwa kuwa ni kutoridhika na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi kwa sehemu kubwa, baadhi ya *program* kutokuwa na mafunzo kwa vitendo, wanafunzi kuishi katika mazingira yasiyoridhisha kusomea na baadhi ya vyuo kudahili wanafunzi kwenye *program* ambazo hazijaidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu na hivyo kukosa mikopo. Zipo pia sababu za Vyuo kutoza ada kubwa au kupandisha ada kwa kiasi kikubwa na katika baadhi ya Vyuo wanafunzi kutaka Serikali iongeze posho ya chakula na malazi kutoka Sh.5000 ya sasa kwa siku na kufikia Sh.10,000. Aidha, zipo sababu za kiutawala ambapo wanafunzi wameonesha kutoridhika na Uongozi na Menejimenti wa baadhi ya Vyuo. Migomo hii imesababisha vurugu Vyuoni na hivyo kuvuruga ratiba za masomo na amani kwa ujumla. Vilevile kutokana na vurugu hizo, muda mwingi umepotea katika kushughulikia ufumbuzi wa migogoro kwa upande wa Vyuo na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sababu ambayo imejitokeza katika kila mgomo ni kuhusu utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu. Hata hivyo, kumekuwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali kutafuta ufumbuzi wa suala hili la mikopo. Itakumbukwa kwamba Serikali iliweka Sera ya Uchangiaji katika Elimu ya Juu mwanzoni mwa miaka 1990 ili kuwawezesha wanafunzi ambao wengi walikuwa hawana uwezo kabisa wa kuchangia kiasi kilichotakiwa kutokana na vyanzo vyao vya mapato. Serikali iliweka utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi hao.

Mheshimiwa Spika, mikopo hiyo ilikuwa inatolewa na Serikali kupitia Wizara iliyokuwa na dhamana ya elimu na ilikuwa inatolewa kwa asilimia 100 kwa maeneo ya chakula, malazi, vitabu, viandikwa, utafiti, ada ya mafunzo, mahitaji maalum ya vitivo na mafunzo kwa vitendo. Mwaka 2004 ilianzishwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ili kusimamia suala zima la utoaji na ukusanyaji wa mikopo. Bodi hiyo ilianza kazi rasmi Julai, 2005. Kwa hiyo, mwaka 2005/2006, Bodi ilitoa mikopo kwa maeneo yote niliyoyataja hapo juu kwa asilimia 100. Mwaka uliofuata 2006/2007, Bodi ilitoa mikopo kwa asilimia 100 kwa maeneo ya chakula, malazi, utafiti, vitabu na viandikwa. Aidha, ilitoa mikopo ya asilimia 60 ya mahitaji ya gharama za ada ya mafunzo, mahitaji maalum ya vitivo na mafunzo kwa vitendo kwa kila mwanafunzi. Hivyo, mwanafunzi alichangia asilimia 40 katika kugharamia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008/2009, utoaji wa mikopo kwa baadhi ya maeneo ilizingatia matokeo ya kitu tulichokiita *Means Testing* ambapo wanafunzi walitengwa katika madaraja sita ya A - F ya asilimia 100 hadi 0. Aidha, kuanzia mwaka 2009/2010, madaraja hayo yaliongezeka kutoka 6 mpaka 11. Maeneo yaliyozingatia matokeo ya *Means Testing*, ni ada ya mafunzo, mahitaji maalum ya kitivo na mafunzo kwa vitendo yaani shilingi 10,000 kwa kila siku zisizozidi 56000 kwa mwaka. Madaraja

hayo yalizingatia historia ya elimu ya mwombaji, kiwango cha elimu ya wazazi na mlezi, shughuli za kiuchumi za mwombaji na mzazi/mlezi, mali za mwombaji na mzazi au mlezi na mahali zilipo, hadhi ya maisha yake na wazazi au walezi wake kijamii, hali ya kijamii ya mwombaji, uyatima na ulemavu. Wanafunzi waliopewa kipaumbele ni wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi kwa kiwango cha Daraja la Kwanza na la Pili katika mitihani ya Kidato cha Sita.

Aidha, wanafunzi wote wanaosomea Masomo ya Sayansi kwa maana Afya za Binadamu na Wanyama, Kozi za Uhandisi, Kilimo, Walimu na kadhalika na wale waliopolekwa kusoma nje ya nchi chini ya makubaliano kati ya Serikali yetu na Serikali zingine wamekuwa wanapewa pia kipaumbele. Hivyo kutokana na sifa hizo, wanafunzi walichangia gharama za mahitaji hayo kwa kiwango mbalimbali kati ya asilimia 0 -100.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya ukopeshaji yafuatayo yaliendelea kupata mikopo kwa asilimia 100. Kwanza, chakula na malazi, kwa sasa ni shilingi 5000 kwa mwanafunzi kwa siku kwa idadi ya siku atakazokaa Chuoni. Pili, vitabu na viandikwa, kwa sasa ni 200,000 kwa wanafunzi kwa mwaka na tatu utafiti kwa sasa ni shilingi 100,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, takwimu za ongezeko la wanafunzi waliokopeshwa na kiasi cha fedha kwa kipindi cha 2004/2005 - 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004/2005, idadi ya wanafunzi waliokopeshwa ilifika 16,345 na kiasi kilichokopeshwa ni shilingi bilioni 9.9. Mwaka 2005/2006, wakaongezeka hadi 42,729 na kiasi kilichotolewa kikawa ni shilingi bilioni 56.1. Mwaka 2006/2007, wanafunzi walikuwa 47,554 na fedha zilizotolewa zikawa shilingi 76.1 bilioni. Mwaka 2007/2008, wanafunzi wakafikia 56,687, fedha zilizotolewa ni shilingi 110.8 bilioni. Mwaka 2008/2009, wanafunzi wakawa 58,796 na fedha zilizotolewa ni shilingi 139 bilioni. Mwaka 2009/2010, wanafunzi wakafikia 72,035 na fedha ya mikopo iliyotolewa ikafikia shilingi 184.7 bilioni. Mwaka 2010/2011, tunatarajia wanafunzi 85,319 na fedha zilizotengwa ni shilingi 237.8 bilioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla takwimu hizo zinaonesha kwamba katika kipindi cha miaka mitano, mwaka 2005 - 2010 iliyopita, idadi ya waliokopeshwa imeongezeka kwa asilimia 100. Muhimu zaidi ni kuwa ongezeko hilo limekuwa linakua mwaka hadi mwaka kutoka mwaka 2006, asilimia 11 hadi mwaka 2009/2010 asilimia 22. Hivyo, ni wazi kuwa kutoa mikopo kwa madaraja kumeongeza uwezo wa Serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi. Aidha, katika kipindi hicho, fedha zilizokopeshwa nazo zimeongezeka kutoka katika kiwango cha shilingi bilioni 56.1 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 184.7 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 229. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Serikali imekuwa ikijitahidi kuwawezesha wanafunzi wengi kupata mikopo kulingana na vigezo vilivyowekwa vya *Means Testing*. Hata hivyo, bado kuna upungufu katika suala zima la viwango na mfumo wa utoaji mikopo vinavyosababisha malalamiko mbalimbali kutoka kwa wadau na wakati mwingine kusababisha migomo.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua suala la migomo, kumekuwepo na mikutano kadhaa iliyohusisha Serikali, Menejimenti za Vyuo na viongozi na wanafunzi, Wahadhiri na hata wakati mwingine kuzungumza na wanafunzi wote ili kutafuta suluhisho la madai hayo. Serikali pia imekuwa ikitoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu kiini cha migomo hii na hatua mbalimbali zinazochukuliwa. Hatua za hivi karibuni ni pamoja na Mheshimiwa Rais kuunda Tume ambayo itatoa mapendezo ya viwango vya mikopo vinavyolingana na hali ya sasa ya uchumi na kushauri namna bora ya kutoa na kurejesha mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Tume hii imeshaanza kazi na inatarajia kutoa ripoti yake kabla ya tarehe 15 Aprili, mwaka huu. Aidha, Serikali imeagiza Tume ya Vyuo Vikuu kushughulikia madai yanayohusu taaluma ili wanafunzi waweze kusoma bila matatizo. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameanza kufanya ukaguzi wa hesabu za Vyuo ili kuishauri Serikali namna ya kuondoa malalamiko yanayohusu fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kuwakumbusha wana Jumuiya wa Vyuo Vikuu kuwa chini ya Hati Idhini ya Vyuo (*Charters*) na Sheria za Wanafunzi, migomo hairuhusiwi vyuoni. Sheria Ndogo za Wanafunzi pia zinatamka kuwa kama wanafunzi watagoma kuingia darasani kwa siku tatu mfululizo, Mkuu wa Chuo anaweza kuwafukuza au kufunga Chuo. Hivyo migomo katika Vyuo Vikuu, ni kinyume cha Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanafunzi pia wakati mwingine hufanya maandamano katika kujaribu kuwasilisha hoja zao kwa Viongozi wa Vyuo na Serikali na pengine bila hata kuwa wamechukua hatua zozote za kuwasilisha malalamiko yao rasmi kwa ngazi zinazohusika. Wakati suala zima la migomo na maandamo linafanyiwa kazi, wito wangu kwa wanavyuo wote ni kwamba kudai haki kwa njia ya migomo na maandamano bado siyo utaratibu mzuri kwani athari zake ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashauri wanavyuo, Wahadhiri na Wafanyakazi wote, kutumia njia ya majadiliano zaidi hadi kufikia muafaka kama njia ya kutatua matatizo yetu. Serikali wakati wote imekuwa sikivu na itaendelea kuwa sikivu ili kudumisha amani na umoja wa nchi yetu. Serikali iko tayari kupokea, kujadili, kuchambua na kufanyia kazi ushauri wowote unaotolewa kwake kwa maslahi ya Watanzania. Milango iko wazi na yeyote mwenye wazo, ushauri, hoja na kero anakaribishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nimeona nieleze haya kama njia ya kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Vyama vyote vya Siasa na wananchi wote, kutambua kwamba si busara kubeza juhudi zenu ambao zimesaidia kuwafikisha hapa. Nawaomba tuungane, naliomba Bunge lako Tukufu, litusaidia katika kutuunganisha katika juhudi za kuwaletea Watanzania maendeleo. Michango yenu Chanya hapa Bungeni na nje ya Bunge, ndiyo kielelezo cha Watanzania walio chini ya msingi muhimu wa Umoja wa Kitaifa. Wote tujiepushe na jambo lolote lenye lengo la kurudisha juhudi hizi nyuma kwa kudhani kwamba zitatuzesha kushika madaraka. Kwani kwa kufanya hivyo na ukaweza kweli kushika madaraka kwa njia ambazo si za amani na utulivu, kazi ya

kujenga amani na utulivu itawachukua miaka mingi sana ambayo ingeweza kutumika kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu pamoja na Naibu Spika wako Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge. Naomba niwapongeze kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuchaguliwa na kupewa dhamana kuwakilisha wananchi katika Bunge letu hili. Kwa namna ya pekee, niipongeze Kambi ya Upinzani, Chini ya Kiongozi wenu, Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuchaguliwa kwenu na Watanzania. Tukumbuke kwamba sisi ndio mboni ya jicho la Watanzania wote waliotuchagua kuja hapa Bungeni. Tunayoyafanya Bungeni yawe kwa maslahi ya wananchi wetu wote. Hivyo katika kutekeleza jukumu hili, ninyi mliopo upande wa Upinzani, ninawasihi sana ushirikiano, kwani ninyi wote mko katika Kambi moja ya Upinzani na ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, tufanye kazi kwa karibu sana. Tujitahidi kuondoa tofauti zetu zote kwa maslahi ya Watanzania. Kwa kuwa sisi ni Wabunge wa Bunge hili, wote ni Watanzania basi hatuna budi kufanya juhudi za dhati za kupendana, kushirikiana na kusaidiana kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza mjadala wetu wa siku tano kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati anafungua Bunge hili, hata nyie Wabunge mmejadili vizuri sana. Kama nilivyokuwa nawaeleza, hapa mlikuwa mnapasha moto, mjadala wenyewe utakuja wakati wa bajeti, pengine mtajipanga vizuri zaidi, pale ndio mtaibana Serikali sawasawa hapa tulikuwa tunaboresha Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ambayo alitoka siku ya kwanza ya kufungua Bunge.

Kwa hiyo, nawashukuru Mawaziri kwa ufafanuzi. Ufafanuzi mwingine tulikuwa tunatamani kuusikiliza sana lakini muda wenyewe ulikuwa dakika kumi. Waheshimiwa Wabunge wengine wameniletea *vi-note*, wanasema haya maelezo kama mnaweza kuwapa kwa maandishi, baadhi ya mambo ni makubwa, wangepurahi. Lakini sijui kama mtakuwa na muda kwa sababu haya yatarudia tena wakati wa kipindi cha bajeti. Mimi nadhani wametufungua macho lakini tuendeleo kufanya utafiti wakati wa kipindi cha bajeti kikija basi mtakuwa mmejiandaa vizuri zaidi kuliko hivi tulivyokuwa tumeweka.

Kwa hiyo, nakushuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhitimisha hoja hii na napenda wote tushirikiane kwamba tuunge mkono tuendelea kuifanyia kazi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki utekelezaji wa Hoja ya Hotuba ya Rais)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kesho ni sikukuu ya Maulid, kwa hiyo, hakutakuwa na kazi hapa Bungeni. Kutokana na ratiba yetu, hapo mwanzo hatukuzingatia sikukuu hii. Kwa hiyo, shughuli ambazo tulipanga zifanyike, zitafanyika tarehe 17 na shughuli ambazo zilikuwa zifanyike tarehe 17 zitafanyika tarehe 18, zile za tarehe 18 kwa kweli itabidi tukubali kwamba hazipo.

Tulikuwa na nafasi pia ya kuweza kuingiza hoja binafsi za Wabunge mpaka tunavyokaribia siku mbili, tatu, inaelekea uzoefu wetu bado ni mgeni wengi hawakuweza kuhitimisha vile inavyostahili. Lakini ni kusudio letu kwamba katika vipindi vijavyo, kila Bunge tutakuwa na siku ya hoja binafsi na wakati wa Bunge la Bajeti, siku zitaongezeka kwa sababu tunakaa muda mrefu. Kwa hiyo, kipindi hiki hatuna hoja ambayo imekamilika kuweza kufika hapa Bungeni. Nyingine zilikuwepo lakini baadaye Serikali ikaja ikahitimisha nadhani wenye hoja pia wameridhika kwamba utaratibu utakaotumiwa na Serikali utatuhusisha sisi wote kujadili kikamilifu namna tunavyotaka suala la Katiba liendeshwe. Kwa hiyo, hizo nazo zimepitwa na wakati. Lakini haidhuru kama kuna hoja zingine, ofisi yangu itaendelea kuwasiliana na ninyi Wabunge mliozileta kwa maana ya kuziboresha lakini kwa Bunge hili, hatuwezi kuzipitisha, hakuna hata moja.

Kwa maana hiyo ni kwamba siku ya Alhamisi maana nimesema kazi za tarehe 16 zitakuwa tarehe 17, tutaanza na kikao cha Bunge kwa kipindi maswali, bahati nzuri Waziri Mkuu utakuwepo, kwa hiyo kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kitakuwepo, halafu tutakuwa na semina tuliyosema. Tarehe 18 ndio ilikuwa tuwe na Semina itahamia tarehe 17, halafu tarehe 18 yenyewe tutaendelea na suala zima la kupanga mkakati kwa ajili ya kazi za Kamati kipindi hiki kifupi kabla ya kumaliza Bunge la Bajeti na kipindi cha mwaka unaofuata. Kwa hiyo, tutazidi kuelekeza wakati ukifika.

Pamoja na hayo, nilikuwa na matangazo machache, bado Mheshimiwa Dkt. Ndugulile anasema Wabunge vijana wa chini ya miaka 45 wakutane pale Ukumbi wa Pius Msekwa, anakumbushia hilo.

Baada ya kusema hayo, lingine nawatakieni sikukuu njema ya kesho, wenye kushiriki kwenye ibada, watuombe wote ili nchi yetu iendelee kuwa na amani na tufaidi matunda ya amani.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho kutwa saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.57 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 17 Februari, 2011, Saa Tatu Asubuhi)*